

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

Kikao cha Arobaini na Tatu – Tarehe 12 Agosti, 2008

(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Na. 372

**Ukosefu wa Huduma ya Mawasiliano
ya Simu- Kongwa**

MHE. GEORGE M. LUBELEJE (K.n.y. MHE. JOB Y. NDUGAI) aliuliza:-

Kwa kuwa, katika Kata ya Chamkoroma, Hogoro, Mkoka na Zoisa Wilayani Kongwa hakuna mawasiliano ya simu; na kwa kuwa wananchi wa maeneo hayo kuitia kwa Mbunge wao wamewasilisha Serikalini maombi yao ya kufikishiwa huduma hiyo:-

Je, Serikali inasema nini kuhusu tatizo hilo?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
aliyibuu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Job Ndugai, Mbunge wa Kongwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya ZAIN ambayo zamani ilikuwa inajulikana kama CELTEL imejenga mnara katika maeneo ya Mkoka na Hogoro na kufikisha huduma ya mawasiliano katika maeneo hayo na maeneo jirani. Hata hivyo, Kampuni hiyo ina mipango ya kujenga mnara eneo la Chamkoroma kabla ya mwisho wa

mwaka huu wa 2008. Pia tafiti za masoko zinaendelea katika eneo la Zoisa ili kufikisha mawasiliano ifikapo Februari 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya Simu ya *VODACOM* iko katika mchakato wa kiufundi kubaini maeneo muafaka kwa ajili ya kujenga mitambo ya mawasiliano katika maeneo ya Wilaya ya Kongwa. Aidha, katika utafiti huo yatajumuishwa maeneo ya Kata za Chamkoroma, Hogoro, Mkoka na Zoisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya *ZANTEL* kwa sasa imefikisha mawasiliano Kongwa. Kampuni hiyo itafanya tafiti katika maeneo mengine yaliyo karibu na Kongwa kwa ajili ya kuweka minara ya mawasiliano.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Kata ya Chamkoroma inapakana na Kata ya Matomondo vijiji vya Tambi, Mlembule, Mwenzele na kwa kuwa mnara huu ukijengwa mawasiliano yatafika mpaka vijiji nilivyovitaja. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba iko haja ya kujenga haraka mnara huo ili wananchi wa Kata ya Matomondo nao waweze kupata mawasiliano.

Lakini swali la pili, kwa kuwa kuna mnara wa *CELTEL* ulijengwa kati ya kijiji cha Lukole, Chiseyu na Mnzase. Na mnara huo sasa una miaka miwili haufanyi kazi. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri ana maelezo gani kwa wananchi wa Wilaya ya Mpwapwa?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nikubaliane naye kwamba kuna mnara wa *CELTEL* pale baada ya kunieleza leo asubuhi ambaao muda mrefu haujafanya kazi lakini naomba nilichukue niliulizie ipasavyo kwa sababu mimi siwezi kutoa jibu sasa hivi nitakuwa namdanganya Mheshimiwa Naibu Spika.

Pili, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya kufikisha mawasiliano katika maeneo ambayo ameyazungumzia Mheshimiwa Job Ndugai ambaye ni karibu sana na maeneo ya Mheshimiwa Mbunge aliyoyaeleza nina hakika mawasiliano katika maeneo hayo ya karibu na vijiji ambavyo amevitaja yatakuwa yamefikiwa. Kama kutakuwa na matatizo zaidi Mheshimiwa Mbunge wa Mpwapwa tuwe tayari kuwasiliana.

MHE. KAIKA S. TELELE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa kijiji cha Engalisero kiko katika eneo la Lake Natron eneo la Mlima Lengai na *Rift Valley*. Na kwa kuwa ndege zimekuwa zikianguka pale helkopta na ndege hizi ndogo na namna ya kuwasiliana kutoa taarifa kwa ajili ya kusaidia uokozi inashindikana kwa sababu hakuna mawasiliano yoyote. Je, Serikali inaweza kutoa tamko gani kuhusiana na kuweka mawasiliano ya simu za mkononi eneo hilo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, swali jipya kabisa kabisa. Mheshimiwa Naibu Waziri kwa sababu ya umahiri wako basi naomba ujibu.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Telele tulishalizungumza suala hili mimi na wewe jana na tukakubaliana kitu cha kufanya.

Napenda nikuhakikishie na niwahakikishie Waheshimiwa wananchi wako katika jimbo lako kwamba tutawasilisha ombi lako hilo kunakohusika ili mawasiliano eneo la *Lake Natron* yaweze kuwafikiia wananchi.

Lakini ukumbuke kwamba vijiji viko mbalimbali sana inawezekana tukafikiwa sehemu nyingine sehemu nyingine kukawa hakutofikiwa kwa uharaaka zaidi. Lakini nilikuahidi na Mheshimiwa nakuahidi tena kwamba tutalishughulikia suala lako.

Na. 373

**Minara ya Simu Kujengwa
Katika Makazi ya Watu**

MHE. KHADIJA SALUM ALLY AL-QASSMY(K.n.y. MHE. NURU A. BAFADHILI) aliuliza:-

Kwa kuwa, Kampuni za *VODACOM*, *CELTEL* na *TIGO* zimejenga minara mingi na mingine ikiwa karibu sana na maeneo ya makazi ya watu:-

Je, Serikalli haioni kuwa athari inayotokana na mionzi ya minara hiyo ni hatari kwa binadamu na inaweza kuwa chanzo cha magonjwa kama Saratani?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA aliujibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nuru Awadhi Bafadhili, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa baadhi ya minara ya Makampuni ya Simu imejengwa karibu na maeneo ya makazi ya watu.

Minara ya simu inayojengwa na Makampuni ya Simu kama vile *TIGO*, *VODACOM* na kadhalika kwenye makazi ya watu haina madhara makubwa sana kama tafiti zilivyosema ikilinganishwa na manufaa ambayo binadamu na Taifa inazipata kutokana na fursa mbalimbali zinazotokana na huduma za mawasiliano. Mawasiliano, licha ya kuziwezesha sekta zingine za jamii na uzalishaji kutoa mchango wake katika uchumi wa Taifa, pia ni kichocheo kinachompa uwezo mwananchi kuibua fursa na kuzitumia kupambana na changamoto za maisha kama vile umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tafiti za kisayansi zinazofanyika hadi sasa na vyombo mbalimbali vya Kimataifa kama vile Shirika la Afya Duniani (*WHO*) na Taasisi za Udhibiti wa Nishati za Mionzi (*Atomic Energy Radiation Control Institute*) hazijathibitisha kuwepo kwa athari kubwa za minara ambayo inasimikwa karibu na makazi ya binadamu. Hata hivyo, Serikali inaendelea kuchukua tahadhari za kutafiti zaidi kuhusu ukweli wa minara ya simu na mionzi yake ili kuepusha madhara mengine ya kiusalama mfano mvurugo wa mawimbi (*interference*), kelele za jenereta zinazosukuma mitambo ya kurushia mawimbi, na usikivu hafifu inayotokana na miingiliano ya miangwi (*echoes*) itokanayo na minara hiyo kuwa karibu na nyaya za umeme mkubwa (*grids*). Hatua mojawapo ya tahadhari ni kuzishawishi Kampuni kuchangia matumizi ya minara ili kupunguza msongamano na kuimarisha utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, suluhisho la kudumu ni ujenzi wa Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano (*National ICT Infrastructure Backbone*) ambao Serikali inakamilisha taratibu za utekelezaji wake. Ujenzi na matumizi ya minara ya simu utapungua Mkonga huu utakapokamilika ambao unatumia teknolojia bora na yenye gharama nafuu. Sanjari na hatua hiyo, Serikali kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mawasiliano (*TCRA*) hivi sasa iko kwenye mchakato wa kufanya mapitio ya Sheria ya Mawasiliano ili kuzifanyia marekebisho ziweze kukidhi mahitaji mbalimbali ikiwemo ya watoa huduma za simu kuchangia minara.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitoe tahadhari na niwaombe Makampuni waache kujenga minara katika mikusanyiko ya watu na ikiwezekana hasa Mashule.

MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa katika upokeaji wa simu tunapoweka kwenye sikio inasemekana kuna madhara ya mionzi ambayo inaweza ikaathiri maungo fulani fulani katika mwili wa binadamu. Mheshimiwa Waziri anaweza akawaambia wananchi je ule utaratibu wa kupokea simu kwa utaratibu wa *blue tooth wireless* kuna madhara yoyote au hakuna madhara?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyokuwa najibu hapa Bungeni siku zote kwamba

kitu kizuri mnaposikiliza simu ndugu zangu Wabunge na Waheshimiwa wananchi mnaonisikiliza mtumie kile kifaa ambacho kinawekwa kwenye sikio na ikiwezekana usizungumze kwa muda mrefu sana. Tafiti zilivyofanyika hivi karibuni zimeeleza kwamba na zimetoa mawaidha kwamba ikiwezekana sikiliza simu yako kwa kutumia sikio la kushoto na sio sikio la kulia kwa sababu wanasema sikio la kulia inakwenda mionzi mara kwa mara na *exposure* hii usikae nayo zaidi ya *one hour*. *One hour* ni nyingi sana kuweka sikioni. Kama mtafanya utafiti ninyi wenyewe mnaposikiliza simu kwa zaidi labda ya nusu saa utasikia sikio lako ni jekundu na linawaka moto hicho si kitu kizuri kwa sababu hii inaongeza *temperature*. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla simu zinapouzwa zinauzwa na hivi vitu vina maana yake mvitumie ili viwasaidie mjikinge na madhara mbalimbali.

Na. 374

Dawa Tata MSD

MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA aliuliza:-

Kwa kuwa, dawa toka *MSD* hazipatikani za kutosha kulingana na mahitaji ya hospitali, vituo vya afya na zahanati zetu wakati Serikali inakuwa imeshawapatia fedha:-

Je, Serikali iko tayari kuwapatia *MSD* nusu ya fedha, na nusu nyingine zikabidhiwe kwa Halmashauri zetu ili zinunue dawa sehemu nyingine ili kuondokana na ukiritimba?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Emmanuel Jumanne Luhahula, Mbunge wa Bukombe kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa linakuwepo tatizo la kukosekana dawa za kutosha katika vituo vya afya na zahanati zetu. Tatizo hili lipo kwa viongozi wa vituo katika Halmashauri yaani Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri na Waganga Wakuu wa Halmashauri katika ukadiriaji wa mahitaji na uagizaji dawa mapema (miezi mitatu kabla ya dawa kuisha). Suala ambalo hupelekea *MSD* kuwa na idadi isiyo sahihi na kuletewa maombi katika muda mfupi.

Kwa kutambua udhaifu huo, Wizara iliendesha mafunzo ya “*Quantification and Forecasting*” kwa watumishi wa hospitali zote za Serikali nchini ili kuwawezesha kuainisha mahitaji yao ya dawa za mwaka mzima. Mwezi Desemba 2007, mahitaji ya dawa za vituo vyote yalijumuishwa ili yatumike katika kuandaa bajeti ya Wizara ya mwaka wa fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, mahitaji hayo yalipelekwa *MSD* ili kuwawezesha kuandaa mipango mizuri ya ununuzi wa dawa zitakazotosheleza wateja wao kwa kipindi cha mwaka mzima wa 2008/09. Katika mwaka ujao wa fedha 2008/2009 *MSD* itaanza

kutoa huduma kwa wateja wake kwa kutumia mfumo wa uagizaji unaojulikana kama “*Budget-Based Ordering (BBO)*”. Chini ya mfumo huu, kila kituo cha afya kitalazimika kuagiza dawa zake kulingana na kiasi cha fedha kilichopo kwenye akaunti ya kituo. Hii itawezesha kituo kuagiza dawa ambazo ni muhimu sana na za kutosheleza kulingana na uwezo wa kifedha katika kituo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara pia imeandaa orodha ya dawa na vifaa tiba ambavyo ni muhimu sana na ambazo hazitakiwi kukosekana katika vituo vya afya wakati wowote (*vital drugs*) na orodha hii imekwishapelekwa kwenye Halmashauri zote nchini. Aidha, Wizara imetoa ruhusa kwa vituo vya afya kununua dawa hizi toka masoko binafsi kwa kutumia vyanzo vya fedha zinazozalishwa katika kituo cha afya kama vile fedha za uchangiaji (*Cost Sharing*), fedha za Mfuko wa Pamoja wa Wahisani (*Basket Fund*), Fedha za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (*NHIF*) na fedha za Mfuko wa Afya ya Jamii (*CHF*). Kwa sababu hii, Serikali haioni sababu ya kupunguza fedha kutoka *MSD* na kuzipatia Halmashauri kwa ajili ya ununuzi wa dawa.

MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri.

Swali la kwanza kwa kuwa tatizo la ukosekanaji wa dawa *MSD* wakati mwengine linasababishwa na kukosekana fedha zilizopelekwa katika *MSD* hasa katika Wilaya ya Bukombe wanapokwenda wakati mwengine Bajeti inakuwa ni ndogo hailingani na hospitali yenewe. Je, Serikali inawahakikishiaje wananchi wa Wilaya ya Bukombe inapewa Bajeti inayofanana na Hospitali ya Wilaya ili waweze kupata dawa kutoka *MSD* pasipo usumbufu?

La pili, kwa kuwa katika majibu yake Mheshimiwa Naibu Waziri amesema viko vifaa tiba na madawa ambayo hayatakiwi kukosekana katika vituo vya afya au hospitali. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri au Serikali mnaweza mkatupatia vifaa hivyo orodha yake kabla ya Bunge hili, ili na sisi tujifahamu?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ambayo inapangwa kwa kila hospitali huwa Makadirio yake yanaanzia katika Halmashauri husika na inakwenda katika mfumo wa Bajeti kama tunavyofanya hapa.

Kwa hiyo, Wilaya ya Bukombe kama fedha inayopatikana haitoshi ina maana wao wenye ndio wanaobajeti na kuleta Wizarani kuona kwamba ni kiasi gani wanahitaji na ile fedha wanayoiomba ndiyo ambayo wanapewa. Hivyo kama Mheshimiwa Mbunge ana taarifa kwamba fedha wanazopewa Bukombe hazitoshi nashauri kwamba wakae waende vizuri ili walete Makadirio yao ili waweze kupata fedha kulingana na mahitaji yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kuhusu vifaa kukosekana kama nilivyokuwa najibu swali la msingi nimesema orodha hii imepelekwa lakini tuko tayari kuwalettea orodha na kuwapa Waheshimiwa Wabunge ili nao wafahamu ni dawa zifi ambazo wanatakiwa kuwa nazo kwa ufahamu tu.

MHE. DR. WILBROD P. SLAA – NAIBU KIONGOZI WA UPINZANI BUNGENI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Naibu Waziri amesema kwamba tatizo la Bajeti huwa linaanza kwenye Halmashauri. Je, anafahamu kwamba fedha zinapoidhinishwa hatimaye huwa inakatwa katika *cealing*. Lakini tatizo la pili vile vile ni kwamba anapoeleza kwamba tatizo ni ukadiriaji wa madawa Waziri atakubaliana nami kwamba amepotoshwa ama amedanganywa na *MSD* kwa kuwa taarifa iliyoko kwenye Kamati yetu ya *LAAC* inaonyesha kwamba *MSD* inalalamikiwa na Halmashauri karibu zote na kwamba dawa zaidi ya mwaka mmoja na nusu hazikupelekwa kwa sababu hazipatikani. Je, walimpotosha au ilikuwaje na Waziri yuko tayari kuchunguza?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Naibu Spika, jibu langu nilivyosema ni kwamba moja ya matatizo ambayo yanasaababisha dawa zisipatikane katika Wilaya ni pamoja na kutoa ile *ordering* mapema ili *MSD* kuiwezesha kuweza kuwapelekea zile dawa husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ni kwamba ni kweli kwamba kuna *cealing* wanaopewa lakini vile lazima Wizara na yenyewe iwape *MSD* fedha ili iweze kununua dawa.

Kwa maana hiyo kama *MSD* kuna dawa ambazo hawajapeleka niko tayari kufanya uchunguzi na hata hivyo tuko katika mkakati wa kuhakikisha kwamba *MSD* inaboreka zaidi. Kwa hiyo, tutashirikiana wote pamoja ili tuweze kuona kwamba dawa zinapatikana kutokana na kiasi cha fedha zilizokuwepo lakini vile vile kwa utaratibu mzuri ambao nimeutaja.

MHE. HAROUB SAID MASOUD: Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina suala moja la nyongeza.

Kwa kuwa orodha inayohusika na madawa ambayo yanatakiwa na zahanati au Halmashauri inaandikwa na wao wenyewe huko huko. Na kwa kuwa leo hii katika vyombo vyta habari na magazeti nimesikia ikitamkwa kwamba kuna zahanati moja au Halmashauri imeomba dawa za malaria lakini matokeo yake wamepelekewa dawa za kuzuia mimba ambazo sizo walizozitaka. Mheshimiwa Naibu Waziri anasemaje jambo hilo?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Naibu Spika, siwezi kuamini kwamba mtu wa *MSD* aweze aka-*confuse* *ALU* kwa dawa za kuzuia uja uzito. Kwa sababu *ALU* kwa kweli jinsi ilivytengenezwa ni tofauti kabisa.

Lakini kama kweli hilo limetokea naomba Mheshimiwa Mbunge anipe hilo jina na sisi tutalifanyia uchunguzi na kama itakuwa ni kweli basi hatua za kisheria zitachukuliwa.

Na. 375

**Usambazaji wa Dawa na Vifaa Katika
Hospitali na Zahanati**

MHE. MGANA I. MSINDAI (K.n.y. MHE. LUCAS L. SELELII) aliuliza:-

Kwa kuwa, hospitali na zahanati hupatiwa dawa kutoka kwenye Idara ya Dawa (*MSD*); na kwa kuwa, dawa zinazosambazwa hazitoshelezi mahitaji ya hospitali zetu:-

- (a) Je, ni kwa nini msambazaji wa dawa ni mmoja tu?
- (b) Je, upo uwezekano wa kuongeza dawa katika *KITS* zinazopakiwa hasa kwa wagonjwa wa malaria?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, napenda kujibu maswali ya Mheshimiwa Lumambo Selelii (Mbunge wa Nzega) (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kwa sasa Bohari ya Madawa (*Medical Stores Department – MSD*) chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ndiyo msambazaji pekee wa dawa na vifaa katika vituo vya kutolea huduma za afya vya umma na Mashirika yasiyokuwa na Kiserikali ambayo yanatoa huduma bila faida. Bohari hiyo inayojitegemea kifedha na kiutawala, ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria Na. 13 ya Mwaka 1993.

Kwa hiyo, ni vigumu kuwepo kwa taasisi nyingine yenyе majukumu yanayofanana na yale ya Bohari hiyo ambayo itajihusisha na usambazaji wa dawa na vifaa katika vituo vya kutolea huduma za afya vya umma bila kubadilisha sheria iliyopo. Lakini pia napenda kurejea maelezo ya ziada kama nilivyojibu kwenye swalii Na. 374 la Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mbunge wa Bukombe kwamba Wizara imeandaa orodha ya dawa na vifaa tiba ambazo ni muhimu sana na ambazo hazitakiwi kukosekana katika vituo vya afya wakati wowote (*vital drugs*).

Orodha hii imekwishapelekwa kwenye Halmashauri zote nchini kama nilivyosema hapo mwanzo. Aidha, Wizara imetoa ruhusa kwa vituo vya afya kununua dawa hizi toka masoko binafsi kama nilivyokuwa nimeelezea katika lile swalii nililojibu hivi punde. Kwa sababu hii Serikali haioni sababu ya kupunguza fedha kutoka MSD na kuzipeleka Halmashauri kwa ununuzi huo.

b) Suala la upungufu wa dawa katika *Kits* limeshughulikiwa kwa kubadili utaratibu wa kuagiza dawa ambao sasa unazingatia mahitaji ya kila kituo. Kama

nilivyoeleza katika jibu la msingi Na. 374 la Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mbunge wa Bukombe kwamba Wizara iliendesha mafunzo ya “*Quantification and Forecasting*” kwa watumishi wa hospitali zote za Serikali nchini ili kuwawezesha kuainisha mahitaji yao ya dawa za mwaka mzima.

Mwezi Desemba 2007, mahitaji ya dawa za vituo vyote yalijumuishwa ili yatumike katika kuandaa bajeti ya Wizara ya mwaka wa fedha 2008/09. Hata hivyo dawa inayotumika kwa sasa ni ALU na ipo ya kutosha zaidi ya hapo vituo vinatakiwa kuagiza dawa kulingana na mahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili swali lilipokuwa limeulizwa ilikuwa ni mwaka 2006 na Mheshimiwa Mbunge alipokuwa ameuliza alizungumzia suala la *SP* na kwa sababu *SP* imetoka katika soko tukabertilisha mfumo ndiyo maana nimetaja *ALU* na nimezungumzia sasa hivi kwa sababu swali la msingi lilikuwa linazungumzia mambo ya *SP*.

MHE. MGANA I. MSINDAI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Kamati yetu ya *LAAC* kwa mwaka mzima tumefanya utafiti juu ya ununuvi wa dawa *MSD*. Na kwa kuwa tumegundua kwamba dawa nyingi hazipo. Halmashauri zetu zikipeleka mahitaji yao dawa zinakuwa hazipo. Kwa kuwa tulipendekeza asilimia 30 ya fedha zinazotengwa kwenda *MSD* zipelekwe Halmashauri ili wanapokosa dawa kule waweze kununua. Waziri anasemaje juu ya hilo?

Pili, kwa kuwa vifaa vinavyopatikana *MSD* vingi havina ubora kwa mfano kama vya kupimia *pressure* na vifaa vingine vingi Serikali iko tayari sasa kuleta vifaa vyenye ubora wa kuwafaa Watanzania?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza kuhusu kutenga asilimia 30 kupelekwa Halmashauri katika zile fedha ambazo zinapelekwa *MSD* hili pia tulizungumza wakati tukileta Bajeti yetu hapa Bungeni. Suala hili tumesema tunalifanyia kazi ili kuweza kuona kwamba hii asilimia 30 itakwenda kule na itatumika namna gani. Lakini vile vile tumesema kwamba kwa sasa hivi wakati tukisubiri uamuzi huo tuendelee kutumia zile fedha zilizoko kule za vyanzo vingine ili tuweze kununulia zile dawa ambazo zinakosekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili kuhusu ubora wa vifaa ambavyo Kamati ya *LAAC* imeona nataka niseme tu kwamba sisi kama Wizara tutakaa tena tuweze kuona lakini ninachofahamu mimi ni kwamba vifaa vinapokuja pale kunakuwa na ushindani. Lakini vile vile vifaa huwa vinakaguliwa na vinapokuja kama vinakuwa sio madhubuti vinapokwenda katika maeneo wanatakiwa walete ripoti mara moja ili yule ambaye ameleta vile vifaa aweze kuchukuliwa hatua. Lakini hata hivyo nasema tu kwamba tutalifanyia kazi vizuri ili tuweze kuona kwamba vyombo vinavyokuja hapa vinakuwa na ubora wa kutosheleza.

MHE. ELIETTA N. SWITI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Kwa kuwa vifaa visivyofaa vimekwishafika katika hospitali kwa mfano hizo BP *machine* zimepatikana katika Hospitali ya Mpanda. Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri anasemaje kuhusu hilo?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *BP machines* kwa kweli tatizo ni kwamba yaani kuna mambo mengi ambayo yanababisha kuona vile vifaa ni vibovu.

Kiutaratibu BP *machines* kwa wale wenzetu nchi zimeendelea unakuta BP *machine* moja anatumia mtu mmoja kwa wagonjwa wake au mgonjwa mmoja.

Lakini tatizo ambalo tunalipata sisi kwenye nchi ambazo zinazoendelea ni kwamba zile *Blood Pressure Machines* amba unaipeleka hata kama ikiwa na ubora wa kutosha lakini unakuta BP *machines* hiyo hiyo inatumika na wodi tatu, wengine inakuwa wodi ya kwanza inaazimwa inakwenda huko inakwenda *OPD*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hili ni tatizo mojawapo ambapo inasababisha hizi *BP Machine* ziharibike hata kama mpya kwa kweli lazima itaharibika. Nitakachokisema hapa ni kwamba zile ambazo ziko kule kama zilikuwa mbovu ilipochukuliwa ya kwanza ikaonekana kama ni mbovu zile nyingine basi zirudishwe.

Lakini kama zimetumika baada ya mwezi mmoja lakini hazikutumika vizuri zikaharibika hapa sasa itabidi tufanye *justification* tuone zimeharibika kwa sababu ya ubora au kwa sababu ya kutumiwa ziada kuliko ilivyo kawaida yake.

Na. 376

Mradi wa Maji wa Vijiji vya Ngasamo- Nguga na Malali

MHE. JACOB D. SHIBILITI (K.n.y. MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI)
aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali kupitia mradin wa TASAF ilifanikiwa kushirikisha wananchi kwa kiwango cha hali ya juu katika Wilaya ya Magu na kwamba mradi wa maji katika

vijiji vya Ngasamo, Nguga na Malili ulikuwa moja kati ya mradi iliyoibuliwa na wananchi kwa matumaini makubwa kwa ajili ya kuwapatia maji safi na salama:-

- (a) Je, mradi huo ulianza kujengwa lini na uligharimu kiasi gani cha fedha kutoka *TASAF* na nguvu za wananchi?
- (b) Je, kwanini mradi huo ambao umegharimu fedha nyingi na nguvu za wananchi hadi sasa haujakamilika?
- (c) Je, kuchelewa kukamilika kwa miradi kama hiyo hakuvunji ari na nguvu ya kujitolea na kuchangia shughuli za Maendeleo?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, Mbunge wa Jimbo la Busega, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mradi wa maji wa Ngasamo, Nguga na Malili ulianza kutekelezwa mwaka 2003 katika awamu ya kwanza ya Mfuko wa *TASAF* chini ya utaratibu wa Mpango wa Jamii yeye njaa lakini yeye uwezo wa kufanya kazi (*food insecure*). Gharama ya mradi ilikadiriwa kuwa shilingi 207,874,666/. Hata hivyo kutokana na upungufu wa fedha uliotokea katika kipindi hicho mradi ulipata shilingi 193,874,666/- ikiwa ni pungufu kwa takriban shilingi milioni 14. Utekelezaji wa mradi huu ulisimama mwezi Novemba 2004. Kazi zilizokuwa zimebaki ni pamoja na kufunga mabomba katika kijiji cha Ngasamo na kujenga kibanda cha mashine ya maji. Wananchi walilipwa ujira wa asilimia 40 ya gharama ya mradi kwa kazi walizofanya ikiwa ni thamani ya nguvu kazi iliyotumika.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kuchelewa kukamilika kwa mradi kumesababishwa na uhaba wa fedha Serikalini. Mwaka 2005 chini ya *TASAF II* mradi huu haukufuzu kupata fedha za kuendelea na utekelezaji. Hata hivyo kulingana na jinsi wananchi walivyoupa umuhimu mrdi huu, waliomba kuendelea nao chini ya *TASAF II* kuitia Mpango wa Jamii yeye Upungufu wa Huduma ya Jamii ambao unawataka wananchi wachangie sehemu ya gharama ya mradi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukamilisha mradi huu jamii ya Ngasamo kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Magu imewasilisha kwa *TASAF* maombi ya fedha kiasi cha shilingi milioni 37.5. Shilingi milioni 30 zimeombwa kutoka kwenye Bajeti ya mwaka 2008/2009 ya Halmashauri ya Wilaya ya Magu na shilingi milioni 7.5 zitatolewa na wananchi wenywewe. Ni matarajio yangu kuwa mradi huu utakamilika katika kipindi cha mwaka 2008/2009.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa kuchelewa kukamilika kwa mradi kunaweza kuvunja ari na nguvu ya kujitolea kuchangia shughuli za Maendeleo. Aidha, miundombinu ya mradi ambayo hajakamilika na rahisi kuharibika au kuibiwa. Kwa mfano, kuchelewa kukamilika kwa mradi huu kumechangia

kwenye wizi wa mabomba 18 ambayo yalikuwa tayari yamefungwa katika kijiji cha Ngasamo.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto iliyopo kwa Halmashauri ya Magu ni kwamba baada ya *TASAF I* kugharimia ujenzi wa mradi kwa zaidi ya asilimia 90 ilikuwa busara kutafuta fedha zilizobaki kutoka kwanye vyanzo vingine ili mradi ukamilike. Kwa uhakika huu ni mradi ambao ungeweza kuonyesha mafanikio haraka na kwa muda mfupi.

Aidha, wananchi hao kupitia uongozi wa vijiji vyao wanatakiwa kusimamia na kulinda mali za mradi wao ukizingatia pia kwamba nao wamechangia sana kazi yao.

MHE. JACOB D. SHIBILITI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mwili ya nyongeza. Kwa kuwa wananchi wa Ngasamo na Ngunga wamekuwa na matatizo makubwa sana ya maji kwa muda mrefu na ahadi za Serikali ni za mara kwa mara mnaahirisha bila utekelezaji. Ni lini hasa wananchi wa Ngasamo na Ngunga ikiwemo Malili nao watamaliziwa tatizo lao hilo?

La pili, kwa kuwa tatizo hilo ni sawa kabisa na tatizo lililoko Misungwi kwenye vijiji vya ng'ombe vijiji vya Ng'ombe na Buduto tatizo lake ni sawa na hilo hilo. Ni lini sasa *TASAF* itakamilisha matatizo hayo?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Ngasamo na Ngunga, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Shibili kwamba tumechukua hatua, tumeshatemebelea miradi hiyo na kazi sasa zinaendelea. Ninachoomba Mheshimiwa Mbunge atuamini kwamba hatuahirishi kukabidhi mradi kwa sababu tunakuwa hatupendi isipokuwa tunakuwa na matatizo ya utekelezaji, matatizo ya fedha na matatizo mengine ambayo yapo nje ya uwezo wetu.

Lakini nataka nimhakikishie kwamba miradi yote hii miwili aliyoisema Ngunga na Ngasamo tunatarajia kabisa kwamba ifikapo mwisho wa mwaka huu 2008 tutakuwa tumefanya kazi ambayo inaridhisha.

Kwa upande wa Ng'omba na Buduto kuhusu *TASAF* mimi nafikiri Mheshimiwa Mbunge ni vizuri ukaenda kuwasiliana na Halmashauri yako kwa sababu *TASAF* nayo ina utaratibu na ina vigezo ambavyo wanavitumia kabla hawajatoa pesa.

Sasa vigezo hivyo lazima Halmashauri ikidhi; kwa hiyo naomba mwendelee tena kuomba kule *TASAF* na m jitahidi kufuata vigezo vile ambavyo *TASAF* inatoa. Lakini pia napenda kusema kwamba kama fedha za *TASAF* hazitoshi basi tusikalili *TASAF* tu, tuangalie na vyanzo vingine ili tuweze kukamilisha miradi hii.

MHE. FELISTA A. BURA aliuliza:-

Kwa kuwa, Wilaya ya Kongwa inakabiliwa na matatizo sugu ya ukosefu wa maji safi na salama; na kwamba baadhi ya maeneo kama vile Kata ya Iduo kulikuwa na mradi wa maji kwa ufadhili wa Benki ya Dunia.

Je, ni lini wananchi wa Wilaya hiyo watapata maji safi na salama hasa kwenye vijiji vya Iduo na Hembahemba?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Felista Bura, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa kama ilivyo kwa sehemu nyingi nchini, Wilaya ya Kongwa inakabiliwa na matatizo ya ukosefu wa maji safi na salama. Kwa bahati nzuri mradi wa maji wa Kongwa na Vijiji vingine 9 ulipata fedha za mkopo wa Benki ya Dunia na kuanza utekelezaji halisi mwaka 2005. Hata hivyo utekelezaji wake uligubikwa na matatizo mengi yakiwemo ya uwezo mdogo wa mkandarasi, urasimu wa malipo kwa wakandarasi na ukosefu wa maji katika visima vilivyo chimbwa.

Terehe 21 Julai, 2008 nilikagua mradi huo wa maji na kutoa maelekezo kwa Halmashauri na wataalam kuhusu hatua za kuchukua ili kurekebisha hali mbaya utekelezaji hafifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ilivyo hivi sasa, hususan katika vijiji vya Iduo na Hembahemba ni kwamba ujenzi wa miundombinu ya maji katika mradi wa Iduo umekamilika na makandarasi atakabidhi mradi mwezi Septemba, 2008.

Aidha, kijiji cha Hembahemba kiliathiriwa na ukosefu wa maji katika visima vilivyo chimbwa awali. Kwa kuwa sasa maji yamepatikana katika kisima cha tatu, ujenzi wa miundombinu unaendelea na kazi inatarajiwaa kukamilika mwezi Novemba, 2008. Baada ya hapo wananchi wa Iduo na Hembahemba watapata maji safi na salama.

MHE. FELISTA A. BURA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri yenyeye matumaini kwa wananchi wa vijiji vya Iduo na Hembahemba naomba sasa kujua kwamba, kwa kuwa mradi wa Benki ya Dunia ilihusu vijiji tisa katika Wilaya ya Kongwa na ni vijiji viwili tu ambavyo vitapata maji mpaka kufikia mwezi Novemba mwaka huu 2008.

Je, vijiji kama Pandambili, Manungu, Kongwa Mjini, Kingarami, Kiteto ambao wako katika mradi huo wa *World Bank* watapata maji lini ili wanawake wanaotembea mchana kutwa wakihangaika kutafuta maji waweze kushiriki shughuli zingine za Maendeleo katika Wilaya Kongwa?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati nzuri Waziri ametembelea Kongwa na kuona hali ilivyo na baadaye ametuma

timu ya wataalam kutoka Wizarani kwenda kuangalia hali ilivyo katika Halmashauri ya Kongwa.

Tumetoa ushauri wa aina tatu, vijiji viwili nya Pandambili na Hembahemba kwamba pamoja na kwamba hapo awali vilikuwa havikujumuishwa katika mradi huu unaofadhiliwa na *World Bank* basi vijumuishwe kusudi kama kutakuwa na mabaki ya kazi pamoja na kwamba kazi zinaendelea basi visije vikaja vikabaki nyuma. Hii inahusu pia vijiji vingine alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge na bado nasisitiza kwamba Halmashauri ya Wilaya ndiyo hiyo hiyo iweze kuangalia vipaumbele katika vijiji hivi. Ni vipi na kuviingiza katika orodha ambayo wahandisi wataalam, washauri wetu wataangalia.

Lakini pia tumeshauri Halmashauri ya Wilaya inunue bomba 36 ambazo ziliibiwa kusudi kazi iweze kuendelea na mwisho kabisa tumewashauri kwamba Halmashauri ipitie kwa makini taarifa za usanifu wa miradi ambayo inafanywa na wahandisi hawa kabla ya kutoa ridhaa yao ili wahandisi hawa waangaliwe kama kuna uwezekano wa kuijumuisha katika *WSDP*.

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Katika miradi ya *World Bank*, miradi ambayo ilikuwa imeandalowi katika Jimbo la Kibakwe ya Kijiji cha Kisima, Chinyanghuku, Kidenge, Nafose, Wienzele Singonali. Katika vijiji hivi nilivyovitaja tulikuwa tunasubiri miradi hii ya *World Bank* lakini hadi mwaka jana tuliambiwa kwamba fedha ziko tayari isipokuwa taratibu zinamaliziwa ili miradi hii iweze kuanza. Wananchi wa maeneo haya wanasubiri wajue hasa ni lini miradi hii itaanza kutekelezwa.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, labda niseme tu kwamba nimkumbushe Mheshimiwa Simbachawene kwamba huko nyuma tulikuwa tuna matatizo ambayo ilimbidi Waziri ayatolee kauli hapa Bungeni. Kwamba kulikuwa na utaratibu na urasimu kidogo wa kupata fedha hizi za *World Bank*. Lakini kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri katika kauli yake ya Serikali *World Bank* tayari imesharahisisha kidogo kwa maana ya kwamba imelegeza yale masharti yake na tunesema Halmashauri 82 ikiwemo Halmashauri ya Kongwa na Mpwapwa. Zote hizi zinaruhusiwa kuendelea na mchakato.

Kwa hiyo, ili watu waweze kutekeleza mradi huo ni juu ya Halmashauri hizo kuhakikisha kwamba mchakato ule wa kuwapata wale washauri jukumu ambalo lipo ndani ya Halmashauri unakamilika. Kinachoendelea sasa hivi ni kuwapatia *request for proposal* na hatimaye tuwapate hawa washauri na kazi zianze.

Na. 378

Kupeleka Umeme Kwenye Kijiji cha Dindira

MHE. LAUS O. MHINA aliuliza:-

Kwa kuwa ni muda mrefu sasa tangu wananchi wa kijiji cha Dindira walipoahidiwa kufikishiwa umeme kijijini kwao; na kwa kuwa walishazifanya *wiring* nyumba zao kama jinsi *TANESCO* ilivyowashauri kufanya:-

Je, ni lini Serikali itapeleka huduma hii muhimu kijijini Dindira kwani wananchi wanasubiri kwa muda usiopungua miaka kumi sasa.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Laus Omar Mhina, Mbunge wa Korogwe Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kijiji cha Dindira kilichoko Kaskazini Magharibi mwa Wilaya ya Korogwe kipo umbali wa kilomita tano (5) kutoka mahali ilipo njia ya umeme ya msongo wa *KV 11* inayopeleka umeme kwenye kiwanda cha chai Dindira na mashamba ya mkonge ya Ambangulu.

Gharama za kufikisha umeme kijijini hapo ni shilingi milioni 200. Kazi zitakazofanyika ni ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa *KV 11* yenye urefu wa kilomita 5.0, ujenzi wa njia ndogo ya kusambaza umeme ya msongo wa *KV 0.4/0.23* yenye umbali wa kilomita moja pamoja na ununuzi wa ufungaji wa transifoma yenye ukubwa wa *KVA 50*.

Tathimini iliyofanyika katika kijiji cha Dindira ilibainisha kuwa wateja wa umeme katika kijiji cha Dindira ni takriban wananchi 150. Wateja wengine ni mashine za nafaka tatu, shule ya sekondori, shule ya msingi na zahanati.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huo utaanza kutekelezwa mara tu baada ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi kupatikana. Kama tulivyokwishaeleza hapa Bungeni, tayari tumewaaagiza Wakala wa Nishati Vijiji (*REA*) na *TANESCO* wakae na kuandaa mpango wa vipaumbele vya miradi ya upelekaji umeme vijijini. Hivyo tunamwomba Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa Jimbo lake wavute subira wakati tukiendelea na mikakati ya kusambaza umeme vijijini kikiwemo kijiji cha Dindira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo tumekuwa tunaeleza hapa Bungeni mara kwa mara, tunatambua na usumbufu unaoweza ukajitokeza pale ambapo matarajio ya kupatiwa umeme hayalingani na utekelezaji. Hali hii inawapata wananchi wa Dindira na Watanzania wengine wa maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Lakini ni mategemeo yetu kuwa kupitia Wakala wa Nishati Vijijini tutaendelea kusambaza umeme vijijini kutegemeana na upatikanaji wa fedha.

MHE. LAUS O. MHINA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwa kuwa mahitaji ni mengi. Je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari nimlelee orodha ya vijiji vyangu ambavyo vinakabiliwa na tatizo hili hususan Kituo cha Afya cha Rosemary kilichopo katika kijiji cha Makole katika Kata ya Mkalamo?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sioni tatizo la kupokea orodha kutoka kwa Mheshimiwa Mhina na nadhani tukishirikiana naye kutambua vijiji hivi atakuwa ametusaidia sana na mimi nitakapopata orodha hiyo tutaishinikiza *REA* na *TANESCO* kutekeleza kazi hii haraka iwezekanavyo.

MHE. MOHAMMED RISHED ABDALLAH: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi tena niulize swalii moja la nyongeza. Kwa kuwa upelekaji wa umeme vijijini kuna tatizo la gharama na hasa nguzo na uhaba wa nguzo.

Je, Serikali inaonaje sasa hivi kufanya utaratibu wa kujenga nguzo za nondo na *cement* ambazo zitakuwa ni nafuu na zitadumu muda mrefu ili kutatua matatizo ya umeme nchi nzima?

NAIBU SPIKA: Unataka miti ya kwetu isiwe na soko? Mheshimiwa Waziri majibu. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani nikubaliane naye kwamba katika mambo yanayoongeza gharama za kuunganisha umeme ni gharama kubwa sana zilizopanda za nguzo. Labda nikubali tu kwamba na nipokee pendekemo lake na niwakabidhi *TANESCO* wafanye tathimini hiyo ya kujua kama kweli tukitumia nguzo za nondo za *cement* zitakuwa zinaleta unafuu wa gharaa ukilinganisha na nguzo za miti ambazo tunaagiza nchi za nje. Lakini pia nimfahamishe Mheshimiwa Rished kwamba labda tuangalie tathimini ya kuzalisha nguzo hizi kama ilivyokuwa ikifanywa zamani kwa miti ya Mufindi. Kwa kusema kweli gharama zinapanda sana ni lazima tuliangalie hili ili wananchi wengi zaidi waweze kunufaika na huduma hii.

Na. 379

**Kung'olewa Nguzo za Umeme na Hasara
Iliyosababishwa na Zoezi Hilo**

MHE. JACOB D. SHIBILITI aliuliza:-

Kwa kuwa kulikuwa na nguzo zilizosimikwa kwenye maeneo ya Buhingo, Seeke, Nyamayinza, Mbalama, Isesa hadi Ihelele na kwamba zikang'olewa na kusababisha uharibifu mkubwa wa mazao ya wananchi:-

- (a) Je, nguzo zilizong'olewa zilichukuliwa na kupelekwa wapi?
- (b) Je, ni nini hatma ya vitu vilivyokuwepo kama vile nyaya, transfoma, vikombe na vitu mbalimbali ambavyo vimehifahidhiwa na wananchi?
- (c) Je, uharibifu uliojitokeza wa kuvuruga mazao kutaka miti bila kuwalipa wananchi utafidiwa na nani?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swal la Mheshimiwa Jacob Dalali Shibili, Mbunge wa Misungwi, naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mkandarasi wa mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kupeleka katika Miji ya Kahama na Shinyanga, kampuni ya *China Civil Engineering Construction Corporation (CCECC)* kutoka China pamoja na kazi zingine alikuwa na kazi ya kusanifu na kujenga njia ya umeme kwa ajili ya kuendesha mitambo ya kuchuja na kusukuma maji katika eneo la Ihelele. Mkandarasi alitoa kazi hiyo kwa *sub-contractor Future Century* ya Tanzania. Njia ya umeme ilijengwa kutoka Inonelwa kuitia Buhingo Seeke, Nyamayinza, Mbalama, Isesa hadi Ihelele.

Hata hivyo ujenzi wa njia hiyo ulifanyika bila idhini ya Mshauri Mwelekezi na mmiliki (Wizara ya Maji na Umwagiliaji), hivyo Mkandarasi hakulipwa kwa kazi hiyo. Vilevile ilibainika kuwa umeme wa njia hiyo ulikuwa hauwezi kukidhi mahitaji ya mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo tulitangazwa zabuni Na. 9/2005/2006 ya kupanua *substation* ya Bulyanhulu, kujenga njia ya umeme ya kilomita 28 kutoka Ikangala hadi Nyamtukuza na kuweka *submarine cable* yenye urefu wa kilomita 1.2 kuvusha umeme hadi Ihelele na kampuni ya *National Contracting Company Limited* ya Saudia, Arabia ikapewa kazi hiyo.

Aidha, kampuni ya *China Civil Engineering Construction Corporation* iliendelea na ujenzi wa njia ya umeme ya umbali wa kilomita 25 kutoka Bulyanhulu hadi Ikangala pamoja na kujenga transfoma za upande wa Ihelele.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, napenda sasa kujibu swal la Mheshimiwa Jacob Dalali Shibili, Mbunge wa Misungwi, lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Naibu Spika, nguzo zilizong'olewa zilichukuliwa na kampuni ya *China Civil Engineering Construction Corporation* kwa sababu ni mali yake na zilipelekwa kuhifadhiwa kwenye ghala la kampuni hiyo.
- (b) Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna wananchi wana nyaya, transfomavikombe na vitu mbalimbali alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge itakuwa ni jambo jema iwapo watasiliana na kampuni ya *China Civil Engineering Construction Corporation* ambaye ndiye mmiliki wa vifaa hivyo.
- (c) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kampuni ya *China Civil Engineering Construction Corporation* ndiyo iliyosabibisha uharibifu wa mali ya wananchi wkti wa kung'oa nguzo hizo, itabidi wananchi walioathirika watasiliane na kampuni ya *China Civil Engineering*

Construction Corporation kwa ajili ya kulipwa fidia. Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Maji na Umwagiliaji tunaendelea kufanya mawasiliano na Mkandarasi ili kufahamu ukweli wa suala lenyewe na tutakuwa tunampatia taarifa Mheshimiwa Mbunge kadri tutakavyokuwa tunapiga hatua katika suala hili.

MHE. JACOB D. SHIBILITI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza nimshukuru Mhesimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake ambayo kwa kweli ameyajibu kwa ufasaha sana. Kwa kuwa wananchi wa Buhingo, Seke, Nyamainza, Mbalama, Isesa hadi Ihelele walijiandaa kikamilifu sana. Lakini kutokana na juhudzi zake Mheshimiwa Naibu Waziri katika Bajeti yao walivitaja vijiji vya Seke na Nyamahinza kwamba vitahusika katika MCC napenda sasa Mheshimiwa Waziri anihakikishie ni pamoja na vijiji vingine alivyovitaja vitapatiwa huduma hiyo na vitapewa kipaumbele katika MCC?

La pili, kwa kuwa Naibu Waziri katika majibu yake ameeleza kwamba atashirikiana na Wizara ya Maji na Umwagiliaji ili kuwasiliana na huyo Mkandarasi na kwa kuwa nategemea wakati wowote kuwa nje ya nchi na yeye na Mheshimiwa Waziri atakuwa ni bora zaidi akifika kwenye eneo la Seke na kufanya mukutano na wananchi kwa kuwa sitakuwepo yupo Mheshimiwa Maria Hewa na Mheshimiwa Esther Nyawazwa atakubali kuambata nao ili angalau shughuli hiyo iweze kufanikiwa? (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimwambie kwamba kwa kutambua kwamba mradi ule ambao ultakiwa upitie kwenye vijiji vile ulikuwa umeshindikana mradi wa MCC umetambua vijiji vya Seke, Nyamahiza na Fela na kama tulivyoleza wakati wa Bajeti ni kwamba fikra iliyopo ni kwamba tutakopofika kwenye vijiji hivyo vitatu itatupa uwezo wa kuendelea baadaye kwa nguvu zetu wenyewe kufika kwenye vijiji vingine.

Kwa hiyo Naomba nimwambie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Misungi kwamba nimelipokea na kama tulivyofanya kwa Jimbo la Nyang'wale la Mheshimiwa Msalika mwezi uliopita tutafanya utafiti wa kujua tunaendeleaje kwenye miradi mingine kwa nguvu zetu wenyewe pale ambapo miradi ya MCC inapoishia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwa unyenyekevu na heshima kubwa nakubali kuongozana na Mheshimiwa Esther Nyawazwa na Mheshimiwa Mama Hewa kwenda huko kwenye ziara hiyo na nitafurahi sana tena sana.

Na. 381

Matatizo ya Ujambazi Chuo cha Mwalimu Nyerere Kivukoni

MHE. MZEE NGWALI ZUBER aliuliza:-

Kwa kuwa wimbi la ujambazi na uporaji wa vitu vya wanafunzi wanaosoma katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere Kivukoni limeongezeka:-

- (a) Je, Serikali haioni kama ni vema sasa Chuo kikawekewa uzio?
- (b) Je, Serikali haioni kuwa ni bora raia wakazuiwa kuingia kiholela Chuoni hapo?
- (c) Je, ni kampuni gani zinalinda Chuoni hapo?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swal la Mheshimiwa Mzee Ngwali Zuber, Mbunge wa Mkwajuni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kinakabiliwa na tatizo la uporaji mdogo mdogo wa vitu kutoka kwa wanachuo wanaosoma katika Chuo hicho kutokana na kutokuwepo na uzio kwenye eneo la Chuo. Uongozi wa Chuo umechukua hatua zifuatazo katika kukabiliana na changamoto hiyo:-

- (i) Michoro (*Architectural Drawings*) ya uzio kuzunguka eneo la Chuo imeandaliwa.
- (ii) Mawasiliano na Manispaa ya Temeke kuomba kibali cha ujenzi wa uzio kwenye eneo la chuo yamefanywa.
- (iii) Baada ya kupata kibali cha Manispaa, kazi ya ujenzi wa uzio itaanza.
- (b) Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada za kudhibiti raia kuingia kiholela chuoni zinakwamishwa na ukosefu wa uzio. Ujenzi wa uzio ukikamilika, tatizo la kuingia kiholela chuoni litapungua kama si kuisha kabisa.
- (c) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivi sasa Chuo kinatumia walini ambao wameajiriwa na Chuo. Walini hao wanafanya doria katika eneo la Chuo hususan eneo linalolekea Feri kwa lengo la kudhibiti vitendo vya uhalifu. Baada ya kukamilika kwa ujenzi wa uzio, Chuo kitatumia kampuni binafsi kwa ajili ya ulinzi wa mali za Chuo na jamii inayoishi ndani ya Chuo.

MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Hicho kibali kitapatikana lini na je, imetengwa fedha ya kujenga uzio huo?

La pili kwa kuwa walini waliopo Chuoni pale ni wachache sana na wakati mwagine unapotokea uhalifu Jeshi la Wananchi wa Tanzania pale Kigamboni ndiyo wanashughulika na masuala hayo. Je, hamuoni kampuni hii kuiajiri hivi sasa na kampuni ya doria kwa hivi sasa?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA): Mheshimiwa Naibu Spika, hicho kibali kimeshapatikana tayari na ujenzi utaanza hivi karibuni na fedha imeshatengwa kwa ajili ya kazi hiyo.

Kuhusu la pili, walinzi waliopo si wachache ni walinzi wanane na wanapeana zamu ya kulinda ingawa kama wanajeshi wanasaidia wanatusaidia kwa ajili ya matakwa lakini tumesema tutapojenga uzio ndiyo tunaweza kuajiri walinzi wa kampuni.

Sasa hivi kwa sababu eneo lipo wazi walinzi wa kampuni mara nyingi hawataki kulinda sehemu ambazo ziko wazi kwa sababu inakuwa kubwa sana. Kwa hiyo, tutawaajiri baada ya kujenga uzio.

Na. 381

Hali ya Shule ya Wavulana Mwenge

MHE. DIANA M. CHILOLO aliuliza:-

Kwa kuwa Shule ya Sekondari ya Wavulana ya Mwenge yenyewe Kidato cha Nne na Sita Mjini Singida inakabiliwa na matatizo mengi sana kama upungufu wa walimu, ukosefu wa vifaa vya maabara na kemikali zake, vitabu, kompyuta na utandawazi pamoja na uzio kwa ajili ya ulinzi wa mali za shule, walimu na wanafunzi. Je, ni lini Serikali itaondoa kero hizo ili kuleta ufanisi wa utoaji na upokeaji wa taaluma shulenii hapo?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Diana M. Chilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kuwa Shule ya Sekondari ya Wavulana ya Mwenge yenyewe Kidato cha Nne na Sita Mjini Singida pamoja na shule nyingine nyingi nchini zinakabiliwa na matatizo mengi kama upungufu wa walimu, ukosefu wa vifaa vya maabara na kemikali zake, vitabu, kompyuta na utandawazi pamoja na uzio kwa ajili ya ulinzi wa mali za shule, walimu na wanafunzi. Katika kukabiliana na tatizo hili, Wizara yangu itaendelea kuajiri na kupanga walimu katika Shule ya Sekondari ya Wavulana ya Mwenge na shule nyingine ambapo wahitimu 12,692 waliomaliza mafunzo ya ualimu mwezi Julai, 2008 katika Vyuo vya Ualimu na Vyuo Vikuu nchini watapangwa. Kuhusu ukosefu wa vifaa vya maabara na kemikali zake, vitabu, kompyuta na utandawazi, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa kuititia Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES), Wizara imekuwa ikituma fedha shulenii kama ruzuku ya uendeshaji kwa ajili kununulia vifaa vya kujifunzia na kufundishia. Aidha, sehemu ya ada wanayotoa wanafunzi inatumika kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa uzio kwenye Shule ya Sekondari ya Mwenge na shule nyingine zenyenye hosteli ni jukumu la shule husika kuitia Kamati/Bodi za Shule na Wadau wengine wa Elimu. Hata hivyo, Wizara itaendelea kuchangia kadri hali ya fedha itakavyoruhusu. (*Makof*)

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, ili niweze kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

(a) Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri anatambua wazi wahitimu tayari wameishahitimu na kupangiwa katika shule mbalimbali za sekondari, je, kuitia jukwaa hili, haoni kwamba ilikuwa ni wakati wake mzuri kutamka idadi kamili ya Walimu ambao watapangiwa shule ya Mwenge ili kuwaondolea kilio wanafunzi na Walimu ambao wanakabiliwa na tatizo kubwa la upungufu wa Walimu?

(b) Kwa kuwa shule ya sekondari Mwenge, ni shule kongwe na iko katikati ya Mji wa Singida na kwa kuwa shule hiyo inakabiliwa na tatizo sugu la wizi wa mchana na usiku pamoja na kwamba tatizo la kujenga uzio ni la Bodi, je, Mheshimiwa Naibu Waziri, yuko tayari kuandamana na mimi pamoja na Mbunge wa Jimbo, kwenda kuona hali halisi ya shule hiyo ambavyo inakabiliwa na tatizo sugu la kukosa *fence* kiasi kwamba inatishia hali ya ulinzi na usalama wa shule hiyo ili aweze kuona namna ya kusaidia?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kuhusiana na idadi ya Walimu watakaopangwa, kwa kuwa hao Walimu ndio wamemaliza na upangaji unaendelea, hapa siwezi kutamka idadi itakayopangwa. Lakini, naomba tu Mkuu wa Shule awasiliane na Wizara au na Mkoa (*REO*), ili aweze kutoa maombi yake ya Walimu anaowahitaji kwa kila somo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, tatizo sugu la uzio na kwamba kama ningependa kwenda Mwenge kuangalia hali halisi, kwanza, nimweleze Mheshimiwa Diana kwamba, shule ya Mwenge ni shule yangu, nimefundisha pale miaka miwili, miaka ya 1980, kwa hiyo ningependa kurudi Mwenge. Lakini pamoja na hiyo, mimi nawahakikishia kwamba kwa kusaidiana na Bodi ya Shule, mimi ningeomba suala hili la uzio lifanyiwe kazi pale pale Mkoani na tunesema Wizara tutachangia pale ambapo tutaweza. Lakini nitapenda kweli kwenda Mwenge kwa mara nyingine kujiona hiyo shule jinsi ilivyo kwa sasa hivi. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante! Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umepita na maswali tumeyamaliza, Tunaendelea na shughuli nyingine.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza kabisa, tunao wageni. Wageni walioko asubuhi Bungeni hapa, kwanza ni wageni wa Mheshimiwa Ludovick Mwananzila na Wabunge wote wa Mkoa wa Rukwa. Wageni wenye kazi pale na kusaidiana na Bodi ya Shule, mimi ningeomba suala hili la uzio lifanyiwe kazi pale pale Mkoani na tunesema Wizara tutachangia pale ambapo tutaweza. Lakini nitapenda kweli kwenda Mwenge kwa mara nyingine kujiona hiyo shule jinsi ilivyo kwa sasa hivi. (*Makof*)

Sichona, Makamu Mwenyekiti, yupo, Mheshimiwa Musa Sungiza, Mkurugenzi na Madiwani wengine wote naomba wasimame. Karibuni sana, hii ni namna ya kujifunza shughuli za Bunge, karibuni sana. (*Makofi*)

Tuna wageni wa Mheshimiwa Al-Shymaa Kwegyir, Mheshimiwa Margreth Mkanga na Mheshimiwa Zuleikha Haji. Hawa wageni wanatoka Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA) Makao Makuu ambao ni Ndugu Felician Mkude, Katibu Mkuu, Ndugu Amon A. Mpanju, Makamu Mwenyekiti, Christopher Andendekisye, Mkurugenzi, Ndugu Abdulrahman Lugone, Mweka Hazina na Ndugu Mary Kalumuna, Mjumbe wa Bodi. Mheshimiwa Kalumuna alikuwa Mbunge mwenzetu katika Bunge hili kwa kipindi kirefu sana na alikuwa mchangiaji hodari sana katika mambo haya, karibu tena katika Bunge lako. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa tuna wageni wa Mheshimiwa Peter Serukamba, yupo Ndugu Nashoni Bioganguze, Meya wa Manispaa ya Kigoma Ujiji na Ndugu Shabani Mambo, Naibu Meya wa Manispaa ya Kigoma, nadhani watakuwepo mahali humu humu ndani. (*Makofi*)

Halafu tuna Maafisa sita kutoka Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora wakiambatana na Viongozi wa Msafara ambao ni Ndugu *Justice Amiri R. Manento*, Mwenyekiti, Mheshimiwa Jaji yuko wapi? Halafu yuko na Ndugu Mahafoudha A. Hamid, Makamu Mwenyekiti. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao Wabunge wawili kutoka Bunge la Msumbiji, ni Wageni wetu kutoka Bunge la Msumbiji ambao ni Mheshimiwa Maria Angelina Enoque, Kiongozi wa msafara. Karibu sana Maria. (*Makofi*)

Kuna Mheshimiwa Moreira Vasco, Mbunge, Karibu sana Mheshimiwa Mbunge. Hawa wanajua Kiswahili! Tunaye Dr. Emilio Machado, Afisa Mkuu, halafu tunaye Dr. Filomena Grachane, Mwanasheria Msaidizi na Ndugu Angelo De Jesus Magaia, Mkalimani. Nategemea unawaeleza vizuri mambo yanayoendelea humu! Ahsanteni sana, Karibuni sana, nadhani tutaonana mchana. (*Makofi*)

Halafu, tuna mgeni wa Mheshimiwa George Simbachawene, Mwalimu Veran Kigosi, Mwalimu wa Shule ya Msingi Pwaga, Kibakwe ambaye ni baba mzazi wa mtoto aliyekuwa wa kwanza Kitaifa kwa shule za msingi kwa mwaka jana. Baba mzazi yuko wapi? Tumefurahi sana kukuona na tunakushukuru na kukupongeza kwa malezi mazuri kwa mtoto huyo. (*Makofi*)

Halafu tuna wageni wa Mheshimiwa Celina Kombani, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI ambao ni Ndugu Tuhuma Lihepa, Katibu wa U.W.T, Wilaya ya Ulanga, Mheshimiwa Christina Fuluwa, Diwani Viti Maalum Kata ya Mahenge Mjini na Mheshimiwa Amina Seif Mgelwa, Diwani wa Viti Maalum, Kata ya Lupilo. Ahsanteni sana, tunashukuru kwa kumsaidia Mheshimiwa Waziri kwa kazi zake huko maana ziko nydingi. (*Makofi*)

Tuna wanafunzi 50 kutoka Shule ya Msingi Kizota na Walimu wao naomba wasimame. Ahsanteni sana, karibuni tena, ninyi wa Dodoma, hili ni Bunge lenu wakati wowote. (*Makofi*)

Kuna wanafunzi 40 kutoka Shule ya Sekondari Nkuhungu. Wako hapo wasimame na Walimu wao kama wapo. Karibuni sana, hata ninyi Bunge liko katika eneo lenu, mnaweza kuja wakati wowote. (*Makofi*)

Tuna wanafunzi wengine 50 kutoka Shule ya Msingi ya Mtakatifu Margreth na wenyewe wasimame na Walimu wao. Karibuni sana, mmepependeza sana katika sare yenu. Karibuni sana! (*Makofi*)

Tuna wageni wengine, hawa wageni wa Mheshimiwa Issa Khatibu, hakupeleka orodha kule. Hawa ni wageni naambiwa wa Mheshimiwa Abdisalaam Khatib pamoja na Mheshimiwa Dr. Ngasongwa, wageni hao ni Mr. Ivo Poparadowisky, *Director General* wa *Abbas IPS Management Company Limited* ya *Czechoslovakia Republic*. Amefuatana na Mr. Anold Mtuli na Mr. Gaston Francis, hawa ni Watanzania. *You are welcome Mr. Ivo and I hope you have a nice time here.* Karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hivyo, nina matangazo ya shughuli za leo, maana yake kazi za Kamati. Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Wilson Masilingi, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo tarehe 12, saa 5.00 asubuhi, watakutana katika chumba namba 231, ghorofa ya pili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Masilingi, karibu sana, ulikuwa haupo kutokana na msiba ule, nashukuru mmezika salama.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali, Mheshimiwa John M. Cheyo, anaomba wajumbe wake wakutane leo tarehe 12 saa 5.00 asubuhi hii katika chumba namba 219. Saa 5.00, chumba namba 219, Kamati ya PAC.

Halafu Mwenyekiti wa Kamati Ndogo ya Uongozi na Tume, Mheshimiwa George Lubeleje, anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati hiyo kwamba leo tarehe 12 wakutane katika Ukumbi wa Spika uliopo katika Jengo la Utawala, saa 5.00 asubuhi wanafanya kazi maalum.

Waheshimiwa Wabunge, halafu jana tulisahau kutangaza matokeo ya mpira wa wiki iliyopita. Siyo mpira tu, yaani na michezo mingine. Timu zetu za *Football, Netball* zimecheza michezo miwili *weekend*. Matokeo yalikuwa hivi:-

Mchezo wa tarehe 8, Siku ya Wakulima, Timu ya Bunge ilicheza na *PPF Combined*. Sasa Bunge ilishinda kwa goli moja na *PPF* sifuri. Halafu Timu ya *Netball* nayo ilicheza na *PPF Combined*, Timu ya Bunge ilipata magoli 34 na kuwashinda wale wa *PPF* kwa magoli manne. Kwa hiyo, 34 kwa 4. (*Makofi*)

Katika mchezo uliochezwa tarehe 09/08/2008, Timu ya Bunge walitoka droo, moja kwa moja na Timu ya *NMB*. Halafu kulikuwa na kuvuta kamba; Bunge *Sports v/s PPF*, Bunge alikuwa mshindi.

MJUMBE FULANI: Alishinda nini?

NAIBU SPIKA: Mimi sijui alishinda nini. (*Kicheko*)

Halafu Bunge *Sports Club v/s NMB* kamba hiyo, Bunge pia lilishinda. Kwa hiyo, naomba niwapongeze wenzetu wote waliofanya vitu vyao pale, nadhani Mheshimiwa Spika anawalisha vizuri ndio maana mnashinda kila siku. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine rasmi, ninapenda kusema kwamba toka wiki iliyopita Mheshimiwa Spika hakuwepo, niliwaitangazia kwamba alikwenda kuhudhuria Mkutano wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola Kuala Lumpur, Malaysia. Mkutano huo umekwisha na Mheshimiwa Spika sasa amechaguliwa kuwa Mwenyekiti wa *Congress ya Commonwealth* Duniani. Alipoondoka alikuwa Makamu Mwenyekiti, sasa wamem-*confirm* kama Mwenyekiti ama tunasema Rais wa ule Mkutano utakaofanyika mwaka kesho Tanzania. Kwa hiyo kuanzia sasa ni Rais na ataendelea kufanya hiyo kazi mpaka Mkutano utakapofanyika mwaka kesho mwezi wa Tisa. Bahati nzuri, leo jioni atakuwepo hapa na pengine kesho atatuelezea zaidi kuhusu mambo yalivyotokea kule. Kwa hiyo, ndio maana unakuta wajumbe wenzetu nao hawajarudi. Lakini wamemaliza vizuri, Mkutano ulikuwa mzuri.

Anaeleza kwamba, kawaida ya ile Mikutano, wale wanaokuwa wenyeji wa Mkutano mwaka mwingine lazima uonyeshe nchi yako ikoje, upeleke na *CD*, basi nasikia watu wametamani sana, wametamani kuja haraka kabisa katika Mkutano huo na ni sehemu ya utalii pia, maana wanakuja wengi tu, wanakuwa zaidi ya elfu moja na zaidi. Kwa hiyo, nadhani tutajiandaa vizuri na Wizara zingine zitasaidia kuandaa Mkutano ule kusudi uwe kweli Mkutano wa Kimataifa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Spika ni Rais wa ule Mkutano wa *Commonwealth*. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

KAULI ZA MAWAZIRI

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na wewe na Waheshimiwa Wabunge wote, kumpongeza Mheshimiwa Spika kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuwa Rais wa Baraza hilo maarufu ulilolitangaza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kupitia Mkurugenzi wa Uvuvi, ilitoa Waraka wenye kumbukumbu Na. KA/594/01/87 wa tarehe 13 Mei, 2008 uliopiga marufuku uvuvi wa kutumia zana na vifaa haribifu za nyavu aina za juya au kokoro, mtando, *ring net* na matumizi ya mitungi ya oksijeni, miwani na viatu vyaa kupiga mbizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waraka huo ulitolewa kulingana na kifungu Na. 4(3) cha Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya mwaka 2003 na Kanuni Na. 14, 15 na 17(2)(a) za Kanuni za Uvuvi za mwaka 2005 ambazo zinampa Mkurugenzi wa Uvuvi mamlaka ya kutoa nyaraka na maelekezo yatakayoimarisha utekelezaji wa Sheria hii ikiwa ni pamoja na kuzuia, kutoa au kufuta leseni ya uvuvi pale ambapo kiwango cha uvunaji wa rasilimali ya uvuvi kinahatarisha uendelevu wa rasilimali hiyo. Kwa mantiki hii, Waraka huu haukukiuka/kuvunja Sheria za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waraka huu unawiana na Kanuni za Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa kuhusu Uvuvi wa Kuwajibika (*FAO Code of Conduct for Responsible Fisheries, 1995*), Kifungu Na. 8.4.2 pamoja na 8.5.1 ambapo Tanzania ni mwanachama kuhusu Mataifa kuzuia matumizi ya mbinu na zana haribifu katika uvuvi.

Aidha, Waraka wa Mkurugenzi, unaendana na makubaliano yaliyosainiwa na Wakuu wa nchi za *SADC*, tarehe 14/08/2001, Mjini Blantyre – Malawi ambapo Rais wa Tanzania alisaini makubaliano hayo kuhusu kutumia mbinu mbalimbali katika kupambana na uvuvi haramu kwa lengo la kulinda rasilimali zilizoko kwenye maji kwa kutumia Sheria za Uvuvi.

Aidha, katika Ibara ya 14(5) ya makubaliano hayo yaliyosainiwa na Wakuu wa nchi, yamesisitiza kutambua maazimio yaliyopitishwa na *SADC* kwa ajili ya kulinda rasilimali zilizo ndani ya maji. Maazimio hayo ni *Arusha Declaration, Seychelles Declaration, Cape Town Declaration* na *Maputo Declaration*.

Halikadhalika, suala la Uvuvi haramu limewekewa Azimio na Mawaziri wa *SADC* wenyе dhamana na Sekta ya Uvuvi tarehe 4/7/2008 huko Windhoek, Namibia. Serikali zetu mbili yaani Tanzania Bara na Tanzania Visiwani, zilishiriki na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikasaini mazimio hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa nchi zilizo ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC*), suala la uvuvi haramu, linasimamiwa chini ya mradi wa *Lake Victoria Fisheries Organisation* wenyе Makao yake Uganda na kwa sasa Tanzania ndio Mwenyekiti. Pia, Waraka huo unaendana na Sheria ya Kulinda na Kuhifadhi Maeneo Tengefu Na. 29 ya mwaka 1994.

Mheshimiwa Naibu Spika, chimbuko la Waraka wa Mkurugenzi wa Uvuvi ni kwamba; mwaka 2007/2008, Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi (*TAFIRI*) iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria Na. 6 ya mwaka 1980, ilifanya utafiti wa uwingi wa samaki na mazingira kwenye bahari yetu na maziwa na kubaini kupungua kwa rasilimali ya uvuvi na uharibifu wa mazingira kwa kiasi kikubwa. Samaki aina ya sangara, samaki wote wa mapezi, kambakoche, ngisi, pweza, majongoo bahari, kambamiti na kadhalika wamepungua kutohana na kutumia zana na mbinu haribifu za uvuvi. Kwa mfano, kambamiti wamepungua kutoka tani 1,320.1 mwaka 2003 hadi chini ya tani 202.5 mwaka 2007. Katika ziwa Victoria, samaki aina ya sangara, wamepungua kutoka tani 750,000 mwaka 2005 hadi tani 375,000 mwezi Februari 2008.

Aidha, jongoo bahari wametowe ka kabisa ukanda wa bahari wa nchi za Kenya, Msambiji, Comoro na kadhalika. Hivyo, Kenya na Tanzania Visiwani wamepiga marufuku kutumia nyavy za mtando (Juya la kojani au Juya la kusini). Tanzania Visiwani imefanya hivyo kwa kutumia Sheria ya Uvuvi Na. 8 ya mwaka 1988 pamoja na mabadiliko yake ya 1998.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nilipowasilisha hotuba yangu ya bajeti ya mwaka 2008/2009, katika Bunge lako Tukufu, Waheshimiwa Wabunge wengi walionyesha kukerwa na uvuvi haramu unaofanywa katika bahari, napenda nirudie sehemu hii, Waheshimiwa Wabunge wengi walionyesha kukerwa na uvuvi haramu unaofanywa katika bahari, maziwa na mito yetu hapa Tanzania. Aidha, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walilalamikia Waraka uliotolewa na Mkurugenzi wa Uvuvi kwamba maelekezo yake ni ya jumla mno na hivyo kukataza hata shughuli halali za uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimetafakari hoja za Waheshimiwa Wabunge na kufuatana na mamlaka niliyopewa kupitia Kanuni ya 101 ya Kanuni za Uvuvi za mwaka 2005 zinazotokana na Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya mwaka 2003, naomba kutoa ufanuzi kuhusu Waraka huo kama ifuatavyo:-

(a) Nyavy za Kuzungusha (*Ring Net*). Waraka ulipiga marufuku uvuvi wa kutumia *Ring Net*. Nimepitia maelezo ya Waheshimiwa Wabunge pia nimepitia Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya mwaka 2003 na kubaini Kanuni 20(a) – (b) inawapa fursa walalamikaji kukata rufaa kwa Waziri mwenye dhamana ya Uvuvi. Hoja za Waheshimiwa Wabunge zilizotolewa ili kutetea wavuvi wakati wa majadiliano ya hotuba yangu ya Bajeti 2008/2009, nimezichukulia kama rufaa.

Hivyo, kwa mujibu wa Kanuni Na. 101 ya Kanuni za Uvuvi za mwaka 2005, nimeamua kuruhusu uvuvi wa kutumia nyavy za *Ring Net* katika maji marefu. Kwenye maji mafupi ambako nyavy zinagusa sakafu ya bahari au ziwa, nyavy hizi haziruhusiwi. Hivyo, matumizi ya *Ring net* kwenye maeneo ya matumbawe, miamba na katika maji yenye kina kifupi yamepigwa marufuku. Napenda nirudie sehemu hii, hivyo, matumizi ya *Ring Net* kwenye maeneo ya matumbawe, miamba na katika maji yenye kina kifupi, yamepigwa marufuku. (*Makofi*)

(b) Uvuvi wa samaki aina ya Pweza. Samaki aina ya Pweza amba pia wamepungua, wanavuliwa na wavuvi wadogo wadogo kwenye maji ya kina kifupi kwa njia mbalimbali, mojawapo ni hii ya kutumia mitego aina ya vikapu (*traps*) na chambo cha samaki aina ya kambakoche kumfanya pweza atoke kwenye pango. Uvuvi wa aina hii kwa wavuvi wadogo wadogo haujazuiliwa. Hivyo, wavuvi wa pweza waendelee kuvua kwa kuzingatia Sheria. (*Makofi*)

(c) Matumizi ya nyavu aina ya *gillnets* (Makila). Nyavu aina ya *gillnets* au makila zinazotumiwa kuvua samaki aina ya kambakoche hazijapigwa marufuku. Hivyo wavuvi waendelee kutumia nyavu hizi kwa kuzingatia Sheria. (*Makofi*)

(d) Uvuvi wa samaki aina ya Furu na dagaa ambao Mheshimiwa Ernest Mabina alisema nchuma boi na kadhalika ambao wameanza kuongezeka katika maziwa, unaruhusiwa ili mradi wavuvi watumie zana zinazokubalika.

Aidha, Uvuvi wa Samaki aina mbalimbali unaowahusisha wavuvi wadogo wadogo kwa ajili ya kupata chakula na kufanya biashara katika bahari, maziwa, mabwawa na mito yetu, unaruhusiwa ili mradi wazingatie Sheria za Uvuvi. (*Makofi*)

(e) Uvuvi wa kutumia baruti, milipuko, sumu na kadhalika umepigwa marufuku katika bahari, maziwa, mabwawa na mito yetu yote. (*Makofi*)

(f) Matumizi ya gesi ya oksijeni, miwani na viatu vya kuogelea. Waraka wa Mkurugenzi, ulipiga marufuku matumizi ya gesi ya oksijeni, miwani na viatu. Hata hivyo, kwa mamlaka niliyopewa kuititia Kanuni Na. 101 ya Kanuni za Uvuvi za mwaka 2005, nimeamua ifuatavyo:-

- Wavuvi wenge leseni za kuvua samaki hai na wa mapambo, nimewaruhusu kutumia vifaa hivi. (*Makofi*)

- Wavuvi wanapovitumia vifaa hivi kwa ajili ya ama usalama wao, kutoa nyavu zinapojizonga kwenye *propeller* za injini za boti au nyavu zinaponasa kwenye magogo na kadhalika, wanaruhusiwa pia kutumia mitungi ya gesi ya oksijeni, miwani na viatu vya kuogelea. (*Makofi*)

- Waogeleaji, burudani, utalii kwenye matumbawe pamoja na utafiti, vifaa hivi vinaruhusiwa kutumika.

Hata hivyo, uvuvi wa kutumia baruti, sumu au zana zingine zote haribifu, umepigwa marufuku kadri Waraka wa Mkurugenzi wa Uvuvi unavyoelekeza. Nasisitiza wavuvi wanaotumia baruti, milipuko, sumu na mabomu ambao hukusanya samaki katika maeneo ya matumbawe wakitumia mitungi ya gesi ya oksijeni, miwani na viatu vya kuogelea, umepigwa marufuku/hawaruhusiwi. Aidha, ikibainika matumizi niliyoyataja hapo juu yanakiukwa, mhusika atashughulikiwa kwa mujibu wa Sheria.

(g) Uvuvi wa kukokota nyavu kwa Meli (*Bottom Trawling*). Uvuvi wa kukokota nyavu kwa Meli (*Bottom Trawling*), uliokuwa ukifanywa na wavuvi wakubwa wenge meli 10 zilizopewa leseni ya kuvua kambamiti na Wizara yangu, umefungwa, kwa maana nyingine umepigwa marufuku. Hata hivyo, wavuvi wadogo wadogo wanaovua kambamiti wanaruhusiwa kuendelea kuvua samaki hao kwa kutumia zana zinazokubalika kwa mujibu wa Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya mwaka 2003 pamoja na Kanuni zake za mwaka 2005. (*Makofi*)

(h) Leseni za uvuvi wa *EEZ* (*Exclusive Economic Zone*). Leseni zilizokuwa zimetolewa kwa wavuvi wakubwa ndani ya *EEZ* zinapitiwa upya na hii ni baada ya kugundulika wizi mkubwa unaofanywa na makampuni ya nje kuiba samaki wetu na kuondoka bila kulipa mapato yoyote na kufanya bahari yetu kama Shamba la Bibi. Kuanzia sasa, Serikali itaanza kutumia vyombo vyake vya dola likiwemo Jeshi la Ulinzi la Wananchi Tanzania (JWTZ) katika kuhakikisha tunapambana na wahujumu uchumi hawa. (*Makofī*)

(i) Matumizi ya Juya au Kokoro (*Beach Seine Net*). Juya linalotumika sana katika Ziwa Victoria na bahari, lakini sehemu nyingine ni nyavu za kuzungusha zinazokuwa na vielezi (*floats*) kwenye kamba ya juu na vizamishi (*sinkers*) kwenye kamba ya chini. Nyavu hizi, huvutwa kwenye maji kuelekea kwenye fukwe. Kitendo cha kukokora, huvunja matumbawe, hung'oa uoto wa asili majini na kuchangia mmomonyoko wa sakafu ya bahari au ziwa na ardhi ya fukwe. Matokeo yake ni kuharibika kwa maeneo ya mazalia, makulia, maficho na malisho ya samaki. Hivyo, nyavu za kokoro zimepigwa marufuku kwa misingi ya uharibifu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uvunjaji Sheria, ufanuzi wangu huu, hauna maana kuwa nafuta Sheria Na. 22 (2003) na Kanuni zake pamoja na Sheria nyingine zinazohusu uvuvi. Sheria itaendelea kutekelezwa na kesi zote zilizokuwa zinaendelea za wavuvi haramu, zinaendelea na vifaa vilivyoshikwa na vinavyoendelea kushikwa, watusika washughulikiwe kwa mujibu wa Sheria za nchi. Hayupo mtu yejote aliye juu ya Sheria na wala hayupo mtu yejote aliye na mamlaka ya kufuta Sheria iliyopitishwa na Bunge hili. Wavuvi watakaovunja Sheria, wapelekwe kwanza Mahakamani kadri Sheria ya Uvuvi Na.22 ya mwaka 2003 inavyoelekeza hususani vifungu 37 – 39 na 47 vikisomwa kwa pamoja na Kanuni za Uvuvi za 2005 kabla ya vifaa vyao kuchomwa moto au kutaifishwa ili kuondoa uonevu unaoweza kutokea. (*Makofī*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu leseni, Serikali inasisitiza kwamba leseni za shughuli za uvuvi ambazo nyingi hutolewa na Halmashauri za Wilaya, zinapaswa kuwa na masharti yanayoonesha zana, vifaa vya kila aina ya uvuvi na mahali zana hizo zitakapotumika kwa urahisi wa ufuatiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa wito kwa wavuvi wote nchini, kuitia vikundi vyao, kutumia miradi mbalimbali ya Kitaifa ambayo imetengewa fedha, baadhi ya miradi hiyo ni Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Bahari *MANCEP*, Mradi wa Kutekeleza Usimamizi wa Uvuvi wa Ziwa Victoria, Mradi wa Bahari na Maeneo Tengefu, Mradi wa Uendelezaji wa Uvuvi katika Ziwa Tanganyika, Vyuo vya Uvuvi vya Nyegezi na Mbegani, Maabara ya Taifa ya Udhibiti wa Ubora wa Samaki Nyegezi, TAFIRI pamoja na Maofisa Uvuvi katika maeneo yao katika kuhakikisha wanapata ushauri katika masuala mbalimbali yanayohusu sekta ya uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilitoa Waraka huo kwa mujibu wa Sheria. Umuhimu wa Waraka huo ni kuzuia matumizi ya zana zinazoharibu mazingira na rasilimali ya uvuvi ili mazingira, samaki na viumbe wengine wasitoweke kutohana na uvuvi wa kutumia zana na mbinu zinazokatazwa na Sheria za Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI pamoja na wadau wengine, itaendelea kutoa elimu kwa jamii ya wavuvi ili kuhakikisha rasilimali ya samaki na viumbe wengine kwenye maji vinalindwa. Pia inasisitizwa sasa tujenge utamaduni wa kufuga samaki suala ambalo Rais wetu Mheshimiwa Mrisho Jakaya Kikwete ameagiza tulizingatie katika sekta hii ya uvuvi, naomba ushirikiano kutoka kwa wavuvi katika kulinda rasilimali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, Serikali kwa hivi sasa inaandaa mkutano maalumu utakaowashirikisha Waheshimiwa Wabunge wote wa maeneo ya uvuvi, Wakuu wa Wilaya wote na Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri zote. Lengo la mkutano huo ni kuendelea kutoa elimu hususani zana haramu za uvuvi. Kwa kupitia viongozi hawa, tuna uhakika wataifikisha elimu hii kwa wavuvi wa maeneo yao. Tarehe na mahali utakapofanyika mkutano, tutatangaza kwenye vyombo vyahabari na kisha kuwatumia wahusika barua maalumu za mwaliko.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge na wadau mbalimbali wa sekta ya uvuvi kwa ushauri wao ambao umetusaidia sana. Wizara itaendelea kutoa ufanuzi kila itakapohitajika kufanya hivyo. kauli hii ya Serikali itasambazwa kwa Wakuu wa Mikoa wote, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi na Watendaji wa Halmashauri na Waheshimiwa Wabunge, ili isaidie kutoa ufanuzi kwa maeneo yanayohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunisikiliza, ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana kwa maelezo hayo, nadhani wavuvi sasa wamepata ahueni.

HOJA ZA SERIKALI

(Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2008/2009 - Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko)

(*Majadiliano yanaendelea*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunayo orodha ya wachangiaji wengi, nadhani tutaweza kuwafikia wengi kasoro wachache sana, tutakaoanza nao asubuhi hii, ni Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Ahmed Ali Salum, Mheshimiwa Kilontsi Mpologomyi, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mheshimiwa Mohammed Habib Mnyaa, Mheshimiwa Vita Kawawa, Mhehsimiwa Richard Ndassa na wengine tutaona kama watafikiwa.

MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii asubuhi hii ya leo.

Kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametufikisha katika hatua hii. Mimi ni Mjumbe katika Kamati ya Viwanda na Biashara na napenda kuunga mkono yale yote ambayo Mwenyekiti aliyasoma jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu pamoja na watendaji wa Wizara hii, kwa kazi nzuri ambayo wameifanya kama inavyoonekana katika kitabu hiki cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo mengi mazuri kama tutafanikiwa kuyatekeleza. Ninapenda tu kuomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tuamini kwamba tunaweza tukafika mahali, tatizo ni kutekeleza tu lakini mipango kama ilivyo, ni mizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niwapongeze pia watendaji wengine ambaa wapo katika Wizara hii kwa mfano *SIDO*, *TIRDO*, *TBS* na Wakala wa Vipimo na wengine, kwa kazi nzuri pia ambazo wanazifanya. Nilipata nafasi ya kuhudhuria Maonyesho ya Sabasaba mwaka huu. Yale maonyesho yamebadilika kwa kiwango kikubwa, Mkurugenzi pamoja na wafanyakazi wenzake wanafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipo kilio kikubwa cha ufinyu wa bajeti na karibu kila Mheshimiwa Mbunge aliposimama, alizungumzia jambo hili. Kilio hiki kipo karibu katika Wizara zote, nilikuwa najiuliza sijui Serikali itafanyaje ili kuweza kuhakikisha na kuona kwamba kila Wizara inapata fedha znazohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulifanya uamuvi, nakumbuka mwaka jana kwenye vipaumbele, tulisema vipaumbele vyetu vitakuwa kwanza kwenye miundombinu, elimu, afya na kadhalika, mimi naamini tukienda namna hii tunaweza tukafika mahali kwa sababu mahitaji yetu ni mengi lakini ni lazima tuchague sehemu zile ambazo tutawekeza na uwekezaji wake utakuwa na athari nzuri katika sekta zingine. Kinachotakiwa ni maunganishi mazuri (*matrix*), kwa mfano, tunaposema tunawekeza katika miundombinu, miundombinu hii inakuwa na athari gani katika mpango wetu wa kuanzisha viwanda? Mwelekeo umekuwa kule kwenye miundombinu mizuri ndiko viwanda vinakokwenda na kwa hivyo tunakuwa na viwanda sehemu moja ya nchi na sehemu nyingine ya nchi inakuwa haina viwanda na hivyo kunaleta manung'uniko kwa Mikoa ile ambayo haina viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nafikiri hii azma ya kuwekeza katika miundombinu ni nzuri na ninaomba Serikali inapowekeza katika miundombinu iweze kuwekeza katika Mikoa yote ili fursa za viwanda zinapotokea ziweze kwenda katika Mikoa yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, sijui kunakuwa na ushirikano kiasi gani kati ya Wizara hii ya Viwanda pamoja na Wizara ya Miundombinu ili kuona kwamba kule ambako kunastahili kwenda viwanda vya aina fulani basi kunakuwa na miundombinu ili wawekezaji wa ndani na wa nje wanapojitokeza pasiwe na kikwazo cha miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kuna suala la *energy* kama umeme ambao pia ni kikwazo katika uwekezaji wa viwanda. Kwa hiyo, tunapowekeza katika umeme, ninahakika tunasaidia sekta hii ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazo fedha nyingi sana pia katika kilimo, Wilaya zinapelekewa hela nyingi sana *DADPs* na Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi, inaongelea juu ya kuongeza thamani ya mazao yetu, huwezi kuongeza thamani ya mazao bila kuwa na viwanda, sasa kuna ushirikianao gani kati ya zile fedha za *DADPs* katika Wilaya na kuanzisha viwanda katika Wilaya zetu? Hili silioni sana likijitokeza katika Wilaya zetu, ninashauri kuwe na ushirikiano zaidi kati ya Wizara ya Viwanda, TAMISEMI na hasa katika Wilaya ili vile vifaa vinavyotengenezwa na taasisi zetu za teknolojia kama *TIRDO*, *CAMARTEC* na *SIDO* na matokeo yote yanayoletwa na taasisi yetu ya *TBS* ziweze kuongezwa na kupelekwa katika Wilaya zetu na ziweze kutumika. Kwa namna hii, tukapunguza kwa kiwango kikubwa kilio cha bajeti kwa sababu fedha zipo katika sekta zingine ingawaje katika sekta hii ya viwanda na biashara kwa mwaka huu haijapata fedha nyingi, lakini tukiwa na ushirikiano wa kutosha ndani ya Serikali kwa maana ya Serikali Kuu na Halmashauri, naamini yale yote ambayo yanatekelezwa na hizi taasisi zilizopo katika Wizara ya Viwanda na Biashara yanaweza yakatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipo kilio kikubwa juu ya *SIDO* yenye na mimi naunga mkono kilio hiki na kimetuathiri sana kule Mbinga kwa sababu *SIDO* iko Mikoani na kule Mikoani, *SIDO* imefanya mambo makubwa sana hasa kule Songea lakini haijafanya mambo mengi Wilayani kwa sababu ya kukosa bajeti ya kwenda huko. Kwa hiyo, kama *SIDO* itapewa fedha za kutosha, ninahakika itakwenda Wilayani kwa urahisi zaidi na pengine lile wazo la Mheshimiwa Mramba la kusema kwamba *SIDO* imekaa Mkoani muda mrefu, ihamie Wilayani, huu ni wakati wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nihamie kwenye suala la kuvutia wawekezaji. Ziko sera zetu hapa, iko *SEZ* na *EPZ*. Lakini *SEZ* toka tumepitisha Sheria mwaka 2006, haijafanya kazi mpaka sasa na hotuba ya Mheshimiwa Waziri inazungumzia juu ya kuainisha sera hizi mbili. Ninapenda azma hiyo iende kwa haraka zaidi ili tuweze kuharakisha maendeleo kwa sababu hizi mbinu mbalimbali za uchumi zinabadilika mwaka hadi mwaka na kwa haraka sana, tunapozidi kuchelewa kuchukua maamuzi, tutakapokuja kuchukua, tutakuwa tupo nyuma na hivyo tutakuwa tunaendela tu kupoteza muda na fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilianza kujenga ile *SEZ* ya Benjamin William Mkapa pale Mabibo Ubungo, ile *SEZ* imechukua muda mrefu sana, ilitakiwa iishe mwaka huu lakini haijazungumzwa kama inaweza zikaisha mwaka huu au hapana na kinatokea nini. Tunapozidi kuchelewa, nchi zingine sasa hivi zinapiga hatua kwa kasi sana kutekeleza *SEZ* zao na sisi tutakapokuwa tunamaliza ya kwetu tayari itakuwa imeshapitwa na wakati, haipo *up to date*, hela ambayo imeshakuwa *invested* pale itakuwa

imepotea. Kwa hiyo, nafikiri haya maamuzi ambayo tunafanya, yangetekelezwa kwa haraka inavyotakiwa ili tuweze kupata yale manufaa ambayo tulitaka yapatikane, hatuwezi kuanza kitu, inapita miaka kumi hatujakitekeleza na tutegemee tutapata mambo yale yale ambayo tutakuwa tunatarajia kuyapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nipongeze mamlaka ya *EPZ* ambayo imeshafanya kazi kubwa sana. Kulikuwa na viwanda vitano sasa hotuba ya Mheshimiwa Waziri inasema kuna viwanda tisa hii ni hatua nzuri lakini pia tunahitaji kupiga hatua zaidi katika masuala haya, tulianza pamoja na Kenya lakini wenzetu Kenya wapo mbali sana sasa, sisi bado tuna suasua.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuishauri Serikali kwamba tunapofanya maamuzi tuyatekeleze, lakini hii dhana ya ufinyu wa bajeti mimi nafikiri ni suala la maamuzi. Nitoe mfano, tulipanga na tukaamua tuwe na Chuo Kikuu Dodoma tunacho, tulipanga na tukaamua tuwe na ukumbi mzuri wa Bunge tunao, katika mambo yale yote tunayopanga na kuamua kwa dhati kuyafanya, yanafanyika, kinatushinda kitu gani kupanga mipango iwe mikubwa na maamuzi makubwa katika mambo ambayo yanaweza yakatuletea maendeleo katika nchi yetu? Nafikiri inawezekana, si suala la bajeti, ni suala la maamuzi zaidi kuliko suala la bajeti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, najaribu kuijiliza dhamira yetu ya kufanya nchi yetu kuwa nchi ya viwanda, kwa sababu sioni mkono wa Serikali halisi katika mambo haya ya viwanda vikubwa wala viwanda vidogo. Labda nianze katika viwanda vidogo. Hizi taasisi zimeshaleta teknolojia kwa mfano unga wa mhogo, ni unga unaotakiwa sana duniani, unatakiwa pia sana hapa nchini na zana za kutengeneza unga wa mhogo zipo lakini wakulima wetu hii teknolojia hawajapelekewa kwa kiwango cha kutosha na wakipelekewa hawatakuwa na uwezo wa kununua hizi mashine kwa sababu hakuna mtu wa kuwawezesha!

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa na Mfuko unaitwa “Mwananchi Empowerment Fund”, ulizinduliwa mwaka jana. Mfuko huo, mpaka sasa haupewi hela. Hawa wanaviwanda ambao tunawahamasisha, watapata wapi hela za kuanzisha viwanda? Ndiyo maana nasema ni suala la maamuzi, tukiamua kwamba *Empowerment Fund* ni kitu muhimu, Serikali itaweka hela kwenye *Empowerment Fund* na kuweza kuweka dhamana hii kwa wale watu ambao wanahitaji zana hizi, tutafika mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna huyu mtu anaitwa Wakala wa Vipimo, anafanya kazi nzuri lakini nafikiri naye anakabiliwa na tatizo la pesa. Lakini kama tunataka kuondoa kero katika vijiji vyetu, kero kutoka kwa wakulima wetu, ni lazima huyu Wakala wa Vipimo pia asaidiwe ili yale mambo ya ‘lumbesa’ na kudhulumiwa katika vipimo kwa wakulima yaweze kuisha. Hiyo ndiyo namna pekee ya kuweza kumsaidia huyu mkulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ngozi, mimi nilikwenda Ethiopia, wanayo majaketi ya ngozi, wana viatu vyta ngozi, wamepiga hatua kubwa sana. Ukilinganisha Ethiopia na sisi, tulikuwa tumewapita mbali sana lakini sasa wametupita mbali sana. Kitu

gani ambacho kinatufanya mpaka leo tunashindwa kuwekeza katika ngozi na mazao yake? Shule tunazo, wanyama tunao, tunacho kila kitu lakini bado hatujapiga hatua katika jambo hili, ndiyo maana nasema ni suala la maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mtume Paulo, alipokuwa anazungumza na Wakorintho alisema ‘apandaye haba atavuna haba’ na sisi tunapopanda haba katika eneo kubwa la uchumi kama hili bila shaka tutavuna haba na hatutakuwa na mtu mwingine wa kumlaumu. Wito wangu kwa Serikali ni kwamba tupande kwa wingi katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna dhana ya ‘Mtanzania nunua bidhaa za Tanzania’. Wakati tulipokuwa kwenye Maonyesho ya Sabasaba, Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuwa anafungua rasmi maonesho hayo, kuna kiongozi, nafikiri yule alikuwa ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Nje, alitoa wito huo, yeye au Mheshimiwa Waziri. Nilikuwa nimekaa karibu na Mwandishi mmoja wa Habari, akasema hili jambo haliwezekani. Nikamuuliza kwa nini? Akasema kwa sababu ukienda kwenye ofisi za Serikali, fenicha zote zimeagizwa nje! Hivi hatuwezi tukafanya maamuzi ya makusudi kwamba ofisi zote za Serikali ni lazima ziwe na fenicha zilizotengenezwa Tanzania, haiwezekani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani tukawa na utaratibu tukasema tutakapokuwa tunamwapisha Rais wetu mwaka 2010, gari litakalomleta kiwanjani liwe limetengenezwa Tanzania, haiwezekani? kwa sababu tunayo Nyumbu, tunazo *institutes* ambazo zinaweza zikatengeneza gari hilo, ni kuwa na malengo na maamuzi tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka leo Waziri Mkuu anatembelea gari ambalo limetengenezwa India, Mawaziri pia wanatembelea magari ambayo yalitengenezwa India na Wabunge wanatumia magari ambayo yametengenezwa India. India yapo magari ya kutoka nje lakini wameweka uamuzi kwamba kiongozi wa Serikali ni lazima atumie mali ya India. Pengine na sisi tunaweza tukajifunza, ni suala la kuangalia na kuona uwezekano wake, inawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudie tena kuipongeza Wizara hii kwa mambo mazuri ambayo wameandika humu ndani ya hotuba, mimi ninawatachia kila la kheri. Ninapoangalia, nawaonea huruma, changamoto zinazowakabili ni nyingi, najua uwezo wa Mheshimiwa Waziri Nagu, najua uwezo wa Mheshimiwa Naibu Waziri na Katibu Mkuu, wana uwezo mkubwa sana, pamoja na changamoto hizi za bajeti mimi nafikiri tusikate tamaa kwa sababu inawezekana kufanya haya mambo tukishirikiana na Wizara zingine kwa sababu Wizara zingine kama Kilimo wanazo hela za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuiomba *SIDO* pia wafikirie sana Wilaya ya Mbinga kwa sababu kule kuna wajasiriamali na wenye uwezo mkubwa tatizo ni kwamba hawajawezeshwa na hawajapewa elimu, Mbinga hatuna haja ya hela tunataka elimu tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii ya kuzungumza machache kuhusiana na Wizara yetu ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kuchangia, naomba nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Spika kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Bunge la *Commonwealth*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa nimekosea vilevile kama nisipompongeza Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, kwa kweli ametoa hotuba nzito ambayo kwa kiasi kikubwa natarajia Mheshimiwa Waziri wakati anajibu atakuja na majibu muafaka yatakayotufanya sisi tusiweze kushika vifungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze moja kwa moja na ukurasa wetu wa tano wa hotuba ya Kambi ya Upinzani ambao tumezungumzia suala zima la *Tanganyika Packers*. Inafahamika kwamba suala zima la ubinafsishaji wa viwanda vyetu Tanzania, limekuwa likiandamana na matatizo mengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitazungumzia *Tanganyika Packers* na *Tanganyika Packers* ambayo nitaizungumzia ni ile *branch* ya Dar es Salaam. Nikianza na suala zima la mkataba wenyewe uliosainiwa, taarifa inaonesha kwamba mkataba ulisainiwa na Mheshimiwa Adamjee, kwa niaba ya yule mwekezajina taarifa zilizopo na zenye ushahidi, zinaonesha vilevile kwamba *Power of Attorney* ambayo inampa mamlaka Mheshimiwa Adamjee kusaini ule mkataba ili kuuwezesha kuwa *valid*, ulisainiwa mwaka mmoja baadaye. Kwa mantiki hiyo, mkataba tu wenyewe wa mauzo ya *Tanganyika Packers*, una mushkeli.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja kwenye kilichokuwemo ndani ya mkataba, sawa mkataba una mushkeli, umeshasainiwa kama ilivyosainiwa mikataba mingine, sasa tuna-*deal* na vipengele vilivyopo ndani. Moja ya vipengele vinasema kwamba mwekezaji anatakiwa kwanza atoe asilimia kumi kabla hajakabidhiwa chochote kisha atoe asilimia 50 ili aweze kukabidhiwa kiwanda kizima.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunaambiwa kwamba mwekezaji amekabidhiwa kiwanda kizima kabla hata ya kutoa 35 percent ya bei nzima ya kile kiwanda ambacho kilitakiwa kuuzwa. Hapa kuna tatizo kubwa sana. Vilevile hii 33 percent ambayo inasemekana ametoa watu wamejaribu kuhoji, ushahidi uliopo pasipo mafanikio. Sasa mimi natarajia Mheshimiwa Waziri Nagu akiwa anajibu maswali kwa kuwa ndiyo sekta nzima ya viwanda, atanitolea majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya kiwanda sasa hivi ni magofu hakuna chochote, mashine zote zilizokuwepo zimeondolewa, hakuna chochote, Mama Nagu, natarajia ataniambia zimeenda wapi.

NAIBU SPIKA: Wanasema Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, Mama Nagu ni akiwa kwake huko nyumbani.

MHE. HALIMA J. MDEE: Sawa, Waziri wa Viwanda Biashara na Masoko, nilifikiria nikitaja hivyo ni heshima zaidi, natarajia Waziri wa Viwanda Biashara na Masoko, atatupa hiyo taarifa na haswa hivyo vifaa vimeenda wapi na kama pesa zililipwa kwa asilimia mia moja, zililipwa katika mchakato gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye *deed of hand over*, ambayo inaendana na huo mchakato mzima wa mkataba, inaonyesha kwamba; kwa sababu hili eneo lligawanywa katika viwanja mbalimbali lakini katika hiyo *deed of hand over* inaonesha kwamba ni kiwanja kimoja ndicho ambacho kimejumuishwa kwenye mkataba. Kwa kuzingatia kwamba kuna viwanja kadhaa ambavyo havijazungumzwa kabisa katika makubaliano husika, inatia mashaka na kwamba yawezekana haya maeneo mengine ambayo hayajatajwa amepewa bure ama kuna watu wamejigawia. Namwomba Mheshimiwa Waziri wakati atakapokuwa anajibu, anieleze kwamba mchakato mzima wa vile viwanja 11 ambavyo vilikuwa vimetengwa kwenye mkataba, umeendajeendaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tumeambiwa kwamba huyu mwekezaji ni wa Dubai na tunajua kabisa kwamba Sheria za Kimataifa zinaruhusu kumshtaki mtu ambaye mnaona amekiuka mkataba, sisi tumezoea kushtakiwa. Tulivunja mkataba *na City Water*, tunapelekwa Mahakamani lakini sisi tunaonewa kila siku, lakini hauoni hata siku moja tuna *guts* za kusema huyu ametuibia twende tumpeleke Mahakamani! Viwanda vyetu vyote vimekufa si kwa sababu ya uzembe wetu pekee mara nyingi mwekezaji *ana-take advantage* ya uzembe wetu anachukua pesa anaondoka, anachukua vifaa vyta kwenye viwanda anaondoka. Sasa nataka mtupe picha kamili kipi ni kipi? Siyo kila siku, mnatuletea hotuba hapa ambayo hata ukisoma huwezi ku-link na hotuba zilizopita ni kama mnatuchanganya tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee na suala zima la makampuni ambayo yanakopeshwa pesa. Jana Waheshimiwa Wabunge wamelalamika sana kuhusu *SIDO*, wamelalamika sana kuhusu *NDC* na haya ni makampuni ama viwanda ambavyo *vinaldeal* moja kwa moja na mwananchi maskini, wa kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana Mama Kilango alilalamika kweli kweli na ana haki ya kulalamika kwa sababu wananchi wake wanajua kwamba kiwanda cha *SIDO*

ndicho kina-deal nao moja kwa moja na si mfanyabiashara mmoja ambaye anapewa fungu la pesa anajua jinsi mwenyewe anavyoenda kulitumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi yetu ya Upinzani, katika maelezo yake, imehoji kuhusu *General Tyre East Africa*, tunaambiya *General Tyre East Africa* imepewa bilioni 12, tunafahamu kweli Serikali ina asilimia 76 ya umiliki, *fine*, lakini tunaambiya leo hii, hiyo bilioni 12 ambayo kuna asilimia mia moja *guarantee* ya Serikali kwamba huyu mtu akikimbia maana yake hili deni nitalilipa. Unaambiya leo kampuni haiwezi kufanya kazi au haiwezi kuzalisha, wakati huo huo kampuni ambayo ina-deal na watu maskini ya *SIDO* imeomba bilioni 5 inapewa bilioni 1, tunakwenda wapi? Je, ni kweli tuna nia ya kuondoa umaskini kwa hawa Watanzania au tunafanya usanii? Ni muhimu tuwe wa kweli ili tueleweke. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye kampuni nyingine ya *Continental Venture*, tunaambiya hii tuliombea mkopo *Gomba Estate*, hii *Gomba Estate* ni kampuni ya mtu binafsi afadhali hata hii *Generel Tyre* tunaambiya kwamba Serikali ina asilimia 76, hii ni ya mtu binafsi amepewa bilioni 5, mtu huyu binafsi anaambiya lete taarifa basi za mwenendo wa kampuni, haleti, hili ni deni ambalo linakufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huo huo tunaambiya *NDC* ambayo inashughulika na utafiti wa Mchuchuma ambao utatuletea sisi umeme na Watanzania wengine wote ambapo tunaweza hata kuuza nchi jirani, imeomba bilioni 7 imepewa milioni 75, hii ni aibu kubwa sana! Sijui ni lini tutaacha kuwadanganya Watanzania kwa maneno matamu na kufanya kwa vitendo! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii kampuni ya *Kagera Sugar*, imepewa bilioni 67 kwa *guarantee* ya Serikali asilimia mia moja na tunaambiya hapa kule hakuna kinachozalishwa ni usanii umechezwa tu. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri wakati ananijibu aniambie kwa dhati kabisa wana mkakati ganI na hawa Watanzania wenzetu maskini ambao wanaomba hata bilioni tano wananyimwa lakini hii kampuni ambayo inakuwa *owned 100 percent* na mtu binafsi inapewa bilioni 65, natagemea atanijibu na atanipa mikakati yake ya mwaka ujao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la mafao ya wafanyakazi katika viwanda vya Serikali vinavyobinafsishwa, leo hii ukitembelea kila kijiji Tanzania hii na ninaamini hata Wabunge wataniunga mkono, hakuna mwananchi ambaye hana lalamiko la kunyimwa mafao yake.

NAIBU SPIKA: Kila mwananchi? Unamaanisha kila mwananchi? Hebu sema vizuri tena.

MHE. HALIMA J. MDEE: Labda nimeweka sentensi vibaya.

NAIBU SPIKA: Sawa weka vizuri.

MHE. HALIMA J. MDEE: Hakuna kijiji utakachotembelea ukakosa hata mwananchi mmoja ambaye hana lalamiko la suala zima la mafao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala la mafao Uvinza ni kitu ambacho kimekomaa. Kiwanda chetu cha Chumvi cha Uvinza kimebinafsishwa toka mwaka 99 mpaka leo wazee wa watu wanakanyaga na miguu, hakuna kitu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barua zinazotoka Wizara ya Nishati na Madini, barua inayotoka kwa Waziri Mkuu aliyekuwa kipindi kilichopita, Mheshimiwa Sumaye, anatoa maagizo Hazina, hawa watu walipwe, hawalipwi. Hizo barua zote zipo, sasa mimi ninachotaka kujuu kwa nini tunakuwa tunafanya mambo ambayo hatujajiandaa?

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi tumezungumza hapa kuhusiana na suala zima la watu kuchukuliwa ardhi yao na kulipwa *compansation* ambayo ni ndogo kuliko thamani halisi. Tunaingia katika masuala ambayo hatujajiandaa, tunaona Mtanzania kwa vile ndiyo hivyo maskini yuko *vulnerable* basi tunamvamia, tunachukua vitu vyake, *this is not fair*. Nitamwomba Mheshimiwa Waziri aniambie mustakabali wa hawa watu wa mafao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kiwanda cha Mgololo, walichozungumzia, kiwanda ambacho Mheshimiwa Naibu Spika, najua kiko kwenye maeneo yako, kuna watu 760 wanadai mafao, mpaka leo wanapigwa danadana. Hii haifai. Wakati huo huo tunaambiwa kwamba kuna mabilioni yamechotwa *EPA*, mtu amejiwekea kibindoni, yameondoka. Hivi vitu haviendi! Halafu tunaambiwa tena hao hao walioiba wanasafishwa, mambo hayaendi hivi jamani!

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, naomba ukiwa unajibu maswali yako, uniambie nini mustakabali wa hawa watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikimalizia, nakumbuka mwaka jana katika hotuba yetu ya Viwanda, Biashara na Masoko, tulihoji suala zima la kiwanda cha Chumvi Uvinza. Tulisema kwamba kiwanda kinatumia magogo. Aliyekuwa Waziri mwenye dhamana, akakataa kwamba kiwanda hakitumii magogo. Mimi kwa miguu yangu nilikwenda hadi Uvinza, kiwanda kinatumia magogo na kuna uharibifu mkubwa wa mazingira. Kwa leo hii uharibifu wa mazingira Uvinza inaweza isionekane lakini miaka 20 ijayo kutakuwa hakuna Uvinza. Miaka 20 ijayo, mazingira yatakuwa yameharibika, kwa sababu tu wanasiwa, wanaambiwa au wanaelekezwa vibaya na watendaji wao, ama kwa makusudi kabisa wanasema kwamba hakuna, kumbe ndivyo ilivyo, kiwanda kile kinatumia kuni na kinatumia juu, inatumia vyote viwili. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri naomba uchunguze hilo suala.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni lile suala zima la baadhi ya vifaa vya kwenye viwanda kutolewa na kusafirishwa na kwenda kuuzwa Iran. Tulitembelea pale na wakakiri kabisa kwamba kuna mtambo mmoja ambao Mheshimiwa Rais sasa hivi alipokuwa ni Waziri wa Nishati na Madini alienda kuzindua kiwanda fulani kidogo, kile kiwanda kimechomolewa chote na kuuzwa Iran.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona muda hauniruhusu, ila naomba Mheshimiwa Waziri alifuatilie hili suala na atupe majibu ya ukweli. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Ahmed Salum, Hayupo! Mheshimiwa Mpologomyi, naye naona hayupo. Basi sasa ni zamu ya Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwananzila na Mheshimiwa Mnyaa awe *standby*!

MHE. SIRAJU J. KABOYONGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia hotuba muhimu ya Wizara yetu ya Viwanda, Biashara na Masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuwashukuru na kuwapongeza Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Mashirika na Taasisi mbalimbali zilizoko chini ya Wizara hii kwa kazi muhimu walioifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama walivyotangulia wenzangu katika kuchangia hotuba hii, nianze kwa kuzungumzia umuhimu wa viwanda katika uchumi wetu. Viwanda ni sekta muhimu sana katika maendeleo ya uchumi kwa sababu ndiyo sekta ambayo inaweza kuwa ni kimbilio la nguvu kazi pale ambapo inaachiwa kutoka kwenye sekta nyingine hususan sekta ya kilimo kwa kadri uchumi wetu unavyoweza kuendelea na kwa hiyo kuondokana na mahitaji makubwa ya nguvukazi mashambani kwa kuwa kule mashambani kutaanza kutumika zana za kisasa. Kwa hiyo, kutakuwa na hazina kubwa ya nguvu kazi ambayo itabidi ihame mashambani ihamie katika uchumi wa kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchumi wa kisasa, ndani yake kuna viwanda, kuna huduma kama vile mabenki, bima na kadhalika. Kwa hiyo, viwanda vinachukua nafasi hiyo, kama kimbilio la nguvukazi ya ziada kutoka kwenye sekta nyingine. Vile vile viwanda ndiyo vinavyozalisha mahitaji takriban ya uchumi wote ikiwa ni pamoja na mahitaji muhimu ya sekta muhimu ya uchumi huu, sekta ya kilimo. Sekta ya kilimo inahitaji mbolea, inahitaji pembejeo, inahitaji zana za kilimo za kisasa, vyote hivi vinazalishwa na viwanda. Ni pale tu utakapokuwa na viwanda imara ambavyo vinaweweza kuzalisha mahitaji ya uchumi wake kama vile zana za kilimo, mbolea na kadhalika ndipo uchumi wetu unakuwa na maingiliano ya sekta zetu ndani kwa ndani. Wakati sekta moja inaingiliana na sekta nyingine ndani kwa ndani, ndipo unapokuwa na uchumi mzuri kuliko ilivyo sasa hivi, wakati ambao uchumi wetu baadhi ya sekta zake ziko Tanzania na

sekta nyingine ziko nje ya Tanzania na ndiyo maana hainishangazi tunapojikuta kwamba sisi tunabaki wazalishaji wa mazao ya kilimo na kwa bahati mbaya sana kwa hivi sasa, kwa kiasi kikubwa tunayauza nchi za nje yakiwa ghafi. Tunachokifanya hapo tuna-export ajira zetu nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mzuri hapa ni kiwanda cha *Tabora Textile* ambacho kinatengeneza nyuzi kutokana na zao letu muhimu la pamba. Kiwanda kile kinatengeneza nyuzi tu, kikishatengeneza nyuzi, ule uzi unapelekwa kuuzwa nchi za nje. Kinachotokea kule nje wanaubadilisha ule uzi ndani ya nguo kwa maana ya bafta au nguo kamili, vitenge na kanga, halafu tunaviagiza sisi Tanzania vitenge na kanga na bafta ambavyo vimetokana na uzi uliotokana na pamba ya Tanzania. Kwa nini haya yote yasifanyike hapa nchini? Sasa ndiyo pale ninaposema ukiwa huna viwanda unajikuta unawapelekea wenzako ajira wakati na wewe unazitaka zile ajira. Kwa hiyo, umuhimu wa viwanda kwa kifupi ni huo pamoja na mengine mengi ambayo kwa sababu ya muda mfupi nilionao siwezi kuyaeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nikirudi kwenye Kiwanda cha Nyuzi, Tabora. Ninachotaka kuiomba Wizara ni kwamba katika mpango wake wa kutengeneza maeneo muhimu ya uchumi (*Special Economic Zone*), hebu Serikali iamue kulifanya eneo lile la kiwanda cha Tabora Nyuzi kuwa ni moja ya maeneo muhimu na ya kipekee kiuchumi ili eneo lile liweze kupata mvuto ili wawekezaji waende pale ili tuweze kukibadili kile kiwanda kitoke kwenye kutengeneza uzi pekee kiwe ni *a fully textile integrated mill* kuanzia pamba, uzi, kanga, bafuta, vitenge na mashuka na kadhalika. Hilo litatusaidia hata pale Tabora kuongeza ajira na umuhimu wa kiwanda hicho utaonekana zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu viwanda vya msingi. Viwanda vya msingi vimezungumziwa sana. Mantiki ni ile ile kwamba ukitaka kuendeleza uchumi wako ni vizuri uwe na viwanda vya msingi ambavyo vinazalisha mahitaji muhimu ya viwanda vingine. Ukiwa huna viwanda vya msingi katika nchi yako, siku zote nchi yako itategemea nchi za nje kupata mashine na vikorombwezo vingine vya kuja kutengeneza viwanda vyako. Jana kimezungumziwa kiwanda cha msingi kimoja cha chuma, kwa umuhimu wake niachie hapo na mimi naunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna viwanda vya msingi vingine kama vya mpira, viwanda vya msingi vya gilasi kwa maana ya vioo, viwanda vya msingi vya *chemicals*, hapa nataka nisisitize *chemical* inayotokana na *Soda Ash* ambayo sisi Tanzania Mungu ametujalia kuwa na *Lake Natron* ambalo linaweza kuzalisha *chemicals* kama *Soda Ash* ambayo ni *ingredient* muhimu sana katika viwanda hapa nchini. Lakini leo hii kuna mjadala mkali sana kuhusu tuanzishe au tusianzishe kiwanda kile kwa sababu ya *flamingo* walioko pale. Naheshimu mawazo ya wote wanaosema *Flamingo* wana haki ya kuishi pale, lakini na nchi nayo ipate maendeleo kutokana na kiwanda cha *chemicals* inayotokana na uwepo wa lile Ziwa la *Lake Natron* pale. Kwa hiyo,

kinachohitajika kufanyika hapa ni kile kinachoitwa kwa lugha ya kigeni *Environmental Impact Assessment* ya uwepo au kutokuwepo kwa kiwanda kile kwa manufaa ya uchumi. Kwa hiyo, Serikali kupitia Wizara hii, hebu iharakishe hiyo *Environmental Impact Assessment* ili tujue mwisho wa siku kiwanda hiki tunacho au hatuna kwa sababu za kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, yako mashirika Serikali imeyaunda kwa ajili ya utafiti na maendeleo kwa lugha ya kigeni wanasema *Research and Development*. Mashirika haya ni pamoja na *CAMARTEC*, *TEMDO* na *TIRDO*. *Research* na *Development*, ni jukumu la Serikali husika. Hakuna nchi duniani itakusaidia wewe kufanya *Research* na *Development* kwa sababu *wakikusaidia* ni kwamba utajing'atua, utatoka kwenye ule mnyororo wa wewe kuwa tegemezi kwao. Kwa maana hiyo, hakuna mfadhili ambaye tunapaswa kumtegemea aje atuibilie *Research* na *Development* zetu. Hili ni jukumu la Serikali na ni lazima Serikali ilifanye kikamilifu wala siyo kwa kubabaisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mathalani *CAMARTEC*, wanatengeneza zana za kilimo, tena zana zile za kilimo ambazo wakulima wetu ambao wanaondokana na matumizi ya jembe la mkono kwenda kwenye trekta dogo wanalloweza kulimudu, kuna mikokoteni ya ng'ombe, kuna mambo chungu nzima, mashine ya kukamua mafuta na vitu kama hivyo. Haya ndiyo maendeleo yanayotakiwa. Lakini shirika hili letu la Serikali linakwama kama vile *TIRDO* inavyokwama, kama vile *TEMDO* inavyokwama kwa sababu hawana fedha za kutosha na hili ni jukumu la Serikali. Nasema hakuna njia ya mkato isipokuwa Serikali kuwekeza katika mashirika haya na kuhakikisha kwamba yanapatiwa fedha za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na mawazo mengi kuhusu *SIDO*. *SIDO* ni shirika, hili si shirika la utafiti, hili ni shirika la uwekezaji mdogo mdogo kwa hiyo hawa *SIDO* wanawekeza wanaweza kukopesheka. Kwa hiyo, malalamishi yanayotokea hapa kwamba Serikali haijawapa fedha za kutosha, ni sawa lakini wao wana njia nyingine. Hii ni *organization* ni *independent entity, it can sue and be sued* na mambo chungu nzima. Waende benki wakakope. Tatizo letu kubwa hatuna *Financial Institution Structure* ambayo inasaidia maendeleo ya viwanda. Tuna *TIB* ilikuwa *under capitalized* ndiyo kwanza imeongeza 21 bilioni lakini 21 bilioni hizo zinaangaliwa na viwanda, zinaangaliwa na kilimo, hazitoshi! Ili uwe na benki inayoweza kukopesha maendeleo ya nchi hii, unahitaji iwe *capitalized* siyo chini ya *1 hundred billion shillings*, ndiyo itafanya maendeleo ya kilimo pamoja na viwanda vyake. Kwa hiyo, hapa sasa ni suala la mfumo tu na *Financial Institution Structure* yetu jinsi ilivyokaa, haiko katika namna ya kuweza kuendeleza kilimo pamoja na viwanda. Tujirekebishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua Serikali haina fedha kutoka kwenye nyanzo vya kodi kuweka huko kwenye benki, itafute njia nyingine ikiwa ni pamoja na kupata *long term bonds* wawekeze huko kwenye *TIB*. Mimi nadhani kwa kutumia utaratibu wa kupata *Sovereign Bonds* kutoka nje, Serikali itakuwa njia ya uhakika itakayoweza kutupatia pesa nyingine za kuwekeza kwenye benki yetu kwa ajili ya maendeleo ya viwanda na kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la *EPA*. *EPA* ninayoizungumzia mimi hapa siyo ile ya mafisadi. Nazungumzia *EPA* ya *Economic Partnership Agreement*. Hii *Economic Partnership Agreement* mpaka sasa hivi, Serikali yetu wanasema wamei-initial mkataba baina ya Tanzania kwa upande mmoja tukiwa pamoja na *EAC countries* na nchi za Ulaya kwa upande mwagine. Naishauri Serikali iende taratibu katika hili. Chini ya *EPA (Economic Partnership Agreement)*, sisi tusipoangalia, tutaendelea kuwa wauzaji wa malighafi za kilimo na waingizaji wa zana za viwandani, utaratibu huu hautatukwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuzingatie kwamba huko huko tunakotaka, kukamilisha na mkataba wa *EPA*, kuna fursa nyingine mbili, moja inaitwa *Everything But Arms* na nyingine ni *GSP+*. *GSP+* inakuruhusu ku-export free qouter bila *Qouter, Duty Fee*, 88% ya *products* zetu, Chini ya *Everything But Arms una-export everything* huko huko Ulaya isipokuwa silaha. Sasa kwa nini tunajifunga kwenye hii *EPA*? Masharti ya kwamba lazima wao tuwaruhusu waje kwenye soko letu watuletee mashine, sisi tuwapelekee malighafi, hilo kwa kweli silitaki na naishauri Serikali ijitazame vizuri juu ya eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Sera za Biashara. Sera yetu ya Biashara tumeifungua sana! Hakuna nchi duniani inaruhusu watu wa nje kwenda kufanya biashara ndogo ndogo katika nchi yake. Tanzania tunafanya hivyo! Tubadilike, turuhusu biashara za ndani zote zifanywe na Watanzania hususan wazalendo. Watu wa nje wakija, kama wanataka wafanye hizo biashara za ndani, basi iwe ni lazima wazifanye kwa kuingia ubia na Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu ilipokuwa inabinafsisha mashirika yetu, tulifanya kosa moja. Hatukuunda chombo ambacho kingekuwa ndiyo hazina ya zile hisa za Serikali zinazobaki, ili tuweze kuwa na utaratibu wa *Private Public Partnership (PPP) contracts*. *NDC* ipo pale, hebu tuiwezeshe hii *NDC*, ndiyo iwe msimamizi mkubwa wa rasilimali ya Taifa kwenye kila shirika linalobinafsisha. Tunaoifahamu historia ya uchumi ya nchi hii, tunakumbuka jinsi *NDC* ilipoanzishwa na majukumu yake. *NDC* ndiyo ilioanzisha viwanda vya ngozi, vya nguo na viwanda chungu nzima ambavyo sasa hivi takribani vyote tumevibinafsisha na vingine chungu nzima vimekuwa, sasa tunahangaika! Hebu turudi kule kwenye *NDC* ya zamani. Tuifanye *NDC* iwe ndiyo kioo au ndiyo mkono wa Serikali katika uwekezaji katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ulivyosema, muda hautoshi, nimezungumza kiasi ambacho nadhani inatosha. Sasa naunga mkono hoja, ahsante sana kwa kunisikiliza. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Mwananzila na Mheshimiwa Mnyaa ajiandaye.

MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu kuhusu Wizara hii ya Viwanda, Biashara na Masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, na Viongozi wengine wote wa Wizara hii, Katibu Mkuu na Wataalamu, wengine kwa jinsi walivyotuletea hotuba ya Wizara hii wakielezea mambo mbalimbali ambayo yatafanyika kusaidia biashara, viwanda na masoko katika nchi hii ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nataka nizungumzie kuhusu Wizara hii ya Viwanda, Biashara na Masoko katika Mkoa wa Rukwa na jinsi Mkoa huu unavyohusiana na Mikoa mingine na nchi jirani zinazotuzunguka na jinsi ambavyo Wizara hii kwa kiwango kikubwa imeshindwa kuwasaidia sana wakulima na wafugaji ili waweze kuboresha bidhaa wanazouza nje ya nchi badala yake tunauza vile vitu ambavyo havijasindikwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Rukwa mwaka jana waliitisha mkutano, wanaita *stakeholders meeting* uliofanyika tarehe 17 mpaka tarehe 18 Mei mwaka 2007. Serikali yote kwa ujumla, ilialikwa na Wizara hii ilialikwa, tukitarajia kwamba watakapokuja kuhudhuria watatushauri, watatusaidia ili tuweze kuwainua wafanyabiashara walioko katika Mkoa wa Rukwa ili waweze kuwa imara ili na wao waweze kuanzisha viwanda vidogo vidogo na kufanya biashara nchi jirani pamoja na nchi yote ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Rukwa, ukitaka kusafirisha bidhaa kuzipeleka Dar es Salaam ambako ndiyo soko kubwa la ulaji wa bidhaa zinazotoka katika Mkoa ule, ni kilomita karibu 1,200, 1,300 kwa kuzingatia unatoka sehemu gani lakini Rukwa kwenda katika nchi ya Zambia ni kilomita chache tu, ukitoka Sumbawanga pale ni kilomita 76, umeshafika nchi ya Zambia, kilomita karibu 95 umeshavuka mpaka unaingia katika nchi ya Zambia unafika mji wa Mbala, ukitoka Kasanga unavuka Ziwa Tanganyika unaingia Congo. Hivyo, nchi hizi zilizo karibu na sisi ndiyo nchi ambazo tunafanya biashara nazo vitu vya kawaida tu kama kuuza mahindi, maharagwe na mazao mengine kama mafuta ya alizeti na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilio cha wananchi wa Mkoa wa Rukwa, ni Wizara hii kusaidia kuwaelimisha wafanyabiashara na wananchi ili waweze kuzalisha zaidi ili tuweze kufanya biashara na nchi hizo jirani. Lakini ni jambo gani ambalo Wizara hii imeweza kuwekeza au kusaidia wakulima au kuwasaidia wafanyabiashara katika eneo hili la nchi ya Tanzania ili waweze kufanya biashara inayoweza kuwasaidia kupata mapato zaidi? Kwa kweli ni kiasi kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi cha miaka saba ambayo mimi nimekuwa Mbunge, eneo la mpakani na nchi ya Zambia kituo cha Kasesya, ni mahali ambapo Wazambia huwa wanakuja kununua bidhaa za Tanzania, kama ilivyo Tunduma. Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa miaka yote hii wameniahidi kwamba watakuja kujenga soko la kisasa pale. Alikuja Elvisi Msiba mwaka 2003 akatoa pale fedha karibu shilingi elfu nne ili maandalizi yaanze kwa ajili ya kujenga soko la pale lakini mpaka leo Wizara hii imenisaidia nini...

NAIBU SPIKA: Umesema elfu nne? (*Kicheko*)

MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA: Mheshimiwa Naibu Spika, shilingi milioni nne, *sorry*, ilikuwa ni dola elfu nne. Ni shilingi milioni nne kwa ajili ya kujenga Kituo cha Kasesha kiwe ni kituo cha biashara kwa ajili ya wafanyabiashara wanaotoka Mkao wa Rukwa na wafanyabiashara wanaotoka nchi ya Zambia, ili waweze kukutana pale waweze kufanya biashara. Kwa sababu mwaka 2000, nilipoingia kama Mbunge, eneo hili wafanyabiashara walikuwa wanakuja wanatandaza biashara zao chini, wengine wanatundika kwenye kamba, tukazungumza na viongozi mbalimbali, wakasema watajenga mahali ambapo wafanyabiashara watakuja kuweka bidhaa zao sehemu ambayo ni salama. Ng'ombe walikuwa wanachinjwa katika mazingira machafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri imejitahidi, imejenga kituo cha kuchinjia mifugo pale na kujenga vyumba 12 vya kuuzia nyama baada ya kilio cha wenzetu wa Zambia ambao hawakutaka kununua tena mifugo kutoka kwetu kwa sababu ya hali hii ambayo hairidhishi. Lakini Wizara imetusaidia vipi ili kuweza kujenga soko hili ili liweze kuvutia walaji kutoka nchi ya Zambia kuja kununua vitu? Hakuna chochote. Mpaka leo wananchi au wafanyabiashara wanaokwenda pale wanatandaza bidhaa zao chini. Ni jambo la kusikitisha na tujue kwamba nchi ya Zambia inategemea bidhaa nyingi za madukani kutoka Tanzania ili kuweza kuuza kwa matumizi mbalimbali. Lakini tumeshindwa kuchukua *opportunity* hiyo ili tuweze kuuza zaidi. Vipo viwanda ambavyo vimeanza kushamiri pale Sumbawanga katika Mkao wa Rukwa na Mpanda, kiwanda cha *Ernery Milling* ambacho sasa kinasindika unga wa mahindi na wanauzu nchi ya Zambia wanauzu hata katika miji mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipo Kiwanda cha Safi, ni kiwanda cha Nyama na viwanda vidogo vidogo vya kukamua mafuta ya alizeti. Lakini viwo viwanda vingine vidogo vidogo kule Mpanda ambavyo vinasindika asali na inauzwa nchini Ujeruman. *SIDO* inajitahidi sana kuwafundisha wananchi stadi mbalimbali ili waweze kuijendeleza lakini bado naona haitoshi kwa sababu wanahitajika waweze kwenda zaidi vijijini wawasaidie wananchi waweze kusindika bidhaa zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala la Stakabadhi ya Mazao Ghalani. Mkao wa Rukwa umeingia katika mpango huu kama ilivyo katika Mikoa ile inayozalisha korosho. Kwa bahati, tulipoanza mwaka jana mpango huu wa Stakabadhi wa Mazao Ghalani, mfuko haukutuwezesha kiasi cha kutosha ili tuweze kuwekeza kwa muda mrefu. Mpango

haukuwa mzuri wa kuwanufaisha vizuri wakulima katika Kijiji cha Matai ambapo ndiyo stakabadhi hii imeanzia. Tunaomba Wizara hii itusaidie ili wananchi waweze kutunza mazao yao katika hali nzuri na ikiwezekana mazao haya yawekewe dawa ili yasiharibikie ghalani halafu kesho na keshokutwa wanapokwenda kutaka kuyauza wanasema mahindi yameharibika au mazao yenu yameharibika, haileti maana ya Stakabadhi ya Mazao Ghalani. Hivyo, tunaomba Wizara hii itusaidie mfuko huu uweze kutupatia zana zinazohitajika ili tuweze kuboresha mazao yale yanayowekwa katika ghalaj. Ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kuhusu bidhaa bandia ambazo zimeenea mno katika nchi yetu hii ya Tanzania. Ni jambo la kusikitisha sana, bidhaa bandia zimejaa sana katika soko la Tanzania, maduka mengi yanauzu bidhaa hizi. Tunaomba tuwashukuru sana wahusika ambao wanazikamata hizi bidhaa bandia na kuziharibu kwa sababu athari za bidhaa hizi bandia mfano vifaa vya umeme, kama nyaya, zinasababisha nyumba nyingi kuungua na wananchi wengi hawaelewi ndiyo maana wanaendelea kuzinunua kwa sababu ya bei yake rahisi, lakini athari zake ni nyumba kuja kuungua kwa sababu zile nyaya haziwezi zikahimili umeme wetu huu ambao una-*fluctuate* yaani unapanda na kushuka. Hivyo, tunaomba chombo kinachohusika na kukamata hizi bidhaa bandia wahakikishe huko zinakotengenezwa haziletwi katika nchi yetu ili kuwanusuru Watanzania wasitumie bidhaa ambazo sio nzuri na badala yake tunaingia katika matatizo ya kuharibikiwa nyumba zetu kuungua na vifaa vya umeme na vifaa vya *electronic* navyo kuharibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka 20 iliyopita, Viwanda vya Zana za Kilimo (UFI) pale Dar es Salaam pamoja na kile cha Zana za Kilimo Mbeya, walikuwa wanatengeneza majembe ya kukokotwa na ng'ombe na majembe ya mkono kwa ajili ya wananchi katika nchi hii lakini viwanda hivi vimekufa vyote, Wizara hii inafanya nini? Kweli hivi ni busara tuendelee kununua majembe ya kukokotwa na ng'ombe pamoja na majembe ya mkono kutoka China au kutoka nchi za mbali? Hivi kweli nchi hii hatuwezi kuhimiza tukapata wawekezaji wakaja wakawekeza tukatengeneza majembe haya hapa hapa nchini kuliko kuagiza nje? Ni fedha kiasi gani tunazopoteza kwa ajili kununua majembe kutoka nchi nyingine? Kwa kweli, ni jambo la aibu, ni lazima Serikali itusaidie, Wizara hii itusaidie tupate majembe ambayo yanatufaa sisi wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Phosphate Minjingu*, ndio wamepewa jukumu la kusambaza mbolea nchi nzima. Lakini je, kweli watatosheleza kufika Rukwa, Mbeya, Songea na sehemu nyingine ambapo tunahitaji mbolea nyingi sana? Lakini mbolea ya *phosphate* ipo Mpanda, imeshafanyiwa uchunguzi na inaweza kuchimbwa pale. Wizara hii inatusaidia vipi tupate wawekezaji? Mkoaa umeshatoa tayari kitabu chake ambacho wamesema:

“*Growth and Prospect of Rukwa Region, Constraints and Opportunities*,” ambacho kilitolewa katika mkutano ule wa wawekezaji. Sijui kama Wizara hii ina kitabu hiki na inajua *opportunity* zilizoko pale na jinsi ya kutusaidia tupate mbolea pale pale ili tuweze kuboresha kilimo na tuweze kuzalisha zaidi kwa ajili ya nchi hii. Kwa kweli ni

jambo la kusikitisha kabisa, hakuna mawasiliiano, hakuna mwingiliano wa mipango na takwimu hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vya samaki katika ziwa Tanganyika. Ziwa Viktoria kule wanazalisha samaki wengi wanauzwa nchi za nje lakini Ziwa Tanganyika kuna samaki wengi na wazuri na ziwa lile halijawa *polluted*, lakini samaki wanavuliwa wanapelekwa Zambia kwa sababu hakuna chochote kinachofanyika na Wizara yetu.

Wapo wananchi wachache wameanzisha shughuli za uvuvi pale na kuanza kusindika lakini bado wanahitaji msaada wa Wizara hii ili waweze kuzalisha zaidi, watumie zana bora katika uvuvi, lakini na viwanda hivi viweze kujandaa kuweza kuza nje. Lakini hatuna mabenki kwa ajili ya kuwasaidia wafanyabiashara na wakulima katika mkoa wa Rukwa. Ni kweli kama Rais, alivyosema, benki sio rafiki wa masikini, benki si rafiki wa wakulima wadogo wadogo, tunaionba Wizara hii ikishirikiana na Wizara ya Kilimo na Wizara nyingine, tuanzishe benki ya wakulima ili waweze kupata mikopo ya kundeleza kilimo na uvuvi Rukwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi hii, naunga mkono hoja.

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii na mimi nitoe mchango wangu kidogo katika hoja hii iliyoko mbele yetu. Sio vibaya na mimi nikamshukuru Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii pamoja na watendaji wake wote na hasa kwa vile Waziri mwenyewe ni mpole sana ambaye tunamtegemea atupe majibu mazuri sana. Lakini nampongeza zaidi Msemaji wa Kambi ya Upinzani, kwa hoja nzito alizoibua ambazo zinapaswa kutolewa majibu sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo na mimi ningependa nianze kuchangia jambo la kwanza na nianze na hii inayoitwa bajeti finyu. Huu ufinyu wa bajeti umekuwa ni mno sasa. Wakati akiwasilisha maoni ya Kamati ya Bunge ya Viwanda na Biashara, Mwenyekiti wa Kamati hii katika ukurasa wa saba alizungumzia kwamba hizi shilingi bilioni 48 zinazoombw na Wizara hii ni kidogo, kwa hivyo ni bajeti finyu.

Tulipozungumzia hotuba ya Wizara ya Nishati na Madini, shilingi bilioni 362.9 Mheshimiwa Waziri alilalamika ni bajeti finyu hazitoshi. Tulipozungumzia Wizara ya Kilimo, shilingi bilioni 113.7 Mheshimiwa Waziri alilalamika ni bajeti finyu hazitoshi, sasa huu ufinyu wa bajeti umekuwa mkubwa mno. Mwaka juzi Wizara zote tulilalamika bajeti finyu, mwaka jana bajeti finyu, mwaka huu bajeti finyu, si hasha na mwakani tutakuja kuambiwa bajeti finyu, kila Wizara italalamika bajeti finyu, huu ufinyu kila siku utakuja kuwaje?

NAIBU SPIKA: Hata nyie Waheshimiwa Wabunge, mnasema hivyo hivyo!

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge pia ni kweli huwa tunasema bajeti finyu. Sasa nini cha kufanya? Mimi nadhani hili suala la ufinyu liondolewe. Ni lazima Serikali iwe na mipango madhubuti ya kutenga fedha za kutosha. Pale wataalamu wanapolalamika Wizara nyingi

mno, ina maana kama hii na sasa ndio tunaiona. Sasa basi nini cha kufanya? Zibakie Wizara hizo hizo, lakini hebu tuweke vipaumbele.

Tuchukue Wizara ya Nishati na Madini, tuipe bajeti ya kutosha, tuchukue Wizara ya Biashara na Viwanda tuipe bajeti ya kutosha, tuchukue Wizara ya Kilimo tuipe bajeti ya kutosha, halafu tuchukue na Miundombinu tuipe bajeti ya kutosha. Mwaka 1980 tuliambiwa tufunge mkanda ambao mpaka leo hatujaambiwa tufungue. Katika suala hili basi na tufungeni mkanda tuzishughulikie hizi Wizara nne ambazo ni Wizara nzito za kuinua maendeleo ya nchi hii, tujifunge mkanda, baadaye tukifanikiwa huku tutakwenda nyingine, lakini hili suala la ufinyu wa bajeti, kila siku bajeti finyu nafikiri tungelifanyia maarifa yoyote likaondoka. Kupanga ni kuchagua.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ambalo ningependa kulizungumzia, kuna kitu kinachoitwa viwanda mama. Mara zote kila tunapozungumzia viwanda mama huwa tunamaanisha ni viwanda vile vya mkaa wa mawe wa Mchuchuma na chuma cha Liganga. Kila tukizungumzia viwanda mama, basi panakuwa na Mchuchuma na Liganga. Lakini hii historia ya Mchuchuma na Liganga imeanza zamani sana na inajulikana toka mwaka 1896 na tafiti nyingi zimefanya kabla ya uhuru na baada ya uhuru. Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 1995 – 2000, 2000 - 2005, 2005 - 2010, zote zinazungumzia Mchuchuma na Liganga. Lakini ni nini tumefanya mpaka leo? Hizi tafiti ziko zilizofanyika 1977 na 1978 za Shirika la Ujerumani GTZ, ziko tafiti za 1995, ziko tafiti zilizofanyika 1997 kampuni ya *CMPD* ya India, *NDC* imefanya tafiti nyingi, sasa kitu gani mpaka leo hizi tafiti hazijakamilisha Liganga na Mchuchuma? Ukurasa wa 22 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Viwanda, wa 22, 23, 24, wote anazungumzia viwanda mama, Mchuchuma na Liganga.

Lakini Waziri amediriki kutueleza kwamba tayari kuna wawekezaji 81, kati ya hao wawekezaji 38 katika masuala ya chuma na wawekezaji 43 katika mkaa wa mawe na kuna makampuni 10 ambayo yameshathibitisha nia yake ya kuwekeza. Sasa ni nini tunachokisubiri? Mheshimiwa Waziri, hebu ukija kufanya majumuisho yako utueleze hizi ni tafiti gani zilizobakia? Kitu gani kilichobakia? Makampuni gani hayo yanayotakiwa? Hayo yote yaliyojitekeza? Sio mwaka huu tu, mwaka juzi wawekezaji walikuwepo, miaka mitano nyuma wawekezaji walikuwepo, lakini kila siku tunasonga mbele, tunataja viwanda mama vya Mchuchuma na Liganga. Hebu tuelezwe wakati wa majumuisho kitu gani kinachokwamisha? Sasa tatizo ni nini hasa? Tuelenze wazi wazi Bunge hili lije!

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la viwanda vingine, kuna viwanda vingi ambavyo vimebinafsishwa, hotuba ya bajeti katika *Hansard* mwaka jana tunaelezwa kwamba 97.6% ya viwanda hivi vinamilikiwa na sekta binafsi. Mwaka huu hotuba ya bajeti tunaambiwa 97% vinamilikiwa na sekta binafsi na Wizara imefanya tathmini ya kutosha, lakini hiyo tathmini mimi nasema haijakamilika. Ni tathmini gani hiyo iliyofanya isitujulishe mambo yafuatayo: kwanza, katika hivi viwanda vilivyobinafsishwa tunataka kujua ni vingapi vilivyobinafsishwa na vingapi vinafanya kazi na vingapi havifanyi kazi? Hivyo vilivyobinafsishwa vimeongeza ajira kwa wananchi wetu kiasi gani au wananchi wetu wamekosa ajira kiasi gani? Kwa sababu lengo la kubinafsisha hivi viwanda ni *development* na ajira kwa watu wetu na kuongeza

pato la Taifa. Sasa sisi kwa kumbukumbu tulizonazo kuna viwanda vingi sana viko Arusha, viko Moshi, viko Dar es Salaam, ambavyo havifanyi kazi na vimebinafsishwa.

Kuna mfano wa *Steel Rolling Mill* ya Tanga, tuna taarifa hakifanyi kazi. Kilipobinafsishwa ilikuwa ni *furnace* tu ndio iliyokuwa mbovu. Hivi sasa imeng'olewa mpaka *panel* yote. *Mkata saw mill*, matrekta yalikuwa yanafanya kazi, mashine zinafanya kazi, jenereta inafanya kazi na hivi sasa ni *scrape*. Sasa tukiambiwa viwanda vinabinafsishwa, yaani ukichukua watu wa *auction* ya kawaida, wewe ukinunua kitu katika *auction* utaambiwa ulipe 25% pale na 75% zilizobakia ulipe labda baada ya wiki mbili.

Leo *PSRC* tunabinafsisha halafu Mheshimiwa Waziri aliwahi kutujibu mwaka jana hapa kwamba kitu ukishabinafsisha umeuza. Kwa hiyo, ametumia, ndivyo hakutumia, basi, hilo ndilo lengo la Serikali? Ikiwa watu wa *auction*, basi kama hujawalipa wiki mbili zilizobakia, basi ile 25% uliyomlipa siyo yako. Lengo la kubinafsisha ni kwamba vifanye kazi, haiwezekani tubinafsishenye viwanda halafu visifanye kazi. Haya matatizo yanababishwa na nini? Haiwezekani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi vile vile ningependa nijue kule hiki kiwanda kinachopigiwa makelele cha *General Tyre*, ambapo ule mpira ulioko visiwani Pemba, Unguja, Kihuhwi, wafanyabiashara sasa hivi imebinafsishwa, wanakwenda kuuza, mpira bora ifanyiwe *chewing gum* kuliko *General Tyre* kupata spare. Kuna nini *General Tyre*? Hebu tueleze Mheshimiwa Waziri, huyu Mwenyekiti wa Bodi ya *General Tyre* kuna taarifa kwamba kajiu zulu. Hebu tupatieni sababu leo za kujiuzulu Mwenyekiti wa Bodi ya *General Tyre*, tuelewe ni kitu gani kilichotendeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile Waheshimiwa Mawaziri, mara nyingi sana kila wakieleza hotuba zao hapa wanasema kwa mujibu wa Ilani ya Uchaguzi ya *CCM*, sasa na mimi nataka niitumie leo ilani ya uchaguzi ya *CCM* na naomba niinukuu. Kwa mujibu wa ilani ya uchaguzi ya *CCM* ukurasa wa 100 na ukurasa wa 101, naomba niinukuu: "Sekta ya Biashara na Viwanda. Kwa kuzingatia kwamba Zanzibar ni visiwa na vinakabiliwa na tatizo la ufinyu wa ardhi, shughuli kubwa za kiuchumi zinahitaji kuelekezwa kwenye viwanda na biashara kwa lengo la kuimarisha na kuendeleza shughuli hizo katika kipindi cha mwaka 2005 mpaka 2010." Inakaribia miaka mitatu inakwenda hiyo: "SMZ chini ya CCM itatekeleza yafuatayo." Sasa nasoma kipengele cha (d). "Kuendeleza jitihada za kuanzisha viwanda vinavyozalisha ajira nyingi kama vile vyta nguo na kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na sekta binafsi." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Waziri, mimi nilitaka unifafanulie katika majumuisho yako mpaka sasa hivi Wizara yako kwa mujibu wa Ilani ya Uchaguzi hii kifungu (d) ukurasa 101. Hii Serikali ya Muungano imesaidia nini? Imeshirikiana vipi na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuendeleza viwanda hivyo vyta nguo vilivyotajwa kwa kuinua uchumi kwa kuzingatia hali ya uchumi wa Zanzibar? Ukija uje utufafanulie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamezungumzwa suala la *SP Mgololo*. Hili ni suala zito na tungependa Mheshimiwa Waziri atuletee majibu haraka kwa sababu mkataba ule wa uuzaaji wa Serikali kupata dola 1,000,000/= na dola 22,000,000/= zikaenda kwa mwekezaji kwa ukarabati wa kiwanda na dola 3,000,000/= pia zikaenda kwa mwenye kiwanda ni kitu cha ajabu kwa sababu hata mitaani kule wale walio na magereji mtu anaweza akanunua gari bovu akaamua kutoa mpira mmoja mmoja akaiza na akitahamaki, basi akiuza *scrape* zote za ile gari amepata faida kuliko tulivyofanya sisi.

Kwa hiyo, pale Mgololo ina maana sisi tungeuza mashine moja moja wale wanaonunua vyuma chakavu tu, basi tungepata zaidi ya hizi pesa zilizotajwa katika mkataba huu. Haiwezekani iwe Serikali ipate Sh. 1,000,000/= tu, tungeuza tairi moja moja, tungeuza vile vyuma chakavu, zile mashine tusingetumia vyovyote tukawauzia hawa wanunuzi wa vyuma chakavu, basi tungepata pesa zaidi ya hivi, acha mashamba yaliyopo, ma-estate yote na ukubwa wake, hekta chungu nzima, nyumba zilizopo, halafu iwe tunaambiwa hivyo. Tuelezwe kuna nini au vinginevyo Kambi ya Upinzani haitaridhika na suala hili. Baada ya kusema haya machache nashukuru. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kutoa mchango wangu katika Wizara yetu hii ya Viwanda na Biashara. Naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, dada yangu Mama Nagu kwa uzoefu alikuwanao wa uongozi katika Serikali, Wizara mbalimbali, amewasilisha vizuri hotuba ya bajeti ya Wizara yake hapo jana. Pia, nampongeza Naibu Waziri, kaka yangu Dr. Cyril Chami, kwa ushirikiano mzuri anaompa Mheshimiwa Waziri na sisi Wabunge na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia, naomba nimpongeze Katibu Mkuu wa Wizara hii, Bibi Taksi kwa kushirikiana na Wakurugenzi wake kuiandaa vizuri bajeti ya Wizara yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nami nianze kwa kunukuu aya ya 29 ukurasa wa 20 na 30. Katika aya ya 29 katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri anasema: "Katika mwaka 2007/2008 kati ya miradi ya viwanda 194 iliyopewa *certificate of incentives* 32% ya miradi hiyo ilihusu kuongeza thamani mazao ya kilimo na mifugo." Mwisho wa kunukuu aya ya 29. Aya ya 30 inasema: "Wizara itatoa taarifa ya kina kuhusu hali ya viwanda vilivyobinafsishwa mara baada ya zoezi la uperembaji kukamilika. Zoezi hili linatarajiwa kukamilika katika mwaka wa 2008/2009." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naiomba Serikali katika uperembaji huu itakapofika katika Kanda ya Kusini watuorodheshe na sisi pale Mkoo wa Ruvuma. Tuna kiwanda cha tumbaku pale Songea. Kiwanda hicho kilikuwa kinamilikiwa na vyama vyaa ushirika vyaa Songea na Namtumbo, *SONAMKU Cooperative Union, Songea Namtumbo Cooperative Union*. Kiwanda hiki wakati ule wa sera ya ubinafsishaji na soko huria ilipofika alitokea mwekezaji ambaye alipewa 40% kuwekeza kwa makubaliano ya kwamba ataendeleza kiwanda kile, lakini mwekezaji huyu aliyepewa 40% imeonekana kwa zaidi ya miaka 11 amekuwa ni *dormant share holder*. Hajafanya kama

walivyokubaliana na kuvifanya vyama vile vy a ushirika kupata hasara kubwa na sasa havina fedha ya kuendeleza kiwanda kile.

Kwa hiyo, kuna wawekezaji ambao wanajitokeza waliokuwa *serious* kuendeleza kiwanda kile, lakini wanashindwa kuingia kwa sababu ya kikwazo cha mwekezaji huyu, *a dormant share holder* kusinzilisha kiwanda kile, sasa wanashindwa ni jinsi gani ya kuingia. Kwa hiyo, tunaomba katika uperembaji huu Serikali ikiorodheshe kiwanda kile ione ni jinsi gani ya kuweza kumwondoa muwekezaji huyu na kuendeleza kiwanda kile.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna hasara kubwa sana tunayoipata kama Mkoa wa Ruvuma. Kwanza kabisa ni mkulima mwenyewe wa zao lile la tumbaku, anagharamia *indirect* kuisafirisha tumbaku ile toka Namtumbo, toka Songea mpaka Morogoro kwenye viwanda vy a tumbaku. Kwa hiyo, inamgharimu katika uzalishaji wake, pia Mkoa unakosa mapato. Mpaka kiwanda kile kinasimama mwaka 2005/2006 kilikuwa kinaajiri watu 3,200 na 80% ya wakazi wa Songea walioajiriwa pale walikuwa ni akina mama na kiwanda kile katika mwaka ule kilikuwa kinalipa Sh. 96,000,000/= kwa mwezi, mishahara kwa wale walioajiriwa pale vibarua. Kwa hiyo, ukitizama kwa ujumla ni hasara kubwa tunayopata sisi wananchi wa Mkoa wa Ruvuma katika Wilaya hizi mbili zinazolima tumbaku kwenye Wilaya ya Songea na Namtumbo.

Lingine ni *TRA*, ilikuwa inakusanya fedha za kutosha, kampuni ya maji ilikuwa inakusanya fedha za kutosha, *local transporters* pale walikuwa wanapata pesa za kutosha kwa sababu sasa hivi inachukuliwa kutoka huko inasafirishwa moja kwa moja na wale wasafirishaji kutoka nje ya Mkoa wa Ruvuma. Lakini wakati kiwanda kinafanya kazi, wale *local transporters* walikuwa wanasafrisha tumbaku hiyo. Pia kubwa zaidi, mabaki ya tumbaku ile wakati kiwanda kinafanya kazi yalikuwa yanatumika kama mbolea ili kupunguza gharama ya mbolea ya chumvi chumvi.

Kwa hiyo, nilikuwa nazungumzia umuhimu wa jinsi gani sisi Mkoa wa Ruvuma tulivyopata hasara, tunaomba Serikali kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara iingize kiwanda hiki katika uperembaji tuone ni jinsi gani ya kumwondoa huyu na kuingiza muwekezaji mwingine, ili kuweza kukuza uchumi wa watu wetu tunaiomba sana Serikali ifanye hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, naomba pia ni-*quote* aya ya 74 ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Katika aya ya 74 ya hotuba yake amesema: “Wizara imekamilisha maandalizi ya mkakati wa kuongeza uzalishaji na kuuza mazao nje, uelekeo wa mkakati huu ni kutatua changamoto na uzalishaji, kuongeza mauzo ya bidhaa, zilizoongezwa thamani, kujiimarisha katika masoko yenye masharti nafuu, masoko ya kikanda, masoko ya upendeleo. Kwa kuanzia mkakati huu umebainisha maeneo yanayoweza kutekelezwa kwa ufanisi mkubwa na kuleta matokeo ya haraka, quick wins, maeneo yafutayo yamebainishwa,” nitazungumzia maeneo ambayo ni ya sekta ya kilimo. Sekta ya kilimo ameyataja korosho, pamba, kahawa, chai, matunda, maua na mboga mboga.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ni-*declare interest* kwa mujibu wa kanuni ya 61(1) kwamba mimi ni Mwenyekiti wa Bodi ya Tumbaku Tanzania. Sasa nitazungumzia

suala la tumbaku kwa sababu katika mazao makuu yanayosaidia uchumi na ukuaji wa uchumi wa nchi yetu, tumbaku ni zao muhimu sana lakini katika mkakati huu tumbaku imeachwa. Kwa hiyo, naomba nizungumzie suala hili, naomba niikumbushe Serikali kuhusu umuhimu wa tumbaku katika ukuzaji na uondoaji umasikini wa nchi yetu. Tumbaku inategemewa kwanza na familia 500,000 ni sawa sawa na 1.3%...

NAIBU SPIKA: Unataka kusema sigara au tumbaku?

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, tumbaku.

NAIBU SPIKA: Kwa sababu tumbaku iko Kilimo, sigara iko kwa hawa.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, ndio nataka kueleza kwa sababu katika sekta ya kilimo katika yale mazao makuu, sigara inatokana na tumbaku na sigara ndio *product* ambayo inatokana na tumbaku lakini inachangia sana pato la Taifa. Ndio maana nilikuwa nazungumzia suala hili na katika sekta hii nimesema katika kilimo yametajwa mazao yote yale makuu pamba, korosho, kahawa, na kadhalika, tumbaku haikutajwa katika mkakati huu.

Kwa hiyo, nilikuwa nataka kueleza umuhimu wake. Pia katika haya mazao makuu imekuwa ya pili ama ya kwanza katika uchangiaji wa pato la Taifa kwa 16.7% na pia imeiingizia Serikali wastani wa bilioni 80 kwa fedha za nje. Hii inachangia pato la Taifa na pia kuondoa umasikini. Pia, kodi za ndani imelipa, kwa mfano kampuni ya sigara imelipa mwaka jana bilioni 90 na ili *i-comply* na *Tanzania Revenue Authority Regulations* na kuwa ya kwanza kwa kulipa kodi.

Kwa hiyo, ina umuhimu sana katika kuwepo katika mkakati huu wa kuondoa matatizo yanayoendana na uzalishaji wa zao hili la tumbaku. Kwa hiyo, nilikuwa ninaiomba Serikali, iingize zao hili la tumbaku katika mkakati huu kwa sababu Mikoa 10 na Halmashauri 22 zinalitegemea zao hili na kila mwaka wanaingiza wastani wa bilioni nne katika Halmashauri hizo. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana, kwa kuwa mchango huu mkubwa wa tumbaku katika kukuza na kuondoa umasikini katika pato la Taifa, unastahilisha sekta hii ya tumbaku kupewa kila aina ya *support* ili kukuza na kuchangia zaidi mauzo ya nje na pato la Taifa na maendeleo kwa wananchi na wakulima wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nataka kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofî*)

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa siku hii ya leo, lakini pia nashukuru sana kwa jinsi ambavyo bajeti hii imewasilishwa kuitia Waziri wake, Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, pamoja na Naibu wake Dr. Chami, pamoja na watendaji wake wakuu. Nimefurahi zaidi kuona kwamba bajeti hii ambayo uongozi wake mkubwa uko mikononi mwa akina mama, imesifiwa na kuonekana imewasilishwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu hasa utakuwa katika masuala ya teknolojia na jinsi ambavyo inaweza kuhamishwa kuwafikia watumiaji. Kwanza kabisa, napenda kushukuru sana taasisi yao ya *TIRDO* kwa jinsi ambavyo imewezesha wananchi wa Mkoa wa Ruvuma hususan akina mama, walemaru na wanaoishi na virusi vya *UKIMWI* kuweza kuongeza vipato vyao kwa kilimo cha uyoga.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona kwamba niyaseme hayo, ukweli ni kwamba Tanzania haina haja ya kuwa masikini kwa sababu utaalamu upo, rasilimali zipo na hata malalamiko mengine sio ya lazima. Mimi sitaweba kusema kwamba bajeti hii niilaumu kwamba haitoshi kwa sababu ndio hali halisi. Japo naona kuna umuhimu wa kuzisaidia hizi taasisi ambazo zinawaendeleza wananchi hasa hawa mmoja mmoja ikiwemo *SIDO*, ikiwemo *CARMATEC*, *TIRDO* na wengineo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudi katika hili suala la teknolojia *TIRDO* pale Dar es Salaam wana uwanja mkubwa sana, wana majengo ambayo hayajakamilika, lakini pia walikuwa hawana hati, nashukuru kwamba Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, juzi ile amesema kwamba sasa wanaweza wakalipia ardhi yao na atakuwa tayari kuwasaidia, nashukuru sana. Naamini kwa kuwa *TIRDO* iko chini ya Wizara hii, basi itachukulia suala hilo kwa msisitizo mkubwa na kuhakikisha kwamba haya yanatekelezeka mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naona kwamba kwanini eneo lile la *TIRDO* lisiwezeshe kuwa ni kituo cha teknolojia ambayo, sio teknolojia katika misingi ya utafiti peke yake lakini tunaweza tukatengeneza kukawa kama ambavyo tunaona kule kwenye maonesho ya Saba Saba kwa mfano, watu wanakuja wanafanya maonyesho mbalimbali.

Basi katika masuala haya ya teknolojia mbalimbali hizo mashine ambazo tunazzungumzia zingeweza kuwekwa pale ikawa kwamba mtu akihitaji kupata teknolojia mojawapo kwa ajili ya kumsaidia kuongeza thamani ya mazao yake ingekuwa ni rahisi kwenda mahali kama pale na kuweza kupata jibu na kwenda kulifanyia kazi. Lakini unakuta hawa wajasiriamali mmoja mmoja inakuwa kwao ni ngumu sana kupata taarifa inayowawezesa wao kwenda hatua inayofuata. Ukitaka taarifa mpaka umfahamu mtu au mtu akubonyeze labda umwone fulani na mara nyingi unapata taarifa ambayo haijakamilika. Kama mimi *Engineer Stella Manyanya* na Ubunge wangu nashindwa kufahamu mpaka sasa hivi nikitaka mashine za ku-process uyoga nazipata wapi: Je, huyu mwingine ambaye hana mawasiliano, anafanyaje?

Kwa hiyo, naomba basi tuanzie na mifano kwa wale ambao tayari wameshakuwa *pro-active*. Mkoa wa Ruvuma walianza kufundishwa tarehe 11 Juni, 2007 kilimo cha uyoga, lakini sasa hivi tayari tuna wakulima 800, mbio za mwenge zilishuhudia wakati zimekuja Ruvuma, 800 ambao wana uwezo wa kulima uyoga. Lakini kikubwa zaidi ni kwamba kilo moja ya uyoga inauzwa Sh. 4,000/= na mkulima mmoja hata yule mzee kabisa anaweza akalima kwa sababu hatumii nguvu, analima akiwa amependeza. Mheshimiwa Mama Mongella, nimemwonyesha wale kina mama wanafanya kazi zao kwa uzuri na kuweza kujingizia kipato mpaka Sh. 100,000/= kwa mwezi, huyu ni mzee. Lakini wale vijana vijana wanakwenda mpaka Sh. 400,000/=, lakini tunabaki

tunalalamika kwamba, ooh, Kenya! Sisi tutakaa tunawazungumzia wenzetu mpaka lini? Tunataka sasa tuzungumzie yetu kwa vitendo kwa sababu uwezekano upo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi naomba kama Wizara hii iko *serious* haitoshi kutufundisha tu namna ya kulima, tunataka kupata *vertical growth* kwa maana kwamba tumeanza kulima kidogo kidogo, tunataka tuuze sasa kwa kilo nyingi na soko tunalolihitaji sisi, hatutaki kuanzia soko la nje. Kwa nini tuuze nje wakati soko la ndani halijajitosheleza? Mpaka sasa hivi hatujaweza hata kuuza nje ya Mkoa wa Ruvuma, tunauza pale Ruvuma na watu wanapata hizo pesa. Kwa nini nikahangaike kuuza mbali wakati hata pale ndani sjatosheleza soko?

Kama watu wanaotoka Mataifa mengine wanagundua soko lao hapa Tanzania kwa sisi tusione kwamba ndiyo tuna soko? Watu milioni 38 tunashindwa kutosheleza soko letu? Sisemi kwamb bidhaa za nje zisifike, zifike tu zipate ushindani lakini zitapata ushindani wa kweli, itakapotokea hawa wa ndani nao wamewezeshwa kuwa na kitu ambacho kina-*counter* ile *product* ambayo inatoka nje, lakini hakuna! Hata tukisema tuwazuie, jamani msiuze matufaa, yaani *apples* hizi zinazotoka nje, huwezi kuwakataza kwa sababu inabidi useme *alternative* unapomkataza asiuze hicho, una nini cha kumpa? Kwa hiyo, naona ipo haja ya kusositiza sasa kwamba teknolojia tulizonazo zisikae kwenye maabara, ziende zikatumike.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nisingependa kwenda nje ya zao hili la uyoga. Bahati nzuri sisi tumeshapata eneo kubwa tu la kuweza kuweka Chuo chetu hicho cha ujasiriamali pamoja viwanda vidogo vya uyoga. Tunachoomba, basi mtuunganishe kwa sababu hata tukisema kwamba teknolojia nyingine tusizitoe nje, hapa hakuna. Sasa tunafanyaje? Mimi nasema tuanze hizo hizo kwa sababu mjasiriamali sio lazima kila kitu ugundue mwenyewe. Kama umeshindwa kutengeneza, basi *copy* na ndiyo wenzetu wanavyofanya. Kwa hiyo, ninachoomba tuwezeshwe kwa kuonyeshwa vilipo na ikibidi sisi tuwe kama mfano watujaribishe ili hata tunaposema kuna masoko ya Agoa yanayotaka kupata mazao mengi tuyasafirishe kwa wakati mmoja. Hii ndiyo njia pekee ya kuwawezesha hawa watu kwa sababu mtu mmoja mmoja ni vigumu sana kufikia soko kubwa.

Nimefika hapa Dodoma kwa kutambua kuwa pia Dodoma kuna wakulima wa uyoga, nimetembelea mashamba yao nikakuta kuna matatizo makubwa, watu walishafanya *investment* kubwa tu, kuna mabanda makubwa kabisa ya uyoga, uyoga upo pale lakini sasa wanaondoka vipi kuanzia pale? Unakuta hakuna anayewa-*support*. Kwa nini watu kama hao hawasakiwi? Tunabaki tunasema mipango kila siku mipango, hii tuliyonayo ni mingi sana hatujaimaliza kuifanyia kazi.

Kwa hiyo, ninashauri tuone kwanza hii tuliyonayo imetufikisha wapi? ama sivyo tutajikuta kila siku sisi tunafikiria jambo jipya tu kumbe hata lile dogo ambalo tunalo lingetuwezesha kuondoka pale tulipo na kutusogea mbali zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la uyoga, uyoga una faida nyingi. Uyoga ni rafiki wa mazingira kwa sababu uyoga unatumia taka. Sasa hivi ukiangalia Iringa

kuna *dust* zile zinazotokana na mbao nyingi sana ambazo zinafaa kwa kilimo cha Uyoga, kuna Michele baada ya kukoboa zile pumba zinafaa kwa ajili ya kilim cha Uyoga, Alizeti ukishakamua mafuta inafaa kwa ajili ya kilimo cha Uyoga, Mahindi na hata Maharage. Kwa hiyo, unaweza kuona tunaraslimali nyingi kiasi gani badala ya kutupa unazirudisha zinakuwa mali, sasa kwa nini tusifanye hivyo? Yote hayo wafadhili wamefanya wametufundisha lakini mwisho wake tunaseme aaaah! viyi unalima? ndiyo mimi nalima na ninajua kulima Uyoga lakini hafanyi hivyo.

Lakini pia Uyoga unarudisha heshima kwenye familia kule kwetu nimeona sasa hivi akina Baba na akina Mama wenyewe wanasikia kule mapenzi yamerudi kwa sababu mambo yale ya kuombana pesa ndogondogo yamekwisha kila mtu anasaidia kuchangia pato la taifa, lakini hata afya, Uyoga una afya unasaidia kurudisha virutubisho mwilini. Wale wagonjwa ambao kidogo ambao hali zao zina wasiwasilishi lakini hata mzima inakusaidia kurudisha afya ya mwili. Sasa ndiyo maana naongea kwa uchungu kumbe tunakosa vitu ambavyo vingetusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, basi kwa sababu nimeshafanya *promotion* sana, nadhani mmenisikia, nadhani mtanisaidia. Kama hili halitawezekana, basi bajeti inayofuata nitasema jamani hizi hadithi tuziache sasa kwa sababu hazitusogezi mbele.

Lakini la mwisho, nililokuwa napenda nilizingumzie pia kwa undani, ni heshima ya mjasiriamali au mfanyabiashara. Mara nyingi mfanyabiashara au yule aliyethubutu kufungua kazi ya kuweza kuzalisha ajira anachukuliwa tu kama mtu mbaya, anachukuliwa tu kwamba ni mwizi, anachukuliwa kama mtu ambaye hana thamani. Lakini ukiangalia Waheshimiwa Wabunge wote tumekaa tunakula pesa za wafanyabiashara, wajasiriamali ambao wanalipa kodi na ndiyo maana tunalamika kwamba bajeti zetu hazitoshi. Kwa nini? Kwa sababu wale wanaotakiwa kupeleka pesa kwenye huo mfuko tunaoutumia sisi kwa haya matumizi ya jumla wanakuwa hawajawezeshwa, mikono yao imekatwa.

Kwa hiyo, ninachoona ufanyike utaratibu maalum. Kuna kile chama ambacho ni cha wenyе lengo la kuwekeza kutoka Marekani yaani *TAIF* ambaо ni Waswahili wenzenetu. Mara ya mwisho nilivyokutana nao walizingumzia suala la kuweka *base* ya taarifa ambayo ile *base* ya taarifa inaweza kusaidia kabisa kuuza taarifa mbalimbali zilizopo nchini mwetu pamoja na kujua tuna wafanyabiashara wangapi, kila mtu anafanya nini kwa sababu kuchangia hili pato la Taifa siyo achangie tu mfanyabiashara au aliyeajiriwa, kuna watu ambao hawapo katika mfumo wa kuchangia hizi kodi zetu, lakini wana uwezo wa kusaidia kuongeza pato la Taifa hili ili bajeti zetu zikawa nzuri, lakini hawajulikani walipo, hawajulikani!

Tuna vitu vingi vya maliasili vimeorodheshwa viro humu kwenye nchi yetu, lakini havijulikani mpaka akifika mtu mwingine anasema mahali fulani nimevumbua kulikuwa na kitu fulani, unavumbua leo wakati hiki kilikuwepo siku zote! Ni kwa sababu taarifa hazipatikani.

Hata masuala ya nguo, mimi nasema tunarudi nyuma kwa sababu mimi ninavyofahamu kwa mfano sisi katika Wilaya yetu ya Mbinga tulianza kutengeneza nguo

siku nyingi kwa kutumia magome ya miti na siku ile akina mama watakapokuwa wanaonyesha mavazi yao mtaziona nguo zetu za asili kutoka Mbinga. Kwa hiyo, mpaka leo kama tunakuwa hatuna viwanda vya kutosha kutengeneza nguo ina maana tumerudi nyuma. Wale wa zamani waliweza wakafikiria hapo kuna mpaka viwanda vya kutengeneza chuma vilikuwepo wakati ule lakini sasa hivi havipo. Kwa nini?

Kwa hiyo, naomba kwa kweli Wizara hii ipewe msukumo kwa sababu inafanya kazi nyingi za utafiti kwa sababu ina uwezo wa katuondoa Tanzania kutoka kwenye umaskini tulionao kwa vitu ambavyo vinapatikana kirahisi. Kwa hiyo, hatuna sababu ya kulia na ninaona katika maeneo mbalimbali hata wenzetu wanapokuja kutusaidia kwamba fanyeni hiki unakuta wameshaona mbali tunasaini, ukishamaliza siku ya pili unajikuta tulikosea, basi kila siku sisi ni watu wa kukosea, kwa sababu gani? Mipango yetu inategemea sana mpaka mzungu kasema nini. Mpango ukianza kauleta Manyanya au mtu mwingine hapa hautiliwi maanani kwa sababu huu aha! Amesema nani? Kwanza ulisikia wapi hilo? Halipo! Akifika mwingine hata kama ni mtoto mdogo ooh! Unasemaje? *Yes, I think this is okey* bila kujali hicho kitu kina manufaa gani kwetu.

Kwa hiyo, mimi naomba Wizara hii akina mama mmekaa hapo na bahati nzuri wote mna elimu ya kutosha, kwa kweli tutawaunga mkono, nadhani bajeti itakayofuata itakuwa ni nzuri zaidi na itawawezesha kufanya kazi zetu kwa uzuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya. Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba kumbe alisema hatachangia, kwa hiyo, nina wasemaji hawa wafutao:-

Mheshimiwa Said Amour Arfi na Mheshimiwa Kaika Saning'o Telele tu. Mheshimiwa Arfi karibu!

MHE. SAID AMOUR ARFI: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha kunipa uhai, pia nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kawaida tu, sasa hivi imekuwa ni mazoea hotuba zinazowasilishwa ndani ya Bunge ni nzuri zinapendeza, zinavutia, zimeandikwa kwa ustadi mkubwa katika hilo la uandishi wa hotuba. Sina budi kupongeza sana kwamba hotuba kwa uandishi ni nzuri. Lakini ninayo mashaka mengi sana. (*Kicheko*)

Nakumbuka siku moja katika Bunge lako hili Tukufu Mheshimiwa Mbunge mmoja alinukuu vitabu vitakatifu akasema: "Wana macho, hawaoni, wana masikio hawasikii." Lakini kwa kawaida ya maneno haya ni sawa sawa na mtu ambaye anacheza mpira ukutani, vyovyote vile unapopiga mpira kwenye ukuta ule mpira ni lazima utakurudia. Kwa hiyo, ndiyo maana Mwalimu akasema kwamba, "Kupanga ni Kuchagua" (*Makofi*)

Lakini hata hivyo nampongeza sana Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake kuweka nukuu ya maneno aliyoyatamka Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete wakati anafungua Bunge katika ukurasa wa 104 naomba ninukuu. Mheshimiwa Rais alisema kwamba: "Uchumi wa nchi yoyote iliyoendelea ulianzia na kilimo na kisha kuwa wa viwanda." Naomba niishie hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba uchumi wa nchi yoyote iliyoendelea ni lazima uanzie na kilimo, kisha baadaye uende kwenye viwanda. Kila wakati najiuliza na ninaendelea kutafakari kwamba je, nchi yetu ni ya kilimo? Je, ni viwanda? Katika kulitafakari hili sana, napenda nimpongeze sana na nimshukuru Mheshimiwa Basil P. Mramba, aliweza kueleza katika Bunge hili, ni wapi tulipokosea. Alisema katika awamu ya kwanza na ya pili ya uongozi wa nchi hii kulikuwa na mipango madhubuti ya kuweza katuondoa na kutupeleka tunapokwenda, lakini ni namna gani tumepeze dira? Mimi sijui!

Ni kwamba sasa hivi hatujui kwamba nchi hii ni ya kilimo kwa sababu hatuweki mkazo katika kilimo. Ukiangalia, taarifa hii ya Waziri wa Biashara na Viwanda katika hotuba yake kwenye majedwali utakuta kwamba bado nchi hii imetumia fedha nyingi katika kuagiza chakula. Lakini katika kuagiza chakula mwaka 2006 imetumia *USD* million 249.2 na mwaka 2007 ilipanda kufikia 3001.3 katika jedwali Na. 5.

Lakini hapo hapo, utaona kwamba mbolea iliyonunuliwa, yaani manunuza kutoka nje kwa mwaka 2007 ni milioni 59.2. Ni dhahiri kwamba hatuna umakini sana kwamba tunataka kuimrisha kilimo. Kama tutaweza kukiimrisha kilimo, basi hata haya matumizi ya kuagiza chakula hayatakuwepo na ndiyo maana wanalamika hapa baadhi ya Wabunge na hata Wizara inalamika kwamba bajeti ni finyu. Lakini hatujaribu kuangalia ni wapi tunapokosea. Tumekuwa tunalamika tu kwamba bajeti ni finyu na kadhalika na hali hii itaendelea kama hatutaweza kubadilika tukaja na mawazo mapya na fikra mpya ili tuweze kuiondoa nchi yetu hapa mahali ilipo.

Njia pekee ya kwanza ni kupunguza gharama za uendeshaji, kama tutaweza kupunguza gharama za uendeshaji, yaani kwa maana ya utawala na tukaweza kudhibiti ubadhilifu na wizi. Nafikiri kwamba tunaweza tukafanya vizuri zaidi katika mambo yetu. Lakini kwa mtindo huu tunaokwenda nao wa matumizi ya anasa hatutafika huko tunakotaka kwenda. Nasema hivyo kwa sababu ukiangalia katika majedwali hayo hayo, matumizi yasiyo ya kawaida ya manunuza ya bidhaa ya kawaida ni zaidi kuliko fedha iliyyotumika ya kuagiza mafuta nchini. Sasa kama haya matumizi tu yanazidi hata hayo mafuta tunayoagiza na bado tunasema kwamba ugumu wa maisha unachangiwa na mafuta, mimi sitaki kuamini hivyo, nataka kuamini kwamba sehemu kubwa ya ugumu wa maisha ya Watanzania inachangiwa pia na matumizi mabaya ya Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, unaponunua *Land Cruiser VX* moja ingeweza kujenga madarasa matano, *VX* moja ingeweza kujenga Zahanati, lakini ni magari ya lazima yawepo katika Serikali, lakini ni kwa watu gani tunaowapa magari hayo? Kwa mfano, unampa Katibu Mkuu *VX*, Katibu Mkuu ambaye haondoki Dar es Salaam, gari hilo anatembelea Dar es Salaam.

Pamoja na kwamba tunahitaji kuwa na magari ya *4Wheel Drive* kwa wale ambao wanakwenda kufanya kazi nje kwenye barabara mbaya, lakini wale wanaofanya kazi Dar es Salaam na hawatoki, Wakurugenzi ambao sana akitoka Dar es Salaam amekuja Dodoma maana yake mimi sikumbuki hata labda nikienda kuangalia vitabu kule katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya sidhani kama kuna Katibu yeoyote Mkuu wa Wizara yoyote ya Serikali hii toka Uhuru kama alifika Mpanda, sina hakika. Sasa anahitaji *VX* ya nini? Hata ukimpa *Escudo* inamtosha. Hata Ma-director hawa, kuna sababu gani ya kuendelea kuwapa magari ya thamani? Mimi sioni umuhimu.

Kwa hiyo, ni lazima tuangalie tufike mahali tuangalie kwamba sasa tunaweka nguvu yetu mahali gani, vinginevyo ni sawa sawa na ile ngoma ya mduara kwamba kwa miaka 46 tunazunguka hapo hapo hatuondoki. Sasa ni lazima tubadilishe wimbo na ni lazima tubadilishe staili ya kucheza ili tuweze kwenda mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano *SIDO* katika miaka ile ya nyuma ilichangia sana kuinua hali ya maisha ya wananchi wa kawaida na *SIDO* ilifanya vizuri sana na *SIDO* ilienea katika Mikoa yote ikiwemo pia Mkoa wa Rukwa. Sasa *SIDO* inakwenda inapunguziwa uwezo wake siku hadi siku, kisingizio kwamba bajeti ni finyu. Lakini ni lazima tufikie mahali sasa tufanye maamuzi tu ya kuweza kuisaidia *SIDO* ikaondoka hapo ili iweze kuwasaidia watu wengi zaidi na kuweza kuendeleza hivi viwanda vidogo vidogo ambavyo vitawanufaisha watu wa vijijini. Kwa maana, kama Serikali inaweza kumwekea *guarantee* mtu mmoja *individual* au kampuni ya mtu binafsi ikachukua mkopo benki, kwa nini Serikali hiyo hiyo inashindwa kuiwekea *guarantee* chombo chake ili kiweze kuchukua mikopo na chenyewe kikopeshe ili kuweza kuendeleza na kuweka kasi katika ukuaji wa viwanda vidogo vidogo vijijini?

Mheshimiwa Naibu Spika, labda sasa nizungumzie kama nilivyoanza kusema kupanga ni kuchagua. Tumekuwa na tatizo sana katika namna gani tunapanga mipango yetu hasa ukiangalia mipangilio ya viwanda huko nyuma, hatukuwa makini sana, kwa sababu unakuta kiwanda cha nyuzi za Pamba kimejengwa Tabora badala ya Shinyanga, kiwanda cha Tumbaku kinajengwa Morogoro badala ya Tabora, Mpanda au badala ya Songea ambapo wanazalisha Tumbaku.

Kwa hiyo, kumekuwa na mpangilio wa hovyo wa viwanda hivyo, lakini najaribu kufarijika tu kwamba Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ameelezea kuhusu *EPZ*, *SEZ* na sasa *EDZ*. Nilikuwa nahitaji nipate maelezo ya kina kama tumefanikiwa kwa kiwango gani na kwa kiasi gani katika mipango ya awali kabla ya kuanzisha mpango mwingine, kwa sababu kama nilivyosema, maneno haya ukiyasikiliza na ukiyasoma hapa yanavutia kweli kweli lakini ni lazima tujue kwamba tumekosea wapi na tunajisahihisha vipi na mpango huu mpya tunaouanzisha wa kanda, tunapeleka viwanda vyetu katika staili gani. Ni lazima tuzingatie sana malighafi inapatikana wapi na kiwanda gani kijengwe mahali gani ili tuweze kwenda vizuri, ili tuweze kupata tija na ili tuweze kupata mafanikio katika eneo hili la viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa nizungumzie suala la biashara. Biashara kwa ujumla wake ni suala la faida na hasara. Sasa sijui Serikali inafanyaje wakati kuna taarifa hii ya Shirika la Petroli yaani *TPDC*, linaonyesha wazi kwamba makampuni kadhaa yakiwemo makampuni ya Saruji yalipobadilisha matumizi kutoka kwenye umeme kwenda kwenye gesi waliweza kuokoa zaidi ya dola bilioni 1.5, lakini bei ya saruji haikushuka. Sasa kama Wizara, mnasemaje katika hili na ninyi mnafahamu kabisa kwamba gharama sasa za uzalishaji za viwanda hivyo zimepungua kwa sababu wametoka kwenye matumizi ya mafuta na umeme wamekuja katika matumizi ya gesi.

Hii faida inaendelea kukusanya na makampuni haya na sijui kama yanatozwa kodi stahiki kutokana na tofauti ya gharama za uendeshaji wa viwanda vyao, lakini bado mwanachi wa kawaida hajanufaika katika bei ya saruji, bati na hata bidhaa chungu nzima ambazo zinazalishwa na viwanda ambavyo vimebadilisha matumizi yake kutoka kwenye umeme kwenda kwenye gesi. Tunaomba tupate maelezo pia katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa kunipa nafasi. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Kaika Saning'o Telele na baadaye Mheshimiwa Richard M. Ndassa.

MHE. KAIKA SANING'O TELELE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Viwanda, Masoko na Ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kawaida nimpongeze Mheshimiwa Waziri Dr. Mary M. Nagu na Mheshimiwa Naibu Waziri Dr. Cyril August Chami, pamoja na wataalamu wote wa Wizara kwa kutuandalia hotuba nzuri ya bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajikita zaidi katika mkutano uliokuwa umefanyika kule Arusha kati ya tarehe 2 - 6 Juni, 2008 mkutano wa Leon Sullivan na wajasiriamali wadogo wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkutano ule ulikuwa ni mkutano wa kihistoria, ni mkutano mkubwa, ulikuwa na ulinzi wa hali ya juu, bahati mbaya wazururaji katika mji wa Arusha walikamatwa kamatwa wengi sana lakini yote haya labda ni katika kuhakikisha kwamba wageni wetu wanakaa salama katika mji ule na kutembelea maeneo ambayo walipangiwa kutembelea. Lakini pia kulikuwa na *patrol* kubwa, siyo tu ya Maaskari. Lakini pia hata kwa helkopta ulinzi ulikuwa ni mkubwa sana na tunashukuru kwamba mkutano ule ulimalizika salama salimini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kuelezea hapa ni kwamba kabla ya mkutano huu Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilifanya kazi kubwa sana ya kuhamasisha wajasiriamali wadogo wadogo kutoka Mikoa 17 ya Tanzania Bara na hata Zanzibar na Kenya wote walialikwa kuhudhuria katika mkutano huo na kuja na bidhaa zao ambazo kwamba wangeweza kuuza katika mkutano ule na wakapangiwa Njiro kwenye viwanja vya Nane Nane.

Bahati mbaya sana kutokana na uhamasishaji huo hakuna hata mgeni mmoja wa Mkutano huo wa Sullivan aliokwenda kuwaona wajasiriamali wale kwa sababu hawakuwekwa katika ratiba ya kwenda viwanja vile badala yake walipangija watembelee maeneo ya vivutio vya utalii, yaani walikwenda *Ngorongoro Crater*, lakini hata kule ambako tulitegemea wangekwenda Laitole ambako *food print* ya binadamu wa kale. Mheshimiwa Rais wetu mtakumbuka kwamba alikwenda kupiga kelele sana na kuwakaribisha Wamarekani akawaambia kwamba nina kitu cha kuonyesha ambacho kwa kweli ni adimu sana hiyo *foot print* ya Laitore. Lakini bahati mbaya hawakuweza kufika, lakini mimi nashukuru kwamba wameweza kufika *Ngorongoro Crater* na nilijitahidi wakatembelea kwenye *cultural bomas* zangu. Kwa hiyo, wajasiriamali wangu wadogo wadogo wamenufaika, wameuza vitu vyao na wamepata kati ya dola 300 mpaka 800, hiyo ni hatua kubwa. Lakini nilipata pia vikwazo kwamba hawana muda. Lakini tulisimama imara na wakatembelea maeneo yale.

Lakini tofauti na wale ambao Serikali imewahamasisha Mikoa 17, lakini hawakukanyaga kule. Kwa kweli hali ilisikitisha kwa sababu Watanzania wale walijizatiti, walikwenda na bidhaa zao kwa lengo kwamba wangeweza kuuza, lakini kwa kweli hawakuza na hawakuwa na pesa yoyote wamekopa kwa rafiki na benki, lakini waliishia kupata hasara kubwa. Lakini baadaye wageni wale wa Sullivan waliweza kwenda kwa wafanyabiashara wakubwa wa pale Arusha mjini kama kwa Ndugu yetu Seif ambaye anamiliki *cultural heritage*, ina vitu vingi kama vinyago, lakini bei ni kubwa, wangekwenda kwa wajasiriamali hawa wadogo wadogo wangenunua vitu vilevile lakini kwa bei ambayo kwa kweli siyo kubwa. Lakini *anyway* kwa kuwa wana fedha nyingi kama tunavyoambiwa, wana fedha na *dollars*, basi wamekwenda kununua huko, lakini wajasiriamali wadogo walipata shida sana na hasara kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niiombe Serikali, kwa sababu Serikali yenye we imepoteza pesa nyingi kuwahamasisha hawa watu na kuwafanya semina na wakaitikia wito wa Serikali wa kwenda kwenye mkutano huo kwa mategemeo kwamba na wenye we wangenufaika baadaye.

Naiomba Serikali wakati mwingine isirudie kosa kama hili kwa sababu nilifikiria kwamba Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Wizara ya Dr. Mary Nagu ya Viwanda, Biashara na Masoko pengine wangeshirikiana hata kuhakikisha tu kama siyo wote, basi wangekwenda wachache kwa kuondoa ile aibu kwamba wajasiriamali hawa wanaiona Serikali yao sasa kama imewatapeli. Lakini walitegemea pia kwamba wangekwenda kuwaona na wangeweza kupata zile *business cards*', wangepata marafiki wa kibiashara na wangeweza kuwasiliana hata baada ya wao kurudi Marekani na wangeweza hata kuleta kampuni za kitalii au kampuni za kibiashara katika Tanzania na hawa wajasiriamali wadogo wadogo wangeweza kunufaika.

Kwa hiyo, nasema kwamba hamasa ya Serikali kwa kweli ilikuwa kubwa, lakini wale wageni sasa hawakuweza kwenda, bahati mbaya mimi mwenye we nilikwenda huko viwanja vya Nane Nane kwa shughuli zangu tu binafsi na kwa sababu nilikuwa na yale medali za Mkutano wa Sullivan wakafikiri kwamba napeleka habari njema kwao kwamba wageni sasa wanakwenda kule. Niliishia kuwa mgeni rasmi bila kutarajiwa,

lakini niliwatia tu moyo kwamba kwa sababu Rais alikuwa kwenye maeneo yale ya AICC na wengine walipiga Kambi kwenye lango kuu ya AICC lakini Rais alisikia kilio chao na aliahidi kwamba kwa kweli makosa haya hatutarudia wakati ujao kwa sababu Arusha wageni wanakuja mara nyingi na kwa hiyo, mipango itawekwa na Serikali vizuri zaidi.

Sasa ninachosisitiza tu ni kwamba tumekuwa tunapenda sana kuwatukuza watu wa nje na kutukuza vitu vya kutoka nje, lakini mimi nafikiri tufike mahali tuwadhamini vilevile wafanyakazi wetu, tuwadhamini wafanyabiashara wetu wakubwa kwa wadogo kwa sababu na wenyewe wanakuwa na mchango wa namna fulani kwa pato la nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nafikiri kwamba Serikali ingefanya utafiti wa kwamba hawa watu waliotoka Mikoa 17 na Zanzibar walikuwa ni wangapi ili kama kuna uwezekano waweze kufidiwa hasara ambayo walikuwa wamepata.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ambalo mimi nilitaka niliseme ni kwamba tu nataka nniombe Serikali watakopokuwa sasa wanafanya utafiti wa kile kiwanda kitajachojengwa *Lake Natron* kiwanda cha *Soda Ash* labda utafiti wa kitaalamu uzingatiwe sana na Serikali na kama alivyosema Professor Mwalyosi jana, kwa kweli mambo ya kitaalamu ni vizuri yakazingatiwa kuliko tu tunafanya mambo juu juu na baadaye tukaja kujikuta kwamba tumefanya makosa na kwa hiyo, kiwanda hicho kikijengwa tunajua kwamba kitakuza uchumi, wananchi wataajiriwa, lakini tuangalie kama manufaa ya kiwanda kile ni makubwa zaidi kuliko pengine ingeendelea kubaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ambalo nataka kulisema ni kwamba, naiomba Serikali watakopokuwa wanafanya utafiti wa kile kiwanda kitajachojengwa *Lake Natron*, Kiwanda cha *Soda Ash*, labda utafiti wa kitaalamu uzingatiwe sana na Serikali na kama alivyosema Prof. Mwalyosi jana. Kwa kweli mambo ya kitaalamu ni vizuri yakazingatiwa kuliko tukifanya mambo juu juu na baadaye tukaja kujikuta kwamba tumefanya makosa. Kiwanda hicho kikijengwa tunajua kwamba kitakuza uchumi, wananchi wataajiriwa lakini tuangalie kama manufaa ya kiwanda kile ni makubwa zaidi kuliko pengine ingeendelea kubaki kama eneo la utalii na kwa manufaa ya *laser flamingo* waliopo pale, manufaa pengine ni makubwa zaidi kuliko pengine kujenga kiwanda pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana kwa kupata nafasi hii adhimu sana asubuhi ya leo kwa sababu sikutegemea kama nitapata nafasi kutokana na ulivytangaza ukasema kwamba wachangiaji ni wengi. Kwa hiyo, kwa kunipa nafasi hii nakushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba uniruhusu kwanza nimpongeze Mama Nagu, Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, Naibu Waziri wake pamoja na Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuandaa bajeti yao ambayo ina maelezo yanayojitosheleza. Kama kweli Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko

ataamua vizuri kufuata na kutekeleza yale yaliyomo humu ndani. Nina uhakika nchi yetu itapaa na hivyo napenda kusema kwamba, namuunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimsaidie kidogo tu, mama yangu Mheshimiwa Nagu, nilikuwa najaribu kuitia kitabu hiki...

MWENYEKITI: Naomba umsaidie Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Sawa. Naomba nimsaidie Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko. Ni shemeji yangu labda ndiyo maana nimezoea kumwita hivyo. Pale katika ukurasa wa kwanza, kwa sababu wenzetu, nafikiri ni wataalam kwenye kitabu chake kuna picha mbili, maelezo yanatofautiana, naomba kwa sababu wao wanayo *TBS* kwa maana ya viwango, vianze kuonekana tangu kwenye vitabu vyao, tulitegemea ile picha ya kwanza ya Makamu wa Rais ingekuzwa na maelezo jinsi yanavyosomeka, wanasema kwamba Makamu wa Rais akiwa kwenye Banda la Wizara ya Viwanda. Hakuna banda hapa, picha imekatwa tu.

Lakini ukija kwenye picha ile ya pili katika *caption* wanasema kwamba, Mheshimiwa Mizengo Pinda akitagua uzalishaji wa mbolea katika Kiwanda cha Minjingu, hakagui hapa. Picha na maelezo viko tofauti, lile jengo analipa mgongo halafu mnasema anakagua. Kwa hiyo, ule ubora wa *caption* na maelezo lazima vifanane.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda katika ukurasa unaofuata ni kama nilivyosema, nitoe ushauri kwamba, ni vizuri ubora wa viwango uanzie kwenye kitabu chenu. Maelezo na picha vifanane na picha ziwe nzuri maana yake ninyi ndio mnaosimamia viwango.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa niende kwenye suala zima la mizani. Juzi nafikiri mlisikia kwamba sasa watu wameshaanza kucheza na mizani ya kuuzia pamba, wamekamatwa Shinyanga, lakini na Mwanza Wilaya ya Kwimba wamekamatwa.

Kitu kibaya ambacho kinafanyika na naomba sana hili tusaidiane, mkulima wetu wa pamba hawezি kunenepa kwa utaratibu huu wa kumwibia kilo zake za pamba. Unapotengeneza mzani halafu una-*temper* na mzani unampunguzia kilo 15 kwa kila mzigo mmoja, unamwibia mkulima aliyeteseka kuanzia Desemba mpaka Juni, Julai au Agosti. Unamwibia kila mzigo wake Sh. 6,000/=, kwa bei ya sasa ya Sh. 400/=, ukichukua kilo 15 kwa kila mzigo, kwa kila mzigo unamwibia Sh. 6,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, huyu mkulima atanenepa lini? Atalipa madeni lini? Ni kwa nini utaratibu huo unaachiwa na watu wa mizani? Maafisa Mizani wamekwenda kukagua pale Kwimba, wakakamata mizani zaidi ya ishirini. Walichofanya maskini ya Mungu eti ni kuwatoza Sh. 10,000/= halafu wakawarudishia ile mizani ili wakawaibie tena wakulima wa pamba. Hivi kweli huyu mkulima wa pamba na mazao mengine tunamthamini, lakini kitengo hiki kipo kwa ajili ya kuwasaidia wale wezi wanaowaibia wakulima?

Tunaomba sana Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko hasa Kitengo cha Mizani, watu hawa kwa sababu wanajulikana, mizani yao ilikamatwa, wafanyiwe mambo mawili kwa sababu ni wezi, moja, wanyang'anywe leseni au pili, wapelekwe Mahakamani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiwaacha hivi hivi tutakuwa tunawaumiza wakulima wetu na wakulima hawa hawana zao lingine zaidi ya pamba. Naomba sana Kitengo cha Mizani kisimame kidete ili tuwasaidie wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, wenzangu wamesema sana humu ndani lakini yamekuwepo maneno mengi. Tanzania kwa sasa ni eneo la kutupia bidhaa mbovu, ni *damp* la bidhaa mbovu, lakini *TBS* wapo, *Tanzania Food and Drugs Agency* ipo.

Nashauri kwamba, tisisubiri mpaka hivi vifaa vije kwenye *godowns* vinaanza kusambazwa eti ndiyo tuanze kuvikamata. Vitu hivi vinapitia bandarini, vinakaguliwa bandarini, kwa nini mnaruhusu mpaka vinaingia kwenye soko? Tuvikamate kule kule bandarini, kama ni kuvichoma kule kule bandarini badala ya kuvichomea huku, lakini vitu vingine havichomwi vyote lakini iko siku kwa sababu hawa wenzetu wanaleta mpaka madawa, tutajikuta tunajiua sisi wenyewe, madawa yanayoingizwa nchini ukiangalia hayana ubora, vifaa havina ubora, tulionyeshwa juzi hapa, *TBS* wapo, inasikitisha!

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana Mwenyekiti wa Bodi ya *TBS*, Mama yangu Mama Peleka hili alipeleke na kulisimamia. Tanzania sio sehemu ya kutupia vitu vibovu, lakini watu wanataka kununua vitu vya bei rahisi kwa sababu wanaona kama ni vizuri, ile *value for money* watu wanataka kununua kusudi vitu hivyo viwasaidie lakini badala ya kuwasaidia vitu hivyo vinaharibika baada ya muda mfupi. Majembe, *radio*, saa, ndiyo hivyo hivyo. Unavaa saa, ukitoka hapa mpaka kwa Mheshimiwa Naibu Spika, saa imesimama. Simu za mkononi, *TBS* wapo, lakini wanaoagiza magari ni tofauti, magari yanakaguliwa kule kule, yanakaguliwa Dubai na Japan.

Kwa hiyo, magari yanayokuja hapa yanakuja yale yenze viwango. Naomba sana ndugu zangu wataalam watusaidie, wamsaidie pia na Waziri wa Viwanda kama walivyosema wenzangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa maelezo yake katika ukurasa wa 49 wa kitabu chake kuhusu mfumo wa stakabadhi za maghala. Hili likisimamiwa vizuri kwa nguvu zote litatusaidia sana hasa kwenye mazao ya pamba. Stakabadhi ghalani, nashukuru imeshaanza Shinyanga katika vijiji kama 16.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa tuhame twende Mwanza, tupate elimu ya kutosha, huyu ndiye mkombozi wa mkulima. Jinsi ilivyoanza Mtwara na imefanyika Shinyanga sasa twende Mwanza. Naomba Wizara ya Viwanda pamoja na Wizara ya Kilimo washirikiane hili ili liwe ndiyo wimbo kwenye maeneo yetu ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, lakini si la mwisho sana, Mwalimu Nyerere katika nchi hii alijenga viwanda na nchi bila viwanda sio nchi tena. Tumezoea kupeleka vitu vyetu malighafi badala ya vilivyoindikwa. Ile *Pugu Road* yote Mwalimu Nyerere aliweka viwanda, leo *Pugu Road* ile ni ya kuuza fenicha sio viwanda tena. Naomba kama tunataka tuendelee na nchi iendelee lazima tuwe na viwanda vingi vya kusindika mazao yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutashangaa sasa robota linatoka Mwanza kwenda Dar es Salaam, kitu ambacho wangepeleka Tabora, pale *Tabotex* wakatengeneza nyuzi, lakini badala yake tunachukua robota Mwanza tunapeleka Dar es Salaam. Zile gharama zinakuwa kubwa zaidi, matokeo yake huyu mkulima hawezi kufaidika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri na kuomba kwamba, tusimamie viwanda. Lakini wenzangu jana walizungumza kuhusu ujenzi wa Kiwanda cha Saruji Mwanza, Mheshimiwa Hewa alizungumza na Balozi Mongella alisema, bado nasisitiza na kuomba kwamba ni lazima mikakati maalum ifanywe ya kujenga kiwanda cha saruji Mwanza. Tukifanya hivyo tutakuwa tumesaidia wananchi wetu hasa upande wa Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huo mfupi, narudia tena kusema kwamba, naunga mkono hoja, lakini yale ambayo nimeyasema kwa njia moja au nyingine sio lazima mwaka huu, lakini inawezekana mwakani basi yatekelezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. DIANA MKUMBO CHILOLO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitumie nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda Biashara na Masoko, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii nzuri na mahiri iliyoonyesha wazi vipaumbele vyake kwa lengo la kuinua uchumi wa Watanzania husuzani wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutamka rasmi kuwa ninaunga mkono hoja hii na ninawataki utekelezaji wenye tija na Mwenyezi Mungu awape afya, nguvu na mshikamano ili waweze kutekeleza azma yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza Serikali kwa mkakati wake wa kuiwezesha *SIDO* ili iweze kuwakopesha wajasiriamali wetu walioko mijini na vijijini ambao wanajitahidi kuondokana na umaskini. Ni kweli usiojificha kuwa *SIDO* inafanya kazi nzuri bali fedha inayotengewa ni ndogo sana. Ninaiomba Serikali kuona namna ya kuiongeza fedha ili iweze kuendeleza kazi yake nzuri ya kuwakopesha wananchi amba wako kwenye harakati ya kujiendeleza kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *SIDO* inapata taabu sana juu ya kutoa mikopo kwa wateja wake kwani sasa ina wateja wengi sana na fedna wanazotengewa ni ndogo sana na

Serikali hali ambayo inawafaya wawe na lugha ya kuwapiga tarehe wateja wake jambo ambalo linawafanya wateja kukarahika sana na usumbufu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Waziri/Serikali iwasaidie kabla ya majumuisho kwani pesa hizi ni ndogo sana hazitoshi kabisa kutoa huduma kwa Watanzania ambao sasa wamejifunga kibwebwe kuzalisha mali kwa maslahi yao na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha kukamua alizeti Singida, ninamwomba Mheshimiwa Waziri arejee swalı langu Bungeni juu ya kuomba Serikali itutafutie wawekezaji wa kutujengea kiwanda cha kukamua alizeti – Singida. Jibu alilonipa ni kuwa kazi ya kutafuta wawekezaji ni ya wana-Singida wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi bado naendelea kuiomba Serikali kuendelea kutambua kuwa kutafuta wawekezaji ni jukumu la Serikali sio wana Singida kwani Serikali ndiyo yenyeye uchungu na wakulima wake. Kazi yetu wananchi wa Singida ni kuibua kero na Serikali kutatua kero kwa kuangalia huduma na faida pande zote mbili, mkulima na mwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Singida wanapata taabu sana kukamua alizeti kwenye mashine ndogo na kuwafanya kushinda kutwa nzima na kukesha hata wiki kwani zoezi hili huenda pole pole kwa ajili ya mashine ndogo zinazotumika. Serikali isikwepe hili, tutafutiwe wawekezaji sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, bei ya mazao yetu iko chini sana. Inafurahisha sana ninapoona wananchi jinsi wanavyojitahidi kulima mazao ya biashara kwa nguvu zao zote na kwa wingi sana. Mazao haya ni pamba, alizeti, ufuta, vitunguu, dengu pia tunazalisha asali, mbao na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha sana kuona mazao haya hasa pamba na alizeti hayana soko. Kama lipo, ni bei ya hasara kabisa, hailingani na gharama inayotumika kwa kulima hadi anapofikisha kwenye soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwekezaji aliyedhamini kununua pamba, kweli hawatendei haki wakulima kwani ananunua kwa bei ya hasara kabisha tena tatizo hili lipo hadi Mkoa wa mtani wangu wa Manyara. Ninaomba Serikali ifanye majadiliano na mwekezaji anayenunua pamba ili kuongeza bei kuliko ilivyo sasa wakulima wanaumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninategemea Mheshimiwa Waziri atatoa maelezo wakati wa majumuisho yake hapo kesho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu bei ya mafuta ya alizeti, napenda kuikumbusha Serikali kuwa wakati Mheshimiwa Lowassa (Mb) alipokuwa Waziri Mkuu aliwatangazia wananchi wa Singida kuwa kuna soko la alizeti nchi za nje. Ninaomba sasa soko hilo wananchi tuelezwe liko wapi ili mafuta yetu safi ya alizeti yapate soko hilo ambalo litaleta tija kwa wakulima wetu. Nitashukuru pia Mheshimiwa Waziri kwenye

majumuisho yake ili nisiharibu udugu wetu wa karibu kwa kutaka ufanuzi, ninaomba sana, wananchi wanasubiri kusikia soko hilo la alizeti nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, usambazaji wa pembejeo na Mbolea, ninakiri kuwa Serikali inajitahidi sana kuwajali wakulima kuhakikisha kuwa wanapata pembejeo na mbolea ili kuinua kilimo chake na kuleta tija zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu ni kuitaka Serikali kutoa huduma ya pembejeo na mbolea mapema ili wakulima waweze kulima kwa wakati kulingana na msimu wenyewe. Ninasema hivi kwani huduma hii huchelewa sana. Hii inatokana na viwanda kuzalisha kidogo. Ninaomba uzalishaji uongezeke ili tuweze kutekeleza ilani ya uchaguzi ya mwaka 2005 hadi 2010 barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kujenga viwanda, nadhani sasa ni wakati muafaka wa kubadilika taratibu za kujenga viwanda. Kulikuwa na tabia, viongozi kupendekeza kujenga viwanda mbali na zao husika linakolimwa. Hivyo, sasa tubadilike endapo pamba inalimwa Singida, basi kiwanda kijengwe Singida ili kupunguza gharama za usafirishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ninaishauri Serikali kuboresha utengenezaji wa bidhaa zetu ili tuweze kutumia wenyewe, tusikimbile nchi za nje mfano *furniture* na vyakula, ama tuboreshe zaidi ili vipate soko zuri nje ili tuzalishe zaidi na kupata fedha za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, kuhusu ajira viwandani, naomba vijana wetu wazalendo wakumbukwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, natamka tena kuwa ninaunga mkono hoja hii na ukweli kwa muda mfupi Waziri ameleta mapinduzi yenyenye maendeleo.

MHE. JUMA SAID OMARI: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya na kuweza kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya viwanda ni sekta muhimu sana ambayo inategemewa na sekta muhimu sana ambayo inategemewa na sekta nyingine muhimu kama vile kilimo, mifugo, uvuvi na kadhalika, kwa kuwa kwa sekta ya viwanda itawezesha kukua kwa sekta za kilimo, mifugo, uvuvi na nyinginezo na hivyo kukuza pato la Taifa na kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa viwanda hapa nchini utawezesha usindikaji wa mazao mbalimbali na kupata faida zaidi kuliko uuzaji wa mazao ghafi kama ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa viwanda utawapatia vijana wengi ajira jambo ambalo litaongeza kipato kwa wananchi na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vitasaidia wananchi badala ya kutumia zaidi bidhaa kutoka nje. Zikiwemo *juice*, mafuta ya kupikia, pamoja na matunda mbalimbali yanayooza bure wakati wa msimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ihamasishe wawekezaji wa ndani na nje wajenge viwanda ili tuweze kuuza nje bidhaa zilizosindikwa badala ya kuuza nje malighafi zinazopunguza pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaagiza *furniture* kutoka nje wakati hapa nchini tuna mbaao za kutosha, magogo na wananchi ambaao wana uwezo wa kutengeneza *furniture* nzuri na zenye ubora. Watanzania tunapaswa kubadilika na Serikali ikiwa na wajibu wa kuongoza mabadiliko hayo ili malighafi za misitu zilizopo nchini ziwe za manufaa kwa Taifa letu na wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la masoko ni muhimu kwa ajili ya uuzaaji wa mazao mbalimbali yanayozalishwa hapa nchini. Kutokana na wakulima wafugaji, wavuvi, mafundi seramala na kadhalika, kuna mazao mbalimbali yakiwemo matunda kama maembe, machungwa, mananasi, nyanya na kadhalika ambayo huoza yakiwa mashambani kwa kukosa masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iandae mikakati ya makusudi itakayoliwezesha Taifa letu kuuza nje bidhaa mbalimbali kupitia kwa wafanyabiashara wetu badala ya kuagiza kutoka nje. Utaratibu huu utaliwezesha Taifa kupata fedha nydingi za kigeni na hivyo kukuza uchumi wa nchi na kuongeza kazi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba bidhaa bandia zipigwe marufuku.

MHE. PAUL P. KIMITI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake na Katibu Mkuu kwa maandalizi mazuri ya hoja hii kwa ukamilifu sana. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atusaidie wanachi wa Rukwa na wakazi wote wa Mikoa ya Ziwa Tanganyika (Kigoma) kuwa kusaidia kuwaelekeza wawekezaji wa viwanda vya samaki waje kwa wingi waendeleze matumizi ya samaki wa ziwa hilo ili walishere majirani – *DRC*, Burundi, Zambia na hata nchi za nje. Samaki wengi wanakosa kusafirishwa hata nje kidogo ya mwambao wa ziwa kwa kukosa wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Sumbawanga ilikubaliana na wafanyakazi/wafanyabiashara wa Mkoa na wa Taifa toka *TCCIA* ili kuanisha soko la kimataifa mpaka wa Zambia na Tanzania eneo la Kasesya. Serikali ya Dermark na baadhi ya *Nordic countries* waliona umuhimu huo. Naiomba Serikali kupitia kwa Mheshimiwa Waziri alifuatilie wazo hilo zuri ili Kasesya itumie kama *Hub* ya biashara kati ya nchi ya Zambia, *DFRC* na sisi wenyewe – Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri atupatie maelezo ya uhakika, nini hatma ya *TIRDO* na *CAMARTEC* katika mtazamo wa nia ya Ilani ya

uchaguzi na mageuzi ya kifikra katika kuendeleza viwanda vidogo ambavyo vinaweza kuzalisha baadaye viwanda vikubwa? Je, wanataluma wa *SIDO* wanasaidiwa vipi ili waondoke hapa walipo ili wangie karne mpya?

Katika Mkoa wa Rukwa lipo tatizo la ukosefu wa miundombinu. Je, Wizara hii inalisikuma vipi suala hili kwa kuutolea Mkoa katika vikao vyta juu ili Serikali ijue nini uwezo wa Mkoa katika kuongeza pato la Taifa kwa kutumia malighafi zinazopatikana Mkoani?

Pia katika kuelekeza wawekezaji waje wajionee utajiri mkubwa uliomo Mkoani mwetu na hasa kwa kuzingatia kuwa *DRC* inatumaini sana Rukwa kuwa na *centre* ya biashara eneo la Kasanga au Kipili ili mizigo yao yote iwe inaingilia hapo. Una baadhi ya wataalamu wanafikiri wazo hilo ambalo nitaomba siku moja liwekwe wazi kwa Wizara siku muafaka ili tuone namna ya kuboresha wazo hili. Soko la ndani ndio msingi wa uchumi wa Taifa letu.

Naunga mkono hoja hii na kumtakia Mheshimiwa Waziri, Naibu, Katibu Mkuu utekelezaji mwema kwa hoja hii ili kufikia bajeti ijayo iunganishe ushauri na maoni haya ya Waheshimiwa Wabunge.

MHE. ALOYCE BENT KIMARO: Mheshimiwa Naibu Spika, bidhaa hafifu na duni ni hatari sana kwa maendeleo ya uchumi na viwanda. Nashauri hatua kali zichukuliwe kwa yejote anayeingiza bidhaa hizi dhaifu hapa nchini. Utaratibu na kukagua bidhaa hizi kabla hazijaingia hapa nchini ufanyike.

Bidhaa bandia na duni zinapogundulika ziharibiwe na mwenye mali kushitakiwa na kutangazwa hadharani kuwa hawa hawaitendei haki nchi yao. Wote tujiulize tumeifanya nini nchi yetu kila mtu kwa nafasi yake?

MHE. RITA L. MLAKI: Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Viwanda na Biashara kwa hotuba nzuri ya bajeti yao. Mheshimiwa Waziri aliyebolea katika viwanda tuna matumaini makubwa na uzoefu wake.

Napenda kuchangia kidogo kuhusiana na uanzishwaji wa viwanda nchini. Ongezeko la viwanda nchini bado ni kwa kasi ndogo. Sera za Serikali zinasema, Serikali haifanyi biashara tena na wameachiwa '*private sector*'.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni sawa hivyo, lakini Serikali isiwaachie bila kuwapa wafanyabiashara msaada wa kutosha. Ni vigumu sana kwa mwekezaji wa ndani au nje kuanzisha biashara. Vikwazo ni vingi sana.

Napendelea tuige mfano wa Malaysia wa kuwasaidia wawekezaji uanzishwaji wa viwanda. Wanalo shirika chini ya Wizara linaitwa *MIDA – Malaysia Industrial Development Authority*. Kazi yao ni kusaidia uanzishwaji wa viwanda, wanaandaa *project write up*, wanatafuta *land*, wanawasaidia wawekezaji kupata *loans*,

wanawafundisha *technology* na wanawatafutia masoko. Inakuwa rahisi na viwanda vingi vinaanzishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali *initiate* na kuwashawishi watu waanzishe viwanda. Tukisubiri wawekezaji waje wenyewe hawawezi wa ndani na nje, kumbukeni nchi yetu ni *very raw/virgin*. Kuna *opportunities* nyingi za viwanda, kila *sector* ina nafasi ya kuanzishwa viwanda.

Pili, Serikali imtafute mtaalam ambaye atatufanyia hayo hapo juu, Serikali imlipe aje nchini na atusaidie uanzishwaji wa viwanda mbalimbali kupitia *private sector*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji mkomo wa Serikali katika kusaidia ukuaji wa viwanda nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, *SIDO*, Karibu 80% ya viwanda nchini ni vya *SIDO*. Sera ya *SME* tayari imekamilika na utekelezaji sio mzuri. Napendekeza itoke Wizarani ipewe *private sector, task force* wasaidie utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo machache naunga mkono hoja.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mama Dr. Mary Nagu, Naibu wake Mheshimiwa Dr. Cyril Chomi, Katibu wake Dr. S. Tay kwa hotuba nzuri pamoja na mikakati iliyotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo langu ni moja tu. Nashukuru mlinipa nafasi ya kuwa majumbe wa Bodi ya *TIRDO*. *TIRDO* imekuwa katika mgogoro wa muda mrefu kuhusu hati ya ardhi yao.

Kama mlivyonitura kuisaidia taasisi hii, mara ya mwisho nikachangia hotuba ya Wizara ya Ardhi, nimejibwa *TIRDO* wakalipie eneo lile lisilo na utata ili wapewe hati yao hata ndani ya siku mbili, kisha wafuatilie lile eneo lililomegwa mara ya pili ambalo lina *infrastructures* za *TIRDO* ili *sewage system*. Naamini *TIRDO* italipia mapema na kuendelea kufuatilia haki zao nyingine, kwani naamini hakuna mkono wa mtu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo hoja ya kuiwezesha *TIRDO* kukopa ili kumalizia majengo yake, kwani ile *location* ni nzuri kwa kuwekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. KAIKA S. TELELE: Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya wajasiriamali wadogo wadogo, Arusha. Mkutano wa kihistoria wa Leon Sullivan ulifanyika Arusha tarehe 2 – 6/June, 2008. Kabla ya mkutano huo, Serikali ya Tanzania ifanye uhamasishaji wa hali ya juu kwa wafanyakishara wadogo wadogo (wajasiriamali) wa Tanzania kujitokeza kwa wingi na bidhaa zao kutoka Mikoa 17 ya Tanzania Bara na Zanzibar na hata na nchi jirani ya Kenya kuja katika maonyesho hayo ya Sullivan.

Mbiu ya Serikali ni kuwa mkuutano wa Sullivan ungeleta neema ya pekee kwa Watanzania kiuchumi kwa vile vivutio vya utalii katika Tanzania vingetangazwa. Lakini kwa wajasiriamali mmoja mmoja wangenufaika kama ifuatavyo: wangweza kuza mali/vitu vyao wanazozalisha/ tengeneza; wangepeana *business cards* kwa ajili ya mawasiliano ya kibiashara; Hamasa ya Serikali kwa wajasiriamali wadogo wadogo ilikuwa kujuana, ilitumia fedha zake yenyewe; kwa ajili hiyo, wajasiriamali wadogo wadogo walijizatiti vilivyo, walikuwa na bidhaa za kila aina ikiwa ni pamoja na zile zilizoandikwa Sullivan.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna malalamiko kama ifuatavyo:- Kwanza, Serikali imewatapeli; wamepata hasara kubwa; bidhaa zao hazijanunuliwa; gharama ya kupangisha mabanda ni kubwa, ni Sh. 75,000/= kila siku; wajasiriamali wadogo hawadhaminiwi na Serikali ya Tanzania ila wageni kutoka nje ya nchi wametelekezwa!

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali hii kauli mbiu ya Serikali ya CCM ya maisha bora kwa kila Mtanzania ni ndoto!

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo ya Taifa lolote duniani yanategemea kuthaminiwa na kusaidiwa na Serikali kwa makundi yafuatayo:-

- (i) Wafanyakazi ngazi zote; na
- (ii) Wafanyabiashara wakubwa na wadogo, mchango wao
kwa pato la Taifa ni kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali isipuuze suala la wajasiriamali wadogo. Ikumbukwe kuwa kundi hili lina viongozi wa vyama vyao ambao wangeweza kuwatumia kutoa tamko lao la kususia wito au mialiko ya Serikali kama njia ya kuelezea hisia zao juu ya jambo fulani (*i.e. the Sullivan*). Wangeweza kufanya hivyo hata kwa sherehe kubwa kubwa kama vile sherehe za Saba Saba (Dar es Salaam na Mikoani), sherehe za Nane Nane (katika kanda) na/au sherehe nyingine kitaifa/kimataifa ambayo kwayo Tanzania imeridhia.

MHE. FELISTA A. BURA: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali iangalie uwezekano wa kuiongezea *SIDO* pesa kwani ndio mkombozi wa wanawake wajasiriamali katika Mkoa wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika aya ya 58 ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri, amenkuu hotuba ya Mheshimiwa Rais Mstaafu Mheshimiwa B. W. Mkapa aliyoitoa tarehe 30 Juni, 2004. Sehemu ya hotuba hiyo inasema: “Tusione fahari kununua bidhaa za wenzetu kutoka nje na akasema angependa kuona mwaka hadi mwaka kiwango cha bidhaa kutoka nje kinapungua.” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, alichokisema Rais Mstaafu mwaka 2004 na kinachoendelea katika ofisi zetu za Serikali ni tofauti kabisa na hata katika nyumba za watumishi wa ngazi za juu Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama sisi viongozi tuliyokabidhiwa dhamana na wananchi hatuko tayari kushiriki katika kujenga uchumi wetu kwa kununua bidhaa za ndani ya nchi, tunamtegemea nani ashiriki? Serikali ionyeshe mfano katika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika *supermarket* za Dar es Salaam, Arusha, Mwanza na kadhalika zinauzwa nyama, maziwa, mboga za majani kutoka Afrika Kusini na hata katika hoteli za kitalii hapa nchini mwetu asilimia kubwa na vyakula na vifaa vinatoka walikotoka wawekezaji hao. Je, hii ni haki? Je, Serikali inawafanyia haki Watanzania? Je, huku sio kumdidimiza Mtanzania? Serikali inawaambia nini Watanzania katika hili?

Viwanda vilivyouzwa kwa wawekezaji na mpaka sasa havijaanza kufanya kazi kama vile *Tanganyika Packers* kwa nini visiuzwe tena kwa wenye uwezo na kuviendezea?

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanda cha *General Tyre* ni kiwanda kikubwa cha magurudumu Afrika Mashariki lakini kiwanda hiki hakifanyi kazi. Kiwanda kilipata mkopo kutoka *NSSF*, hata hivyo, bado hakijaweza kuzalisha. Wananchi na umma wa Watanzania wanataka kujua tatizo la kiwanda ni nini? Pesa walizokopeshwa na *NSSF* zimefanya kazi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 111 – 114 inaonyesha hali ya mauzo nje ya nchi na manunuzi kutoka nje ya nchi. Hali ya mauzo nje ya nchi inaonekana kupanda kwa mwaka 2007/2008 kwa bidhaa chache sana. Kilichotuokoa mauzo ya nje ni kahawa iliyosindikwa, pamba na bidhaa nyingine. Manunuzi kutoka nje yamepanda kwa 24.9% ukilinganisha na mwaka 2006. Hali hii inaonesha ukuaji mdogo sana wa sekta ya viwanda, biashara na masoko nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ifike wakati sasa Serikali iweke mikakati madhubuti kwa bidhaa zinazozalishwa nchini kuwa na ubora wa viwango vinavyokubalika kimataifa kuokoa bidhaa zetu katika soko la kimataifa. Shirika la *TBS* ni mdau mkubwa katika kufanikisha hili. Naunga mkono hoja.

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na wenzangu kumpongeza sana dada yangu Mheshimiwa Dr. Mary Nagu – Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, Naibu wake - Mheshimiwa Cyril Chami, pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri sana ya uandaaji wa bajeti ya Wizara.

Kigezo cha kupima umasikini wa nchini yoyote ni kule uchumi wa nchi hiyo kutegemea kilimo. Tanzania uchumi wake kwa sehemu kubwa unategemea kilimo na ndiyo maana ni ya tatu kutoka mwisho kuwa nchi masikini duniani. Kwa upande mwingine nchi kuwa tajiri ni dhahiri uchumi wake hutegemea viwanda na biashara. Changamoto kubwa tuliyonayo ni kwa nchi yetu kuachana na kutegemea kilimo kwa uchumi wake na kuelekea kwenye utegemezi wa viwanda. Hii itachukua muda mrefu

sana kwa kuwa hata kilimo chenyewe hakijaboreshw. Ukiangalia ufugaji, ndiyo kabisa. Bado wafugaji wetu wanahangaika kuhamahama kutafuta miundimbinu ya mifugo (malisho, majosho na kadhalika). Uvuvi nao bado wavuvi wanalamika, haujaboreshw.

Kilimo bora, ufugaji bora na uvuvi ndiyo tu sekta zitakazotuelekeza kwenye viwanda na kuzalisha kwa thamani kukabiliana na soko huria na utandawazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba kuwe na *Time frame* ya kukamilisha barabara zote nchini maana viwanda bila barabara havifai. Pia kuwe na *Time frame* ya kusambaza umeme wa uhakika mijini na vijijini. Bila nishati ya umeme hatufikii viwanda kirahisi; kuwe na miundombinu sahihi ya maeneo ya wafugaji ili kuboresha mifugo, malisho, majosho, maji na kadhalika ili sekta ya mifugo iongeze thamani ya mazao ya mifugo; uvuvi bora utaongeza thamani ya samaki baada ya uboreshaji wa maeneo niliyotaja, ndipo hatua ya viwanda nchini itaweba kufikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kufikiria uanzishwaji wa haraka wa viwanda bila kuwa na mikakati sahihi ya masoko ya uhakika. Wakulima wetu hawana shida ya kuzalisha kama watawezeshw kwa kupatiwa pembejeo, bali shida kubwa ni soko la uhakika linalokidhi matarajio yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, bei zinazohamasisha uzalishaji utarahisisha uanzishwaji wa viwanda. Uhakika wa soko la nyama utarahisisha ufugaji bora. Masoko yatasaidia kuwepo mzunguko wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasisitiza tuwe na *Time Frame* kukamilisha barabara zote nchini, nishati ya umeme, maji, afya na uvuvi wa kisasa. Mheshimiwa Waziri kabla hajahama Wizara hii ya viwanda na Biashara, wananchi wa Manyara tunaomba ahakikishe tunapata kiwanda cha kukamua alizeti na au mbaazi Mjini Babati au hata Hanang. Tuna mbaazi bora duniani Mkoa wa Manyara.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Kiwanda cha kusindika Maziwa – Orkesmet.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa silimia mia moja. Ahsante.

MHE. FATUMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kusoma vizuri bajeti. Kusudi langu ni kuomba mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mtusaidie kutuletea wawekezaji wa viwanda vya chumvi. Kuna chumvi nyingi sana Lindi, lakini huwa tunanunua chumvi ya Kenya kwa matumizi iliyosindikwa.

Lingine, tunaomba wawekezaji wa viwanda vya *cement* Lindi. Kwani kuna malighafi ya *gypsum* yenyenye *content* ya ubora wa asilimia 90, ndani yake na ni nyingi sana. Umeme utakuwepo, maji yatakuwepo na barabara itakuwepo na bandari ipo, *gas* muda sio mrefu. Tunaomba Kiwanda cha *cement*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *EPZ* ya kanda ya kusini tunataka tafadhali ianze.

Mheshimiwa Naibu Spika, wamachinga wengi waliopo Dar es Salaam hasa Kariakoo, ni kutoka Lindi na Mtwara. Hii ni kwa sababu huku hakuna kiwanda chochote hata kama kuna korosho, ufuta, *gypsum*, *gas*, chumvi, lakini hatuna fursa. Tunaomba Mheshimiwa Waziri atutazame kwa jicho la huruma, angalau kiwanda kimoja, tafadhali. Ahsante.

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa kazi nzuri aliyoifanya Mheshimiwa Waziri na watumishi wake wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Wizara kwamba wajasiriamali wanaobuni mashine mbalimbali wawekewe eneo/kijiji cha wavumbuzi ili wabadilishane mawazo na kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanda cha *SPM (Mgololo)* watumishi walioachishwa miaka mitatu na hawajalipwa, tena bado wanakaa hapo na hawalipwi, Watanzania wenzetu wananyanyaswa. Msikumbatie wageni kuwa ni dhahabu na sisi wenye nchi ni vyuma chakavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshauri Mheshimiwa Waziri mwenyewe aende *Mgololo (SPM)* akaongee nao ana kwa ana na awatembelee katika makazi yao. Akague kuona matatizo na jinsi wanavyoathirika. Aunde tume huru ili ikachunguze ukweli uliopo maana hata tamko la Serikali kuhusu ubinafsishaji wa kiwanda cha *Southern Paper Mills Limited (SPM)* ilikuwa na mapungufu mengi yaliyoficha ukweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba maelezo zaidi kama kweli Mheshimiwa Waziri atatekeleza yote mawili.

MHE. CPT. JOHN D. KOMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Dr. Mary Nagu Waziri pamoja na Naibu wake kwa juhudni uwezo wao mkubwa katika kuongoza Wizara hii. Wizara hii ni moja kati ya Wizara ambazo zina uwezo wa kuinua hali ya maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Wizara ione kuwa Tanzania ni kubwa, hivyo fursa za uwekezaji nazo zimetapakaa nchi nzima. Naomba Serikali ipeleke jicho lake Kusini mwa nchi yetu hasa Mwambao mwa Ziwa Nyasa. Wenzetu upande wa pili wa Ziwa hili yaani Malawi, uwekezaji na biashara kule ni ya hali ya juu sana.

Baadhi ya viwanda vya kusindika samaki, mahotelii ya *five stars* na biashara mbalimbali zinafanyika kule mwambao wa Ziwa Nyasa na hivyo kuongeza pato kwa nchi ile. Mazingira yaliyoko kule ni yale yale ambayo nasi tunayo kwa upande wetu. Kwa nini tusichangamkiele jambo hili? Nashauri wataalamu wa Wizara hii watembelee Malawi na kupata “*experience*.”

Naiomba Serikali itutafutie wawekezaji hasa wa minofu ya samaki na samaki wa mapambo ambao biashara yake inalipa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kando kando mwa Ziwa Nyasa kuna mazao mengi ya matunda kama maembe na mananasi. Wizara ione haja ya kutafuta masoko ya matunda hayo kwa faida ya watu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. AL-SHYAMAA J. KWEGYIR: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nampongeza Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko - Mheshimiwa Mary Nagu, Naibu Waziri - Mheshimiwa Cyril Chami, Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa hotuba nzuri.

Nitaanza na usindikaji wa matunda, kiwanda au viwanda hivi vikifufuliwa vitasaidia ajira kwa wananchi na pia thamani ya mavuno itapatikana. Nitatoa mfano wa Mkoa wa Tanga ambao una matunda mengi sana. Badala ya matunda hayo kuoza yatakuwa na thamani kubwa kwa kuyasindika.

Pili, ni viwanda vidogo vidogo. Ni muhimu kwani wananchi watajajiri kutokana na mazao wanayozalisha. Mfano, kazi za ngozi za wanyama mbalimbali, ukilinganisha na bidhaa nyingine nyingi.

Tatu, ni *SIDO*. Serikali kupitia Wizara hii, iongezwe pesa, kwani katika shilingi billioni tano, wamepatiwa shilingi billion moja ambayo ni ndogo sana. Haiwezi kuendana na mahitaji ya sasa na usambazaji wa teknolojia muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, namaliza kwa kusema kwamba naunga mkono hoja mia kwa mia.

MHE. BENSON M. MPESYA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba kuunga mkono hoja iliyo mbele yetu kwa asilimia mia moja, kwa sababu zifuatazo:-

(a) Nina tumaini kubwa sana na utendaji wa Wizara hii, hasa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu wao pamoja na Wakurugenzi wote na taasisi zilizo chini ya Wizara hii.

(b) Mipango iliyo katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri inatia tumaini katika kusukuma mbele suala zima la uchumi wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nielekeze mchango wangu wa maandishi katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nizungumzie kuhusu ujenzi wa kiwanda cha bia Mbeya. Naipongeza kampuni ya *TBL* kwa dhati ya moyo wangu na kwa niaba ya wakazi wa Jiji la Mbeya na vitongoje vyake.

Ninaamini kuwepo kwa kiwanda kutaongeza ajira na soko la ngano inayosindikwa kwa ajili ya bia. Ninashauri tuelezwe aina ya ngano (*barrey*) inayofaa kwa kutengeneza bia ili tuwahamasishe wananchi kulima zao hili. Naomba tujue uwezo wa kampuni kununua ngano hiyo kama malighafi ya kiwanda. Wananchi wa Mbeya wana uwezo mkubwa sana wa kuzalisha malighafi hiyo bila hata kuagiza toka nje ya Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *EPZ – Mini Tiger Plan 2025*; kwa kuwa eneo limeshapatikana kwa ajili ya ujenzi wa *Economic Processing Zone* eneo la Iwambi kwa ajili ya soko lililo tayari la nchi za *SADC*, nitapenda kujua ni lini hasa utekelezaji utaanza kama sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya CCM – 2005 ya kufufua viwanda ndani ya Jiji la Mbeya?

Mheshimiwa Naibu Spika, Toka Kiwanda cha Zana za Kilimo – Mbeya kiwe mikononi mwa *PSRC* na kumpata mwekezaji, mpaka sasa hakuna chochote kilichofanyika na aliyekinunua, hachukua hatua zozote za kukiendeleza kiwanda hiki. Kwa kuwa Mr. Edeturn – *Engineer* wa Sweden aliyefunga mashine za *ZZK* aliomba kiwanda hiki ili aanze kuzalisha majembe, jambo ambalo hata *CHC* chini ya Mama Lupembe inalijua suala hili, kwa nini Msueden huyu asipewe kiwanda hiki ili aanze kuzalisha majembe na kutoa ajira kwa wakazi wa Mbeya?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iijitahidi sana katika masuala ya kuwa na ufanisi – *efficiency, umakini – effective* na kuwezesha – *facilitative*.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kuunga mkono hoja hii. Nawasilisha.

MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa ulinzi wake ambapo anaendelea kutupa uzima tulionao hadi leo.

Nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wa Wizara hii, jinsi walivyoadaa hotuba inayotoa mwelekeo wa kutekeleza Ulani ya CCM 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu viwanda vidogo vidogo, katika kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa 57, mkakati wa kukuza mauzo ya nje, yapo maeneo yaliyoainishwa yenye kuleta matokeo ya haraka (*quick wins*). Maeneo hayo mojawapo ni sekta ya misitu na nyuki.

Bukombe ni moja ya maeneo yenye mazao yatokanayo na misitu, asali na nta. Wananchi wafugaji wa nyuki wanazalisha sana, lakini hakuna kiwanda cha kuandaa mazao yao. Sio hivyo tu, hata soko la kuuza mazao yao kwa faida halipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iangalie uwezekano wa kuziwezesha *SACCOS* za warina asali mbili za Bukombe ili wapate vifaa vy'a kisasa vitakavyowasaidia kusindika mazao yao pamoja na soko la uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wangu wanafuga kienyeji, wanarina kienyeji na wanauzwa kienyeji. Ni lini watayapata maisha bora? Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha, naomba awaeleze wafugaji wa nyuki Bukombe, Serikali itawafanya nini katika kusindika mazao yao, yaani asali na nta na itawapatia soko la uhakika?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mfuko wa Stakabadhi ya Mazao Ghalani, kama alivyoleza Mheshimiwa Waziri, mfumo huu ni mzuri sana, lakini mimi umenikwaza kweli.

Mheshimiwa Waziri ameomba Wabunge tusaidie katika hotuba yake ukurasa wa 49 mpaka 56. Ni kweli nimehamasisha sana mfumo huu katika Wilaya ya Bukombe, lakini mpaka ninapoandika vyama vyangu vya ushirika Lungunga Amco na Bulugala Amco (Nyasato) vimekwama kununua.

Kwanza, mfumo huu umenivurugia kura zangu kwa wananchi wakullima wameona kwamba mimi ni mwongo ni mfumo ambao hautekelezeki. Vyama vyetu vya msingi havikopesheki wanashindwa kupata hela toka benki.

Naiomba Serikali, mfumo huu sehemu zote upitie *NMB* na Serikali itoe dhamana kwa vyama vya msingi (ushirika). Kwa nini serikali hii moja ilitia mdhamana kwa vyama vya ushirika kwenye korosho? Serikali inaona ugumu gani kutoa mdhamana kwenye pamba ili vyama hivi vifanye kazi? Naona kama Serikali bado inafanya ubaguzi, kanda ya ziwa hususan Wilaya yangu tumeachwa, wananchi watajuana na Mbunge wao aliyehamasisha mfumo huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali mtatuacha tuhamasishe halafu msifanye lolote mnatukatisha tamaa sana kama nilivyokata tamaa kuendelea kuhamasisha mfumo huu. Naamini Serikali itakapotoa mfano wa kusimamia vizuri mfumo huu kama Mtwara nami mtanitia moyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno hayo, naunga mkono hoja.

MHE. DR. WILBROD PETER SLAA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hoja ya viwanda na biashara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kuna utata mkubwa kuhusu usajili ya baadhi ya makampuni na kumbukumbu za makampuni hayo kutokuonekana Brella, nimeona nimwandikie Mheshimiwa Waziri ili afanye maandalizi ya kutafuta kumbukumbu ili siku ya hotuba yake isije ikawa hana muda wa kutosha kuzitafuta. Sasa basi, Kampuni ya *Deep Green Finance Co. Ltd*, suala ambalo haliko katika makampuni 22 yanayochunguzwa chini ya *EPA*, ilisajiliwa hasa tarehe ngapi? Wakurugenzi wa kampuni hii ni akina nani wakati wa usajili na kama kumekuwa na mabadiliko ya wakurugenzi katika kipindi chote cha uhai wa kampuni hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, wanahisa wa kampuni hiyo ni akina nani na kila mmoja alimiliki au ameendelea kumiliki hisa kiasi gani katika kipindi chote cha uhai wa

kampuni hiyo? Taarifa niliyonayo ni kuwa, kampuni hiyo imefunga (*wind up/shughuli zake*): Je, kampuni hiyo imefunga (*wind up*) tarehe ngapi/gani na mwaka gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna taarifa kuwa nyaraka zote muhimu kama vile *memorandum and articles of association, return forms* za kila mwaka na kadhalika hazionekani Brella isipokuwa “*winding up*” *document/form*. Je, kuna ukweli gani katika jambo hili? Kama ni kweli Mheshimiwa Waziri anaeleza nini kuhusu hali hii ya nyaraka muhimu kama hizi kupotea *Brella*?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nyaraka zote muhimu zipo Serikali iko tayari kuziwasilisha kwa Katibu wa Bunge ili ziweze kuwekwa kwenye *archive/library* ya Bunge ili Waheshimiwa Wabunge wanaohitaji waweze kuzipitia kwa lengo la Wabunge kutimiza wajibu wao wa kusimamia Serikali kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa mjadala wa Richmond hali kama hiyo ilitokea na nyaraka muhimu za usajili zinasemekana zilipotea. Je, Serikali sasa inasemaje kuhusu upotevu wa nyaraka hizo muhimu za usajili wa kampuni ya Richmond iliyokuwa inachunguzwa na Kamati Teule ya Bunge? Kama zimepatikana, Mheshimiwa waziri yuko tayari kuziwasilisha kwa Katibu wa Bunge kwa lengo la kuwekwa kwenye *archive* ya Bunge?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati teule, pamoja na nyaraka nyingine barua iliyokuwa inasema kuna mtumishi wa *Brella* aliyezinyofoa nyaraka kwa lengo la kuficha ukweli na kuwa mtumishi huyo kama bakshishi amejengewa nyumba maeneo ya Chang’ombe Wilaya ya Temeke. Je, Wizara imefanya uchunguzi na kumtambua mtumishi huyo? Kama imegundua, amechukuliwa hatua gani? Kama uchunguzi huo haujafanyika, Mheshimiwa Waziri anatoa kauli gani kwa Bunge hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Sheria ya Vileo ya mwaka 1968 (RE 1971) kuhusu sera za kufungua na kufunga *bar* inalalamikiwa sana na wadau mbalimbali kama inavyoonekana kwenye magazeti, mathalan, Nipashe 1 August, 2003, “Wizara Yachunguza Saa za Kufunga Baa” na hakuna lilitotokea tangu wakati huo na tena 27 Februari, 2004 “Chama cha Wenye Mabaa Chalia na Sheria”, kilio hicho nacho hakikufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ina takriban mabaa na *ma-pub* milion moja bila kuhesabu hoteli, *guest* zinazouza vimeo, stoo bubu zinazofanya kazi bila leseni. Mabaa na *pub* hizo zimeajiri wahudumu (wafanyakazi) wengi sana, hivyo ni nafasi ya ajira kwa vijana wengi, japo katika mazingira magumu sana. Hivi karibuni Serikali imetangaza kima cha chini cha mishahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo yote, kwa sheria ya 1968 (RE) *bar* hizo zinatakiwa kufunguliwa saa 12.00 jioni hadi saa 5.00 usiku, yaani muda usiozidi masaa manne ya kazi (kuondoa muda wa maandalizi ya kufungua na kufunga).

Mshahara wa kima cha chini ni Sh. 80,000/= jambo ambalo ni gumu sana kwa fedha hizo kupatikana kuwalipa wahudumu wote kwani mauzo ni wastani wa *crate* nne tu kwa muda huo. Matokeo ni vijana wengi kupunguzwa kutokana na tatizo la malipo na hivyo vijana wengi watapoteza ajira. Serikali kwa sheria, hiyo nayo inapoteza mapato kwa vile muda wa saa 12.00 ni “odd”.

Katika nchi nyingi, *bar* zinafunguliwa toka baada ya saa rasmi ya kazi – lengo ikiwa ni wafanyakazi wasishawishike kwenda kunywa wakati wa kazi. Hivyo hakuna sababu *bar* kutofunguliwa tangu saa 10.00 alasiri na kufungwa angalau saa 6.00 usiku.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ilivyo hivi sasa, baa nyingi zinafunguliwa, watu wanaendelea kunywa kinyume na sheria na hakuna anayeweza kusimamia. Kwa nini tuwafanye watu wetu wavunje sheria? Mtindo wa sasa unaruhusu rushwa na pia Serikali kupoteza mapato yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mtindo wa kufunga saa 5.00 usiku kucha pombe inanyweka kwenye “*night clubs*” bubu manyumbani kwa watu, jambo linaloleta usumbufu mkubwa kwa raia na pia kuikosesha Serikali mapato halali. Kutokana na hayo, Je, Serikali itafanya mabadiliko makubwa sheria hiyo ya 1968 (RE) lini ili kuendana na mazingira ya sasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, natanguliza shukurani za dhati.

MHE. JOEL N. BENDERA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam wa Wizara hii, kwa hotuba nzuri, ilioandalialiwa kitaalam na kuwapa moyo Watanzania walio wengi nchini. Ninawatakia kila la kheri katika utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu nitauelekeza hasa katika kufufua Kiwanda cha Matunda Korogwe (*TANGOLD*). Korogwe na Mkoa mzima wa Tanga, unalima sana matunda na kiwanda kilichokuwa kinategemewa kusindika matunda ni *TANGOLD* Korogwe.

Kiwanda hiki kimeshindwa kusindika matunda toka mwaka 1994. Toka nimeingia ndani ya Bunge hili mwaka 1995, nimekuwa nikifanya juhudhi kubwa ya Serikali kufufua kiwanda hiki lakini hadi hivi sasa juhudhi hizo zimegonga mwamba.

Najua sasa hivi Serikali imejitoa kwenye biashara lakini nimejitahidi kutafuta wawekezaji mbalimbali ili wakifufue kiwanda hiki, mpaka sasa mwekezaji wa uhakika hajapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu ninaomba Wizara isaidie sana kupatikana kwa mwekezaji wa Kiwanda hiki ili kuokoa matunda yanayooza kwa ujumla.

Wapo wawekezaji wazalendo waliojiteza kukifufua kiwanda hicho, lakini cha kusikitisha wanakatishwa tamaa na urasimu uliopo ndani ya Wizara ya Viwanda na

wengine wengi wameleta maombi Wizarani; sasa ni zaidi ya mwaka hawapati majibu ya kufanikisha zoezi hilo. Hivi ni kwa nini hali hiyo inajitokeza?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba majibu kwa suala hili muhimu. Mimi naamini kiwanda cha *TANGOLD* Korogwe kikifufuliwa, kitaondoa umaskini wa wananchi wetu wa Mkoa wa Tanga, ambapo baada ya zao la mkonge kudorora sasa zao wananolitegemea kiuchumi ni matunda. Kwa bahati nzuri, wakazi wote wa Mkoa wa Tanga wanalima sana matunda hasa machungwa, maembe na nyanya.

Ninaomba sana wananchi hawa walijitokeza kuwekeza, Wizara yako iwapatie kibali. Wananchi hawa sasa wameanza kukata tama, tuokoe kiwanda hiki sasa kinakuwa gofu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. KABUZI F. RWILOMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Pamoja na kuunga mkono, napenda niiombe Wizara itupie jicho maeneo ya pembezoni katika kuwawezesha kimaendeleo.

Geita kuna matunda mengi yanaoza ovyo, kuna mananasi ya kutosha na matikiti maji yanaoza. Nashauri Serikali ifikirie kuwekeza katika kiwanda cha kusindika matunda (juice), badala ya kuagiza juice kutoka nje. Hili litainua kipato cha nchi na wakulima mazao hayo badala ya kuyaacha yakaoza. Naiomba Serikali ijenge kiwanda cha kuchenjua dhahabu. Dhahabu iwe *processed* hapa badala ya kupelekwa dhahabu ghafi. Kiwanda hicho nashauri kijengwe Geita.

Kwa kuwa eneo la Katoro – Geita ni maarufu kwa biashara na hivi sasa wafanyabiashara wa mchele wanatoka Rwanda, Burundi, Uganda na DRC; kwa nini lisijegwe Soko la Kimataifa eneo la Katoro Geita ili kuingiza pesa za kigeni?

Katoro kumekuwa na uvamizi wa mara kwa mara kwa sababu watu huweka pesa zao nyumbani; kwa nini Serikali isizishauri benki kama NBC, CRDB na NMB kujenga benki Katoro ili wanachi waweze kutunza pesa zao?

Kwa kifupi tunaomba tupatiwe kiwanda cha matunda Geita; kiwanda cha kuchenjua Dhahabu Geita; Soko la Kimataifa Katoro; na Benki Katoro.

MHE. ANNE K. MALECELA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nianze kwa kuwapongeza kwa dhati Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote, kwa kutuwasilishia hotuba hii ya Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kuunga mkono hoja kabla sijapitiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa lolote lile duniani ili lipige hatua mbele kiuchumi ni lazima na ni muhimu lijikite katika mfumo wa uzalishaji wa kutumia viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda ni kichocheo kikuu cha maendeleo ya nchi. Maendeleo kiuchumi duniani yalianzia Ulaya kati ya Karne ya 14 hadi ya 17. Maendeleo hayo ya kiuchumi yaliendelea kusogea Amerika ya Kusini, Amerika ya Kaskazini, Australia, Asia na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kichocheo kikuu hasa kilichopelekea maendeleo ya kiuchumi kule Ulaya na kadhalika ni pale tu wenzetu wa Ulaya walipoamua kwa nguvu zao zote, kuachana na mfumo wa kuuza mazao ghafi na kuyasindika kupitia viwanda. Hivyo, viwanda ndiyo vilivyochoea maendeleo ya kiuchumi Ulaya wakawenza kuzalisha kwa wingi na kuwa na ziada ya kuuza nchi za nje kwa wingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ziaidi ya asilimia 80 ya Watanzania ni wakulima. Vilevile ni vyema tukakiri kwamba, Watanzania hawa pamoja na kujitahidi sana katika kilimo, lakini wanazidi kuwa maskini na kupoteza nguvu ya kupanua kilimo chao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu kubwa inayowasababishia wananchi wetu kuwa maskini ni bei ndogo wanayoipata kwa kuuza mazao ghafi. Bei wanayopewa na wafanyabiashara ni ndogo na hailingani na kazi wanayoifanya. Ili tuwakomboe wakulima ambao kilimo chao kinazidi kuwaleta umaskini ni vyema sasa tukaanza operesheni maalum, yenye *timeframe* ya kujenga viwanda vidogo kule kote ambako Watanzania wanazalisha mazao ambayo yanaweza kusindikwa kama vile Kahawa, Chai, Katani, Mboga, Matunda, Ngano, Mahindi, Tangawizi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna jambo lisilowezekana, iwapo Wizara ya Viwanda itaweka nia thabiti, mikakati kivitendo na kutayarisha operesheni maalum. Kinachotakiwa hapa ni kushirikiana kwa nguvu zetu zote; Serikali Kuu; Halmasahuri zetu; Wabunge; na Wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ni Taifa changa; ni vyema tukajikita sana katika kuanzisha viwanda vidogo vya usindikaji, ambavyo vitakuwa ni mali ya wananchi wenyewe kupitia ushirika na kuhusisha *SIDO* kuliko kujikita katika viwanda vikubwa, kwani hivi vitatulazimisha zaidi kujikita kwa wawekezaji kutoka mataifa makubwa. Kwa utafiti wangu, wawekezaji wakubwa wao wanafaidi sana katika uwezekaji kwa nchi maskini kama Tanzania kuliko atakavyofaidika Mtanzania, kwani naye nia yake kubwa itakuwa ni kupata faida kubwa sana, bila ya kujali kama Mtanzania (mkulima maskini) anafaidika au la.

Mheshimiwa Naibu Spika, naisihi Serikali yetu iamue sasa kuwaondoa Watanzania maskini ambao ni wakulima katika mfumo wa kuuza mali ghafi na kuingia katika usindikaji – Operesheni Maalum yenye muda maalum na tuihusishe *SIDO* kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipounda *SIDO* kisheria, madhumuni yake ilikuwa ni kuiwezesha ifanye kazi ya usindikaji na kuongeza thamani ya mazao na hivyo kumkomboa Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, *SIDO* ina uwezo mkubwa wa usindikaji uwezo mkubwa wa usindikaji wa nafaka, matunda na mboga. Ina uwezo mkubwa sana wa kufundisha teknolojia ya jinsi ya kusindika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi Jimboni kwangu Same Mashariki, tuna *project* nzito ya kujenga kiwanda kidogo cha kusindika Tangawizi, ili tuiongezee thamani yake tuweze kuiiza nje ya nchi na ndani. Halmashauri za Wilaya zina uwezo mkubwa sana wa kusimamia hili na Wabunge wana uwezo mkubwa sana wa kuwashamasisha wananchi wajunge kwenye ushirika na kuchangia ujenzi wa viwanda vidogo vyta kusindika mazao. Kwa kutumia maelekezo kutoka *SIDO* na kutumia nguvu zao za hali na mali; na iwapo Serikali Kuu itawaunga mkono wananchi hawa; wana uwezo wa kujenga viwanda vidogo na inapobidi watakopa pia benki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ianzishe operesheni maalum ya kuwashamasisha ujenzi wa viwanda vidogo vyta kusindika mali za wakulima wenyewe na kwa kutumia *SIDO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MGANA I. MSINDAI: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wengine wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kuendeleza Viwanda, Biashara na Masoko hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwasaidia wakulima wadogo wadogo wa alizeti wa Mikoa ya Singida, Manyara, Dodoma, Arusha, Shinyanga na mikoa mingine inayolima zao la alizeti; Serikali irudishe haraka sana asilimia kumi ya mafuta yanayotoka nje ya nchi na kuingizwa hapa nchini. Nafahamu kabisa kwamba, lengo la Serikali ni kuwawezesha wananchi kuondoa umaskini kwa kufuta kodi hiyo, maana yake mafuta mengi yataingizwa kutoka nje; hivyo kuwaumiza wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa umefika wakati wa Serikali kutafuta bei nzuri ya mazao yetu kama karanga, giligilani, alizeti, kunde, mtama na mazao mengine yanayolimwa mikoa kame. Pia tunaomba bodi itakayoshughulikia uzalishaji na uuzaaji wa mazao haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa umefika wakati kwa Serikali kusambaza viwanda vipyta vinavyoanzishwa kwenye mikoa mbalimbali kuliko kuvirundika Dar es Salaam, Tanga, Moshi, Arusha, Mwanza na Mbeya tu.

MHE. ERNEST G. MABINA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Pili, napenda kumpongeza Waziri Mheshimiwa Mary Nagu, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wafanyakazi wote wa Wizara hii, kwa kazi wanayoifanya ngumu na kwa mazingira yasiyoridhisha, lakini kwa umahiri wa utendaji kazi wao; inaonekana kama rahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilayani Geita wananchi wanajishughulisha na shughuli nyingi za uzalishaji kama vile kilimo; uvuvi; ufugaji; madini kwa wachimbaji wakubwa na wadogo; na wafanyabiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na shughuli za Wananchi wa Geita, tunaiomba Wizara hii iitupie jicho Wilaya hii kwa kuwa hakuna kiwanda cha aina yoyote wala soko kwa ajili ya bidhaa zinazozalishwa Wilayani kwetu. Napenda kuiomba Wizara ijenge angalau viwanda viwili kama ifautavyo:-

Kama nilivyoainisha kuwa, Geita tuna wawekezaji katika shughuli za madini wakubwa na wadogo na wakati shughuli hizi zinafanyika, dhahabu nyingi zinatoka kama *raw material* na kupelekwa nje kwenye masoko ambayo hayaaminiki hasa kwa wachimbaji wadogo wadogo. Kwa nini Wizara isijenge kiwanda cha kuchakata dhahabu kutoka *raw material* hadi *finished goods*, pamoja na kuweka soko la kimataifa la dhahabu liwe Geita kwa dhahabu ya Tanzania nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Geita ina matunda mengi sana hasa mananasi na maembe ambayo inapofika wakati wa msimu wa mavuno matunda haya yanakosa soko kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba Wizara ijenge kiwanda cha matunda Geita, kwa matunda yote ya Kanda ya Ziwa ili kuweza kunusuru matunda yanayooza na kuwakosesha ajira na kuditimiza uchumi wa Wananchi wa Geita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mantiki hiyo, naomba mambo matatu katika Wizara hii kama ifuatavyo: Kiwanda cha kuchakata dhahabu kutoka *raw material* hadi *finished goods*; Soko la Kitaifa la bidhaa zinazotokana na dhahabu liwe Geita kwa Tanzania nzima; na kiwanda cha matunda yote yanayopatikana Kanda ya Ziwa kiwe Geita.

MHE. AZIZA S. ALLY: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ishirikiane na *SIDO* kuweza kuangalia *SIDO* iweze kuongezewa pesa kwani ndio inayofanya kazi na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwepo kwa utaratibu wa kuangalia viwanda vidogo vidogo ambavyo vinafanya kazi huko vijijini mfano, wakulima wa alizeti wameanza kununua mashine za kukamulia mafuta ya alizeti na karanga; kwa nini Wizara haiandai taratibu za kuomba Serikali ili kuondoa kodi kwenye mashine hizo ambazo zinasaidia wananchi kupata mafuta bora na mazuri kwa afya zao?

Wajasiriamali wanaosaidiwa na Waheshimiwa Wabunge, wapewe kipaumbele huko Wilayani mwao, kwani wananchi wengi hulalamika kutoshirikishwa na kupata mikopo ambayo itawasaidia kwa muda mrefu na kusaidia ili kuendelea wananchi hawa wawe na ujasiriamali endelevu.

Naomba Mheshimiwa Waziri anijibu; kwa nini mgawanyo wa kutoa elimu ya wajasiriamali hutofautiana katika kila mkoa na mikoa mingine kama Tabora kutopata elimu hiyo mfano ya utengenezaji wa batiki?

MHE. CASTOR R. LIGALLAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda nimpongeze Waziri, Naibu Waziri, pamoja na Katibu Mkuu, kwa hotuba yenye mtiririko mzuri.

Mchango wangu utahusu Bodi ya Mazao mchanganyiko. Mchakato mzima wa kuanzisha Bodi ya Mazao Mchanganyiko, unategemea Sera ya Masoko ambayo inashughulikiwa na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko.

Katika hotuba yake ya bajeti, Waziri wa Kilimo alitueleza kuwa Bodi hii itaaniszwa mara Wizara hii itakapomala mchakato wa kutengeneza Sera ya Masoko. Mchakato ambao ulikuwa umeripotiwa kukaribia kukamilika.

Mahitaji ya mazao yote ambayo yanahitajika kwenye soko la *AGOA*, yanategemea sana kuwa na chombo cha kushughulikia mazao hayo.

Wenzetu nchi jirani wame-exploit soko hili la *AGOA*, jambo ambalo halitawezekana bila ya kuwa na chombo kiunganishi kitakachosimamia bei, masoko na namna bora ya uzalishaji. Mazao kama ufuta, alizeti na kakao yanazidi kuchukua nafasi kubwa katika uchumi wa nchi yetu.

Namwomba Waziri katika majumuisho yake, atueleze amefikia wapi na mchakato wa sera hii ya masoko ili Wizara ya Kilimo iweze kuanzisha Bodi hii ya Mazao Mchanganyiko (*Mixed Crop Board*), kama ilivyokuwa *GAPEx* zamani.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam wao wote, kwa kuandaa bajeti na kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu. Hata hivyo, nina mambo machache ya kuchangia:-

Mheshimiwa Naibu Spika, maisha bora kwa Watanzania, yatategemea sana uwezo wao wa kifedha wa kununua vifaa mbalimbali hususan saruji na mabati kwa ajili ya ujenzi wa nyumba. Leo hii bei za saruji na mabati ni kubwa sana; kwa mfano, mfuksa mmoja wa saruji kule Mbeya unauzwa kwa wastani wa Sh. 15,000 na bati huuza kwa kati ya Sh. 10,000 hadi 30,000, kutegemeana na futi na *gauge* ya bati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mtanzania gani hasa yule wa kijijini ataweza bei hizo? Naomba Mheshimiwa Waziri, atueleze nini mkakati wa Wizara hii katika kudhibiti bei za bidhaa hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni kumekuwa na wimbi wa vifaa vya viwandani visivyokidhi viwango kuingizwa nchini kutoka ng'ambo. Kwa mfano, vifaa kama pasi, vitasa vya milango, vifaa vya umeme, majembe ya mkono na kadhalika.

Vifaa hivyo vinaponunuliwa na mtumiaji hutumika muda mfupi kisha huharibika! Naiomba Wizara kutumia taasisi yake ya udhibiti wa vifaa vinavyoingia nchini, ihakikishe kwamba, bidhaa na vifaa mbalimbali vya viwanda vinavyoingia nchini, viwe na viwango vinavyokubalika kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Small Industries Development Organization (SIDO)*, bado haijapewa msukumo wa kutosha. *SIDO* haikui na haipewi pesa ya kutosha ili kujiendesha kwa ufanisi na kupanua shughuli zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama *SIDO* ingepewa msukumo unaostahili, ingeweza kuwa mkombozi wa wajasiriamali wadogo hasa vijijini ambako viwanda vidogo vingeweza kuanzishwa na hivyo kuwakomboa wananchi wengi. Naiomba Wizara na hususan Waziri, atueleze ni jinsi gani wamejipanga sasa ili kutoa msukumo mkubwa kwa *SIDO* ili iweze kutoa mchango mkubwa wa kumletea Mtanzania maisha bora kama inavyoiezwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Hata hivyo, ninapenda kuchangia machache kama ifuatavyo:-

(a) Nilituma ombi la Wafanyabiashara wa Wilaya ya Kasulu (*Kasulu Chamber of Commerce*) ili Wizara yako itume wataalam waje waendeshe mafunzo kwa wafanyabiashara ambao wapo *organized*. Ni kweli kwa sababu Wilaya ya Kasulu ipo mpakani mwa Burundi na *DRC*, bila shaka elimu hii ingesaidia sekta ya biasahra kupanuka na kukabiliana na changamoto zilizopo (mfumo wa ulipaji kodi, biashara ya nje na kadhalika). Hadi sasa ombi hili lililotumwa kwa Katibu Mkuu 2006/2007 limegonga mwamba, tatizo ni nini? Basi 2008/2009 njoo ni Kasulu mtoe mafunzo.

(b) Upo ukweli na ushahidi kwamba, Biashara ya Tanzania imedhibitiwa na Wahindi (*Trade and Industry by 67%*) ni nini mkakati wa kuvunja *Trend* hii? Uko wapi mkakati wa kusaidia Watanzania wazawa kuanzisha biashara kubwa na viwanda? Je, Serikali haioni hatari iliyo mbele yetu ya kukumbatia Wahindi eti/na ni Watanzania wenyе asili ya Asia?

(c) Mkoa wa Kigoma ni kati ya Mikoa yenye rutuba sana, hali nzuri ya hewa na mvua ya kutosha. Mpango wa stakabadhi ghalani haujaanza na sioni dalili za Wizara yako ku-*facilitate* jambo hili. Mpango huu utaanzishwa lini katika Wilaya za Mkoa wa Kigoma na hasa Wilaya kubwa ya Kasulu, ambayo ni Wilaya ya Kilimo (kilimo cha mazao ya chakula)?

Je, Wizara yako pamoja na Wizara ya Kilimo, hamuoni kwamba ni wakati muafaka sasa kujenga maghala ya kuhifadhia nafaka na chakula ili kuboresha masoko ya wakulima?

(d) Taasisi ya kudhibiti bidhaa bandia iimarishe kwa kuongeza idadi ya wataalam na hasa wakaguzi wa mizigo katika maeneo mbalimbali ya mipaka ya nchi

yetu, pamoja na mpaka wa Kigoma Bandarini na Kituo cha Manyovu katika Wilaya ya Kasulu, kwa sababu ni njia kuu ya kwenda Burundi na *DRC*. Kwa sababu ya uhaba wa bajeti, basi kitengo hiki kishirikiane kwa karibu na *TRA* ili kusimamia bidhaa bandia ambazo zimezagaa katika nchi yetu.

Hongereni kwa kazi na chapeni kazi bila kuchoka. Naunga mkono hoja.

MHE. SAVELINA S. MWIJAGE: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nipate uafanuzi kwenye hotuba ya viwanda; sioni mikakati yoyote kwenye Wizara hii. Mkoa wa Kagera ni sehemu yenyе kusahaulika; je, viwanda viliyyopo vitaimarishwa lini; kwa mfano, *SIDO*, *Kagera Sugar*, *TANICA*, viwanda vya kahawa (Bukop Tanica na Bukoba Tai), Mamlaka ya Chai? Viwanda hivi vinaendelea kusuasua.

Karagwe kuna viwanda vya watu binafsi, kwa nini Serikali isivitambue ili kuvipa nguvu wakulima waweze kuboresha kilimo cha Kahawa waache kuuza mazao hayo hasa kahawa ambazo ni mbichi kuzipeleka nchi jirani? Uganda nilishangaa sana soko wanaloza; je ni soko la wapi ni kwa nini Wizara hii isiandae au kuna mikakati madhubuti kwa wananchi hao wakauze huko kwenye bei nzuri?

Nimeona kwenye hotuba hii Mikakati mizuri tu; je, na Kagera imo kwenye mikakati kuhusu wajasiriamali wa maonyesho; wanawake, watoto na *SIDO*? Je, hizo pesa (2.5) na Kagera wamo?

Naomba nipate maelezo kuhusu matangazo ya wafanyabiashara ndani na nje ili na Mkoa wa Kagera uwemo. Je na mashine zilizoko kwenye hotuba ni Kagera waliopata au ni wapi? Je, ni lini Wizara hii itakuwa na mikakati madhubuti; kuwa na huruma na kuwapatia ajira Wananchi wa Mkoa wa Kagera soko la kuunganisha Mkoa mzima pamoja na nchi jirani kama Uganda wanavyo chukua mazao yetu (ndizi, matunda, pamoja na viwanda vya samaki, maharage, karanga, njugu mawe, mihogo na kadhalika)?

Je, wao wanauza wapi? Sisi pamoja na Serikali yetu tufanye mikakati tuuze wenyewe na kuingiza kipato kwenye nchi yetu na kuamua Wananchi wa Kagera na mikoa jirani. Naomba nipewe majibu.

Sisi tukiona mazao yetu yanavuka kwenda huko, turuhusu wananchi wetu wauze kuliko kuwabana kiasi kikubwa sana ili Serikali iwe inaandaa Viwanda na Masoko ya hapa nchini, pamoja na kuendeleza viwanda mikoani kwa mfano; Mtwara, Tanga, Moshi na Mwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ina mikakati gani ili kumaliza umaskini kwenye nchi yetu? Pamoja na hayo, naomba Wizara iwe macho na wawekezaji wa viwanda vyetu; wanashindwa kuviendeleza badala yake wanang'oa vifaa. Nimeona sehemu nyingi vinasuasua kama Tanga, Mtwara, Bukoba (Kiwanda cha Chai) na Mradi wa Liganga Mchuchuma. Je, Serikali ina mkakati gani kuhusu mashamba ya mpira?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba majibu. Namwombea mpendwa wangu, Mheshimiwa Waziri, bajeti yake ya kwanza ipite salama.

MHE. MERYCE M. EMMANUEL: Mheshimiwa Naibu Spika, nami pia naomba nichangie kwa ufupi, hotuba hii iliyoko mbele yetu ya Viwanda na Biashara. Naomba nimpongeze Waziri na Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara. Ninawapongeza pia Wakuu wa Idara wote, waliohusika kuandaa bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naomba nichangie hali halisi ya mlipuko wa bei viwandani kwa kasi kubwa mno. Mtanzania wa hali ya chini ni kweli kwamba, hivi sasa inamuwia vigumu mno kukabiliana na bei hiyo, hususan vifaa vyta ujenzi. Nashauri Serikali ijaribu kukabiliana na mfumko huo angalau bidhaa ziwe za kununulika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, Mkoa wa Shinyaga ni Mkoa wa Kwanza kwa ufgaji na kwamba, uzalishaji wa nyama au upatikanaji wa nyama unategemea Shinyanga na Mwanza. Vilevile ni kweli kwamba, Serikali inaendelea na mchakato wa kufungua kiwanda cha nyama Shinyanga. Ushauri wangu; naomba habari hii isiwe hadithi ya kila kikao, Serikali ifikie hatma sasa ya ufunguzi wa kiwanda hiki, kwani habari hii imekuwa ikitajwa mara kwa mara bila utekekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa hotuba ya Waziri amesema, Serikali inaendelea na mpango wa uanzishwaji wa Kiwanda cha Ngozi Mwanza. Kama nilivyokwishesema kuwa Mwanza na Shinyanga ni wafugaji wakubwa wa ng'ombe; ni kweli kuwa kiwanda hiki kitakuwa na uzalishaji mzuri zaidi ukilinganisha na ujirani wa mikoa hii ya wafugaji ikiwemo Arusha. Hivyo, naiomba Wizara ifanye hima ili kuhakikisha kiwanda hiki kinaanza kazi mapema na wafugaji waweze kufaidi uzalishaji huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam wa Wizara, kwa hotuba nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kauli ya Waziri katika maeneo yafuatayo:-

Bei kuwa za bidhaa muhimu zinazogusa wananchi wengi hasa Bati na Saruji; Serikali ina mkakati gani utakaosaidia bei ya bidhaa hizi ishuke ili wananchi wengi vijijini waweze kujijengea nyumba bora zahanati, shule na kadhalika?

Shirika la *SIDO* limewezesha Wilaya nyingi zipige hatua kubwa za maendeleo ya viwanda vidogo na usindikaji katika Wilaya ya hizo. Kwa sababu zifi hadi leo *SIDO* haioni umuhimu wa kuanzisha centre Wilaya ya Lushoto?

Ibara ya 74(a) inahusu zao la chai; hivi Serikali inashindwaje kutatua mgogoro wa Shamba la Kuni la Sakare, hali ambayo imezorotesha zao la chai na Kiwanda cha Chai Mponde Lushoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. YONO S. KEVELA: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Waziri, Mheshimiwa Dr. Mary M. Nagu, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Cyril A. Chami, Katibu Mkuu, Dr. Stargomena Tax Bamwenda, Naibu Katibu Mkuu, Dr. Floren S. M. Turuka na Wataalam wote wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko na Taasisi zake zote, kwa kazi nzuri na uchapaji mzuri wa kazi, licha ya bajeti finyu toka Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchumi wa nchi yoyote iliyoendelea ulianza na kilimo na kisha kuwa na viwanda. Serikali ielekeze nguvu na kuweka mikakati maalum katika kukuza na kuendeleza viwanda nchini. Je, Serikali imejipanga vipi wakati Wizara inapewa bajeti finyu?

Katika Wilaya ya Njombe, Mkoa wa Iringa, kuna muwekezaji wa kutoka Marekani, ameonyesha nia ya kuuandikia Mkoa na Wizara, kujenga kiwanda cha kutolea mbolea ya *organic* (mbolea ya mboji hai), kupitia *TIG Company Ltd* ya mzalendo wa hapa nchini. Naomba Serikali iweze kushirikiana na muwekezaji huyu ili kupata miundombinu ya umeme wa gridi na maji ya kutosha katika eneo husika. Eneo lipi katika Kata ya Wanging'ombe, Kijiji cha Mig'elenge, Njombe; amepewa ekari 150.

Pia naiomba Serikali iweze kuelekeza nguvu kwenye viwanda vya Arusha, Minjingu na vile vilivyoko Mtwara vya gesi ambayo vitatoa mbolea, kwani itakuwa nafuu kwa mkulima kupata mbolea ya bei nafuu.

Mfumo wa stakabadhi za maghala ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu. Mfumo huu pia uangalie na mazao mengine, ambayo ni muhimu kibiashara hasa zao la alizeti, kwani wakulima wananyonywa sana msimu wa mavuno. Kama ilivyo mpunga na korosho, bei ya debe la alizeti ni Sh. 6,000 hadi 8,000. Zao hili linatoa mafuta bora ya kula na hayana athari kwa mtumiaji. Hivyo, naomba Wizara itusaidie sana kupata Bodi ya Alizeti. Mikoa ya Iringa, Singida na Mikoa mingine inayolima alizeti watafurahia sana kuwa na Bodi hiyo. Alizeti ina *grade* mbalimbali.

Nashauri kwa vile na mimi ni mtaalam wa ugavi kama *an authorized supplies officer*, nilisajiliwa na Bodi ya Ugavi na Ununuzi (*NBMM*), naiomba na kuishauri Serikali iweze kuishirikisha sana Bodi hii hasa *Registration*. Dr. Tesha anaweze kutoa mchango mkubwa na wenzetu wa *PPRA* watumiwe kikamilifu kwenye Sheria ya Stakabadhi za Maghala.

MHE. MBARUK K. MWANDORO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii, kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam wote wa Wizara hii na taasisi zake, kwa hotuba nzuri na utekelezaji

bora wa sera, mipango na mikakati ya Wizara, pamoja na ufinyu mkubwa wa fedha kulingana na majukumu makubwa na yaliyopanuka ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni mtambuka, kwa maana kwamba, shughuli zake zinagusa na kuleta msukumo na athari kubwa, takriban kwa sekta zote za uchumi na sehemu kubwa ya Sekta za huduma za jamii. Vifaa vya kilimo na pembejeo za kilimo, ufügaji na uvuvi, pamoja na vifaa vya shughuli za migodini na usafirishaji wa bidhaa za sekta hizi, vinatokana na viwanda. Aidha, dawa kwa binadamu, wanyama na mimea zinatokana na viwanda. Vifaa kwa matumizi ya mashulenii, mahospitalini, ofisini, viwandani na sehemu mbalimbali, kwa sehemu kubwa vinatokana na viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa kuzingatia hayo, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, imeitambua Sekta ya Viwanda kama Sekta Kiongozi, ambayo inastahili kipaumbele maalum; kimipango na kirasilimali. La kusikitisha ni kwamba, kihalisi si Wizara hii wala si taasisi zake, zinapewa kipaumbele kinachostahili kimipango au kirasilimali. Hapana budi Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, pamoja na taasisi zake, kupewa kipaumbele kama ilivyobainishwa na Ilani ya Uchaguzi ili iweze kuwa kichocheo cha ukuzaji wa uchumi kwa kasi kubwa zaidi na kuleta Mapinduzi ya Kilimo na Mapinduzi ya Viwanda; hivyo, kuongeza Pato la Taifa kutokana na kuongezeka thamani ya bidhaa zetu, kuongeza ajira na kuimarisha sekta nyingine za uchumi kwa jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya maelezo haya ya jumla, ningependa kusisitiza yale yaliyobainishwa na Kamati ya Viwanda na Biashara kuwa, Taasisi za Utafiti na Maendeleo kama vile *CARMATEC*, *TIRDO* na *TEMDO* ni muhimu sana kwa uboreshaji wa teknolojia na michakato ya uzalishaji katika Sekta ya Viwanda, Kilimo na Sekta nyingine za uchumi. Matarajio ya matokeo ya utafiti wa taasisi hizi ni kuongeza tija katika uzalishaji na ubora wa bidhaa zinazozalishwa viwandani na sekta nyingine za uzalishaji. Shughuli hizi ni muhimu kwa taifa letu kuerekana na utegemezi na kuhimiza ushindahi mkali katika dunia hii ya utandawazi. Kwa kuzingatia haya, taasisi hizi za utafiti na Maendeleo ya Viwanda na Sekta nyingine za uchumi, zinastahili kipaumbele cha juu zaidi kimipango na katika kupatiwa rasilimali. Mgao wa fedha zinazopatiwa taasisi hizi hivi sasa haziwezi kuwezesha taasisi hizi kuleta *modernisation* ya uchumi wa kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, taasisi za maendeleo ya viwanda zikiwemo *NDC* na *SIDO* zina umuhimu mkubwa kwa maendeleo ya viwanda mama na viwanda vidogo hapa nchini kwetu. Historia inatoa mifano mingi ya michango ya taasisi hizi hapa Tanzania.

Kutokana na mazingara mapya na majukumu yaliyonayo taasisi hizi hivi sasa hapana budi taasisi hizi zikapewa fedha na vitendea kazi vya kutosha ili taasisi hizi ziweze kuchangia kama inavyotarajiwa. Vinginevyo, dhamira ya kujenga na kuendeleza viwanda mama hasa kupitia Miradi ya Liganga na Mchuchuma na kuendeleza ujasiriamali kwa upande wa viwanda vidogo itakuwa ndoto tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu pia kuhusishwa kwamba, taasisi za ukuzaji viwanda na biashara kama vile *EPZ*, *SEZ*, *BET* na Vituo vya Biashara vya London na Dubai, hazipo kama mtindo (*fashion*), bali kama vyombo mahuhusi vya kujenga na kuendeleza uwezo wa Tanzania kiushindani katika nyaja ya uwekezaji na ukuzaji wa mauzo ya nje ya Tanzania. Shughuli za utafiti na ukuzaji wa Masoko hasa katika zama hizi za utandawazi ni ngumu sana na zenye gharama kubwa sana. Hivyo, tusizitarajie taasisi hizi kupata mafanikio tunayotarajia. Ili taasisi hizi zitekeleze wajibu wake kwa ufanisi na mafanikio tunayotarajia, hapana budi kwa dhati kabisa, kuzipatia taasisi hizi fedha, vitendea kazi na wataalam wa kutosha kulingana na hali halisi ya ushindani mkali uliopo duniani kote hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na maelezo hapo juu, kuna umuhimu mkubwa wa kuwa na wataalam wenye ujuzi na uzoefu wa kutoka katika Balozi zetu zote, hasa za nchi kwa nchi (*Bilateral*). Hapana budi wataalam hao wakawa na taaluma ya biashara na uchumi, badala ya utaratibu wa waambata wa biashara wasio na taaluma ya kibiasara. Aidha, wataalam hawa wapatiwe fedha za kutosha kwa ajili ya sampuli, ziara na shughuli nyingine za ukuzaji masoko, pamoja na mawasiliano ya kisasa kwa ukuzaji masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya mpya na changa ya Mkinga, ina nafasi nzuri ya kufaidika na huduma za Wizara hii kwa maendeleo ya viwanda. Aidha, ina nafasi nzuri ya kufaidika na mipango na mikakati ya biashara na masoko yaliyoainishwa katika Hotuba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa viwanda, Wilaya ya Nkinga ina mazao mengi ya kilimo yakiwemo matunda, samaki na viungo ambavyo tungeweza kuyaongezea thamani kwa kuyasindika. Hili ni eneo ambalo *SIDO* na *TIRDO* zingeweza kuhudumia Wilaya hii kuitia teknolojia sahihi, utaalamu na mikopo. Kwa upande wa viwanda vikubwa, moja ya eneo Wilaya ya Mkinga inatarajia kushiriki ni kiwanda cha mazao ya magadi soda. Matumaini yetu ni kwamba, changamoto zinazokabili uanzishwaji wa migodi ya kiwanda mama huko Manyara, zitapata ufumbuzi muafaka na kuanza uzalishaji mapema iwezekanavyo. Vile vile Wilaya ya Mkinga, ina nafasi nzuri kwa *EPZ*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Mkinga inasubiri kufikishwa kwa mfumo wa stakabadhi za maghala Wilayani hapo mapema iwezekanavyo, hasa kwa zao la korosho. Aidha, hatua za ujenzi wa Soko la Kimataifa la Segera litakuwa na manufaa makubwa kwa Wilaya ya Mkinga endapo litajengwa mapema iwezekanavyo. Kwa upande mwengine, Wilaya hii ya mpakani, ingependa elimu na ufanuzi utolewe kuhusu ushirikiano wa Afrika Mashariki ili Wananchi wa Wilaya hizo waweze kufaidika na Jumuiya ya Forodha na hatimaye soko la pamoja la Afrika Mashariki. Vile vile uimarishaji wa magilio Wilayani hapo, sio tu kutachangia kuimarisha soko la ndani, bali pia kuimarisha biashara ya nje, hasa nchi jirani. Mchango wa Wizara na taasisi zake ni muhimu kwa kutekeleza azma hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. BERNADETA K. MUSHASHU: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu kwa kuandaa hotuba nzuri iliyoandalishi kitaalam. Nawapongeza kwa mafanikio makubwa mliyoyapata katika kipindi kilichopita na mipango mizuri iliyobainishwa kwenye bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanzisha utaratibu wa kutenga Maeneo Maalum ya Kiuchumi (*Special Economic Zones – SEZs*), kwa ajili ya uzalishaji ambao unalenga masoko ya ndani na nje. Vile vile Serikali inaendelea kuhamasisha uanzishwaji wa maeneo ya uzalishaji kwa ajili ya uuzaaji nje (*Export Processing Zones*) na uwekezaji katika viwanda ndani ya maeneo hayo. Kwa bahati mbaya, Mikoa ya pembezoni kama Mkoa wa Kagera, mipango mizuri kama hii inavyoanzishwa, Mikoa hii husahaulika au hukumbukwa mwishoni.

Ili kufanikisha mipango hii, lazima Serikali iwekeze kwa kiwango kikubwa, kuhakikisha kwenye maeneo haya kuna miundombinu inayohitajika, ili kuvutia wawekezaji wa nje na ndani. Je, ni maeneo gani yametengwa kwa ajili ya *SEZs* na *EPZ*, katika Mkoa wa Kagera? Je, kuna maandalizi gani ya kupeleka miundombinu husika? Ikumbukwe wazi kuwa Mkoa wa Kagera umepakana na nchi jirani za Kenya, Uganda, Rwanda, Burudi na Congo, DRC. Hivyo maeneo kama haya (*EPZ, SEZs*), yanageainishwa Mkoani Kagera, Tanzania ingeweza kufaidika zaidi. Ninapenda Waziri anieleze katika *SEZ* na *EPZ*, Mkoa wa Kagera utahusikaje na wananchi wake watafaidikaje?

Mheshimiwa Spika, nchi ya Tanzania imebahatika kupata rasilimali ardhii. Sehemu nyingi za nchi hii, zina rutuba, mvua za kutosha na wakulima wanalima matunda na mboga za majani kwa wingi lakini matunda mengi wakati wa msimu yanaozea mashambani, magulioni kwa sababu ya kuuza mazao ghafi. Hivi kweli tumeshindwa kuendeleza viwanda vidogo vidogo ili mazao yasindikwe ili kuuzwa yakiwa yameongezwa thamani? Kwa kufanya hivyo, tutaongeza kipato kwa mkulima na kuinua uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kagera, hususan Bukoba vijijini Misenyi, Karagwe na Muleba, ni wakulima wazuri wa machungwa, matunda ya *passion*, maembe, *avocado* na ndizi. Ndizi sasa zinaliwa duniani kote, ndizi vile vile zinaweza kutengeneza *juice, wine, konyagi* na *whisky*. Wakazi wa Mkoa huu, wameendelea kuwa maskini kwa sababu hawana elimu ya namna ya kuziongeza thamani ndizi zile na vile vile hakuna viwanda vya usindikaji labda kiwanda kidogo cha *Mali Juice* kilichoko Muleba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri anieleze, Serikali ina mpango gani wa kuleta wataalamu na viwanda ili mazao kama ndizi na kadhalika yasindikwe na hivyo kuboresha hali ya kipato cha wakazi wa Kagera?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MUHAMMAD A. CHOMBOH: Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuanza kwa kutoa pongezi zangu kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa hotuba yao nzuri ya bajeti ya mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu ni kuhusu kuendeleza au kutekeleza sera ya Serikali yetu ya kufungua masoko ya biashara na mazao yetu hapa nchini ili kukuza kipato cha wakulima wetu kote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, imekuwa ni tatizo sugu kwa Serikali yetu kupanga mipango mizuri ya maendeleo lakini utekelezaji wake ni mbovu au hautekelezwi kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa soko la matunda la Segera (Tanga) na lile la Makambako (Iringa), ni muhimu sana kujengwa sasa ili tuweze kuwanufaisha wakulima wetu wafanyabiashara na kukuza uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. HEMED MOHAMMED HEMED: Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia siku ya leo na kuliona jua hali nikiwa mzima, *Alhamdulillah!*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake iliyojaa sura ya nuru kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia maelezo ya Waziri, ni vema Watanzania tuenzi vitu vyetu vinavyozalishwa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kujuua haya, nami nitoe mchango wangu katika hutuba husika kwa kuanza kuzungumzia suala la upandaji wa mafuta nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, upandaji wa mafuta siku hadi siku, ndio chachu ya upandaji wa umeme nchini. Kitendo hiki ndicho kinachopelekea ughali wa vitu vinavyozalishwa na viwanda vyetu nchini kwani gharama za uzalishaji, inapelekea ughali wa bidhaa zetu viwandani. Ili tufikie maisha bora kwa kila Mtanzania, ni vema Serikali ikemee upandaji wa mafuta na umeme ili tumwezeshe Mtanzania kutumia bidhaa zinazozaliwashwa na viwanda vyetu nchini. La kusikitisha, viwanda vingi hapa nchini vinafanya kazi zake kwa kutumia nishati ya gesi asilia katika uzalishaji wake, lakini bado bei ya vitu vya viwanda hivyo vimebakia kuwa lulu kibei. Kwa hili ni vema Serikali itueleze kwa kina sababu zinazopelekea ughali wa bidhaa hizo ilhali vinatumia gesi asilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya viwanda, tunaweza kusema mengi juu ya Serikali kutokuwa tayari kumsaidia mkulima wa nchi hii. Wakulima walio wengi hupata hasara kubwa kwa mazao yao kutokana na ukosefu wa viwanda nchini. Ni vema Serikali itueleze, kuna kigugumizi gani katika kufanikisha suala hili la viwanda?

Mheshimiwa Naibu Spika, ukosefu wa masoko, pia kunampelekea mkulima kuwa na njia za panya kusafirisha mazao yao nje ya nchi, Serikali imeshindwa kuwapatia

masoko wakulima wetu. Ni jambo la kushangaza sana kuona anapopatikana mnunuzi wa bidhaa za wakulima ambaye yuko nje ya nchi ni kosa kwa mkulima kuuza mazao yake kwa mtu huyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM, iliahidi kufanya mambo yafuatayo katika kumwezesha Mtanzania kuondokana na umaskini.

- (1) Kujuenga rasilimali watu wenye elimu na maarifa ya kufanya kazi mbalimbali;
- (2) Kufanya mapinduzi katika kilimo; na
- (3) Kufanya mapinduzi ya viwanda na miundombinu ya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo haya, ni ahadi kwa Watanzania. Je, ahadi hizi zimeteklezwa vipi kwa Watanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, mapinduzi ya kilimo na viwanda ndizo kazi za muhimu ambazo zikitekelezwa kwa ufanisi, zitaliwezesha Taifa kukuza uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo yangu hayo, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake, niseme Mwenyezi Mungu awape kauli thabiti kwa Watanzania wote nchini.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri yenye ufanuzi wa kina kuhusu Wizara yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Pamoja na kuunga mkono hoja hii, naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kwa kuwa hivi sasa wananchi wa Mkoa wa Dodoma, wameitikia wito wa Serikali wa kuzalisha zaidi zao la zabibu na wananchi wanalima mashamba makubwa ya zabibu, tatizo kubwa ni soko la kuuza zabibu na kwa kuwa Mkoa wa Dodoma kuna kiwanda kikubwa cha *DOWICO* na kiwanda hiki ndicho kilikuwa kinanunua zabibu za wakulima wa zabibu na hivi sasa kiwanda hicho cha *DOWICO* kimekufa na hakifanyi kazi kwa muda mrefu. Je, Serikali imeweka mkakati gani wa kufufua kiwanda cha *DOWICO* ili wakulima wa zabibu wa Mkoa wa Dodoma wapate soko la kuuza zabibu zao? Je, kufufuliwa kwa kiwanda cha *DOWICO*, Serikali haioni kwamba vijana wa Dodoma watapata ajira?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hapa Dodoma kulikuwa na Kiwanda cha Magodoro na kiwanda hicho kilihamishwa Dar es Salaam lakini mmiliki wa Kiwanda hicho bado anatumia jina la Dodoma kama *Trade Mark* yake wakati kiwanda kipo Dar es Salaam. Je, kwa nini kiwanda hicho kisifufuliwe hapa Dodoma ili kutoa ajira kwa vijana wetu wa Dodoma?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. KABWE ZUBERI ZITTO: Mheshimiwa Naibu Spika, nimepitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri, nimeona maeneo ambayo yanatia moyo sana kuhusiana na uendelezai wa viwanda. *Idea ya Waterfront Industrial na Export Frontiers*, ni nzuri sana. Wasiwaso wangu ni kuwa mipango hii ni mungu sana na utekelezaji wake hauleti matumaini. Matokeo yake ni kuwa kila mwaka tunaimba mapato mapya.

Mfano, Serikali ilianzisha *EPZ* mwaka 2002 na baadaye mwaka 2006, ilianzisha *SEZ* baadhi yetu tulisema kuwa hii ni *impractical*. Leo Serikali inakubali (baada ya kupoteza muda mrefu) na kuanzisha *EDZ*.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujua maana maudhui ya Ibara 37 na 40 za hotuba yake kuhusiana na EPZ, SEZ na EDZ, zinapingana. *Will EDZ Act lead to repeal of EPZ and SEZ Acts?* Serikali iwe wazi katika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, *EPA – Economic Partnerships Agreements, EAC – EU – EPA*, nimefurahi kuwa hatimaye Serikali imekubaliana na hoja yangu ya muda mrefu kuwa tuwe na *EAC – EU – EPA* (Ibara ya 87 ya hotuba). Serikali ijifunze kuchukua hatua kwa mawazo yanayotoka pande zote za Bunge kwani imechukua muda mrefu sana kutekeleza ushauri huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kufahamu ripoti rasmi ya “*Impact Assessment*” ya *EPA* na hasa *revenue import* kama imekamilika na imeonesha nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni nini madhara ya *ki-revenue* katika *EAC Common Market* ndani ya *EAC – EU – EPA*? Kama madhara haya hayajulikana, warsha za Kikanda kuhusu *EPA* zinawaelimisha nini wananchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 94 ya hotuba inasema jasi ni *bauxite* – hii ni sahihi? Nadhani jasi ni *gypsum*, naomba nipatiwe tafsiri sahihi ili tuwe na *record* sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishauri Serikali kupitia Wizara ya Viwanda na Wizara nyingine muhimu, waanze kozi ya kushawishi *DRC* kuingia katika *protocol* ya *Common Market* na *EAC* ili Tanzania ifaidike na soko la *DRC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Wizara, sijaona ni vipi Wizara imejipanga kutekeleza mapendekezo ya Kamati ya Bomani yanayohusiana na *NDC* kwamba *NDC* kuwa *Resource Development Company* kuhusiana na kuendeleza *mineral resources* za Liganga na Mchuchuma. Hii kitu inayoitwa kasi mpya ni nini? Ina manufaa gani kwa Taifa?

Mheshimiwa Naibu Spika, *NDC* imelalamikiwa kuhusiana na kuuza nyumba zake kwa upendeleo. Kuna kina mama akiwemo Tunu Mwapachu ambapo nyumba waliyokuwa wanaishi, imevunjwa bila kuwapa kipaumbele wapangaji hawa, utatuzi wa suala hili umefikia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kupatiwa ripoti ya “*Impact Study of EAC – EU-EPA*” na pia *Impact Study* ya *EAC Common Market* katika muhtasari, matokeo yanaonyesha nini?

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata fursa hii ili nami niweze kuchangia hoja hii. Kwanza, nampongeza Waziri na watendaji wote, kwa hotuba nzuri na mpangilio wa kazi waliojipangia. La msingi ni kuwa waaminifu katika kuyatekeleza yote kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu kwa kuanza ni juu ya viwanda vidogo vidogo vilivyopo Mikoani. Viwanda hivi bado Wizara hajatoa ushirikiano wa dhati na hasa katika kuvisimamia na kuhakikisha vinatoa mchango mzuri katika uchumi wa nchi na kuinua vipato vya wananchi hasa wakulima. Mfano, viwanda vya kukamulia alizeti (mafuta) vilivyopo Mkoa wa Singida vinashindwa kukidhi mahitaji ya wakulima wa alizeti kwa kushindwa kuwa na mtaji wa kutosha kununua alizeti na hata kuongeza kilimo kwa zao hili. Hivyo, wakulima hulima kidogo tu kwa kuwa soko si zuri. Hivyo, Wizara isimamie na kutowabagua wenye viwanda hivi kwa kutowapa au kupata mikopo, wapewe sawa na wenye nazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ya pili ni kuhusu *COSOTA*. *COSOTA* hadi sasa haina bodi, kwa wajumbe waliochaguliwa, Waziri hajawaidhinisha. Hivyo namwomba Waziri awaidhinishe waliochaguliwa au atoe tamko la kuwaruhusu waliokuwepo mwanzo waendelee, ili waweze kufanya marekebisho ya sheria ya kuchagua au kuteua wajumbe wa bodi. Pia Sheria ya *COSOTA* iliyopo irekebishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, naomba Waziri atusaidie, sisi wasanii juu ya *COSOTA*, kwani inaonekana inachenga kutusaidia ipasavyo hasa pale matatizo yanapotokea. Sasa huenda ni kutokana na Bodi kutokuwa makini na kushindwa kusimamia haki za wasanii ipasavyo au lah!

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasononeshwa sana kuona wasanii wenzangu wanavyopata taabu hasa pale wanapotaka kuinuka kiuchumi na badala yake kudidimizwa na chombo cha Serikali (*COSOTA*). Je, Waziri anatoa tamko gani kuhusu kikundi cha ‘*Ze Comedy*’ ambacho kimezuiwa kufanya shuguli zake? Je, anaweza kuniambia hawezি kutoa tamko lolote ili ‘*Ze Comedy*’ wasaidiwe na *COSOTA* warudi kazini? Je, huu si uonevu?

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine wanafanya kazi, lakini hawa watoto wamepigwa kitanzi cha kutojipatia riziki zao kwa kosa ambalo mimi silioni. Tafadhalii Waziri kimbilio letu leo wasanii, toa tamko ili *COSOTA* waruhusu ‘*Ze Comedy*’ warudi kazini ama sivyo nitaomba kuleta hoja binafsi ili tuone haki iko wapi kwetu wasanii.

Naongea hivyo kwa kuwa na mimi ni mwimbaji (msanii/mwanamuziki), mikataba mibovu, elimu ya *COSOTA* hakuna na kuna mengi ya kuelimishwa juu ya haki zetu wasanii lakini hayawafikii walio wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha, naunga mkono hoja.

MHE. STEPHEN J. GALINOMA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kupongeza Wizara hii kwa bajeti nzuri inayoashiria msukumo mpya wa kuendeleza sekta hii. Nina mchango mdogo tu kama ifuatavyo:-

Kwanza, Jimbo langu la Kalenga halina viwanda isipokuwa kimoja tu cha kusindika maji/juice. Inasikitisha kwamba kiwanda pekee cha kutengeneza sigara kilikufa kutokana na “*corporate take over*” ambapo ni jambo la kawaida katika biashara lakini, je, haiwezekani kutafuta na kuhamasisha uwekezaji mbadala? Kwa maana hiyo, naiomba Wizara ijenge mazingira ya uwekezaji kwani tunalima tumbaku (malighafi) kwa miaka zaidi ya 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, sasa hivi tuna tatizo linalozidi kukua la vijana kwenda mjini kutafuta starehe na kazi ambazo ni adimu au hakuna. Matokeo yake ni pamoja na kuvunjika kwa maadili na uhalifu (*social disintegration and crime*). Njia mojawapo, ni kuboresha maisha ya vijana kuyafanya yafananefanane na ya mijini. Kwa hiyo, nashauri Serikali itafakari na kutekeleza mkakati wa makusudi kabisa kupeleka viwanda vijijini vitakavyoajiri vijana wetu. Tusikimbile viwanda vikubwa vinavyohitaji uwekezaji mkubwa, *SIDO* ni ndogo mno na kwa maoni yangu haikidhi hiki ninachosema. Itapendeza kama viwanda hivyo *medium –scale*, vingeanzishwa sehemu nyingi na kadri inavyowezekana vitumie mazao ya kilimo (*agro-based factories*) ili kuua ndege wawili kwa jiwe moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nina imani kubwa kwa Waziri Nagu, ukiwa na sifa ya kuwa “*a jack of all trades*” utaleta sura mpya katika mtizamo wa sekta hii. Ukombozi wa uchumi wetu uko katika sekta hii ikizingatiwa kwamba kilimo huenda kikapungua katika mchango wake katika pato la taifa kutokana na hali ya hewa isiyotabirika na kuchujuka kwa ardhi sehemu kubwa ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono na kuitakia Wizara hii kila la kheri na nitafurahi zaidi iwapo utaweza kujibu ushauri huu wakati wa majumuisho.

MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, Mheshimiwa Mary M. Nagu, (Mb), pamoja na Naibu Waziri, kwa kazi nzuri katika Wizara yao na kwa ushirikiano kuanzia kwako pamoja na watendaji wote pia na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda na Biashara na Masoko, chini ya usimamizi wa Mwenyekiti Abdusalam na wajumbe wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii ni nzuri lakini ina uchache wa fedha. Kwa hiyo kwa sasa itumike hii hii ili tujali msemo kwamba ‘kuwa na kidogo tugawane kidogo kidogo kuliko kuwa na kingi na kuanza kugombea’. Kwa hiyo, naiomba Serikali, fedha zitumike vizuri na zisimamiwe kwa sekta zote na kwa mwaka mwengine fedha za Wizara

hii iongezwe bajeti kwa maslahi ya Tanzania na iwe nchi iliyoendelea kwa viwanda na masoko na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, bidhaa bandia ndani ya nchi yetu, kumekuwa na matatizo mengi sasa kuhusu bidhaa bandia pia bidhaa hafifu na kuleta hasara na ajali, vifo, maradhi na mambo mengi kutokana na tatizo hili la bidhaa hafifu. Kwa hiyo, inakuwaje na kwa sababu zipi? Hata hivyo, naiomba Serikali, Wizara, kupitia bajeti hii, iwe makini na ihakikishe kwamba suala hili linakwisha ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu biashara na wafanyabiashara, naomba wafanyabiashara wawezeshwe zaidi na biashara zikue na wananchi wadogo wawezeshwe na mabenki na *SACCOS* na Vyama vya Ushirika mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, bei za vyakula na mambo ya ujenzi, mbona mfumuko wa bei ni mkubwa? Naiomba Serikali suala hili ilione na kulipatia ufumbuzi na kujali wananchi wetu wa chini hasa wakulima vijijini, bei zipunguzwe kwa mahataji ya yao ya lazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Magogoni na mimi naunga mkono hoja.

MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Viongozi wa Idara na watumishi wote wa Wizara hii, kwa kutuletea hotuba nzuri yenye kutia matumaini kwa wananchi. Mimi ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile Wizara hii imepewa majukumu makubwa na mazito, naiomba sana Serikali Kuu iongeze bajeti ya Wizara hii ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa sababu inashughulikia masuala mtambuka. Mkulima kule Rufiji atataka auze mazao yake na anunue bidhaa na mahitaji yake ya kila siku, kufikisha huduma hizi kwa wananchi nchi mzima, ni shughuli inayohitaji kujituma sana na fedha nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba viongozi wa Wizara hii, waanze kubadilika, kwanza uwiano wa viwanda kati ya miji/majiji na vijiji/miji vya Wilaya, ni mbaya sana. Takwimu za Afrika, zinaonyesha kuwa viwanda viko mijini kwa zaidi ya asilimia 80. Kupeleka viwanda vijijini/miji midogo, ndio liwe lengo kuu. Kuna haja ya kupeleka kiwanda cha kukamua matunda kule kule wanakolima sana matunda kama Bagamoyo/Chalinze kwa mananası, Muheza kwa machungwa na machenza, machungwa, Rufiji na Kilwa. Faida ya kupeleka viwanda vijijini na miji midogo, kutaleta maendeleo makubwa sana na miji mikubwa ibakie na viwanda vikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *SIDO*, tunaomba ifanywe tathmini nzuri ili ituonyeshe ni sehemu gani ya Mikoa yetu imepata bahati ya kupata huduma za *SIDO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa nchi hii ni kubwa basi *SIDO* itanuke (ipanuke), ili iwafikie wananchi wengi. Kule Rufiji sasa tumeahidiwa umeme mwaka

huu, nakuomba Mheshimiwa Waziri mwaka huu uwakumbuke wananchi wa Rufiji ili wafikiwe na baraka za *SIDO*. Aidha, tunaiomba Wizara iongeze bajeti ya *SIDO* ili itufikie na sisi wengine (*marginalized*).

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ya biashara, wananchi wengi hawajui biashara, wajasiriamali walio wengi hawajaua faida na hasara. Tunaomba Wizara iwe na mpango mahsuswi wa kufundisha elimu ya biashara kwa wananchi wa kawaida, hasa kule Rufiji ambako elimu iko chini.

Aidha, Serikali, ikubali kupeleka somo la biashara mpaka katika elimu ya msingi ili kama vijana wakifeli mitihani ya Darasa la Saba basi waweze kutumia elimu hiyo ya biashara katika maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba viongozi wa Wizara mumuunge mkono Waziri ili asaidie kuleta mabadiliko makubwa tunayoyatazamia katika ya biashara nchini. Ahsante sana, naunga mkono hoja 100%.

MHE. COL. FETEH SAAD MGENI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, ninaomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa hotuba nzuri waliyoiwasilisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Waziri, inagusa maeneo mengi muhimu ambayo endapo tutayashughulikia ipasavyo basi kweli uchumi wa nchi yetu utakuja juu na kuondoa umaskini uliopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia maeneo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, uimarishaji wa viwanda. Viwanda ndio njia moja kuu ya kuimarisha uchumi wa nchi yetu. Nchi za Ulaya zilinyanyua uchumi wake kwa mapinduzi ya viwanda. Tanzania ina rasilimali nyingi sana, ina matunda mengi ya aina mbalimbali, ina madini muhimu sana ya kuunda zana za kilimo na mambo mbalimbali ya kimaendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Kiwanda cha *SIDO*, tumeona jinsi tulivyokianzisha na kilileta mafanikio makubwa kwa upande wa kilimo na mambo mengineyo. Ninashauri mkazo mkubwa uwekwe katika kuimarisha viwanda vyetu vidogo vidogo na sasa lazima turejee kwenye hivyo viwanda vikubwa tuwekeze.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana tuimarishe viwanda vyta aina zote, turejee kwenye viwanda vyta kusindika nyama, samaki wa aina zote. Aidha, tuimarishe viwanda vyta matunda yetu pamoja na mafuta ya alizeti na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, masoko, suala la masoko lazima tuliiamarishe, lazima tuwe na masoko ya kileo kwa sababu sasa ni wakati wa ushindani wa biashara tutashindana vipi katika masoko huria na hasa katika soko la ushindani wa Afrika Mashariki na Masoko mbalimbali ya Afrika na duniani kote bila kuwa na masoko?

Ninashauri Serikali itumie nguvu zake katika kuwekeza katika masoko yetu kwanza ya ndani na tuelekee kwa masoko makuu ya nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango wangu huu ambao ni mchache sana, sasa kwa heshima kubwa, ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia.

MHE. GOSBERT B. BLANDES: Mheshimiwa Naibu Spika, bei ya mazao ya chakula kwa mfano ndizi na maharagwe, kabla sijaanza kuzungumzia bei ya mazao haya, kwanza nichukue nafasi hii kumpungeza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda Biashara na Masoko kwa hotuba nzuri sana aliyoasilisha leo hii. Ni hotuba inayoleta matumaini kwa Watanzania.

Pia nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kumsaidia Waziri na kwa umahiri wake wa kujibu maswali kwa umakini na ushahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, naomba nitoe machache kuhusu matatizo ya soko la ndizi na maharagwe yanayozalishwa Mkoani Kagera hasa Wilaya ya Karagwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Karagwe inazalisha maharagwe na ndizi kwa wingi, tatizo ni soko na bei ndogo sana inayokatisha tamaa wakulima. Bei ya mkungu wa ndizi unaokadirwa kuwa na kilo kati ya 25 – 50, inauzwa kati ya Sh.500 – 2,000 tu. Wanunuzi hawapatikani kwa urahisi kwani wanazalisha ndizi.

Pamoja na dunia kukumbwa na uhaba wa chakula, bado ndizi Wilayani Karagwe hazina soko. Uhaba wa soko lenye tija, imedumaza uchumi na wakulima wa Karagwe. Wimbo huu ni ule ule kuhusu maharagwe. Maharagwe yanazalishwa kwa wingi Wilayani Karagwe lakini bahati mbaya soko lake ni la kubabaisha. Debe lenye uzito wa kilo 20 - 25 linauzwa kwa Sh.4,000 – 5,000 tu! Kwa mantiki hiyo, tunaomba Serikali itutafutie masoko ya uhakika ya ndizi na maharagwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu bei za vifaa vya ujenzi kwa mfano bati na sementi, bei ya bati lenye futi kumi, *gauge* 28, linauzwa kati ya Sh.20,000 – 25,000/- Wilayani Karagwe. Bei ya mfuko mmoja wa cementi ni kati ya Sh.20,000 – 25,000=/. Hizi bei ziko juu sana. Tunaomba na tunashauri wamiliki wa viwanda hivi wafungue *depot* zao Mikoani kama wenzao wa viwanda vya bia na soda. Kwa kufanya hivyo, bei ya mabati na *cement* iwe ni moja kwa nchi nzima kwani kinyume na hayo Mikoa ya pembezoni kama Kagera, Kigoma na Mara, itadumaa ki-maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la *furniture* kutoka nje, hazina ubora wala uimara ingawa bei ni za juu sana. Pia *furniture* toka nje zinaua soko letu la ndani. Nashauri na kupendekeza *furniture* kutoka nje zipigwe marufuku kabisa. Wakati huo huo tupeleke watu wetu nje wajifunze namna ya kutengeneza *furniture* nzuri hasa upande wa *finishing*. Taifa letu linayo miti ya mbao ya kutosha lakina haina soko la uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, waliokuwa wafanyakazi wa Kiwanda cha Kuchonga Almasi Iringa (TANCUT ALMAS), baada ya kiwanda hiki kufungwa, wafanyakazi wake

ama hawakulipwa vizuri au hawakulipwa. Wafanyakazi hao wameathirika sana kwa kukosa mafao yao. Wengi wao wameshindwa kusomesha watoto wao, ndoa zao zimevunjika na wengine wamekufa na walio hai wana hali mbaya. Nashauri Serikali iende Iringa iwasikilize, iwalipe mafao yao haraka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. MASOLOWA C. MASOLWA: Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na wenzangu kwa kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara hii, kwa maandalizi mazuri ya hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu wa Wizara hii kiuchumi, fedha ilizotengewa hazitoshi hata kidogo kufanikisha malengo yake ukizingatia kuwa uchumi wa nchi iliyo imara hutegemea viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilianza vizuri miaka ya nyuma kwa kuanzisha/kujenga viwanda vingi nchini, viwanda ambavyo kama vingeendelezwa hadi leo uchumi wa nchi yetu ungekuwa katika hatua nzuri na ya kujivunia. Viwanda vingi vimekufa kabisa na vilivyopo uzalishaji wake si wa kuridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna haja ya kuangalia upya ubinafsishaji wa viwanda vyetu pamoja na kuwa karibu viwanda vyote vimebinafsishwa kwa wawekezaji, kuna haja ya kuwabana wawekezaji hao ambao wameshindwa kuviendeleza kama walivyoahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imejaliwa kuwa na Mikoa inayozalisha matunda kwa wingi kwa msimu mzima. Matunda hayo huishia kuoza tu kwa vile hakuna viwanda vyta kusindika matunda na *juice* inayotokana na matunda hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ichukue hatua za dhati za kutafuta jinsi gani ya kuanzisha viwanda japo vidogo vidogo vya kusindika matunda katika Mikoa ambayo matunda yanapatikana kwa wingi kwa mfano, Mikoa ya Morogoro, Tanga, Pwani na kadhalika. Kuanzishwa kwa viwanda hivyo, kutachangia pato la nchi, wananchi watapata ajira na wakulima wetu watapata soko la kuuzia matunda yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tunauza magogo nje, magogo ambayo hutengenezwa samani (*furniture*) ambazo nchi hizo hujipatia fedha nyingi za kigeni kwa kuuza samani hizo na wakati mwingine hata nchi yetu hununua samani hizo kwa fedha nyingi. Hivi ni kwa nini taasisi zetu za Kiserikali (Magereza, JKT na kadhalika), haziwezesewi kifedha ili zikaanzisha viwanda vya kutengeneza samani hizo na kuziua nje badala ya kuuza magogo yetu nje ya nchi kihasara? Ninaishauri Serikali iangalie upya suala la ununuza wa baadhi ya samani kutoka nje ya nchi ikiwezekana samani zote za ofisi zinunuliwe hapa hapa nchini ili kukoa fedha zetu za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Serikali kwa kuruhusu wafanyabiashara kuingiza saruji ya nje nchini ili kupunguza ughali wa saruji inayotengenezwa hapa nchini ambayo ilikuwa inapanda kwa kasi sana na hivyo Watanzania kushindwa kununua saruji

hiyo baada ya Afrika ya Kusini kuingia mikataba na viwanda vyetu nya saruji hapa nchini ya kuwauzia saruji hiyo kwa wingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishauri Serikali iendelee kuwaruhusu wafanyabiashara hao kuingiza nchini saruji hiyo hata Afrika ya Kusini watakapoacha kununua saruji hiyo kutoka kwenye viwanda vyetu baada ya kukamilisha mahitaji yao. Hivyo itasaidia sana kwa wananchi wetu kumudu gharama ya ununuzi wa saruji hiyo kwa vile upatikanaji wa saruji utakuwa hausumbui na biashara itakuwa ni ya ushindani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia iwaruhusu wafanyabiashara kuingiza bidhaa nyineza za ujenzi nchini kama vile batu na kadhalika ili kuondoa ukiritimba wa bidhaa hizo hapa Tanzania. Kuwepo kwa bidhaa hiyo, wananchi itawawekea mazingira mazuri ya kuwa na nyumba bora na maisha yaliyo bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania imekuwa jalala la kuuzia bidhaa hafifu na taka kuanzia miaka ya hivi karibuni. Pamoja na juhudini inazozichukua Serikali zikiwemo za kuziangamiza bidhaa hizo mara wanapozibaini, hata hivyo, bado kuna haja ya makusudi ya kurekebisha sheria zetu ili kuwawezesha wadhibiti wetu kuwapa uwezo wa kungia hadi kwenye maghala ya bidhaa zinazohifadhiwa na wafanyabiashara hao ambazo zinapenya kwa njia zisizo rasmi.

Aidha, Sheria iruhusu kukaguliwa kwa bidhaa zake au hafifu kwenye maduka yote na kuchukuliwa hatua kwa wanaouza bidhaa hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iweke Sheria ya kuzisusia bidhaa hafifu na taka zinazoingizwa nchini kwa kuijulisha nchi husika ilikotoka bidhaa hizo kimaandishi. Vinginevyo Serikali ijifunze kutoka nchi za wenzetu ni jinsi gani zinadhibiti uingizaji wa bidhaa hafifu na taka kwenye nchi zao ili tatizo hili liondoke. Vinginevyo nchi yetu itaendelea kuwa jaa la bidhaa hafifu na taka kitu ambacho kitawaongezea umaskini Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nondo zinazotengenezwa kiwanda cha Tanga, zinasemekana ni dhaifu Serikali inasemaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri na wafanyakazi wetu wa Wizara hii. Naiomba kukazia mambo yafuatayo:-

Kwanza, vipimo (*weight and measures*). Hivi karibuni kumekuwa na shinikizo la kupandisha bei ya pamba hadi kufikia Sh.500 kwa kilo. Tumevutana, leo tunaona bei imeanza kufikia Sh.520. Bei haijapanda, wanunuza walio wengi wanakarabati mizani ili kufidia kiasi cha bei iliyopanda. Huu ni wizi. Tunachouliza watumishi wa Idara ya Vipimo wako wapi? Kumezuka viwanda vidogo nya kukarabati mizani za pamba na udhibiti wa Serikali kwa jambo hili ni mdogo sana. Ili bei nzuri iwe bei nzuri kweli na siyo wizi kwa wakulima wanaojitahidi sana kulima, ni lazima Serikali iwe makini kuhusu suala hili la mizani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, mkakati wa kuhamasisha wazalendo kuwekeza katika viwanda. Nakubaliana na Mheshimiwa Waziri, viwanda ndiyo kichocheo cha kilimo. Wakulima wakijua mazao yao yatanunuliwa na viwanda, mazao yataongezeka. Kianzio kipo, viwanda vya pamba vimeleta ushindani katika kununua kwa ‘cash’ pamba. *Ginneries* nyingi Kanda ya Ziwa, ni chimbuko la viwanda vya kusindika mafuta ya kula. Mashudu yanachangia kutoa chakula cha ng’ombe ambayo kiwanda cha nyama kinahitaji. Aidha, maganda ya mbegu, yanatumika kwa wafugaji wa ng’ombe wa kuuza nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama historia inavyosema, miaka ya 1975/1980, tulifika kiasi cha kutumia asilimia 80% ya pamba yote kwa viwanda vyetu vya ndani. Wakati huo Serikali ilikuwa inasaidia kupekeka vijana wenye kusomea *Textile* nje.

Leo mpango huu haupo na ni kawaida kuona Wahindi na Wachina kufanya kazi ya utaalam wa *Textile*. Pamoja na *Universities* kuongezeka, hakuna chuo kinachofundisha fani hii. Serikali nyingi duniani, zina *affirmative action* kwa wawekezaji wazalendo. *South Africa*, viwanda vinavyojikita kusindika mazao, Serikali lilipa mishahara yote ya kiwanda kwa wafanyakazi waliotumikia viwanda vya *exports*. Najua kuna aina ya vivutio katika *EPZ* lakini taswira ya *EPZ* inajikita zaidi kwa wagensi. Nashauri utafiti ufanyike ili kupata vivutio zaidi kwa wazalendo ili wengi wapende kuwekeza katika viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, bidhaa za mitumba kama nguo ni adui mkubwa sana wa viwanda. Najua mitumba ni siasa zaidi wakati huu ambapo vitu vingi ni aghali sana. Aidha, biashara hafifu kutoka China, ni adui mwagine wa viwanda vya ndani. Kuna umuhimu kuimarisha ukaguzi wa *TBS* ili izuie badala ya kuchoma vifaa kwani fedha zimeishalipwa.

MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote kwa kazi nzuri. Hivyo naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, *SIDO* Shinyanga. *SIDO* Shinyanga ni kama imetelekezwa, hawana bajeti ya maana kupanua kazi zao na hivyo kuongeza ajira kwa vijana wa Shinyanga. Hivyo, naomba kuwepo/kuwekwe mpango wa bajeti endelevu kwa maendeleo ya *SIDO* Shinyanga. Hii itafanyika? Naomba jibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilichokuwa Kiwanda cha Soda Shinyanga - *Shinyanga Double Cola*. Naomba kufahamishwa, ni nani mliki wa kilichokuwa kiwanda cha soda Shinyanga (*Double Cola*)? Mmiliki huyu yuko wapi sasa? Nauliza haya kwa sababu juhudhi zangu za kuyaelewa haya hazijafanikiwa. Tunataka kuelewa ni nani na mahali alipo ili sisi wa Shinyanga tuweze kujua mpango wake wa kutumia eneo la kiwanda kwa kuendeleza kiwanda/viwanda pale. Namwomba Mheshimiwa Waziri anijibu wakati akihitimisha hoja yake, vinginevyo nitasimama wakati wa kupitia vifungu vya bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TANCEM Limited* Shinyanga. Kama mnavyofahamu, Kiwanda cha Saruji kiko mbioni kujengwa katika eneo la Kizumbi, Jimboni Shinyanga Mjini. Mwekezaji ni *TANCEM Ltd.* tayari alishamilikishwa eneo la kiwanda, amekwishalipa fidia kwa wananchi walioguswa na mradi. Pia *TANCEM Ltd.* tayari amelipia gharama za kufanya tathmini ya kuunganisha umeme katika eneo kitakapojengwa kiwanda. Hivyo, naomba Wizara ihmize *TANESCO* kufanya tathmini hiyo na hatimaye wapeleke umeme haraka ili mwekezaji alete mitambo ya kiwanda na kuanza uzalishaji kadri ya mpango wake. Kiwanda hiki kitakuwa ni mkombozi kwa ukanda wa ziwa kwa mahitaji ya saruji. Naomba uhakikisho wa kusaidia *TANCEM* kupata umeme.

MHE. KHADIJA SALUM AL-QASSMY: Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuamka nikiwa mzima, pia nimponeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake ilijoja matumaini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo yangu hayo sasa napenda kutoa mchango wangu katika hotuba husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhana ya hotuba ya Waziri inaonyesha wazi kwamba Bajeti ya Wizara ni ndogo na haiwezi kukidhi hoja kwa kuiwezesha nchi kupata mapato yatakayoweza kuisaidia Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ilani ya Uchaguzi ya CCM imesema mengi juu ya nia yake katika Wizara hii. Serikali itaanzisha mchakato wa kujenga uchumi wa kisasa ambao utajikita katika maeneo makuu matatu. Kwanza, kujenga rasilimali watu wenye elimu na maarifa ya kufanya kazi, pili, kufanya mapinduzi katika kilimo na tatu, kufanya mapinduzi ya viwanda na miundombinu ya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapinduzi ya kilimo na viwanda ndio maeneo yanayoweza kukuza uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, matamko haya yatabaki kusomwa katika makaratasu tu na si kwa vitendo. Maendeleo ya nchi hupatikana kupitia kilimo na viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yapaswa ileze ni kitu gani kinachopelekea mazao ya wakulima kama vile machungwa, mananasi na kadhalika kuharibika kwa ukosefu wa viwanda. Tunamsaidia nini mkulima, la kusikitisha sana kuona viwanda vya kutengenezea vinywaji kama vile bia vinafanya kazi, lakini viwanda vya kumsaidia mkulima na mazao yake imeshhindikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali bado haijawasaidia wafanyabiashara wa ndani ambao biashara zao ni ndogo. Fursa kubwa wamepewa wafanyabiashara wakubwa ambao ni wawekezaji kuwalegezea masharti ya biashara. Hii sio sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ina miti ya mbao zilizo nzuri zenye ubora. Hivi sasa wafanyabiashara kutoka China wanafanya biashara za ndani ya nchi kwa kuza

vitu vinavyotengenezewa mbao kama vile vitanda, milango na kadhalika. Hii ni haki ya Watanzania na sio ya China. Kuwepo kwa viwanda kutamsaidia Mtanzania kuweza kufikia azma ya maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo yangu hayo napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake kwa umahiri wao wa kutekeleza majukumu yao. Ahsante.

MHE. BUJIKU P. SAKILA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. Nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri inayooonesha vizuri njia ikitupa matumaini makubwa kwa maendeleo ya viwanda na kuimarisha biashara na kupanua wigo wa mazao na bidhaa kwa nchi yetu. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa ujasiri na kujihamini alivyovionyesha wakati akisoma hotuba yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati akisoma alionyesha wazi kuwa alichokuwa anasoma anavielewa na kuvihamini. Hivyo ilikuwa fursa nzuri ya kuwashawishi Wabunge na wasikilizaji waliokuwa wakifutilia waamini alichokuwa akikisoma, alifanikiwa. Nampongeza sana.

Aidha, nawapongeza wote walioshirikiana na Mheshimiwa Waziri kuiandaa hotuba hiyo. Ubora wa hotuba hii unaonyesha kuna mshikamano mkubwa katika Wizara hii. Hivyo nawapongeza kwa dhati, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote na wengine wote walioshiriki.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizi naomba kufanya maombi yafuatayo, kwanza naomba sana ufanuzi kama utaratibu utaruhusu sera za kuendeleza biashara, viwanda na masoko zinaweza kufanyiwa marekebisho ili kuwataka wale wote wanaoanzisha viwanda hapa nchini wasiuze nje bidhaa ambazo hazijaongezwa thamani mfano, *ginnery* zote ziwe zikiungana kujenga viwanda vya nguo kwa utaratibu wowote huo ili viwe vikiuza nje na ndani nguo na siyo nyuzi wala pamba. Pamba ya ziada tu ndiyo iweze kuuzwa nje. Pia viwanda vya matunda viuze bidhaa iliyotokana na kusindikwa matunda hayo. Matunda ya kuuzwa nje yawe ni yale tu yanayozidi uwezo wa kusindika matunda yale.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia wafanyabiashara ya nafaka kadri iwezekanavyo unga uuze nje badala ya nafaka. Wafanyabiashara ya alizeti na mbegu zingine zitoazo mafuta wawe na viwanda vya kusindika waweze kuuza mafuta nje ya nchi badala ya mbegu hizo. Naomba ufanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utafiti wa teknolojia na maendeleo na matokeo yake, teknolojia ni bidhaa muhimu, huuzwa nje na huweza kutumika nchini na inagundulika kusaidia wananchi kuboresha maisha yao ikiwa ni pamoja na kuongeza thamani ya vitu vizalishwazo katika nchi husika. Yapo mambo mengi yanayoendelea kugunduliwa hapa nchini. Teknolojia hizi hazitangazwi kikamilifu na kufanya teknolojia hizo mbali mbali zitumike kikamilifu na wananchi wetu. Naomba teknolojia hizo zifanyiwe utaratibu mzuri wa kuwa zinatangazwa hadi kwa wnanchi. Nashauri

makampuni kama *CARMATEC*, *TIRDO* na *SIDO* yawe na matawi hadi ngazi za Wilaya kuwezesha wananchi wengi kuyatembelea maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, halmashauri zetu ziwekewe utaratibu wa kujulishwa kila kinachojitokeza kiteknolojia katika taasisi/viwanda hivyo. Taasisi hizi zitakiwe kuwa na *showroom* na maduka ya vifaa/bidhaa zao hadi ngazi za Wilaya badala ya kutegemea sherehe za maonyesho ya biashara wakati wa saba saba, Nane Nane na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sera ya kulinda bidhaa zitokanazo na viwanda vya hapa nchini ipewe nguvu zaidi. Hivyo wanunuzi wote wanunue vitu/bidhaa za nje tupate ambapo bidhaa bora na imara za hapa nchi itathibitika kuwa havipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha na naunga mkono hoja.

MHE. ALI JUMA HAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Dr. Mary Nagu, Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Cyril Chami, Katibu Mkuu, Dr. Stergomena L. Tax pamoja na watendaji wao wote ambao wametoa mchango wao katika kufanikisha hotuba hii ambayo kwa kiasi fulani inatoa mwanga wa mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kutoa mchango kuhusiana na bidhaa nyingi zinazoagizwa kutoka nje kama vile *furniture* na kadhalika ambavyo malighafi zake asilimia kubwa zinatoka hapa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali umefika wakati sasa kuelekeza nguvu zake kubwa kujenga viwanda ili mali ghafi zetu zitumike hapa nchini na kutengeneza bidhaa zilizo bora na baadae sisi tuweze kuuza nchi za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itakapojikita katika ujenzi wa viwanda tutaweza kuokoa mali ghafi zetu, tutaweza kutengeneza ajira nyingi kwa vijana wetu kupitia viwanda hivyo pia tutaweza kupunguza hali ya umasikini kwa wananchi wetu kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kuhusu wajasiariamali wetu ambao wanajishughulisha sana na biashara mbalimbali lakini jambo la kusikitisha wanakosa masoko ya uhakika ya kuuza bidhaa zao baada ya kuzalisha, jambo ambalo kwa kiasi fulani linawavunja moyo wajasiariamali wetu na jambo hili badala ya kuwapeleka mbele kimaendeleo wananchi wetu, ni wazi litawarudisha nyuma na kuwadumaza kimaendeleo na hatimaye kuwabakisha katika dimbwi lile lile la umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo naiomba Serikali kuhakikisha inawapatia masoko ya uhakika wajasiariamali wetu kwa bidhaa zao zote wanazozalisha iwe masoko ya ndani ama ya nje ya nchi.

Jambo hili la kuwatafutia masoko litaboreka vizuri iwapo litakwenda sambamba na kuwatengeneza miundombinu ya uhakika kama vile barabara, umeme na kadhalika,

ili wakulima wanapozalisha mazao yao waweze kusafirisha kwa urahisi na uhakika wa kufika katika masoko hayo au viwanda vitakavyojengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Nibu Spika, taasisi ya *CARMATEC* ni moja ya taasisi muhimu kwa wakulima nchini. Kuna taarifa kwamba taasisi ya Nelson Mandela inategemea kujenga *college* kwenye eneo la taasisi hii. Ningependa kupata uthibitisho kama kweli kunaweza kuwa na maamuzi ya namna hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, biashara ya kuuza visu, vitu vyenye ncha kali na *toy guns* (silaha bandia). Kwa vile kuna wimbi la ujambazi na uhalifu upo wa hali ya juu na tunaona visu vinauzwa barabarani ambavyo wauzaji wanaweza kuporwa na majambazi na kuvitumia kufanya uhalifu au watu wenye ugonjwa wa akili wakavitumia kudhuru watu. Vile vile kuna matokeo kadhaa ya ujambazi ambayo majambazi haya yametumia hizo *toy guns* kufanya ujambazi.

Ushauri, kuna haja ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko pamoja na Wizara ya Mambo ya Ndani kukaa pamoja na kutunga sheria ya kuzuia uuwaji wa visu au vitu vyenye ncha kali kiholela au kuuzia barabarani. Tukizingatia nchi yetu haina utamaduni wa silaha kuna haja ya kutunga sheria ya uingizwaji wa hizi *toy guns* nchini. Kuhusu viwanda vya nguo, nampongeza Waziri na kutuhimiza kuvala nguo za Tanzania lakini kuna haja ya kufufua viwanda vya sindano na vifungo. Je, viwanda hivi viro?

Angalizo langu ni kuwa Kiwanda cha *Kibo Match* kile cha viberiti karibu kinakufa kabisa sababu ya viberiti vingi sana vinakuja kutoka nje. Je, Wizara ina mikakati gani ya kukinusuru kiwanda hiki ambacho kina ajira ya watu wengi sana?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kiwanda cha *Alaf*, kiwanda hiki kilikuwa na section nyingi mfano *Still Company*, *Pipe Company*, *Aluminium Company*. Kiwanda cha *ALUCO* katika miaka ya 1980 hadi 1990 Serikali ilikuwa na 51% na *ALUCO* walikuwa na 49% na kiwanda hiki kilisifika kwa kutengeneza mabati mia kwa saa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba majibu kama yafuatayo, ni sababu zipo zilipelekea kiwanda hiki kifungwe na mpaka sasa hivi kuna *share* ngapi katika kiwanda hiki?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *agent* wa kukagua magari Dubai, ningependa kujua ni kiasi gani Wizara/Serikali imeshafaidika na kutoka kwa *agent* huyu na huyu *agent* anayekagua magari Dubai alipatikana kwa kufuata taratibu za Serikali za manunu?

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nawashukuru sana Mheshimiwa Waziri, Naibu wake pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa hotuba hii na kuleta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wengi wa Mkoa wa Tabora wamekuwa wanazalisha kwa wingi mazao ya karanga, mpunga na ufuta. Hata hivyo wamekuwa hawanufaiki na kilimo hicho kwa sababu hakuna viwanda nya kukobolea nafaka hizi ili ziweze kuongezewa thamani. Wanalamika kuuza huko mashambani kwa bei ndogo sana. Hakuna vipimo nya kilo, wanauzwa kwenye magunia yaliyoshindiliwa kwa kukadiria bei.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iwasaidie wananchi hawa wapate mashine za kukobolea mazao haya ili waweze kuuza kwa bei halali.

Pia naiomba Serikali itoe mwongozo kwa wafanyabiashara ambao wanunua mazao kwa magunia na madebe na waweze kununua kwa kilo ili wananchi waweze kunufaika kwa kilimo chao na kujikomboa na umaskini. Serikali kwa kutumia ofisi zao zilizoko mikoani wahakikishe wafanyabiashara wanatekeleza maagizo ya Serikali ya kutumia vipimo vinavyokubalika kupimia kununulia mazao kutoka kwa wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa inatamka hapa Bungeni kuwa suala la viwanda nya kusindika mazao ya kilimo na mifugo limeachwa kwenye sekta binafsi na wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali suala muhimu kama hili kuachwa mikononi mwa sekta binafsi na wawekezaji Serikali ichukue wajibu wa kuwekeza kwenye eneo hili muhimu kama kweli tunataka tuwainue wakulima na wafugaji wetu. Tumeshuhudia jinsi gani mazao mbalimbali yakiharibika mfano matunda, mbogamboga, maziwa kwa kukosa viwanda nya kusindika na matokeo yake tumebaki kuingiza juisi, maziwa yaliyosindikwa kutoka nje ya nchi na ndivyo vimejaa kwenye *super market* na madukani wakati vyetu vinaoza na kuvitupa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la viwanda nya usindikaji wa vyakula ni suala muhimu sana na Serikali ilipe uzito wa kutosha na siyo kusubiri mwekezaji aje kuwekeza.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nawapongeza kwa hotuba nzuri iliyozingatia jinsia. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto iko tayari kushirikiana nanyi katika kusaidia wanawake wajasiriamali kwa utaratibu tutakaokubaliana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawatakia kazi njema.

MHE. DR. AISHA O. KIGODA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Nampongeza Waziri Mheshimiwa Dr. Mary Nagu na Naibu Waziri, Mheshimiwa

Dr. Cyril Chami, kwa hotuba nzuri. Nampongeza Katibu Mkuu na Wakurugenzi wa Wizara na taasisi zake. Baada ya pongezi nachangia kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Viwanda Vidogo vidogo (*SIDO*). Nalipongeza sana *SIDO* kwa mchango wao mkubwa kuwawezesha wajasiriamali wadogo wadogo nchini kote. Binafsi naipongeza kwa kazi nzuri walioifanya katika Mkoa wa Tanga. Lakini bado huduma hizi hawajafaidika wanawake wa Wilaya ya Kilindi. Kikundi kimoja tu cha akinamama wasindikaji wa matunda, Meneja wa Mkoa tusaidieni na Makao Makuu kutuwezesha.

Kuhusu Bajeti ya *SIDO* bado haitoshi, bahati nzuri niliwahi kuwa mmoja wa wakurugenzi wa bodi mara tatu kwa miaka zaidi ya tisa, sasa kila mara tumekuwa tukilalamika Bajeti ndogo. Tatizo ni nini, au bado umuhimu wake hatujuauona? Naamini wote tunaojua mchango wake kwa vile unagusa watu wa kada ya chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi za pekee kwa *SIDO*. Wakati wa maonesho ya *DITF* nilibahatika kutembelea mabanda ya wajasiriamali. Kimenifurahisha kuona kuna vikundi vingi vilivyokuwa vimefundishwa na kulelewa na *SIDO* vimeweza kujiunga na kujitegemea kufungua banda lao nje kabisa ya *SIDO* kama ilivyokuwa zamani. Hii inaonyesha wazi mchango mkubwa wa *SIDO*, hongereni sana.

Otherwise, Mheshimiwa Waziri na Naibu wako mnauwezo mkubwa na upeo, nawatakia kila la kheri, tunawaunga mkono ili mtekeleze majukumu yenu. *All the best*.

MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpongeza Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, Naibu Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara hii kwa hotuba yao nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja asilimia mia moja. Baada ya hapo naomba kuchangia mambo machache ambayo ni muhimu kuhusu Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii inazo taasisi nyingi, kama vile *SIDO*, *NDC*, *TIRDO*, *TEMDO*, *CAMARTEC* ambazo zinapewa fedha ya kulipia mishahara tu na hazipewi fedha yoyote ya kufanya kazi. Jambo hili sio zuri kwani taasisi hizi bila fedha haziwezi kufanya kazi, hivyo ni kuwatesa watalaamu ambao hulipwa mishahara na kuachwa wamekaa tu bila kufanya kazi yoyote. Tunaomba miaka ijayo hizi taasisi zipewe fedha ili ziweze kufanya kazi kwa tija. Kama hamna fedha basi zifutwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimetembelea maonyesho katika nchi za nje ambayo maofisa wa *BET* hupelekwa kuratibu na kuhakikisha kuwa wafanyabiashara wa Kitanzania wanapatiwa huduma nzuri. Kinachosikitisha ni namna maofisa wa *BET* wanavyotoa huduma mbaya sana na kutia aibu sana wanavyoratibu kazi zao katika maonyesho hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2005 nilihudhuria *Expo* iliyofanyika Nagoya, Japan. Katika maonyesho haya wafanyabiashara wengi mizigo yao ilichelewa kufika kutokana na taarifa mbaya waliyopewa na *BET* kibaya zaidi waliofika walikuta hawana mahali pa kuweka vitu vyao na wala walishindwa kupata malazi kwani *BET* walikuwa hakuwabookia sehemu za malazi. *BET* ilitia aibu sana na kusababisha wafanyabiashara kupata hasara kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitembelea maonyesho ya Dubai ya mwaka 2006. Nilipofika kwenye maonesho Afisa wa *BET* hakuwepo na kibanda chake kilikuwa kinatumika kama stoo na afisa wa *BET* alikuwa ameingia mitini. Wafanyabiashara walikuwa hawakupangiwa sehemu ya kuweka vitu vyao na wala hamna mipango ya malazi kwa wafanyabiashara haikuwa imefanywa. Wanyabiashara wengi waliingia hasara kubwa na wengine kama Mama Kirigili aliuziwa shamba lake ili kulipia mkopo wa asali ambayo haikupata soko kwa kuchelewa kuwasili inatia aibu sana kwa *BET* kutoa huduma mbovu kama hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, aibu *BET* inayoitia nchi ilifikia kilele hapo majuzi wakati wa maonyesho yaliyofanyika Gologonza, Spain. Akinamama walilipia *USD 2800* kwa ajili ya *stand*, vile vile walilipia *USD 2200* tiketi ya ndege kwenda huko. Walipofika Gologonza, usiku walipompigia simu afisa *BET* awapokee hakupokea simu na ilibidi hawa mama walale *stand* kutojua wanatakiwa kufikia wapi. Kibaya zaidi walipoenda kwenye maonyesho, hawakuruhusiwa kuingia kwani hawakuwa *registered* na hivyo walirudi bila kuingia kwenye maonyesho. Hivi afisa wa *BET* aliyetangulia huko alienda kufanya nini?

Mheshimiwa Naibu Spika kama *BET* ilichukua dola zao za kulipia *stand* kwa nini hawakulipa. Hivi hizo hasara za akinamama hao wajasiriamali wameingia nani atawalipa? Aibu hizi za *BET* ni lazima zikomeshwe mara moja na akinamama hawa lazima warudishiwe fedha zao na kulipwa gharama za usumbu.

MHE. HAJI JUMA SEREWAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu kuchangia hoja hii. Kabla sijachangia hoja hii kwa niaba yangu na wananchi wangu wa Jimbo la Mwanakwerekwe naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza hotuba ya Waziri kwa jinsi ilivyojieleza vizuri. Lakini nasikitika sana kutokana na Bajeti ndogo inayopewa Wizara hii kutokana na majukumu yake na kazi zake zilivyo muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali ya viwanda vingi havifanyi kazi hivi Serikali itabidi ichukue hatua ya kuvitengeza kwa ajili ya kuwa tayari kwa kufanya au kutafuta wawekezaji wawekeze kwenye viwanda hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa Tanzania wananchi wake wanajishughulisha na kilimo. Lakini huwa wanapata hasara kubwa sana kutokana na matunda kuoza au kuharibika baada ya kukaa kwa muda mrefu bila ya kupata soko.

Pendekezo, Wizara isimamie kuwepo viwanda vidogo vidogo kwa ajili ya kusindika matunda na kupata *juice* na kadhalika, ili wananchi wafaidike na kilimo chao.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku nyingi Serikali huzungumzia soko la kisasa. Jambo ambalo bado kabisa soko hilo kuwepo. Napendekeza Wizara isimamie ujenzi wa soko hilo ili matunda yawe na uwezo wa kukaa muda mrefu bila ya kuharibika ili matunda nchini yakiwa mengi yaweze kuhifadhiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *SIDO* ipewe uwezo wa kusimamia na kwa kujiendesha ili iimarike kwa ajili ya kuwepo viwanda vidogo vidogo hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazidi kukushukuru wewe kwa kuniruhusu kuchangia hoja hii, pia nazidi kuunga mkono mia kwa mia. Ahsante.

MHE. ANIA SAID CHAUREMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hoja hii ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko ya mwaka 2008/2009. Nampongeza Waziri, Naibu Waziri na wataalamu kwa kazi nzuri wanayofanya katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni kumekuwa na taarifa ya ukiukwaji wa agizo alilotoa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa mazao ya chakula yasiuzwe nchi jirani ili kukidhi haja ya tishio la upungufu wa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kushangaza mipaka ya Mkoa wa Kilimanjaro na Mombasa sehemu za Himo kumekamatwa tani zaidi ya mia tatu za nafaka zinapelekwa nchi jirani, ningependa kupewa ufanuzi ni sababu zippi hasa? Upungufu wa watendaji, kufuutilia au huwa wanapita wapi zaidi ya barabara ambazo zina vizuizi vyta ukaguzi? Kukamatwa kwao kunatokana na zoezi maalumu, inaonekana bidhaa nyingi zinaingia nchi jirani katika mipaka yetu, mfano Zambia, Malawi, Uganda na nchi nyingine, je, hakujatokea tatizo kama la Moshi?

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuiomba Wizara hii hivi sasa wajasiriamali ni wengi wameinua maisha yao kwa kufanya biashara ndogo ndogo za kusindika mazao na matunda, lakini bado tatizo hili na katika hotuba ya Kamati imesema kuna soko kubwa Dubai na nchi za Falme za Kiarabu nakubaliana na hili, hivi sasa msimu wa matunda mengi yanaoza hasa machungwa, mananasi, ndizi, embe na matunda mengine ni vyema viwanda vipatikane, ni muhimu na soko hilo la nje lifuatiliwe haraka ili kuokoa mazao haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa wafanyabiashara wamachinga, hivi sasa katika jiji la Dar es Salaam ni mfano mzuri wa majengo yatakayoendelea kujengwa katika Wilaya ya Ilala, majengo haya ni vyema yakajengwa maeneo mengine ya nchi ili kupungunza wimbi la vijana kukimbilia katika jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujua pale Mbagala Rangi Tatu kuna kiwanda kilicho jengwa lakini hakijafanya kazi na wala hakijaisha inasemekana ni cha *glass*, ni nini hatma ya kiwanda hicho ni cha Serikali au cha mtu binafsi?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huu, naunga mkono hoja.

MHE. MHONGA S. RUHWANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yoyote inafanikiwa ikiwa na sera za kumlinda mjasiriamali wa Kitanzania ingawa liko kwenye soko huria. Mfano Wachina wanafanyabiashara ndogo ndogo ambazo zingeweza kufanywa na Watanzania ukienda Kariakoo utashuhudia yote hayo.

Kuhusu vyuo vya VETA, Wizara hii inahusika kwani vijana wanaotokea katika vyuo hivi wanaitegemea Wizara hii iwalinde. Lakini utashangaa uendeshaji wa biashara ya *garage* nyingi nchini ziko chini ya Wachina na Wachina hao wanafanyakazi ambazo kijana kutoka VETA anaweza kuzifanya kiasi kwamba ajira ambayo wange pata vijana hao inachukuliwa na wageni, Wizara iangalie hili kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani. Serikali ina nia ya kuongeza ajira lakini hali halisi haiendani na nia hiyo ya kuongeza ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna haja ya Serikali hii kuwa na mpango thabiti wa pamoa utakaozihusisha sekta mbalimbali (*integrated sector strategic plan*). Sekta ya viwanda haiwezi kufanikiwa ikiwa maji hakuna, umeme na nishati mbalimbali hakuna na vile vile kama miundombinu si ya uhakika kwa maana ya reli, barabara, usafiri wa anga na maji. Bila kusahau sekta nyeti ya kilimo ambayo kazi yake itakuwa ku-feed/kulisha viwanda kwa maana ya malighafi. Hivyo kilimo chetu kitakuwa chenye tija kwani wakulima watakuwa wenyewe uhakika na soko la bidhaa wanazozalisha mfano matunda, pamba, korosho, mazao ya wanyama, ngozi, maziwa, nyama na vingine vingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, toka mwaka 2007 tunaihoji Serikali juu ya mchakato wa uimarishaji na ufufuaji wa viwanda vilivyobinafsishwa. Waziri atueleze mpaka sasa Serikali imeshachukua hatua gani katika mpango mzima wa ufufuaji wa viwanda vifuatavyo, *General Tyre* cha Arusha, *Kilimanjaro Machine Tools*, Kiwanda cha Magunia, Kiwanda cha *Tanganyika Packers* na cha Ngozi Mjini Moshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda hivi vikifanyakazi kama vilivvokusudiwa wakati vikijengwa vitasaidia ajira na bidhaa ambazo zipatikana hapa hapa nchini badala ya Watanzania kuagiza vitu hivyo nje ya nchi wakati viwanda viwo. Serikali itoe maelezo ya kina kuhusiana na viwanda hivyo hasa *General Tyre* ambacho Serikali ina hisa 76% na mbia 24%. Tatizo ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanda cha chumvi Uvinza, kinasikitisha mpaka sasa kiwanda kinatumia magogo, wakati kinabinafsishwa ilitakiwa kiendelezwe vizuri na vile vile nishati ya umeme itatumika. Serikali itueleze mpaka lini kiwanda cha chumvi Uvinza kitaendelea katika hali ile? Kiko katika hali mbaya na mazingira ya Uvinza yatageuka jangwa maana miti inakatwa sana ili kupata magogo. Vile vile Serikali itupe nini hatma ya kiwanda cha *Tanganyika Packers* na mwelekeo ukoje?

Mwisho, nashauri Serikali iwe makini katika kubinafsisha na kuuza viwanda kwani uzoefu unaonyesha walionunua viwanda hawana uwezo wa kuviendeleza. Hivyo Serikali ichukue hatua inayostahili kwani wanunuzi wamekiuka mikataba, hivyo kusidio la Serikali la viwanda kuendelea kuzalisha na kutoa ajira nchini halikutimia.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Naibu Spika, mojawapo ya mambo yaliyoturudisha nyuma kwenye viwanda ni *misallocation* kwa mfano Kiwanda cha Pareto kwa nini kiwekwe Arusha/Moshi badala ya Iringa ambapo pareto hulimwa? Pia almasi ilichimbwa Mwadui lakini Kiwanda cha *Tancut* kikawekwa Iringa na kadhalika.

Misallocation hizi zilikuwa za makusudi ili kukidhi siasa za kutambuana (*The Politics of Patronage*) ilikuwa siyo kiwanda kijengwe wapi kulingana na malighafi, bali ilikuwa kiwanda kijengwe wapi ili kumjenga mtu hata kama mahali hapo hakuna malighafi.

Wizara iachane na makosa ya kurundika viwanda sehemu moja au *zone* moja. Kiwanda cha Saruji, naiomba Wizara ihamasishe na ilekeze wawekezaji wa kiwanda cha saruji waje Itigi na si *Lake Zone* kama wengine wanavyotaka. Tayari Mwanza wana kiwanda cha bia na sasa wanataka kiwanda cha saruji hata kama hawana malighafi. Hii itakuwa kuwekeza kiwanda kwa sababu za kisiasa (*political patronage*) kwa mtindo wa kufahamiana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wiki iliyopita Wachina walifika Mkoa wa Singida, wakafika Itigi, wakapata *sample* ya *gypsum*, ikaonekana *gypsum* hiyo ina kiwango bora zaidi kuliko *gypsum* yoyote duniani (93%, *Calcium Contents*). Pia jirani na Itigi Magharibi kiasi cha kilometra 50 ipo *Limestone* (chokaa) ya kutosha eneo la Ugwandi karibu na mbuga za Wambure. *Deposits* zake ni nyingi sana kiasi cha kuchimbwa kwa karne moja ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wachina wamevutiwa sana na wameahidi kurejea mwakani baada ya kufanyia kazi mipango yao. Miundombinu ya Itigi imekaa vizuri.

Lakini kwa hali ilivyo nchini mwetu, watu hawa (wawekezaji) wanaweza kupelekwa sehemu nyingine kuwekeza kiwanda kwa utaratibu huo wa *political patronage*. Ukiweka kiwanda Itigi ambako ni katikati ya nchi usambazaji wa saruji utakwenda kirahisi kabissa *Western Zone*, *Lake Zone*, *Central Zone* na hata Kaskazini na Kusini mwa nchi maana kuna barabara na reli pande zote pale Itigi. Umeme wa *National Grid* upo.

Pia, kiusalama hatuwezi kuweka viwanda vyetu vyote miji ya pemberi mwa nchi. Ni vyema vingine tukaweka katikati ya nchi ili viwe salama wakati panapozuka vita. Naomba kiwanda Itigi.

MHE. DAMAS P. NAKEI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nimpongeze Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko,

Naibu Waziri Dr. Cryil Chami na watendaji wote wa Wizara kwa maandalizi na hatimaye hotuba nzuri Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mmoja wetu anazungumzia umuhimu wa viwanda katika nchi, kwamba nchi zote zilizoendelea zinajivunia viwanda na inasemekana *primary industries* kutokana na bidhaa za kilimo ndiyo msingi wa maendeleo ya viwanda na maendeleo ya nchi kwa ujumla. Hii lugha ya umuhimu wa viwanda ni ya siku nyingi sana. Kwa nini hatupigi hatua yoyote ya kuridhisha?

Mheshimiwa Naibu Spika, Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere alifanya kazi nzuri sana (*he did wonderful job indeed!*)! Viwanda vingi vilianzishwa/vilijengwa wakati wake. Aliweka misingi yote iliyotakiwa kwa nchi yoyote changa. Nchi yetu inalo deni kubwa la kuendeleza kile alichokipigania. Lakini tulichoshuhudia kwa muda mrefu ni kufifia ama kufa kwa viwanda katika nchi yetu, ndiyo maana uchumi wetu hadi sasa si imara, haustahimili changamoto za ushindani! Ni kitu gani kilichotokea na kinachoendelea kwenye viwanda vya nguo, viwanda vya ngozi, matunda, maziwa na kadhalika?

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vingi vilivyouzwa/vilivyobinafsishwa vilitarajiwu kubadilisha mwelekeo wa maendeleo ya viwanda nchini. Je, hiyo ndiyo hali halisi? Nadhani tuitie upya sera zetu za maendeleo ya viwanda tuone kama zinafanya kazi. Tuige mfano kutoka *best practices* kwingineko duniani. Hata jirani zetu Kenya wanatupita kwa mbali, tuige, tutafute siri ya mafanikio yao. Lakini mwisho ni dhahiri hatuna uzalendo, hatuipendi nchi yetu. Tubadilike, ni dhahiri tuko nyuma sana, tukimbie maana tunaachwa! Naunga mkono hoja.

MHE. ANNE S. MAKINDA: Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wakurugenzi wote nawapongeza kwa hotuba yenu nzuri sana ambayo imeandaliwa kwa utaalamu mkubwa sana. Nawatakia utekelezaji mzuri.

Ombi langu la kuanzisha mtaa wa viwanda vidogo vidogo Njombe Mjini eneo la Mjmwema lina muda wa miaka minne, je, kwa sasa mmevikia wapi au mnataka sisi halmashauri tufanye nini? Naunga mkono hotuba yako.

MHE. MAULIDAH ANNA KOMU: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwanza kuwapa pongezi wale wote ambao wameshirikiana na Waziri kutengeneza hotuba hii ya Bajeti kwa mwaka huu wa 2008/2009, kwani kwa kweli ni kazi ngumu sana ya kusimamia viwanda, biashara na masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana michango mingi ilitolewa hapa Bungeni kwa Wizara hii nyeti, kwani kama tunasema kilimo ni uti wa mgongo basi viwanda, biashara na masoko ni moyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 14 wa hotuba ya Waziri nanukuu; “Viwanda vina mchangano mkubwa katika kuleta mapinduzi ya kilimo” na hapo hapo tunasema wito wa kilimo kwa mwaka huu ni mapinduzi ya kijani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapinduzi ya kijani bila viwanda, na masoko bora hakuna faida yoyote. Leo hii ndio kwanza tunaandaa kuwapa mafunzo wakulima wetu eti waweze kuzalisha mazao yenyenye ubora eti tupate matunda mazuri ndio tuanze viwanda. Hadithi zimekuwa nyingi kila mwaka ni kuandaa, kuandaa mpaka lini? Naomba niwaulize Wizara, hebu tuone kauli ya uhakika ni lini tutaanza kusindika matunda yetu? Ni lini tutakuza *SIDO* ili wapate kutoa mashine nzuri na za uhakika za kuwezesha wakulima wetu na ushirika waweze kupata viwanda?

Mheshimiwa Naibu Spika, tumechoshwa na hadithi hebu sasa tuanze vitendo. Biashara na masoko ni vitu vinyavyofuatana, unapokuwa na biashara unachotafuta ni masoko, lakini ni masikitiko makubwa kwamba vijana wetu na wanawake wanajitahidi sana kutumia mikono yao na akili kutengeneza vitu mbalimbali lakini hakuna masoko wala Serikali haionekani kufanya bidii yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunalia sana na makusanyo ya kodi lakini hatutaki kutumia nguvu kazi, vijana wanahangaika na vibiashara vyta mikononi lakini kuna njia nyingi za kuwfanya watumie nguvu zao kuzalisha na Serikali itafute soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina haja ya kuorodhesha mali ambazo zimo ndani ya nchi hii na tukivitumia tutaweza kuondokana na umaskini tulionao, kwani tuna mali nyingi sana kwa uchache tu, ni ardhi kubwa tulionayo na ina rutuba ya kutosha tuitumie ipasavyo na baada ya kuitumia Wizara itafute masoko ya uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ubinafsishaji wa viwanda vyetu ni ubabaishaji mtupu umegubikwa na mikataba ya ajabu, hivi kuna nini? Kwa nini hatuna huruma na nchi yetu? Tuwe wa wazi katika kubinafsisha na Katiba ya nchi yetu inaongea vizuri naomba ninukuu Ibara ya 9(i) inasema kwamba; “matumizi ya utajiri wa Taifa yanatilia mkazo maendeleo ya wananchi na hasa zaidi yanaelekezwa kwenye jitihada ya kuondoa umaskini, ujingga na maradhi.” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo inayotolewa yote haina maana kama hatutaweka mkazo kwenye kilimo, viwanda, biashara na masoko, tunatoa mikopo lakini mpaka leo hao wanaokopa ni wachache wanifuwa, masoko yako wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, tujitahidi kukaa kujipanga, kuijandaa na kujua tunachotaka kufanya kama kweli tutaweza na kitatoa tija kwa wananchi wetu na kuwaondoa kwenye umaskini?

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa ushauri kama ifuatavyo, tuache kuuza mbao zetu yaani magogo nje na sisi kuendelea kununua samani ya kutoka nje mfano ni samani tulionayo hapa hapa Bungeni. Tuache kuwa na mikataba mibovu ya kubinafsisha viwanda vyetu, tujikite kuangalia maslahi yetu kwanza.

Pia tutoe mikopo kwa wananchi tukizingatia nguvu kazi, elimu itolewe kwanza ya biashara na wanaopewa mikopo wasimamiwe kutengeneza bidhaa zilizo bora na wapatiwe masoko. Viwanda vidogo vidogo viwepo vingi kila penye mazao yanayoweza kusindikwa kama matunda, bidhaa zinazotoa mafuta ya kula, nyama, samaki na

vinginevyo. Turudishe viwanda nya nguo vilivyokuwepo kwani majengo yapo yanakuwa nyumba za popo.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kusema sasa wakati umefika wa vitendo kuacha tena kuongea tutafanya, sasa basi tuanze, muda ni mrefu sasa umepita.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchumi wa nchi yetu unategemea sana *imports* kuliko *exports*. Sasa katika bidhaa zinazoingia nchini zipo ambazo ziko chini ya viwango. Hata kama Serikali inajitahidi kuzikamata na kuziteketeza, zipo zinazofika kwa mlaji.

Naomba sana Wizara kwa ushirikiano na wadau wengine waje na sheria ya kumlinda mlaji au *consumer protection bill*. Huu Muswada ukipita na kuwa sheria, itasaidia sana kuwalinda walaji na bidhaa mbovu zinazoingia nchini.

Naipongeza sana kampuni ya bia (*TBL*) kwa kuamua kujenga kiwanda cha kuzalisha bidhaa zao huko Mbeya. Naomba Wizara ikishirikiane na Wizara ya Kilimo, wawahamashe wananchi wa mikoa ya nyanda za juu kujipanga kulima shayiri ambayo ni malighafi ya kuzalisha bidhaa za *TBL*. Itakuwa ni aibu kama kiwanda kinajengwa Mbeya halafu shayiri itoke nje ya nchi.

Kuhusu uwanja wa ndege wa Songwe utakuwa tayari baada ya miaka miwili. Naomba Wizara iwahamashe wananchi kujipanga kulima mazao ya kuuza nje ya nchi kama vile maua, ndizi na kadhalika ili kuutumia vizuri uwanja huo utakapokuwa tayari.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni nyeti sana na ndio msingi wa maendeleo ya nchi yoyote ile. Cha ajabu Wizara hii inapata Bajeti ndogo sana hivyo watashindwa kabisa kusaidia ujenzi wa nchi yetu. Wizara hii ndio inayobeba jukumu la biashara na hivyo kukuza pato la nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *SIDO*, nchi yetu siku za nyuma iliweza kujitegemea na kuwa na viwanda vidogo vidogo na hivyo kusaidia ajira. Cha ajabu viwanda vingi vimekuwa na hata *SIDO* pamoja na juhudzi za kusaidia kwa kutoa mafunzo bado Wizara imeshindwa kuwapa fedha za kutosheleza.

Lakini cha kusikitisha zaidi ni suala zima la viwanda vyetu vikubwa na vidogo kutokufanya kazi au kufungwa? Hivi ni sababu gani za msingi za kufungwa au kutokufanya kazi kwa viwanda hivyo nya *Tanganyika Packers, General Tyre* na *MUTEX* na kadhalika. Hivi kweli kiwanda kama *General Tyre* kilichokuwa kinatengeneza *tyres* nzuri na bora Afrika leo hakipo kwenye *list*? Huku tukiagiza *tyres* kutoka nje ambavyo havidumu? Hivi tukiendelea kuwaachia wawekezaji na tumeshaona madhara ya ubinafsishaji/uwekezaji, tunakwenda wapi? Kwa kweli ni muhimu sana tuwe na bidhaa za kwetu lakini cha ajabu Tanzania hatuna chetu hata viberiti tunaagiza nje wakati tuna

Kibo Match pale Moshi. Sasa hivi Tanzania tuna pamba kibao lakini nguo zetu zote tunazipata toka nje tena zisizo na ubora sana, leo madukani ni kanga za India ambayo ukivaa mara moja ukafua inaharibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ina changamoto kubwa ya kuhakikisha kuwa inatoa elimu kwa wadau mbalimbali wakiwemo wakulima, wafanyabiashara, wavuvi na kadhalika ili waweze kufanya shughuli zao kitaalam zaidi ili waweze kuboresha shughuli hizo lakini, pia kuongeza kipato chao na Pato kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyabiashara wadogo wadogo (*matching guys*). Ni ukweli uliodhahiri kuwa wafanyabiashara hawa wamekuwa si tu kuingiza pato nchini, bali pia wameweza kujikimu na kuleta biashara/chakula karibu na wadau hususan pale masoko yaliyo mbali. Lakini cha ajabu watu hawa wamekuwa wakisakamwa na Serikali hivyo kuishi kama yatima. Kama Serikali inaona wanavunja sheria basi Serikali iwajengee mahali pazuri pa biashara zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudzi za Serikali za maisha bora kwa kila Mtanzania bado *slogan* hii itabaki kuwa kichekesho kwani maisha bora hayo wananchi wanapotaka kujiletea Serikali inawanyang'anya kwa kuchukua bidhaa zao na hivyo mitaji yao kuisha kabisa hivyo kubaki waombaji au majambazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la Wachina wanaofanya biashara ndogo ndogo. Hivi ni sheria ya wapi kwa mtu wa nje kufanya biashara za ndani? Kibaya zaidi hata wale Watanzania waliokuwa wanafanyabiashara kwa kwenda kuchukuwa bidhaa China wameshindwa kwani Wachina sasa wanaleta wenyewe mizigo hiyo na hivyo kwa kuwa ni wao wenyewe hata bei zinakuwa rahisi. Hali hii imefanya wananchi wa Tanzania kushindwa biashara.

Naiomba Serikali ifanye kila jithadi kwa ajili ya ujenzi wa viwanda hasa vya kusindika mazao hususan matunda. Kanda ya Kaskazini - Tanga, Kilimanjaro na Arusha kuna matunda ya kila aina mbalimbali ambayo uwepo wa viwanda vya usindikaji ungesaidia sana vipato vya wananchi hao.

Mwisho naomba Wizara hii ihakikishe kuwa viwanda vinavyobinafsishwa na vinafanya kazi iliyokusudiwa na si vinginevyo kwani baadhi ya hivyo vimebaki *magodown* na mengine magofu. Hali hii imepelekea Tanzania tusiwe na chochote cha kuringia kwani vyote tunaagiza nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa *cement* ni muhimu sana kwa maendeleo ya wananchi. Ombi ni kwamba walau Serikali yenye kiwanda cha *cement* Kanda ya Ziwa kwani kuna idadi kubwa ya watu wahitaji.

MHE. RUTH B. MSAFIRI: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, nampongeza mtoa hoja. Naishauri Wizara kwa yafuatayo, *SIDO* iongezewe fedha. *SIDO* ni mkombozi wa wajasiriamali wadogo wadogo ambao ndio tumaini la kukuza uchumi kwa kasi kubwa kwa Watanzania wenzetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, *SIDO* imefanya kazi hii kwa muda mrefu kwa njia za kubangaiza hali inayoshusha ufanisi wake. Hakika *SIDO* wakiwa na fedha wanawenza kufanya miujiza katika uchumi wetu, ukakua haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali iangalie upya mapesa ya JK ambayo yanatolewa kwenye benki za *NMB* na *CRDB*. Hivi ilikuwaje *SIDO* ikasahaulika? *SIDO* walau nayo ingeonekana kama mkoa, ikapewa walau shilingi bilioni moja na ikatakiwa kutoa maelezo ya matumizi. Nina hakika ingefanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali sasa, itakapotoa awamu ya pili ya mkopo wa JK isiiyahau *SIDO*. *SIDO* inaweza na ina watu walio na moyo wa kazi yao. *SIDO* ienee hadi wilayani. Serikali iiunge mkono, itasaidia hata uanzishaji wa *SACCOS* zenyenye tija maana wana uwezo wa kufundisha, kufuatilia na wamesaidia sana.

Kuhusu viwango vya bidhaa zinazotengenezwa nchini viangaliwe mara kwa mara. Bidhaa zetu zinakuwa na viwango wakati wa usajili, ikifika wakati wa uzalishaji wanakiuka viwango. Hili ndilo linashusha soko la bidhaa za nchi, mfano *Whitedent Herbal* ilipoanza ilikuwa na *seal* sasa *seal* imeondolewa, kwa nini? Mimi nilipoinunua isiyo na *seal* nilidhani ni *fake*.

Mheshimiwa Naibu Spika, vifungushio vya bidhaa, wazalishaji wetu wadogo wadogo hata pale wanapothubutu wanakosa vifungashio vyenye hadhi. Vifungashio hivi ni muhimu katika ku-process bidhaa zetu, yakiwemo matunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali inunue vifungashio vya bidhaa zetu za ndani. Mfano, *Air Tanzania* ilitaka kutumia mvinyo wa Dodoma katika huduma ya wateja wake, lakini kiwanda kidogo cha wajasiriamali Dodoma hawana chupa ndogo, kwa hiyo, wamekosa hii biashara. Hapa hatuwezi kusaidia, kuzalisha bidhaa za ndani bila masoko hasa ya ndani. Vile vile, wanaotengeneza maji ya matunda, asali na kadhalika vifungashio ni taabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuchangia hayo, nawasilisha.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kwenye orodha ya walioomba kuchangia nimeishiwa na wachangiaji, lakini hatuna watu wengine wa kuendelea kuchangia.

Jioni tukirudi tutawapa Waziri na Naibu wake dakika 75 na hiyo ni kwamba, Naibu Waziri kama mchangiaji ni 15, mtoa hoja ni saa moja, jumla ni 75 wanawenza kugawana wenye wanavyofikiri watataka kugawana ili waweze kujibu hoja mbalimbali, halafu tutaendelea kama kawaida kwenye Kamati ya Matumizi.

Kwa hiyo, naomba niwatakie mchana mwema mpaka tutakopokutana saa 11.00 jioni.

(Saa 6.41 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nilipositisha Shughuli za Bunge mchana, nilisema wachangiaji wote walikuwa wamekwishachangia na hatukuwa na Waheshimiwa Wabunge wengine wa kuendelea kuchangia. Tulikubaliana kwamba tukirudi saa 11.00 jioni Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri wataanza kujibu hoja zenu. Sasa dakika 30 atachukua Mheshimiwa Naibu Waziri na dakika 45 Mheshimiwa Waziri mtoha hoja. Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Waziri. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuanza kuichangia hoja hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uzima na afya. (*Makofi*)

Pili, namshukuru Rais Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa imani ambayo ameendelea kuwa nayo juu yangu kwa kunteua niendelee kulitumikia Taifa letu katika nafasi hii ya Unaibu Waziri katika Wizara hii muhimu. Namshukuru pia Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ushauri na maelekezo yake mbalimbali yanayonisaidia kuyamudu vyema majukumu yangu. Namshukuru sana Waziri wangu Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, kwanza kwa imani yake kubwa sana anayoonyesha kwangu kwa kunishirikisha kwa karibu sana katika kuiongoza Wizara hii na pili, kwa umahiri wake katika uongozi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Katibu Mkuu Dr. Tax Bamwenda, ambaye kama Waziri Mheshimiwa Dr. Mary Nagu ni mwanamama mahiri, mzalendo, mchapa kazi asiyechoka na anayefahamu vyema sekta hii pana ya Viwanda, Biashara na Masoko. Namshukuru sana ndugu yangu Naibu Katibu Mkuu Dr. Florence Turuka kwa uchapakazi wake wa kutolea mfano na kwa ushirikiano mkubwa anaonipa. Aidha, nawashukuru kwa dhati kabisa Wakurugenzi wote waliopo Makao Makuu na wa Taasisi zilizo chini ya Wizara na pia wafanyakazi wote wa Wizara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Spika, kwa kuteuliwa kuwa Rais wa Chama cha Mabunge ya Jumuiya ya Madola na kwa jinsi anavyoshirikiana nawe, Wenyeviti wa Bunge na watendaji wa Bunge kuliendesha Bunge letu vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kutumia fursa hii kuwashukuru wapigakura wa Jimbo la Moshi Vijijini kwa kuendelea kuniunga mkono kwa vitendo, nawashukuru hasa kwa moyo wao wa kujitolea katika kulilettea Jimbo letu maendeleo mbalimbali hasa katika sekta za elimu, maji, miundombinu, mazingira na kilimo. Pamoja na wananchi hao ninaushukuru uongozi wa Chama na Serikali katika Wilaya ya Moshi na katika Mkoa mzima wa Kilimanjaro kwa ujumla kwa jinsi wanavyoshirikiana nami kupeleka maendeleo Moshi Vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru pia familia yangu na marafiki zangu kwa uvumilivu na uelewa wao, mambo yanayonisaidia kutekeleza wajibu wangu kwa amani na kwa ufanisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno hayo ya awali, naomba kwanza kabisa niseme kwamba naiunga mkono hoja hii. Pili, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kuichangia hoja hii na tatu, naomba nijielekeze katika kutoa mchango wangu kwa kujibu baadhi ya hoja zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kwanza, inahusu ufinyu wa Bajeti nayo inasema kwamba Wizara na Taasisi zake pamoja na majukumu makubwa waliyonayo imetengewa fedha kidogo ambazo hazikidhi mahitaji. Wametolea mfano, *SIDO* ambayo iliomba shilingi bilioni tano lakini imetengewa kiasi cha shilingi bilioni moja tu. Nyingine ambazo zimetolewa mfano ni *EPZA*, *CAMARTEC* na *TIRDO*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hii imechangiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi na idadi yao ni 12, nikianza na Mheshimiwa Yono Kevela, Mheshimiwa Abdallah Salum Sumry, Mheshimiwa Basil Mramba, Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia, Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa Anne Malecela, Mheshimiwa Margreth Mkanga na Mheshimiwa Diana Chilolo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2008/2009 Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko pamoja na Taasisi zake imetengewa kiasi cha shilingi 39,260,643,600/= kati ya fedha hizi kiasi cha shilingi 7,998,509,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 31,262,134,600/= ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Wizara imetengewa shilingi 4,733,385,000/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 4,615,394,600/= kwa matumizi ya maendeleo. Taasisi ambazo zipo chini ya Wizara zimetengewa kiasi cha shilingi bilioni 4.3 kwa matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 26.6 kwa matumizi ya maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa hapa nitaje baadhi ya hizo Taasisi ambazo Waheshimiwa Wabunge wameziulizia, taasisi ya kwanza ni *EPZA* ambayo imetengewa shilingi milioni 400 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 13.9 kwa ajili ya maendeleo na jumla ni shilingi bilioni 14.3. Taasisi ya *SIDO* ambayo Waheshimiwa Wabunge wengi sana wameonyesha kwamba inahitaji kuongezewa fedha imetengewa shilingi 1,100,793,800/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 7,242,317,00/= kwa ajili ya matumizi ya maendeleo, jumla *SIDO* imetengewa shilingi 8,343,110,800=/. Taasisi ya *CAMARTEC* imetengewa shilingi 202,378,600/= kwa shughulil za kawaida na shilingi bilioni 3.9 kwa ajili ya shughulil za maendeleo jumla shilingi 4,102,378,600=/. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunakiri kwamba Bajeti hii si kubwa sana, lakini tutajitahidi Taasisi hizi zitatimiza wajibu wake kadri inavyowezekana na ndani ya uwezo tuliyopewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili, ni ya wafanyakazi wa Kiwanda cha *Mufindi Paper Mills* kwamba ulipwaji wa haki za waliokuwa wafanyakazi wa Kiwanda cha Karatasi cha Mgololo haujafanyika na kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wawili wameuliza Wizara itoe ufanuzi. Waheshimiwa Wabunge hao ni Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa wa Karatu na Mheshimiwa Benito Malangalila wa Mufindi Kusini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba lipo tatizo la malipo kati ya wafanyakazi na kiwanda hiki na tatizo hilo lilienda Mahakama na Mahakama Kuu kitengo cha kazi mnamo mwezi Desemba, 2007 lilitolewa hukumu na katika hukumu hiyo iliamuliwa wafanyakazi walipwe shilingi bilioni mbili, fedha ambazo Kiwanda cha *SPM* wameomba marejeo yake katika Mahakama na Kitengo cha Kazi cha Mahakama Kuu bado kinayafanya kazi na hakijayatolea maamuzi. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge hao wasubiri mpaka Mahakama itakapotoa uamuzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Mheshimiwa Benito Malangalila, Mbunge wa Mufindi Kusini, amemwomba Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko atembelee Kiwanda cha Mgololo na aongee na wafanyakazi waliokuwa wameachishwa kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kutumia fursa hii kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wangu kumshukuru sana Mheshimiwa Benito Malangalila kwa maneno yake mazuri jana ya kuonyesha kwamba kile Kiwanda kilikuwa na umuhimu kabisa wa kubinafsishwa na vile vile kwa kutambua kwamba kubinafsishwa huko kumewezekana kutohana na juhudu kubwa zilizofanyika kufufua kiwanda hicho ikiwa ni pamoja na juhudu kubwa za Serikali. Mheshimiwa Waziri wangu anaahidi kwamba mara apatapo muda atakitembelea kiwanda hicho na ataongea na wafanyakazi hao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni hoja inayozungumzia suala la ubinafsishaji wa viwanda ambavyo havijaanza kufanya kazi. Waheshimiwa Wabunge wameuliza Wizara, hivyo viwanda ambavyo havijaanza kufanya kazi utaratibu wake ukoje? Waheshimiwa Wabunge hao ni Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella na Mheshimiwa Benson Mpesa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, majibu yake ni kwamba Serikali imekuwa ikiweka mazingira ya uwezeshi ili wawekezaji wanaonunua viwanda wavifufue. Kama nilivyokwishaeleza hapa Bungeni katika mojawapo ya majibu ya maswali ya hapa Bungeni baada ya zoezi la uperembaji kukamilika katika Kanda zote ikiwa ni pamoja na viwanda vya Kanda ya Kaskazini, Kanda ya Ziwa na Nyanda za Juu Kusini kwa mwaka huu wa fedha Wizara itapendekeza hatua za kuchukuliwa. Kwa hiyo, endapo kuna viwanda ambavyo vitakuwa havijafanya kazi tangu vimebinafsishwa na ikaonekana kabisa kwamba viwanda hivyo haviteweza kufufuka, basi Wizara itatoa mapendelekezo virudishwe Serikalini ili watafutwe wawekezaji wengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni kuhusu kufufua Kiwanda cha Matunda cha Korogwe, hoja hii imeletwa na Mheshimiwa Joel Bendera, napenda

kumjibu Mheshimiwa Joel Bendera kaka yangu kwamba suala la ubinafsishaji wa Kiwanda cha *TANGOLD* limekuwa likishughulikiwa na linaendelea kushughulikiwa na *Consolidated Holding Corporation* iliyochukua shughuli za Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma (*PSRC*) kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Napenda kumuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara yangu itatoa ushirikiano kadri unavyohitajika na namwomba tuwasiliane ili kwa pamoja tuweze kulipa msukumo mpya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyine ni hii ambayo ameizungumzia Mheshimiwa Benito Malangalila ambayo alisema kuna wafanyakazi walikuwa wa Kiwanda cha Pareto hawakulipwa mafao yao halisi. Mheshimiwa Waziri anatakiwa atoe maelezo kuhusu lini watamaliziwa kulipwa mafao yao. Hoja hizi tumezipokea na tutazifanya kazi kwa kushirikiana kwa karibu sana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na tutakapozifanya kazi, basi Mheshimiwa Mbunge atapata majibu ya uhakika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyine ni hoja ya Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa ambayo ameulizia usajili wa Makampuni. Kwanza, ameulizia usajili wa Kampuni ya *Deep Green Finance Company Limited* ilisajiliwa lini? Pili, anaulizia Wakurugenzi wa Kampuni hiyo walikuwa akina nani wakati wa usajili na kama kumekuwepo na mabadiliko wakati wa uhai wa Kampuni na tatu, wamiliki wa Kampuni hiyo ni akina nani na kila mmoja anamiliki au ameendelea kumiliki kiasi gani cha hisa katika kipindi cha uhai wa Kampuni. Nne, taarifa alizonazo ni kuwa Kampuni hiyo imefungwa, je, ilifungwa lini? Tano, kuna taarifa kwamba nyaraka muhimu hazionekani, je, kuna ukweli gani kuhusu haya na pia kama nyaraka hizo zipo kwa nini Serikali iziwasilishé kwa Katibu wa Bunge ili ziwekwe kwenye Maktaba ya Bunge?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa kama ifuatavyo, Kampuni ya *Deep Green Finance Company Limited* ilisajiliwa tarehe 18 Machi, 2005 na kupewa namba ya usajili 51870, wakati wa usajili wanahissa walikuwa Protase R.G. Ishengoma na Stella Ndikimi wote wa Sanduku la Posta 72484 Dar es Salaam, kila mmoja akimiliki hisa moja moja. Aidha, wakati huo wa usajili Kampuni ilikuwa na Wakurugenzi wawili Bwana Marco Weston, raia wa New Zealand na Anthony Tajadi, raia wa Afrika ya Kusini. Tarehe 8 Aprili, 2005 yalifanyika mabadiliko ambapo Ludovick Fan Scripher, raia wa Afrika ya Kusini aliongezeka kama Mkurugenzi wa tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 25 Septemba, 2007 Kampuni iliwasilisha fomu ya *Annual Return* ikionyesha ya kuwa Bwana Protase R.G. Ishengoma alihamisha hisa zake kwenda kwa *Ned Bank Limited* ya Afrika Kusini hapo tarehe 15 Aprili, 2005 na tarehe hiyo Stella Ndikimi alihamisha hisa yake kwenda *Ned Bank Africa Investment Limited* nayo ya Afrika Kusini. Fomu hiyo inaonyesha pia kuwa *Ned Bank Investment Limited* nayo ilihamisha hisa yake kwenye *SPM Medical Holding Limited* ya Mauritius. Kulingana na Azimio la hiari Kampuni hii ilifungwa tarehe 27 Agosti, 2007. Wizara ipo tayari kuwasilisha kwa Bunge lako Tukufu jalada la Kampuni hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyine inahusu usajili wa Richmond. Hoja hii imeletwa na Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa naye anauliza kwanza, Serikali inasemaje

kuhusu upotevu wa nyaraka muhimu za usajili wa Kampuni ya Richmond iliyochunguzwa na Kamati Teule ya Bunge? Pili, kama zikipatikana, Wizara ipo tayari kuziwasilisha kwa Katibu wa Bunge ili ziwekwe Maktaba? Tatu, kuna barua ilisema mtumishi wa BRELA aliyenyofoa nyaraka ili kuficha ukweli alipewa bakishishi na Serikali ya kujengewa nyumba Chang'ombe Temeke, je, Wizara imefanya uchunguzi na kama uchunguzi haujafanya Waziri anatoa kauli gani? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sakata hili la Richmond naomba nilifahamishe Bunge lako Tukufu kuwa Kampuni ya *Richmond Development Company LCC* ya Houston Texas, Marekani iliyoshinda zabuni ya kuzalisha umeme wa dharura haijawahi kusajiliwa na BRELA, hivyo haiwezekani kuficha au kubadilisha kumbukumbu za jadala ambalo halijawahi kuwepo BRELA. Kampuni iliyosajiliwa na BRELA ni *Richmond Development Company (T) Limited* iliyosajiliwa tarehe 12 Julai, 2006 jalada la Kampuni hii na taarifa zake zipo. Mpaka sasa hivi Wizara haijaweza kuthibitisha tuhuma za Afisa mmoja wa BRELA kupewa nyumba kama bakishishi baada ya kufanikisha kazi ya kunyofoa nyaraka. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, namshauri Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, kama hajaridhika na maelezo haya awasilishe vithibitisho vya tuhuma zilizotolewa ili hatua muafaka za kisheria ziweze kuchukuliwa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni hoja ya Mheshimiwa Kabwe Zitto ambaye ameuliza Ibara ya 94 inasema Jasi (*bauxite*) hii ni sahihi, lakini ye ye anadhani kwamba jasi ni *gypsum* na akawa anaomba tafsiri sahihi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kusema kwamba ni kweli kuwa jasi ni *gypsum* kama alivyosema Mheshimiwa Kabwe Zitto na napenda kumshukuru kwa kuliona hilo na tunaomba radhi kwa kosa hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni ya Mheshimiwa Abdallah Salum Sumry ambaye amesema Serikali iandae utaratibu wa kuangalia mgawanyiko wa rasilimali yaani *mapping* Mkoani Rukwa ili kuanzisha viwanda vikiwemo vya samaki, *gypsum* na kadhalika. Jibu lake ni kwamba ushauri umepokelewa na Wizara itaufanyia ushauri huu kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni hoja ya Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba na Mheshimiwa Ernest Mabina ambao kwa pamoja wanaomba kiwanda cha kuchengua dhahabu kijengwe Geita. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa NDC kwa kushirikiana na Wizara ya Miundombinu, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na Wizara ya Nishati na Madini wanafanya utafiti wa miradi yote iliyopo kwenye Kanda ya Kati yaani *Central Development Corridor*. Kanda hii ni moja ya Kanda tatu za maendeleo zilizopo kwenye majukumu ya NDC na inajumuisha Zanzibar na Pemba, Dar es Salaam na Pwani, Morogoro, Dodoma, Singida, Tabora, Shinyanga, Mwanza, Kigoma na Kagera na

kuunganisha nchi jirani ya Rwanda ambayo tunashirikiana nayo hasa katika ujenzi wa Reli ya Kati hadi Kigali. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa utafiti wa miradi umefanyiwa kazi kwa msaada wa fedha kutoka Serikali ya Afrika Kusini kupitia *Development Bank of South Africa* na *consultants* wanaofanya kazi hii wamefikia mwisho. Ifikapo mwezi Oktoba mwaka huu miradi inayohusika itawekwa bayana kwa ajili ya kuitafutia wawekezaji baada ya Serikali kuridhia.

Katika mchakato huo inapendekezwa kuanzisha Kiwanda kimoja cha kusafisha dhahabu, inapendekezwa pia kuanzisha viwanda vya wajasiriamali wadogo wawze kutengeneza bidhaa zitokanazo na dhahabu kama mikufu na kadhalika. Wajasiriamali hao watawezesha kama inavyofanyika Afrika Kusini kwa kukopeshwa fedha za kununua dhahabu, kupatiwa eneo la kufanya kazi na kurejesha mikopo mara wauzapo bidhaa zao. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nytingine ni hoja ya hao hao Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba pamoja na Mheshimiwa Ernest Mabina ambao wanaomba kiwanda cha matunda kijengwe Geita kwani eneo hilo lina matunda mengi. Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na viwanda vya kusindika mazao ya kilimo hususan matunda. Kwa kuzingatia umuhimu huo Serikali itawasiliana na Halmashauri ya Wilaya ya Geita ili ifanye tathmini ya uwezekano wa ujenzi wa kiwanda cha kusindika matunda Wilayani Geita kabla ya kuweka pendelezo hilo katika Mpango wa Maendeleo wa Halmashauri ya Wilaya na kutenga fedha kwa ajili ya uanzishwaji wa kiwanda hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nytingine ni hoja ya Mheshimiwa Mgana Msindai ambayo imejumuisha na hoja ya Mheshimiwa Savelina Mwijage pamoja na hoja ya Mheshimiwa Prof. Idris Mtulia ambao kwa ujumla wameuliza kwamba viwanda vipyta vianzishwe Mikoani pia badala ya kulundikana Dar es Salaam, Tanga, Moshi, Arusha, Mwanza na Mbeya tu, na hata katika Mikoa vipelekwe katika maeneo ya vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu kama ifuatavyo:- Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na viwanda katika sehemu mbalimbali nchini ikiwa ni pamoja na Mikoa ambayo kwa sasa ipo nyuma katika maendeleo ya viwanda. Sera ya Serikali ni kuweka mazingira wezeshi ya kuvutia wawekezaji. Kwa kuzingatia maendeleo yaliyotarajiwa kikanda Wizara inaandaa Mkakati Uganishi na Mpango Kabambe wa Kuendeleza Viwanda Nchini. Katika hatua za awali mkakati huu umebuni mwambao wa Pwani kuwa kitovu cha maendeleo vya viwanda na mauzo nje kwa kutumia bandari na rasilimali zilizopo katika Kanda tatu za Mtwara, Dar es Salaam na Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, msisitizo umewekwa katika usindikaji wa mazao ambapo usindikaji wa mwanzo Mikoani na usindikaji wa kati na usindikaji kwa ajili ya mauzo nje utafanyika katika Mwambao wa Pwani. Uwekezaji katika Kanda hizi za Mwambao wa Pwani unalenga viwanda vya kuzalisha pembejeo na zana za kilimo ili kuongeza uzalishaji wa mazao na uhakika wa malighafi kwa viwanda vya usindikaji vilivyopo na vitakavyoanzishwa, na ili kuhakikisha upatikanaji wa malighafi kwa

viwanda hivi Serikali imeweka mkazo kuwawezesha wenyewe viwanda kuingia mikataba na wakulima kwa kutoa mafunzo na kuwezesha upatikanaji wa pembejeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati mwagine ni kuhimiza uanzishwaji wa viwanda vidogo vya usindikaji wa mazao kupitia Mradi wa Muunganisho Ujasiriamali Vijijini ambao pamoja na mambo mengine unahimiza kuongeza thamani ya mazao kwa kuhimiza sekta binafsi kuanzisha viwanda Mikoani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni hoja ya Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama ambaye ameuliza Serikali ina mkakati gani wa kushusha bei za bati na saruji?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hatua ya muda mfupi, Serikali imeruhusu uingizaji wa bidhaa hizi hususan saruji hapa nchini kwa lengo la kupunguza kupanda kwa bei kunakotokana na ongezeko la mahitaji katika sekta ya ujenzi. Aidha, bei hizi zitapungua kwa kadri ya uzalishaji hapa nchini unavyoongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni hoja ya Mheshimiwa Hemed Mohammed Hemed ambayo vile vile inaunganishwa na hoja ya Mheshimiwa Lucy Owenya ambao wamesema kwa nini bei za baadhi ya bidhaa vipo juu wakati viwanda vyake vinatumia gesi asilia? Kwa nini matumizi ya gesi hayapunguzi zipo gharama za uzalishaji? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bei ya gesi asilia inayotumika hapa Tanzania ni kati ya *dollar* za Kimarekani 3 hadi 4 kwa *gigajoule* moja yaani kipimo cha nishati. Bei ya gesi asilia kwenye nchi zinazozalisha mafuta ni *dollar* za Kimarekani 0.75 kwa *gigajoule* moja, hii ni kwa sababu kwa upande hao wanaozalisha mafuta, gesi asilia ni bidhaa ya nyongeza yaani *by product* hivyo haibebeshwi gharama za msingi za uzalishaji na hivyo kufanya bei yake kuwa nafuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Tanzania gesi asilia ndiyo bidhaa kuu hivyo hubebeshwa gharama zote zinazohusu uzalishaji na hivyo kufanya bei yake isiwe nafuu na hivyo kufanya bidhaa zinazozalishwa kwa kutumia gesi hii gharama zake zisishuke kwa kasi inayotegemewa. Aidha, gesi asilia ni sehemu tu ya gharama za uzalishaji kwenye viwanda hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, gesi asilia inatoa unafuu mkubwa kwa wazalishaji wetu wa viwandani kwani wangkuwa bado wanatumia mathalani mafuta machafu, bei ya *gigajoule* moja kwa bei za mafuta za sasa ingekuwa siyo chini ya *dollar* za Kimarekani 20 na hii ni mara tanoya gharama za gesi asilia. Hivyo, Tanzania tunanufaika kwa kuwa na gesi asilia yake kwani mfumuko wa bei unaotokana na kutumia gesi asilia ni mdogo kuliko ule ambao ungetokana na matumizi ya mafuta yatokanayo na petroli yaani *heavy refinery oil*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lingine wameuliza Serikali ina kigugumizi gani kufanikisha viwanda ili kumkomboa mkulima. Jibu ni kwamba Serikali inaendeleza

juhudzi za kufufua na kuanzisha viwanda vinavyozalisha pembejeo na kusindika mazao ya kilimo ili kuleta mapinduzi ya kilimo na hivyo kumkomboa mkulima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lingine Wizara imetekeleza vipi ahadi zifuatazo, kwanza, kufanya mapinduzi katika viwanda, pili, kufanya mapinduzi katika kilimo na tatu, kujenga rasilimali watu? Jibu Serikali inatekeleza mikakati na programu mbalimbali ili kuwezesha mapinduzi ya viwanda na kilimo. Mikakati hiyo ni pamoja na kuandaa Mkakati Uunganishi na Mpango Kabambe wa Maendeleo ya Viwanda, Mkakati wa Kukuza Mauzo Nje, *Tanzania Trade Integration Strategy* na pia *Agricultural Sector Development Programme*. Juhudi zote hizi zimelenga kufanya mapinduzi ya sekta ya viwanda na kilimo ikiwa ni pamoja na kujenga rasilimali watu ifikapo mwaka 2025 kama dira ya maendeleo ya Taifa inavyoolekeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni ile ambayo inasema Serikali imeweka mikakati gani kufufua Kiwanda cha *DOWICO* ili wakulima wa zabibu katika Mkoa wa Dodoma wapate soko la kuuza zabibu na ili vijana waweze kupata ajira? La pili, kiwanda cha magodoro ya Dodoma kimehamishiwa Dar es Salaam na mmiliki wake anaendelea kutumia jina la Dodoma kama *Trademark* yake, je, kwa nini kiwanda hiki kisifufuliwe hapa Dodoma ili kutoa ajira kwa vijana wa Dodoma? Swali hili limeulizwa na Mheshimiwa George Lubeleje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, majibu ni kwamba Serikali imefanya tathmini ya viwanda vilivyopo nchini, hivi sasa uchambuzi wa taarifa unafanywa na taarifa ya tathmini hiyo itatuwezesha kujua nini kilitokea katika kiwanda cha *DOWICO* na hatua muafaka za kuchukua. Kuhusu kiwanda cha magodoro, chini ya Sheria ya Alama ya Biashara na Huduma ya mwaka 1986 ikiwa mmiliki wa alama ya biashara yaani *Trademark* ni huyo huyo na anaitumia hapa hapa nchini kwa bidhaa hiyo hiyo hatendi kosa la kutumia alama ya biashara hiyo huko Dar es Salaam, Serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi ili kuvutia wawekezaji kuja kuanzisha viwanda vya aina mbalimbali katika Mkoa wa Dodoma ili kuongeza ajira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine, Serikali ifufue kiwanda cha ngozi Mwanza na kuanzisha Shinyanga ili kuboresha hali za wafugaji. Swali hili limeulizwa na Mheshimiwa Meryce Emmanuel. Majibu Serikali inatambua umuhimu wa sekta ya ngozi ikiwa ni pamoja na viwanda vya ngozi. Kwa kutambua umuhimu huu Serikali inatekeleza mkakati wa kufufua na kuendeleza sekta ya viwanda vya ngozi, lengo ni kuhakikisha kwamba viwanda vinasindika ngozi hadi hatua ya mwisho ili kupata ngozi zitakazotumika na viwanda vya bidhaa za ngozi nchini. Mkakati huu pia unalenga kuhamasisha sekta binafsi kufufua na kuanzisha viwanda vya kusindika ngozi ghafi na kutengeneza bidhaa za ngozi hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni hoja ya Mheshimiwa Yono Kevela, ambaye amesema Kata ya Wanging'ombe kijiji cha Ingelege Njombe kimepewa ekari 150 kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha mbolea hai yaani *organic fertilizer* kwa msaada wa mwekezaji kutoka Marekani, anaomba Serikali ishirikiane na mwekezaji aliyepatikana kujenga miundombinu ya umeme na maji katika eneo hilo ili kiwanda hicho kianze kufanya kazi mwaka 2010. Majibu ni kwamba Serikali kwa kushirikiana na

wadau wengine itaendelea kuimarisha miundombinu mbalimbali ikiwa ni pamoja na barabara, umeme na maji na kuboresha huduma nyingine muhimu kwa maendeleo ya viwanda hapa nchini ikiwa ni pamoja na kiwanda cha mbolea hai *organic fertilizer* katika kijiji alichokisema Mheshimiwa Mbunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili anasema Serikali ielekeze nguvu kwenye viwanda vya gesi nya Arusha, Minjingu na Mtwara katika uzalishaji wa mbolea. Jibu ni kwamba Wizara inaendelea na juhudi za kuhamasisha uwekezaji katika viwanda vypa nya mbolea, tayari Serikali imekwishafanya mazungumzo na menejimenti ya kiwanda cha *Minjingu Mines and Fertilizer Limited* kupanua uzalishaji wa *Minjingu Rock Phosphate*. Aidha, kwa kutambua ongezeko la mahitaji ya mbolea nchini na kuwepo gesi asilia Serikali imefanya juhudi za kuvutia wawekezaji na tayari kampuni 12 zimejitokeza kuonyesha nia ya kuwekeza katika viwanda vya mbolea kwa kutumia gesi asilia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni ya Mheshimiwa Janeth Massaburi ambaye amesema asilimia 20 ya korosho iliyosindikwa na asilimia 80 ya korosho ghafi huuzwa nje na kati ya asilimia 35 mpaka 40 tu ya ngozi iliyosindikwa na kati ya asilimia 60 mpaka 65 ya ngozi ghafi huuzwa nje. Hali hii ya kuuza bidhaa ghafi badala ya *processed goods* itaendelea mpaka lini. Majibu hivi sasa kuna viwanda vitano vya kubangua korosho hapa nchini na baadhi yake vimebinafishwa kwa wawekezaji wazalendo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na jitihada za kuwaunganisha wawekezaji wazalendo walionunua viwanda vya kubangua korosho na wabia ili kupata mitaji itakayowezesha kufufuliwa kwa viwanda vya kubangua korosho na hivyo kuongeza kiasi cha korosho kilichobanguliwa na kusindikwa kabla ya kuuzwa nje. Lengo ni kuhakikisha kuwa korosho yote inayozalishwa hapa nchini inauzwa nje ikiwa imeongezwa thamani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ngozi Serikali imeanza kutekeleza Mkakati Unganishi wa Kufufua na Kuendeleza Sekta ya Viwanda vya Ngozi Nchini kwa kuhusisha wadau mbalimbali, mkakati huu unalenga kukuza uwezo wa viwanda vya ndani ili kusindika ngozi zote hapa nchini badala ya kuziuza nje zikiwa ghafi kwa kuhakikisha kuwa ngozi zinazozalishwa ni bora na zinazalishwa kwa utaalim unaotakiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lingine la Mheshimiwa Janeth Massaburi ni kwa nini hatujali bidhaa za ndani ili kuwapa uwezo na nguvu wazalishaji wa ndani. Jibu Serikali inajali na kuthamini bidhaa zinazozalishwa hapa nchini na kwa kuzingatia umuhimu huo Serikali inafanya mapitio ya sheria iliyoanzisha *BET* ili kuihuisha na kuanzisha *TANTRADE* ambayo itakuwa na jukumu la kuendeleza biashara ya ndani na nje. (*Makofi*)

Aidha, Serikali inaendelea kuhamasisha wazalishaji wa ndani kuboresha bidhaa zinazozalishwa ili ziweze kuwavutia Watanzania, pia Watanzania wanaendelea

kuhamasishwa kuenzi bidhaa zinazozalishwa hapa nchini. Kauli mbiu yetu kwa Watanzania ni “Nunua Bidhaa za Tanzania, Jenga Tanzania. (Makofi)

Hoja nyingine ya Mheshimiwa Anne Kilango Malecela ambaye anasema Serikali lazima iingie katika mfumo wa viwanda ili kuongeza thamani ya bidhaa zetu kabla ya kuziuza nje na ndani ya nchi. Ushauri huu umepokelewa na utafanyiwa kazi. Mheshimiwa Aloyce Kimaro anasema viwanda vijengwe maeneo yanakopatikana mazao au malighafi kwa mfano hatuna kiwanda cha juisi au kusindika matunda yanakolimwa matunda yenyewe. Jibu ni kwamba ushauri huu tumeupokea na utaendelewa kufanyiwa kazi. (Makofi)

Hoja ya Mheshimiwa Stephen Galinoma, Mbunge wa Kalenga anasema jimbo la Kalenga lina kiwanda kimoja tu cha kusindika *juice*, kiwanda pekee kilichokuwepo cha sigara kilikufa kwa *corporate take over* ambalo ni jambo la kawaida katika biashara. Je, haiwezekani kuhamasisha uwekezaji mbadala kwani kuna tumbaku inayolimwa ya kutosha? Jibu Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine itaendelea na wajibu wake wa msingi wa kuboresha mazingira ya biashara na kuhamasisha uwekezaji katika maeneo mbalimbali ya nchi ambako malighafi inapatikana kwa wingi ikiwa ni pamoja na Kalenga, ili kutosheleza mahitaji ya viwanda na hivyo kuchochea maendeleo ya viwanda hapa nchini. (Makofi)

Mheshimiwa Basil Mramba anasema *basic industry strategy* bado hajatekelezwa na hivyo nchi haiwezi kuwa na viwanda. Jibu kwa sasa Wizara inaandaa mkakati unganishi na mpango kabambe wa kuendeleza sekta ya viwanda. Pamoja na mambo mengine mkakati huu utarejea utekelezaji wa mipango mizuri iliyokuwemo ndani ya *basic industry strategy* ili kutimiza azma ya Serikali ya Tanzania kuwa na maendeleo ya uchumi wa viwanda unaoongozwa na mauzo nje kama ilivyoinishwa katika dira ya maendeleo ya Taifa. (Makofi)

Mheshimiwa Kanali Feteh Saad Mgeni, Mbunge wa Bumbwini anasema tuimarishe viwanda maana ndio msingi wa kuimarisha uchumi wa kisasa. Jibu ushauri umepokelewa na tutaufanya kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Benson Mpesya, Mbunge wa Mbeya Mjini anasema Kiwanda cha *New Mbeya Textiles Mills* kiwezeshwe kupata malighafi kwa kilimo cha pamba kurejeshwa Mkoa wa Mbeya. Jibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika wakati wa kuhitimisha hotuba yake ya Bajeti ya mwaka huu alisema utafiti juu suala la kuruhusu kilimo cha pamba umekamilika na kinachofanyika sasa ni kufanya tathmini ya kiuchumi ili Serikali iweze kutoa maamuzi. Kwa wakati huu tunaposubiri uamuzi wa Serikali Kiwanda cha *New Mbeya Textiles Mills* kinashauriwa kununua pamba ghafi kutoka mikoa ya Kanda ya Ziwa badala ya Cameroon na Nigeria. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja hii. (Makofi)

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru tena kwa kunipa nafasi hii na nakushukuru sana kwa kuendelea kuwepo wakati Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko inatoa hoja yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nichukue nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe tena na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kusikiliza bila kuonyesha kuchoka wakati nilipokuwa nawasilisha makadirio ya matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka 2008/2009. (*Makofi*)

Aidha, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa njia ya maandishi au kwa kuzungumza wakati Waziri Mkuu alipowasilisha hoja yake na wakati Waziri wa Fedha alivyowasilisha hoja na Mawaziri wengine jana na leo wakati Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko ikiwa inawasilisha hoja yao na madhumuni ya hoja zote ni kutushauri na kuboresha utendaji wa kazi ya Wizara yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru kwa moyo wa dhati Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatib, Mbunge wa Makunduchi na Mwenyekiti wa Kamati yetu na anayemsaidia Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mbunge wa Mkinga, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Viwanda na Biashara kwa hoja walizotoa na ushauri waliota wajume wa Kamati wote wakisaidiana kuimarisha Wizara yangu ninawashukuru sana. Vile vile napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Lucy Owenya, Mbunge wa Viti Maalum, CHADEMA, Msemaji Mkuu wa Upinzani wa Wizara hii kwa kutoa ushauri na kutoa mambo mengi ambayo nina hakika kama tutayafulilia yatatusaidia sana katika kuimarisha Wizara yetu na kwa pamoja kujenga Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja na michango iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge katika kujadili hotuba yangu inaonyesha nia thabiti ya ushirikiano wenu na Wizara yangu katika kuziendezea sekta za Viwanda, Biashara na Masoko na kusukuma mbele gurudumu la maendeleo ya Taifa letu nimetiwa moyo na nimetiwa faraja kubwa kwa mambo mawili, kwanza kukubaliana nami katika mambo ya msingi. Hata Wapinzani wamekubaliana nami kwenye mambo ya msingi inaonyesha kwamba wote tuko hapa katika kujenga Taifa letu. (*Makofi*)

Pili, kutetea kwa nguvu zenu zote maslahi ya Taifa na wananchi tunaowawakilisha. Kwa ujumla hoja na michango mingi imelenga maeneo makuu kama yalivyokuwa nimyaeleza kwenye hotuba ya Bajeti yangu, ya kwanza ni ufinyu wa Bajeti na umuhimu wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara katika ujenzi wa maendeleo ya Taifa na ya pili ni ari kubwa ya kuendeleza viwanda ili itie msukumo kwenye uchumi wa nchi yetu na ya tatu, ni kuendeleza biashara na viwanda vidogo, nne, ni kuendeleza biashara kubwa, tano kuendeleza masoko na mwisho ushirikiano wa kibiashara baina ya nchi na nchi kikanda na Kimataifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya Waheshimiwa Wabunge 68 walichangia hoja zinazohusu Wizara yangu, wakati wakichangia hotuba za Wizara mbalimbali ikiwemo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Aidha, jumla ya Waheshimiwa Wabunge 26 walichangia

hotuba yangu kwa kauli jana na leo na Waheshimiwa Wabunge wapatao 71 walichangia kwa maandishi. Utaona kwamba inaonyesha jinsi ambavyo Wabunge wameiona Wizara hii ni muhimu kwa michango yao mingi na nina hakika hata wale ambao hawakutoa michango tayari wametambua ni kwa namna gani Wizara hii ni muhimu. (*Makofi*)

Michango ya Waheshimiwa Wabunge ni mingi na muhimu na inayohitaji majibu ya kina. Kwa muda mfupi nilionao majibu yangu yameelekezwa katika maeneo makuu yaliyochangiwa kama nilivyooleza hapo juu. Hata hivyo nawahakikishia Wabunge wote waliochangia kwamba majibu ya kina yatajibiwa na kila Mbunge atapewa majibu ya maandishi. Ikitokea mmoja ambaye nimemsahau basi anisamehe sio kwa sababu sipendi awepo ni kwa sababu ya ubinadamu wangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile Wabunge 68 waliochangia wakati wa hoja ya Waziri Mkuu na Mawaziri wengine wamekwishatambuliwa naomba kwa sababu ya muda nilionao nisiwataje tena bali nianzie kuwatambua Waheshimiwa Wabunge waliochangia hotuba yangu kwanza kwa kauli na baadaye kwa maandishi. Wale waliochangia kwa kauli ni kama ifuatavyo, Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatib, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Abdallah Salum Sumry, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa Anne Malecela, Mheshimiwa Aloyce Kimaro, Mheshimiwa Benito Malangalila, Mheshimiwa Basil Mramba na Mheshimiwa Herbert Mntangi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Benson Mpesa, Mheshimiwa Yono Kevela, Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Margreth Mkanga, Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mheshimiwa Ludovick Mwananza, Mheshimiwa Habib Juma Mnyaa, Mheshimiwa Vita Kawawa, Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, Mheshimiwa Said Arfi, Mheshimiwa Kaika Telele, Mheshimiwa Richard Ndassa na Mheshimiwa Dr. Cyril Chami, Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko ambaye amenisaidia sana kuchangia hoja za Wabunge kwa umahiri mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge waliochangia kwa maandishi ni hawa wafuatao, Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatib, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Ernest Mabina, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mheshimiwa Castor Ligallama, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Meryce Emmanuel, Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama, Mheshimiwa Yono Kevela, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro na Mheshimiwa Bernardeta Mushashu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Mohamed Amour Chomboh, Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, nimetamka vizuri jina la kaka yangu. (*Makofi/Kicheko*)

Wengine ni Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Stephen Galinoma, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia, Mbunge wa Rufiji, Mheshimiwa Kanali Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Aloyce Kimaro, Mheshimiwa Rita Mlaki, Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, Mheshimiwa Kaika Telele na Mheshimiwa Felista Bura. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Fatma Abdallah Mikidadi, Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mheshimiwa Kapteni John Komba, Mheshimiwa AL-Shymaa Kwegyir, Mheshimiwa Benson Mpresa, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Khadija Ally Al-Qassmy, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Margaret Sitta, Mheshimiwa Dr. Omar Kigoda, Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Ania Chaurembo, Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, Mheshimiwa John Lwanji, Mheshimiwa Damas Nakei, Mheshimiwa Anne Makinda, Mheshimiwa Anna Maulidah Komu, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Dr. Emmanuel Nchimbi, Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari na Mheshimiwa George Lubeleje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa sababu umeniambia muda wangu hautachukuliwa katika kutambua majina ya Wabunge ama sivyo dakika nyingi zingekuwa zimeondoka. Napenda nianzie na hoja ya Wabunge wengi lakini ningependa sana kabla ya kwenda kwenye hoja ya Wabunge hoja za Kamati yangu ya Viwanda na Biashara na baadaye hoja ya Kambi ya Upinzani ziniongoze wakati nikizijibu nitakuwa nawataja na Wabunge wengine ambao wameongelea hoja hizo hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ufinyu wa Bajeti ambayo Kamati yangu iliongelea kwa nguvu zote kwamba Bajeti ya Serikali iliyotengwa ni ndogo na Mheshimiwa Naibu Waziri aliitolea ufanuzi kwa ufasaha sana kuhusu ufinyu wa Bajeti. Kwanza inaonyesha jinsi mlivyotambua umuhimu wa Wizara hii. Lakini vile vile mnajua unyeti wa Wizara hii kuibua tija na ufanisi katika sekta zingine. Nataka kuwashakikisha kwamba zaidi ya Kamati yangu ikiongozwa na Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatib hoja hii vile vige iliungwa mkono au ilitoka vige vige Kambi ya Upinzani. Kwa hivyo, pande zote mbili zinaona kwamba kuna ufinyu wa Bajeti wanassema hivi kwa sababu wanaona kwamba pengine majukumu yetu hayatekelezwi ipasavyo kutokana na ufinyu huo wa Bajeti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa Wizara hii pamoja na taasisi zake. Kulingana na wingi wa majukumu na ufinyu wa Bajeti kwa sasa sekta zilizopewa kipaumbele ni elimu, afya, maji, kilimo na miundombinu. Ukiangalia sekta hizo nazo zina uhusiano wa karibu sana na sekta ya viwanda. Kwa sababu *issue* ya maji ni muhimu sana kwa hivyo sekta ya maji inavyopewa nguvu na kupeleka maji viwandani kwa namna moja au nyingine sekta ya viwanda vige vige inaimarishwa. Ukiangalia

miundombinu, malighafi za viwanda zinatoka vijijini na bidhaa za viwanda lazima zirudi kwa walaji bila miundombinu huwezi ukafanya hivyo. Kwa hivyo, ni matumaini yangu kwamba vipaumbele hivi vya Serikali navyo vimepangwa kwa namna ambayo itasaidia kusukuma na sekta ya viwanda lakini hata hivyo kwa miaka ijayo nina hakika baada ya kuimarisha hizi sekta ambazo zina uhusiano wa karibu na sekta kama ya viwanda na zingine basi na Wizara ya Viwanda kutokana na hoja mliyojenga itaingia katika kipaumbele cha Serikali. Nawashukuru sana kunisaidia kujenga hiyo hoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Viwanda na Biashara ya Bunge pamoja na Kambi ya Upinzani kwa pamoja waliona umuhimu mkubwa sana kwa taasisi ambazo ziko chini ya Wizara yangu. Huwezi ukakosa kuona umuhimu wa taasisi kama *SIDO*. *SIDO* ni mkombozi wa wanyonge. *SIDO* ndiyo inahudumia viwanda vidogo na wajasirimamali wadogo. Huwezi ukakosa kuona umuhimu wa taasisi kama *NDC*, taasisi ambayo imepewa kuanzisha viwanda msingi au viwanda mama. *NDC* inakwenda kuanzisha viwanda pale ambapo sekta binafsi haioni faida na kwa hivyo, yenewe inaingia pale kwa niaba ya Serikali. (*Makofi*)

Kwa hivyo, umuhimu unaonekana, vile vile huwezi kukosa kuona umuhimu wa Taasisi za Utafiti kama *TIRDO*, *CAMARTEC*, *TEMDO* na zingine zote zilizo chini ya Wizara yangu. Kama kungekuwa na uwezo na kama kungekuwa na fedha za kutosha basi Serikali isingesita kutoa fedha kwa kujua umuhimu wa taasisi hizi. Lakini pamoja na taasisi hizi za *NDC* na *SIDO* ambazo moja kwa moja inawezesha wananchi kuondokana na umaskini lakini kuna taasisi zile za udhibiti kama *TBS*, *Fair Competition*, mizani na zenyewe ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mmeona wakulima wanavyoibiwa kupitia mizani. Mmeona wakulima wanavyoibiwa kupitia viwango kwa mfano katika biashara ya ngozi, ngozi ya mkulima ikafanywa ya *grade four* wakati ni *grade one* maana yake umemuibia fedha nydingi sana. Kwa hivyo, taasisi hizi za udhibiti nazo ni muhimu sana na naishukuru Serikali imeipa umuhimu kama huo ufinyu wa Bajeti basi na zenyewe zingepewa Bajeti za kutosha lakini katika siku hizi za ushirikiano wa karibu kati ya Serikali na sekta binafsi na hata *NGO's* basi utajaribu kuona ni namna gani ya kutafuta vyanzo vingine vya fedha ili kuweza kuimarisha taasisi hizi ambazo ni muhimu bila ya kusahau kwamba Serikali ndio majukumu yake makuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mfumo wa stakabadhi ya mazao ghalani nimelielezea kwa urefu sana kuhusiana na umuhimu wake na kwamba inahitaji fedha za kutosha, inahitaji ushirikiano na Halmashauri mbalimbali, inahitaji vyama vya msingi vya ushirika vilivyo imara, inahitaji vyombo vya fedha au taasisi za fedha na mimi Wizara yangu itakuwa karibu sana na wadau wote wanaohusika katika kuimarisha mfumo huu ambao utausaidia sana pengine utawakomboa wakulima kutokana na makucha ya *middle man* ambao wanatoza bei ndogo sana kwa mazao ya kilimo. Suala lingine ambalo lililoongelewa na Kamati ni kwamba Baraza litoe elimu kwa umma kuhusu mfumo wa stakabadhi za maghala. Ushauri huu tunaupokea kwa moyo mkunjufu na ninaahidi totalifanya hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *NDC* nimeliongelea pamoja na taasisi zingine chini ya Wizara yangu sasa naomba niende katika Mashirika yaliyobinafsishwa. Viwanda na Mashirika mengine yalibinafsishwa kutokana na mabadiliko ya sera za Serikali, kwamba Serikali inajiondoa kwenye biashara na kwenye uzalishaji na ijikite zaidi kwenye utawala na kujenga mazingira mazuri kwa sekta binafsi kufanya kazi yake vizuri. Sasa hilo lilikuwa moja lakini la pili ni kwamba Bajeti ya Serikali ni vyema ikaenda zaidi kwenye huduma za jamii badala ya kwenda kwenye uzalishaji na biashara ambapo pengine Serikali si kazi yake ya msingi. Kwa hivyo kuanzia mwaka 1992 Serikali ilibinafsisha makampuni mengi na mengi yalikuwa kwenye sekta ya viwanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kubinafsisha kampuni hizi kulikuwa na makubaliano ambayo yalikuwa yanaitwa *Sale Agreement*. Katika *Sale Agreement* zile kulikuwa na makubaliano kwamba kwanza kulikuwa na ubinafsishaji wa aina nyingi. Unaweza ukawa ni *Asset Sale* au kuuza mali ya kiwanda ama unauzu biashara ya kiwanda. Sasa vyote vyote itakavyokuwa lakini kulikuwa na makubaliano yaliyokuwa yamefikiwa baina ya mnunuzi na Serikali iliyokuwa inabinafsisha.

Sasa ni jukumu la Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa makampuni ambayo yako chini yake kufuatilia kwamba makubaliano yale kama wale walionunua wanayaafuata. Nataka niwaambie kwamba wakati wa ubinafsishaji viwanda vingi mimi mwenyewe nilikuwa nafanya kazi viwandani vilikuwa na hali mbaya sana na vingi vilikuwa haviuziki kama *going concern* au kama biashara. Lakini Serikali ilijitahidi sana katika majadiliano ili viwanda vile viuzwe kama *going concern* kwa sababu huduma zilizokuwa zinatokana na makampuni yale ilikuwa bado ni muhimu kwa Serikali. Kwa hivyo, mengi ya makampuni yale hayakuuzwa kwa bei ambayo sisi wote tungependa, yaliuzwa kwa bei ambayo ilikuwa inaonyesha hali yake na kwamba Serikali ilikuwa inataka kuyafufua zaidi kuliko kupata fedha wakati ule. (*Makofi*)

Kwa hivyo, Waheshimiwa Wabunge moja ya Kiwanda hicho ni Kiwanda cha *SPM* wakati ule sasa hivi *MPM*. Kiwanda cha *MPM* au *SPM* wakati ule kiliuzwa kama mali, lakini Serikali ilikuwa na nia ya kwamba kazi au shughuli zilizokuwa zinafanywa na *SPM* ziendelee kwa umuhimu wa *SPM*. Kwanza kwa sababu ilikuwa inatumia malighafi kutoka eneo lile la Nyanda za Juu, lakini pili kulinda ajira ya Watanzania. Tatu kupata bidhaa zilizokuwa zinatokana na *SPM*. Kwa hiyo, kwa Serikali wakati ule kupata fedha kama *value* ilivyokuwa inaonyesha, thamani ilivyokuwa inaonyesha dola milioni 26 haikuwa ni kipaumbele chake, kipaumbele ilikuwa kuendeleza kazi iliyokuwa inafanywa na *SPM* na ndiyo maana ikauzwa kwa *concept* ya *one dollar* kwamba chukua kwa kiasi chochote lakini nataka uzalishaji wa karatasi kwa matumizi ya Tanzania uendeleee na kwa ajili ya kuuza nje uendeleee. Nina hakika Mheshimiwa kaka yangu atakubaliana na mimi na Kambi ya Upinzani itakubaliana na mimi kwamba majukumu yale yamefanywa kwa kweli kwa ufanisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Benito Malangalila ambaye Kiwanda kiko jimboni kwake anawakilisha maoni ya wapigakura wake kwamba kwa madhumuni ya kuzalisha karatasi *MPM* imetekeleza wajibu wake. Sasa ambacho mnakiuliza kwa nini kimeuzwa kwa dola milioni moja badala ya kuuzwa kwa dola

milioni 26. Ingeuzwa kwa dola milioni 26 *RAI Group* wakati ule ingekuwa na hiyari ya kukongoloa mashine zile na kupeleka Kenya na sisi manufaa yetu yangekuwa ni dola milioni 26. Lakini kwa sababu tumeiruhusu inunuliwe kwa dola milioni moja wawekezaji mpaka sasa wameweza kuwekeza dola milioni 40, wamekwishafufua sehemu moja ya kiwanda bado wanaendelea kufufua sehemu ya pili. Pamoja na fedha shilingi milioni 40 zilizowekezwa Watanzania wanaendelea kupata ajira ingawa si kwa wingi ule ambao walikuwepo kwa sababu wakati *SPM* ilikuwa haijauzwa kulikuwa na wafanyakazi 1,200. Lakini hata hivyo mkumbuke kabla ya kuuza *SPM* Serikali ilikuwa inatumia fedha za walipa kodi ambao ingetumiwa kununua dawa, ambayo ingetumiwa kuboresha elimu ya watoto wetu, kulpia *SPM* ili iweze kuzungushwa kwa sababu mashine zingeharibika na vile vile kulikuwa na kemikali ambayo ilikuwa hatari kwa mazingira na vile vile kwa maisha ya watu ndiyo maana *concept* ya *one dollar* ikabidi Serikali ichukue kuliko kubaki kuendelea kukaa na *SPM* na kuendelea kutoa fedha ambazo zingewenza kufanya shughuli zingine ambazo ni muhimu sana. (*Makofi*)

Kuhusu *SPM* kulikuwa na jambo ambalo nilitakiwa nilieleze kwamba Angel Hurst ni nani? Naomba niwambie kwamba Angel Hurst ni mwekezaji mwingine baada ya *RAI Group* kununua *SPM* na kuisajili kama *MPM* iliwekeza fedha na kutokana na uwekezaji huo *RAI* wale kaka watatu wakaamua kwamba wa *note share* 99, ngapi zile kwa Angel Hurst ndiyo ukweli ninaojua mimi kama kuna ukweli mwingine basi tutapeana huo ukweli na tutajadiliana mpaka tufikie pale ambapo tunaelewana. Mimi niko tayari kupata taarifa zaidi na niko tayari kutoa maelezo zaidi. (*Makofi*)

Kwa hiyo, Angel Hurst ni mwekezaji ambaye ameungana na *RAI Group* katika kuwekeza ndani ya *SPM* na taarifa hizo ziko *BRELA*. *RAI Group* haikusajiliwa kama *RAI Group* kilichosajiliwa ni *MPM* kwa sababu *RAI Group* isingeweza kufanya biashara bila kusajili *MPM*. Kwa hivyo, *MPM* inajulikana *BRELA* na *BRELA* inajua katika uwekezaji wa *MPM* wako wale *RAI Group* kwa zile *shares* ambazo kidogo walizonazo pamoja na Angel Hurst. Kwa hiyo, naiomba Kambi ya Upinzani maelezo niliyonayo nimewapeni kama kuna maelezo zaidi tuendelee kujadiliana mpaka tufikie mahali na Watanzania wanaelewa kitu kinachoendelea *SPM*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanda kingine ambacho napenda niongelee mahususi ni kiwanda cha *General Tyre*. Kiwanda hiki hakijabinafsishwa mpaka leo. Utendaji wa kiwanda hiki ulikuwa mzuri pale awali miaka ya nyuma lakini baadae kidogo kidogo utendaji wa *General Tyre* ukadorora. Wakati kiwanda kinazalisha kwa ufanisi kiwango cha juu cha matumizi ya uwezo uliowekezwa kilikuwa ni asilimia 76 mwaka 1977. Kufikia mwaka 2005 kabla ya kupata mkopo uwezo ulikuwa asilimia 11 na kuanzia Septemba, 2007 uzalishaji ulisamama kabida hadi sasa.

Aidha, tatizo lingine lililokikumba kiwanda hiki ni madeni makubwa ya mabenki ya nje yaliyotishia kufilisi kiwanda hicho. Ili kukiinurusu kiwanda hiki taasisi ya *NSSF* ilitoa mkopo wa dola za Marekani milioni 10. Baada ya kupokea fedha hizo kiwanda kililipa madeni ya mabenki ambayo yalikuwa yanatishia kufilisi kiasi cha dola milioni 4.8. Kiasi kilichobaki cha mkopo kilitakiwa kitumike kununua malighafi ili kufufua kiwanda. Hata hivyo uzalishaji wa mataili umekuwa unatumia alama ya biashara ya *General Tyre* inayomilikiwa na mbia mwenza wa kampuni ya *Continental*. Alama ya

biashara ya huduma za kiufundi vile vile zaidi ya alama hiyo *Continental* ilipewa kazi ya ku-manage *General Tyre*. Tulifanya hivyo kwa imani kwa kujua kwamba *General Tyre* ni mbia mwenza lakini vile vile amebobea katika kutengeneza matairi na vile vile katika uwezo wake wa uendeshaji pamoja na kwamba sera hiyo haijaleta matokeo mazuri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa uendeshaji na usimamiaji wa kiwanda upo kwenye ngazi mbili. Ngazi ya juu ni ya bodi na ngazi ya pili ni ya menejimenti. Sasa ili uone kwamba Serikali ilikuwa na mkono wake pale katika Bodi ya *General Tyre* Serikali iliwalishwa na wajumbe wanne pamoja na Mwenyekiti, wakati *Continental* iliwalishwa na mjumbe mmoja. Lakini wao ndio tumewapa menejimenti. Sasa Serikali inafanya majadiliano na mbia mwenza. Kwanza muda wa menejimenti umekwisha na Serikali inataka kurudisha menejimenti ndani ya nchi kumweka Mtanzania anayeweza kuendesha lakini kama tutakubaliana tuendelee na *trade mark* na vile vile mbia mwenza tujadiliane naye namna ya kufufua kiwanda chetu cha *General Tyre*. Ni imani yangu kwamba tutafikia makubaliano mazuri na nia ya Serikali kufufua *General Tyre* kwa sababu Kiwanda hiki ni moja ya viwanda muhimu pengine ni sawa sawa msingi. (*Makofî*)

Kwanza kwa sababu inatumia mpira unaolimwa Tanzania, pili matairi yake ni mazuri ndiyo yanayopendwa na wakulima wetu kwenye matrekta yao na hata malori yalikuwa yanatumia sana matairi ya *General Tyre*. Kwa hiyo, Serikali inataka kukifufua kiwanda hiki na tunafanya majadiliano *as follow back position* kama tutashindwa na mbia huyu tutatafuta namna nyngine ya kufufua *General Tyre* yetu na kwa hiyo, wafanyakazi wa Arusha wasiwe na wasiwasi na Mbunge wao hana sababu ya kuwa na wasiwasi kwa sababu Serikali ina nia njema. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu amelisimamia sana hili kwa kujua umuhimu wa Kiwanda hiki. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo Kamati iliongelea na kwa hili nafikiri Wapinzani hawakuliongelea sana lakini Mheshimiwa Profesa Mwalyosi aliliongelea sana ni kuhusu Mradi wa Chuma wa Liganga na Makaa ya Mawe ya Mchuchuma. Wote tunajua mapinduzi ya viwanda yanatokana na chuma dunia nzima. Chuma na makaa ya mawe ni msingi wa viwanda. Kwa hiyo, Liganga na Mchuchuma kwa Watanzania inapewa umuhimu sana ili tuje tulete mapinduzi ya viwanda na baadaye mapinduzi ya kilimo yaende kwa haraka zaidi. Ni kweli kabisa imechukua muda mrefu kwamba tumefanya utafiti Liganga na Mchuchuma lakini unajua kwamba mali kubwa ya Taifa ipo pale na kwa hiyo, kuna kila sababu ya kuwa makini na kuchukua muda ili mali hiyo gafi itumike kwa maslahi ya Taifa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hapa tulipofikia tuna matumaini na nilieleza kwamba kuna wawekezaji wengi ambao wako tayari kuwekeza Liganga na Mchuchuma ili hatimaye tuweze kupata chuma ghafi na baadaye tupate chuma cha pua. Tumepata matumaini zaidi katika kuharakisha au kuongeza kasi ya kuweza kupata au kutumia hii malighafi. Mheshimiwa Rais ametuelekeza kwamba twende kwa haraka kwa kujaribu kuwa na mwekezaji ambaye yuko tayari kuchoronga, pamoja na utafiti uliofanywa tunataka kujua kwamba *iron* ipo kiasi gani, *vanadium* iko kiasi gani, *titanium* ipo kiasi

gani kwa sababu wawekezaji wengi ni wajanja tunataka tujue mali yetu ipo kiasi gani ili baadae tusije tukaibiwa. Hiyo kazi imefikia mbali na matumaini yangu kwamba tutaenda kwa kasi zaidi na suala la kulipa fidia ni muhimu sana tena fidia ambayo Mtanzania baadae hatakuja kuilaumu Serikali yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu viwanda vidogo na biashara ndogo ndogo. Ukitaka viwanda vikubwa viendelee lazima uwe na watu wanaita watu wenye utajiri wa kati ili mahitaji yao ndio iwe soko la viwanda vikubwa. Watu hawa wanatokana na viwanda vidogo vidogo na wajasiriamali wadogo. Kwa hiyo, suala la kusimamia viwanda vidogo ni la kufa na kupona. Ilianza tangu enzi ya Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere namshukuru Mheshimiwa Basil Mramba ambaye ndiye alikuwa *Director General* wa kwanza wa *SIDO*. Dhana ile ya *SIDO* ipo pale pale. Zaidi ya ile dhana iliyokuwepo wakati ilipoanzishwa sasa tutaiboresha kwa kuwa na sheria nzuri ili *SIDO* iweze kuwajibika ipasavyo na kama uchumi wa siku hizi unavyohitaji. Suala lingine ambalo kwa ujumla nilipenda niliongelee ni la Kamati iliongelea ni suala la wamachinga. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, wamachinga ni watoto wetu na vijana wetu na wao ndiyo wanaofanya uchumi wetu uchangamke kwa wingi wao na wamachinga tukiwaachia hivi tutakuwa tunajijengea Taifa ambalo halina mwelekeo. Lakini tusiwaachie wawe watumwa ndani ya nchi yao. Nyie wote mnajua wamachinga Dar es Salaam na mimi nawajua wengi ni marafiki zangu. Unakuta nguo waliyoivaa jumatatu ni ile ndiyo ameivaa jumapili. Kandambili walizovaa jumapili ndiyo hizo walizovaa jumatatu. Maana yake wanafanya kazi kubwa bila ya mafao stahili. Kwa hiyo, lazima tuwa-*organise* wamachinga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hicho ndicho ambacho Serikali ya awamu ya nne ya CCM inavyofanya. Tunajaribu kuainisha maeneo ambayo vijana wetu watafanya biashara ambayo itawaletea heshima. Sio kwenda kuchukua mali ya matajiri na kuuza halafu wanepewa senti tano. Tunataka wafanye kazi ambazo zinajulikana kama wanapewa mali na wale wenye mali kubwa basi ijulikane kwamba ujira wao nao ni mkubwa na hili tutalisimamia pamoja na Wizara ya kazi pamoja na maendeleo ya vijana. (*Makofi*)

Kwanza kwa kuhakikisha lile jumba lao linalojengwa linakamilika na pili, maeneo mengine Wilayani yanakuwepo kwa wamachinga kufanya biashara. Pamoja na wamachinga pia akinamama wenzangu wa mama lishe na wao tumefanya kazi kubwa sana kuboresha maeneo yao ya kufanya kazi. Lakini bado kuna kazi kubwa ya kufanya na kwa hiyo, tutashirikiana na Kambi ya Upinzani watupe ushauri na sisi tutaupokea ili kuberresha nguvu kazi hii muhimu ndani ya Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine lililoulizwa na Kamati yangu pamoja na Kambi ya Upinzani ni suala la fedha zilizotolewa na Rais Mheshimiwa Jakaya Kikwete. Nataka niwaombe Waheshimiwa Wabunge wa Upinzani fedha zile kama mlivyosema kwetu sisi wanasema tena neno ulilosema kwamba ni zawadi ya uchaguzi si kweli na huko ni kupotosha ukweli. Fedha zile zinatolewa kuwawezesha Watanzania ambao hawana uwezo wa kukopa Benki waweze kuwa na mtaji angalau mdogo wa kuweza

kuibua miradi yao. Kama mlivyopendekeza nakubaliana na ninyi na tutatoa ushauri kwenye Baraza kwamba na *SIDO* nao wapewe mgao wao ili na yenyewe nayo ichangie katika kuibua miradi ya hawa ambao bila kuwasaidia hawawezi kupata mitaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *TANTRADE* ni kweli huwezi kuwa na biashara ya nje iliyo imara bila ya kuwa na biashara ya ndani iliyokuwa imara. Biashara ya Nje ni *extension* ya biashara ya ndani. Kama ilivyo muhimu kwa sisi kufanya biashara na Ulaya na Marekani kwanza tuimarishe biashara ya Afrika. Ni muhimu kuimarisha biashara ya ndani na namna pekee ya kuimarisha biashara ya ndani ni kuwa na sheria mpya sasa tuwe na *TANTRADE*, *Tanzania Trade Authority* ambayo itasaidia kujenga biashara ya ndani ambayo itatoa msukumo kwa biashara kwa biashara ya nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo Msemaji Mkuu wa Upinzani aliliongelea ni kuhusu viwanda vya Kilimanjaro. Viwanda vya Kilimanjaro kama vilivyokuwa viwanda vingine vya umma vilibinafsishwa, kipo *Tanzania Co-operation Bag*, kipo *Tanzania Tanneries*, kipo *Machine Tools* na vingine. Vyote vimebinafsishwa lakini havifanyi vizuri. Nataka kuwashakikishieni kwamba nitavifutilia niweze kujua kwa nini haviafufuka na suala la Mheshimiwa Philemon Ndesamburo kusema kwamba apewe yeye, nilikwenda kupekuwa na sikukuta maombi yake. Sasa ikitokea kwamba kutakuwa na sababu za msingi za kwa nini hazijafufuka tuna uwezo wa kuzirudisha basi wakati huo Mheshimiwa Philemon Ndesamburo alete maombi yake na tutamu-*assess* na wengine wote watakaoomba lakini nawahakikishia kwamba tutayafutilia kama tutakavyofutilia viwanda vya Mbeya, Tanga na viwanda vingine ambavyo viko Mwanza na sehemu nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Lucy Owenya alitushauri kwamba viwanda vilenge katika uzalishaji wa ushindani. Ni kweli na akaleta suala la *Heineken*. *Heineken* inaitwa *Mabibo Beer* na akatoka mfanyakishara mmoja ambaye anataka kuuza *Heineken*, kwa mawazo yake yeye yule anayekuja wa pili alizuiwa na yule wa kwanza. Sasa akaenda *fair competition* akashauriwa kwamba alete malalamiko yake na aende Mahakamani. Sasa hivi yupo *Fair Competition Tribunal* na kwa sababu yupo huko na kwa misingi yetu, taratibu na kanuni zetu tuwaachie *Fair Competition Tribunal* iweze kuangalia kesi hiyo na mimi nitaifuutilia kwa karibu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Lucy Owenya aliuliza ni viwanda gani vimechangia katika ajira na katika uchumi wa Taifa. Tathmini tuliyofanya ya ufanisi katika maendeleo ya sekta ya viwanda mwaka 2007/2008 ilibaini kuwa sekta ndogo ya viwanda ya chakula inayojumuisha viwanda vya kusindika mazao ya kilimo na uvuvi zilichangia ajira 44,204 sawa na asilimia 48 ikifuatia sekta ndogo ya ufumaji na ushonaji kwa asilimia 11.3 na sekta ndogo ya viwanda vya tumbaku kama alivyosema Mheshimiwa Vita Kawawa ilichangia asilimia 7.7. Vile vile sekta hii ya viwanda imechangia kulipa kodi, imekuwa na mchango zaidi wa kuweza kuzalisha bidhaa na kwa hiyo, Mheshimiwa Owenya kama atakuja nitampa *list* hii na nitamwonyesha ni kiasi gani viwanda hivyo vitachangia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *SPM* nimelieleza kwa kirefu na ni mategemeo yangu kwamba Wabunge wenzangu kama watakuwa wanahitaji maelezo zaidi naomba sana wanijie na kwa pamoja tutashirikiana kupata taarifa zaidi na kukiweka kiwanda chetu kwenye hali ambayo Watanzania tunataka. (*Makofi*)

Sasa kulikuwa kuna suala la *NGO* inaitwa *INCOMENT* ilipewa hekta 2000 lakini ikapewa hatimiliki ya hekta 28,000 akauliza ni ya nani? Ilikwishalipa shilingi milioni 15. *INCOMENT* ilisajiliwa chini ya Sheria Makampuni na kupatiwa cheti cha usajili kilichotolewa mwaka tarehe 25 Mei, 2001, ilipatiwa cheti cha ukubalifu (*Certificate of Compliance*) tarehe 5 Aprili, 2007 chini ya Sheria za *NGO* namba 24 ya mwaka 2002. Inafanya kazi ya kuhudumia wakulima, wafanyabiashara wadogo, uimarishaji wa miundombinu ya ufundi na viongozi wake ni kama ifuatavyo, Tasili Mgoda ni Mwenyekiti, Benito Malangalila, Katibu, Joseph Mungai, Mjumbe, Peter Mawele, Mjumbe, Petro Mng'ong'o Mjumbe na Khalfani Hilda, Mjumbe. Sasa kama kuna taarifa nyingine Waheshimiwa Wabunge tutaelezana. Lakini naomba kwa madhumuni ya leo maelezo yangu haya yatosheke. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na suala la polisi kwenda *MPM* wakati fujo zilipotokea *MPM* kwa sababu wafanyakazi walikuwa wanadai maslahi yao na ilikuwa ni wajibu wa Serikali kuona kwamba hali inakuwa shwari sio tu kwa ajili ya kiwanda peke yake na wenye kiwanda, ilikuwa ni kwa ajili ya wote ambao wanazunguka kwenye kiwanda kile pamoja na wafanyakazi na mali yote ya kiwanda ambayo vile vile ipo kwa maslahi ya Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Lucy Owenya alitaka kujua kama maeneo ya *EPZ* hayana miundombinu ya kuridhisha Serikali inafanya nini. Nataka kumhakikisha Mheshimiwa Lucy Owenya na Kambi ya Upinzani kwamba Serikali inathamini sana na ndiyo maana Serikali imenzisha *EPZ* lakini sasa hivi ili kupata manufaa zaidi tunataka kuunganisha *EPZ* na *SEZ* ili tuanzishe *EDZ*. Sasa hatuachi mazuri ya *EPZ* wala hatuachi mazuri ya *SEZ*, tunachotaka tuweke taasisi hizi pamoja ili tuanze kupata mafao makubwa zaidi. Chini ya *EDZ* kutakuwa na makazi, kutakuwa na *communication* na *information areas*, kutakuwa na bandari na kutakuwa na miundombinu inayotakiwa katika uwekezaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *EPZ* inajielekeza zaidi katika miundombinu lakini kuhakikisha kwamba kuna kuwa na *export* lakini *EDZ* itakuwa *for export* vile vile na kwa ajili ya mahitaji ya ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kiwanda *Machine Tools* cha Moshi. Kiwanda hiki kilianzishwa kwa kushirikiana na Serikali ya Bulgaria na mpaka sasa deni la Bulgaria limelipwa. Sasa hivi tuna wawekezaji ambao wameonyesha *interest* kupenda kuwekeza kwenye *Machine Tools* Moshi na majadiliano yanaendelea. Maslahi ya Taifa na ya Kilimanjaro yatazingatiwa. Hadi sasa hakuna aliyepewa *Machine Tools*. Lakini kuna mmoja ambaye amesaini *MOU* na *NDC*. Lakini *MOU* ni katika ku-facilitate makubaliano baadaye yawezekane. Kwa hiyo, *Machine Tools* ya Moshi haijapewa mtu lakini kuna wawekezaji wawili ambao wamejitokeza, huyu wa kwanza isipowezekana

tuna *follow back position* kwa hiyo uwezekano ni mkubwa sana wa kuweza kuboresha *Machine Tools Moshi*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, najua Wabunge wengi pengine hatukuweza kujielekeza kwenye hoja zao, lakini niwaahidi kwamba tutawaletea majibu kwa maandishi. Ninawahakikishia watu wa *Lake Zone* kwamba suala la kutawanya viwanda vy a simenti ni muhimu sana na kwa hiyo, tutaangalia uwezekano wa kuanzisha kiwanda cha simenti kwenye *Lake Zone* ili isiwe mbali sana na hawa watu. Vile vile kuna soko kubwa sana nje ya Tanzania katika nchi ambazo zinapakana na Tanzania kwa Magharibi. Lakini kuna malighafi katika Mkoa wa Singida na hususan Manyoni, viwanda vy a simenti vinatakiwa vingi sana na kwa hiyo hata umuhimu wa kuanzisha kiwanda cha simenti katika Kanda ya Kati ni muhimu kwa hivyo hakuna sababu ya kuwa na wasiwasi kwamba tukianzisha Mwanza hatuwezi kuanzisha Manyoni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumalizia kwa kusisitiza kwamba nitawapa majibu kwa maandishi kwa wale wote ambao sijawataja lakini nimetambua michango yao. Napenda kusisitiza kuwa sekta ya viwanda ndiyo inayowezesha matumizi ya sayansi na teknolojia katika nchi yoyote ile. Matumizi ya sayansi na teknolojia ndiyo msingi wa kuongeza tija na ufanisi katika shughuli za kiuchumi. Tofauti kati ya nchi zilizoendela na zinazoendelea ambazo nyingi ni maskini inatokana na tofauti ya kiwango cha tija na ufanisi na ndiyo chimbuko la urari hasi wa maendeleo kati ya nchi hizo. Siri ya kuondokana na urari huo basi ipo katika kuendeleza matumizi ya sayansi ya teknolojia ili kuongeza tija na ufanisi katika shughuli za kiuchumi. Hili ndilo jukumu kuu la sekta ya viwanda, biashara na masoko na ndiyo maana ya kuwa sekta kiongozi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, azma ya shughuli yoyote ya kiuchumi ni kufidia gharama na hatimaye kutengeneza faidi na faida inapatikana kwa kufanya mauzo. Kwa hiyo, biashara ndiyo inayosukuma maendeleo katika nchi yoyote. Afrika bado haijawa sehemu muhimu ya biashara ya Kimataifa hivyo hainufaiki ipasavyo. Aidha, biashara kati ya nchi za Kiafrika ni chini ya asilimia kumi na mgao wa Tanzania ni mdogo zaidi. Ili kuongeza biashara kati ya nchi za Kiafrika ni vyema kuimarisha ushirikiano wa kibashara baina ya nchi hizi na pia tujiunganishe ipasavyo na biashara ya Kimataifa kama tunataka twende haraka kimaendeleo. Hivyo ni dhahiri kuwa bila biashara maendeleo ya kiuchumi yatakuwa duni. Kutakuwa na ajira chache na itakuwa ni vigumu kuleta maisha bora. Biashara inachochea ajira na kujenga utu hata hivyo inakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wengine itajielekeza kukabiliana nazo katika mwaka 2008/2009. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto hizo ni pamoja upatikanaji wa mitaji ili kujenga uwezo na kuondo pingamizi ya biashara, kutumia kikamilifu fursa za masoko ya ndani Kikanda na Kimataifa, kuendeleza mapinduzi ya kilimo kwa kuhamasisha matumizi ya sayansi na teknolojia katika uzalishaji, usindikaji na uongezaji wa thamani. Wakati tunadai nchi zinazoendelea ziongeze kuongeza mtaji ili Afrika inufaikie na biashara ya Kimataifa nchi yetu ijjtahidi kufanya yale yaliyo katika uwezo wetu ili kujikwamua kiuchumi kwa mfano matumizi ya gesi asilia, matumizi ya *phosphate* katika kutengeneza mbolea ni muhimu sana, kuimarisha taasisi za fedha, kutokuruhusu hata

kidogo rushwa, viwanda kama vya *Soda-ash* ambavyo wanamazingira wanaona kwamba ni lazima tufanye *environmental impact assessment*. Lakini mimi sidhani kama kuna jambo ambalo binadamu analifanya bila kugusa mazingira, la muhimu ni kuangalia kwamba kazi yetu imefanywa vizuri na ikibidi hata kiwanda cha *Soda-ash* tukipeleke Mto wa Mbu hata kama ni mbali tunahitaji *Soda-ash* ni moja ya viwanda msingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, uhaba wa miundombinu ikiwa ni pamoja na barabara, reli, viwanja vya ndege pamoja na huduma za mawasiliano ni muhimu sana. Kutokuwa na kiwango cha elimu ya kutosha cha elimu, ujuzi na ubunifu ni *limitation* kubwa sana. Haya yote yanawezekana kama tukianza kujipanga kwa dhati kushughulikia masuala ya changamoto zilizo chini ya uwezo wetu. Safari ndefu inaanza kwa hatua ya kwanza. Marehemu Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere alishatuanzishia hatua ya kwanza, sisi lazima tuendelee kufanya yale yaliyo kwenye uwezo wetu, kutumia fursa zilizopo na katika yote tuwe pamoja badala ya kuhitilafiana twende kwa pamoja, tuwe na nguvu moja kujenga nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kwa dakika chache ninataka kuwashakikisha wakulima wote wa Tanzania kwamba kupitia wakala wa mizani tutahakikisha wafanyabiashara hawaendelei kuwaibia na mamlaka yenyewe ya mizani haitawaiba. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)
KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 44 – Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko

Kifungu 1001 – *Administration and General... Sh. 4,688,285,300*

MHE. ESTHER K. NYAWAZWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, *Vote 44, Subvote 1001, ...*

NAIBU SPIKA: Naomba, kwa sababu tunataka mshahara wa Waziri, msipoteze muda kwa hizo *votes*. *Vote*, tutaingia Kitabu cha Nne.

MHE. ESTHER K. NYAWAZWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Mimi nimeridhika kabisa na maelezo ya Mheshimiwa Waziri, lakini naomba tu anisaidie kunipa mikakati ambayo itatusaidia Wananchi wa Wilaya ya Ukerewe, angalau kwenye kipaumbele amesema kwamba kuvutia wawekezaji; atatusaidiaje kuhakikisha wawekezaji wanaelekea kwenye maeneo hayo? Ahsante sana.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Nyawazwa, kwa kunitaka nisimame ili na Wananchi wa Ukerewe wasikie kwamba Mheshimiwa ameuliza kwa niaba yao kwamba, namna gani tutawavutia wawekezaji waende Ukerewe.

Jambo la kwanza ni kuimarisha miundombinu. Nashukuru sana umeme umefika Ukerewe. Ukerewe kuna maliasili nyingi; samaki wengi sana, matunda mengi sana na wanalima sana watu wa Ukerewe. Kwa hiyo, sisi katika sera zetu na hasa katika Mkakati wa kuweza kuongeza viwanda, tunesema kwamba, viwanda vikubwa vitakuwa kwenye maeneo ya bandari. Kule kwenye Wilaya na Vijijini, ndipo ambapo tutakuwa tunaweka viwanda vya kusindika mazao ya kilimo na maliasili nyingine. Kwa hiyo, tutajitahidi sana kupitia *Centres* zetu kama za Dubai na ile ya London, kuweza kuona kama tutawapata wawekezaji ama wa nje na wa humu ndani kuweza kuwekeza basi kwenye kusindika mazao ya kilimo na hasa kuweka kiwanda cha samaki, kwa sababu Wakerewe wangepata ajira na wangeweza kuongeza muda mrefu wa samaki kukaa kwani bila kusindikwa huwa wanaharibika upesi sana. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Labda ilikuwa ni katika ile aliyotangulia kusema Mheshimiwa Waziri wangu kwamba, wananchi wasikie. Wamekuwa wakisikiliza toka jana na mchana huu nilivyokuwa naingia ndani, bahati nzuri tumeingia naye, nikajua nitajibiwa na sitakuwa na haja ya kuzungumza lolote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilio cha Wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro ni kikubwa kuhusu hivyo viwanda. Nilitaraji Serikali ingetupa majibu ya matumaini, lakini jibu nililopata hapa ni la ujumla kwamba, Serikali inaendelea kuangalia. Jibu hili limekuwa likitolewa huku ndani takriban miaka kumi kabla hata ya mimi kuingia Bungeni. Sasa mimi nauliza; hivi Serikali inaangalia kwa muda gani?

Kwa wale wasiojua, Mji wa Moshi unalala mchana watu wanafanya kazi, usiku wanakwenda, tunaita Mgombani kulala. Sasa eneo hili la viwanda (*Industrial Area*), limekuwa ndio giza kabisa, hakuna umeme na uhalifu mwingu unafanyika. Bahati nzuri kuna wengine wameanza sasa shughuli, wamefungua *recreation area*. Kuna *Pub* imefunguliwa kwenye *Industrial Area* na hii imebidi iwe hivyo kwa sababu viwanda hakuna. Kilimanjaro *Timber Utilization* giza, Tanzania Tanneries giza, na Kiwanda cha Ngozi giza. Sasa mimi nauliza na niliomba kabla ya kuuliza, endapo viwanda hivyo havitaendelezwu tena, iruhusiwe sasa majengo hayo yatolewe kwa shughuli nyingine kama taasisi za elimu na nikatoa mfano; Mheshimiwa Mwenyekiti, naona unaanza kukosa uvumilivu labda dakika tano zimeisha, lakini mimi ningeomba tu...

MWENYEKITI: Sema wewe muda ukiisha utapigiwa kengele! (*Kicheko*)

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Yale mengine yote niliyochangia ikiwepo samani nimeyaacha *pending*. Naomba hili la viwanda tujue sasa ni kwa muda gani Serikali itatoa majibu ili wananchi wale wasikae kulilia viongozi wote wanaotembelea Mkoa ule kuhusu viwanda kufunguliwa. Ahsante. (*Makofi*)

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana mdogo wangu, Mheshimiwa Shally na yeze ananipa nafasi pengine ya kujibu kwa usafaha. Kwanza kabisa, viwanda vilivyobinafsishwa Kilimanjaro, kama alivyosema ni pamoja na Kiwanda cha Tanzania Tanneries. Kiwanda ambacho nakifahamu sana mimi, kiwanda cha magunia kilikuwa kinaitwa *Beck Corporation* na nilijaribu hata kuyasema pale wakati najibu na Kiwanda cha *Pesticide Manufactures*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Kiwanda cha Tanzania Tanneries; viwanda vya ngozi pale awali vilikuwa na matatizo vyote, lakini hapa tulipo, Kiwanda cha Morogoro Tanneries kimefuliwa. Aliyenunua Kiwanda cha Morogoro Tanneries na Kiwanda cha Mwanza Tanneries ni mmoja na mimi mwenyewe nimekwenda Morogoro, akaniahidi kwamba, baada ya Morogoro Tanneries, anakwenda Moshi.

Kiwanda cha Tanzania Tanneries kilinunuliwa na Aga Khan *Group* na siku moja Meneja wao au *Owner* alikuja ofisini kwangu akalalamika kwamba, ushuru tunaotoza wa asilimia 40 kwenye ngozi ghafi, hazizuii ngozi kuuzwa nje zikiwa ghafi kwa sababu ya *under declaration*. Nimechukua hatua na kuandika kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ambaye aliahidi kwamba, ataangalia kutoza *absolute amount* badala ya ile *percentage*. Vile vile nikamwambia hana sababu ya yeze kutokufufua kiwanda kwa sababu yule wa Morogoro Tanneries ana *the same environment* lakini amekifufua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nasema kama nilivyosema awali kwamba, nitafuatalia na nitatoa muda kamili na kama kiwanda hakifufuki, tutatumia ile *Sell Agreement* kuchukua hatua ambazo zipo kwenye *Sell Agreement* ya kuchukua ili ikibidi basi, irudi Serikalini na tumtafute mtu mwengine ambaye atawekeza, kwa sababu viwanda vya ngozi ni viwanda ambavyo kwa kweli vinaweza vikasukuma uchumi wa nchi hii na kwa sababu zamani tulikuwa tukizalisha ngozi, hatuna sababu yoyote. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Shally na watu wa Kilimanjaro, waelewe hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kiwanda cha *Beck Corporation* kilikuwa kinaitwa kama sikosei cha magunia. Aliyenunua Kiwanda cha Magunia cha Morogoro, ndiye huyo huyo aliyenunua Kiwanda cha Magunia Moshi. Pengine tatizo ni mtu mmoja kununua makampuni mawili. Kama ndio hivyo, basi tutaangalia lakini kama kuna tatizo lingine ambalo linahitaji msukumo wa Serikali, tutafanya hivyo na ikibidi basi, baada ya muda ambao tutapeana, tutachukua hatua madhubuti ya kuweza kumpa mtu mwengine ambaye anaweza akafufua kiwanda. Nataka niwaeleze kwamba, viwanda vya magunia yanayotumia katani, Vinakutana na ushindani mkali sana na magunia ya *jute* na sasa hivi kuna mwekezaji mmoja ambaye anajenga kiwanda cha *jute* hapa Tanzania. Sasa tutaangalia yale ambayo ni ya msingi na yale ambayo yanataka kurekebika yarekebishwe, kama hayarekebishwi, ninawaahidi Serikali itachukua hatua. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda kingine ni kile cha *Pestside*; kiwanda hiki cha kuzalisha dawa za kuulia wadudu waharibifu wa mazao kilifufuliwa baada ya kubinafsishwa ila uzalishaji ulifanyika kwa muda mfupi na kwa kwa kiwango kidogo

kutokana na kupanda sana bei ya shaba katika soko la dunia, kiwanda hicho kikadorora. Sasa hili ni tatizo ambalo tunalifuatilia, kama kweli ni tatizo la msingi na viwanda vingi vitakutwa na hali hilo, kama tatizo ni la msingi, sote tutajielekeza kwenye hilo tatizo na tutalitafutia jawabu. Hata hivyo, kuna viwanda vipyta vimefunguliwa Kilimanjaro. Nawapongeza wale ambao wamefungua viwanda vipyta Kilimanjaro na katika uchumi wa soko, viwanda vingine vitakufa na vingine vitajengwa, ndiyo ilivyo uchumi wa soko. Nataka vikifa Kilimanjaro, viwanda vingine vingi zaidi vijengwe na sisi tutajielekeza huko.

MWENYEKITI: Miaka kumi ya mwanzo ilikuwa ya wanaume, sasa hivi anatawala mwanamke, kwa hiyo, aamini tu mambo yatakwenda vizuri. Tunaendelea. (*Kicheko*)

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii. Kwanza, labda niseme tu ni kwa mujibu wa taratibu, lakini sina haja ya kushika mshahara wa mama yangu, Mheshimiwa Dr. Nagu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa kuzungumza, nilizungumzia na nili-quote kifungu cha 74, ukurasa wa 57 wa Hotuba ya Waziri ambao ulikuwa unaelezea maandalizi ya mkakati wa kuongeza uzalishaji na kukuza mauzo nje na mwelekeo wa mkakati huu ni kutatua changamoto za uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilizungumzia pia katika mkakati huu, sekta ndogo ya tumbaku haipo katika makati huu na nilielezea umuhimu wa sekta hii ndogo ya tumbaku. Sasa ninataka kumwomba Mheshimiwa Waziri atolee ufanuzi, wanaweza wakatuingiza katika mkakati huu kwa sababu sekta hii ndogo ya tumbaku kama tunavyofahamu, kiwanda tu cha sigara kodi yake ya mwaka jana tu ililipa shilingi bilioni 90, ina uwezo wa kuendesha Wizara mbili kwa mwaka mzima.

Kwa hiyo, ina umuhimu sana sekta hii na asilimia 90 ya tumbaku inayozalishwa inauzwa nje, asilimia kumi inayozalishwa ndani ni asilimia tatu tu ndio inatumika ndani lakini asilimia saba ya hiyo asilimia kumi inauzwa nje nayo. Kwa hiyo, ni muhimu sana kuweka katika mkakati huu ili tuzalishe zaidi tumbaku hii na tuweze *ku-export* na kukuza mauzo yetu ya nje na kuingiza fedha nyingi zaidi za kigeni. Naomba ufanuzi kama mtatuingiza. Ahsante sana!

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Vita Kawawa na nilimtaja ila nilikosea tu kwa sababu ya mambo yenyewe yanavyokwenda na muda. Mkakati ni kusindika mazao ya kilimo na nilivyokuwa nimeweka *list* pengine ndiyo nilichokosea nisingeweka, kwa sababu haikuwa *exhaustive*, sikuweka yote. Nilisema kawaha, pamba na kadhalika. Sasa naomba nimwambie kwamba, tumbaku ni zao la kilimo, nayo vile vile tutaiweka kwenye mkakati wa kusindika. Pamoja na hivyo, tunaangalia na yale ambayo yanatakiwa kuzingatiwa ili afya ya wananchi isiathirike. (*Makofi*)

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Mheshimiwa Dr. Mary Nagu ni rafiki yangu na ni mtani wangu, lakini napenda tu anifafanulie kwa maslahi ya Wananchi wa Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia mchango wangu wa maandishi, nimeelezea kuhusu adha wanayoipata Wakulima wa Mkoa wa Singida katika ukamuaji wa mafuta ya alizeti. Kazi ya Viongozi wa Mkoa wa Singida ni kuhamasisha wakulima na kazi hiyo imefanyika kikamilifu na wanasiasa. Wabunge wa Majimbo kwa kushirikiana na sisi wa Viti Maalum, kazi hiyo tumeifanya kikamilifu, tumewahamasisha wakulima wamelima alizeti kweli kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa wakulima wetu wanapata tabu ya ukamuaji. Mashine zilizopo Singida ni ndogo ndogo, ambazo hazina hata uwezo wa kukamua mafuta ambayo yanaweza yakaingia kwenye kiwango cha ushindani wa soko. Nimemwomba Mheshimiwa Waziri, atafute wataalam wake waje Singida, waangalie kazi kubwa iliyofanywa na Wakulima wa Singida; aone uwezekano wa kututafutia mwekezaji afunge kiwanda kitakachoweza kukamua mafuta ya alizeti yatakayoingia kwenye ushindani wa soko, kwa sababu tumeishaambiwa na Serikali kwamba kuna soko nje, mafuta yetu hayataweza kwa sababu hayana kiwango.

Ninaomba Mheshimiwa Waziri, atusaidie hili, wananchi wetu wanakesha, wanashinda kutwa nzima wanakamua mafuta. Hii ni karaha kubwa, hela wanazipata kwa tabu na ni ndogo sana. (*Makofi*)

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Diana ni mtani wangu na zaidi ya kuwa rafiki ni mdogo wangu. Mimi kwetu ni karibu sana na Singida na ninaijua Singida sana na watu wote wa Manyara au wa Hanang, lazima waijue Singida kwa sababu wanazozijua wao. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kusindika mbegu za mafuta ni muhimu sana katika kutawanya mapato, wakulima wadogo wakawa na mashine hizi ndogo nyingi ili tuwe na *central pool* ya kusafisha mafuta yale *for export*. Kwa hiyo, nakubaliana naye kwamba, tutamtafuta mwekezaji ambaye atapeleka hii mashine ya kusafisha mafuta ya alizeti na ya karanga. Ameshindwa kusema, watani wangu wanalima na karanga. Kwa hivyo, nitatafuta mwekezaji ambaye atasafisha mafuta ambayo ni *crude* yatatoka kwa wakulima wadogo, ambao nao watakuwa wamejiongezea kipato. (*Makofi*)

MHE. BENSON M. MPESYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika mchango wangu wa kuzungumza hapa Bungeni, nilirejea juu ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwamba, mambo mengi ya kufufua viwanda yapo kwa ujumla, lakini hili la Mbeya liliwekwa ndani ya Ilani kwamba, tutafufua viwanda vilivyopo Mbeya baada ya kuona kwamba Mbeya *is a dying city*. Katika mchango wangu nimelieleza hili, ningependa kuja tu kwa ajili ya kusaidiana, maana tunakoenda huko unga robo,

tusicheze mbali. Ninataka kujua nini mkakati hasa wa Serikali wa kuhakikisha kwamba, hili lililopo ndani ya Ilani linatekelezeka la kufufua viwanda Mbeya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha ZZK kwa mfano, tulipata mwekezaji ambaye ni miongoni mwa Waswidishi waliofunga mashine zile. Alikuwa tayari kukichukua kiwanda na kuanza uzalishaji, lakini mpaka sasa hakuna kinachoendelea. Ninaomba kujua ni lini ahadi hii itatekelezwa?

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Mpesa. Kwa sababu ya muda, sikuweza kwenda kwenye *details* za mkoaa mmoja mmoja. Nataka nimwambie kwamba, Kiwanda cha Zana za Kilimo Mbeya ni muhimu sana kwa ajli ya wakulima na Mbeya ni eneo muhimu kwa kilimo. Kama kuna mwekezaji na yeye amesema kuna mwekezaji, tupo tayari kuona anapewa hiyo haki na kama kuna wengine tutaweza kuwashamasisha kwa viwanda vingine, tutafanya hivyo.

Sisi tunazingatia Ilani ya Uchaguzi, tutasaidiana na Mheshimiwa Mpesa, kuona kwamba tunaharakisha ufufuaji wa viwanda hivyo, kikiwemo Kiwanda cha Zana za Kilimo Mbeya. (*Makofi*)

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii. Kwa kuwa *slogan* iliyotawala katika masikio ya wananchi wengi wa Tanzania ni “maisha bora kwa kila Mtanzania”; na kwa kuwa maisha bora kwa kila Mtanzania maana yake ni mwananchi apate lishe bora, lakini vile vile apate mahali pazuri pa kuishi; ni jambo la kusikitisha sana kuona kwamba, Tanzania imeruhusu watu kutoka nje kufanya biashara ndogo kama za umachinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi hawa wamejithidi wakiwa na mitaji yao midogo kuweza kufanya biashara (Wananchi wa Tanzania), lakini biashara zao sasa hivi zimekwamishwa kwa kiasi kikubwa sana na Wachina wanaofanya biashara hizo ndogo ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile utakubaliana nami kwamba, hata wanawake wengi sasa hivi ambao wamekuwa wajasiriamali, wamekuwa wakienda mpaka China na Hong Kong kuleta biashara, lakini kwa sasa hivi imeshindikana kwa sababu Wachina hao sasa hivi wanaleta mizigo mikubwa kutoka China na kwa bei nafuu sana; hivyo, Wananchi wa Tanzania ambao tunawatachia maisha bora, wameshindwa kufanya biashara hizo na kuzifunga. Ninaomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri; ni sheria gani inayoruhusu Wachina kufanya biashara ndogo humu nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ningependa kumuuliza Mheshimiwa Waziri, wakati anajibu suala hilo hilo la kuhusu maisha bora kwa kila Mtanzania; suala la Mabibo Wine ni muhimu sana. Kijana huyo ambaye amekopa shilingi zaidi ya milioni 500 kuleta vinywaji hivyo na aliruhusiwa, vimefika nchini halafu Mheshimiwa Waziri anasema kwamba, Mabibo Wine wamemzuia; hao Mabibo Wine wana uwezo gani wa kumzuua kijana huyu ambaye anafanya biashara ya aina hiyo? Je, ni Serikali hii hii

iliyomruhusu kuleta hizo bia au ni watu wengine na kwa nini huyo Mabibo Wine amzuie kuuza biashara yake? Ninaomba ufanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, jibu swali la kwanza, la pili usijibu bado lipo mahakamani.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Susan kwa kutaka ufanuzi na kama ulivyoelekeza wewe, suala la Mabibo Wine lipo Mahakamani. Narudia ...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri?

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Ndiyo!

MWENYEKITI: Nimetolea uamuzi kuhusu Mabibo Wine; nimesema jibu la kwanza.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunisaidia. Kuhusu wageni kuuza bidhaa kwenye Soko la Tanzania ambalo linapaswa liwe la Watanzania wenye, hilo tutalifanya kazi. Kama alivyosema, Wachina na wengine wote, nitashirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Wizara nyingine kama ya Mambo ya Ndani, kuona kwamba hilo tunakabiliana nalo na pengine kuongea na Balozi naye atusidie kusudi hawa wageni wasishindane kwenye maeneo ambayo ni ya wananchi wetu na vile vile pengine kuangalia na sheria zetu. Kwa kuanza, tutakaa mara moja na Wizara zinazohusika, kuliangalia tatizo hilo ambalo linawakwaza Watanzania kwa nia ya kuliondoa.

MWENYEKITI: Kwa hiyo, hakuna sheria au; maana aliuliza kuna sheria gani inayowaruhusu hao kufanya hayo?

WAZIRI WA VIWANDA, BAISHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kwa mtu ye yeyote kufanya biashara, lazima apate leseni na awe na *registered company*. Kwa hiyo, tutaangalia hizo sheria ili tuzitumie sasa kuwakabili hao watu wanaofanya hiyo biashara.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri anasema kwamba, sasa hivi ndio watakaa na Wizara nyingine, lakini suala la Wachina hata mwaka jana na mwaka juzi tulilionelea. Kwa hiyo, inaelekea Wziara haiko makini kufuutilia mambo hayo, kwa sababu sisi tunachoamini ni kwamba, sheria haipo ya kuwaruhusu hawa wamachinga wa kutoka nchi za nje na hakuna nchi nyingine yoyote...

MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mudhihir, kuhusu utaratibu!

MHE. MUDHIHIRI M. MUDHIHIR: Kifungu cha 64(1)(g).

MWENYEKITI: Unasema?

MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR: Kifungu cha 64(1)(g).

MWENYEKITI: Naomba ukisome.

MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR: Hapa sina Kanuni, lakini ipo kichwani kuhusu neno la kuudhi.

MWENYEKITI: Ehe, nani kakuudhi? (*Kicheko*)

MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR: Mheshimiwa Mwenyekiti, tumestahimili sana sisi Wamachinga, kwa maana ya Kabilia la Wamachinga. Mtu akiwa hapa Dodoma si rahisi kujua kwamba Musoma kuna makabila zaidi ya Wakurya na Waruo, lakini ni kweli kabisa kuna makabila mengine mengi tu. Inawezekana Wabunge hapa, pamoja na Serikali wanajua kwamba, Lindi wanatoka Wamwela tu, lakini tupo na Wamachinga. Imekuwa sasa ni tamko rasmi la Serikali kwamba, wafanyabiashara ndogo ndogo wao ni Wamachinga. Kwamba, Wamachinga tunavaa kandambili hiyo hiyo Jumapili mpaka Jumatatu! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo haya yanaudhi sana! Kilichotufanya watu wa Mikoa ya Lindi na Mtwara kuja Dar es Salaam wakati huo kuhangaika barabarani ni Serikali yenyewe, ambayo iliitenga Mikoa ile kama *Buffer Zone*. Sasa mambo haya ya vita yamekwisha, tunaomba turejeshewe heshima yetu, maana hata Katiba ya nchi hii inakataza kuwabagua watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona linaendelea kutajwa neno la Wamachinga na Serikali bahati nzuri wana Mswahili wa kuzaliwa na wa kusoma, Mheshimiwa Mohammed Seif Khatib; unatoho neno la kigeni pale ambapo neno la asili halipo. Kama *marching guys* nilivyojibiwa jana na Mheshimiwa Mwenyekiti hapo mezani, maana yake Wamachinga linatokana na *marching guys*, wafanyabiashara ndogo ndogo lipo. Watu wa Lindi na Mtwara msitulazimishe kuleta hoja binafsi ya kurejesha heshima yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba neno hili kuanzia sasa litolewe maamuzi au watumie biashara ndogo ndogo au wakiwazungumza Wamachinga waje kule Mchinga watusaidie sisi Wamachinga. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge, hapa tukiita mtu ambaye hayupo tunasema Mtera, kwa kweli kama neno linakuudhi na unataka liondoke utaleta hoja wewe. Tulivyoongea sisi ni *marching guys*, wala hata hatufiki ya kwamba watu wanazungumzia huko hakuna, mpaka na Njombe wapo wala siyo Mchinga na kila mahali. Kama *seriously* unataka, basi lete hoja sisi tukubaliane hapa. Lakini ni neno ambalo lipo linazungumzwa kama tunavyosema Mtera (mitini).

Mtera ni Jimbo la Mzee pale; historia yake ilikuwa siku moja tulikuwa na matatizo ya umeme, Rais akawa amekweda Mtera kukagua umeme na Wabunge wengine wakaenda huko. Kwa hiyo, kila aliyeitwa, tunaambiwa yuko Mtera, Mtera mpaka leo ni Mtera tu. Kwa hiyo, sisi nadhani hatuna mamlaka ya kulipigia marufuku wala kusema tunamaanisha hiyo ya huko Mtwara. Lakini kama uko *serious*, utaratibu upo, fuata Kanuni. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR: Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa! Nakushukuru kwa maelekezo yako, tutaleta hoja binafsi na kwa kweli tunaomba Serikali wakati tunasubiri kuleta hoja binafsi, wasitufanye watu wa Lindi na Mtwara kama Raia wa Msumbiji.

MWENYEKIDI: Mpaka utakapoleta hoja binafsi na kuamuliwa, wataendelea na Machinga! Mheshimiwa Susan, tulikuwa tumekukatisha tulifiki utaratibu kuhusu wewe. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kutoa ufanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu la nyongeza kwa Mheshimiwa Waziri, amesema kwamba, watakaa na Wizara *as if* sasa hivi ndiyo tunatoa hili suala la wafanyabiashara kutoka China. Toka mwaka juzi tumelizungumza, mwaka jana tumelizungumza, lakini bado Wizara haijachukua hatua za wazi kuonyesha kwamba, tunawajali Watanzania ambao wana mitaji midogo na wanafanya biashara ndogo ndogo. Kwa hiyo, tunaomba kujua ni kwa nini Wizara haijashughulikia jambo hili mpaka sasa hivi?

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, niliposema tutashirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Wizara nyingine zinazohusika, nilikuwa najaribu kuwa na tahadhari kwamba, nisichukue *mandate* ya kusemea mambo ya watu wengine.

Nakubaliana na yeze kwamba, ajira za Watanzania na biashara za Watanzania hatuna budi kuzilinda; na kwa hiyo, nina hakika kuna hatua zimechukuliwa kwa mtu mmoja mmoja lakini labda tatizo limekuwa kubwa sasa. Tatalichukulia kwa ukubwa wake na tatalitafutia ufumbuzi na tena wa haraka, lakini siyo mimi nikiwa peke yangu, kwa sababu *mandate* ni pana zaidi kuliko ya Wizara yangu.

MWENYEKIDI: Ahsante yeze ataongoza hiyo *mandate*.

MHE. ANNA M. KOMU: Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. Naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri kwamba, kwenye Hotuba ya Kambi ya Upinzani, ukurasa wa nne ibara ya 18; Kilimanjaro *Machines Tools*, kuna swali hapa ambalo tuliliuliza na tuna hamu kweli kutaka kujua kama kweli kiwanda hiki kinadaiwa na nchi ya Bulgaria;

na kama kinadaiwa ni kiasi gani; na kwa nini kiwanda hiki kilifungwa wakati kilikuwa bado kinaendelea kuzalisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo hicho tu nilichokuwa nataka kukijua ambacho Mheshimiwa Waziri hajatoa ufanuzi.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Komu kwa kutaka ufanuzi zaidi, baada ya kujibu kwamba mwaka 2004, serikali baada ya majadiliano, ililipa deni la Wabulgaria lilitotokana na Kiwanda cha *Machine Tools*.

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo pamba. Namshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa kumbukuka kuzungumzia juu ya mizani, lakini Mheshimiwa Waziri anajua kwamba kule tunakolima pamba Wizara ya Viwanda haipo. Kwa hiyo, unaponiambia ortalishughulikia ungeniambia kwamba, umemnong'oneza Mheshimiwa Waziri Mkuu alishughulikie kwa nguvu ningeweza nikakubaliana na wewe.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Cheyo, siyo *protocol* Waziri amwambie Waziri Mkuu afanye tena kwa nguvu.

MHE. JOHN M. CHEYO: Mimi naona uniachie nafasi nielezee swalı langu ninavyotaka, kama unataka kuniulizia niulizie.

MWENYEKITI: Hapana hatusemi hivyo, tunasema *is not in order* kwamba, Waziri amwagize Waziri Mkuu, haiwezekani labda ungesema *in other way!* Haya endelea bwana.

MHE. JOHN M. CHEYO: Sitarishana na Kiti, lakini naelewa unaelewa nataka kusema nini; kwa hiyo, ninachotaka kusema wale ambao wanashughulika na biashara hiyo ni *DCs*, Wakurugenzi na vitu kama hivyo.

Kwa hiyo, ndiyo maana nikaelekeza hilo jambo kwa *PM Office*, lakini kwa jinsi ulivyosema, naona kama umelisema *lightly* kidogo. Mimi ningependa uweke mkazo zaidi juu ya hilo jambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichonisumbua zaidi ni jibu la Mheshimiwa Waziri, juu ya *General Tyre* kwamba, kuna dola milioni kumi za wafanyakazi; kwanza ni nani aliyeruhusu fedha za wafanyakazi zikawekwa katika *risk business*; maana yake mpaka sasa hivi haijulikani kama kile kiwanda kitafufuka au kitakufa na kama kikifa ni nani ambaye ameihakikishia *NSSF* kwamba, fedha ya wafanyakazi itarudishwa?

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa John Cheyo, kwa kutaka mimi niweke uzito juu ya mambo ambayo tayari nimeelezea kuhusu vipimo vya lumbesa na vipimo vinavyotumika vibaya kuwaibia wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakala wa vipimo wapo chini ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko na wapo mpaka Wilayani. Kwa hiyo, kupitia Wakala wa Vipimo, tutahakikisha kwamba wakulima hawaibiwi na nitumie Bunge lako Tukufu kuwaomba Wakuu wa Mikoa na Wilaya kuhakikisha kwamba, wale ambao ndiyo wadau wao hawaibiwi na wote kwa pamoja tutawasaidia wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *General Tyre*, nilitoa maelezo nilidhani kwamba ni fasaha lakini kama hayajatosheleza, naomba kumweleza Mheshimiwa John Cheyo kwamba, dola milioni kumi zilizotolewa na *NSSF* kwenda *General Tyre* zilikuwa *guaranteed* na Serikali kwa kuona kwamba *NSSF* ni taasisi ya wananchi, kwa hiyo inapaswa kulindwa. Vile vile kwa kuona manufaa ya *General Tyre* kwa ajili ya Taifa letu na kwa wananchi, ikaona kwamba hizo fedha zitolewe. Kama *General Tyre* itashindwa kulipa, basi aliyetoa *guarantee* ndiye atakayehakikisha kwamba, *NSSF* inapata fedha hizo. Kwa hiyo, Wanachama wote wa *NSSF* wasiwe na wasiwasi.

MHE. DR. WILBROD P. SLAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi, sina nia ya kushika shilingi ya Waziri lakini ikilazimu nitaishika. Ninazungumzia bado suala la ubinafsishaji wa *SPM*; nataka kwanza nimhakikishie Waziri kwamba, hoja yetu haikuwa suala la ubinafsishaji, hakuna mwenye tatizo la kubinafsisha, hakuna ambaye hakutaka karatasi zitengenezwe, wala hakuna ambaye hakujua kwamba dawa zilizopo pale zilikuwa na athari; tatizo la msingi ni utata ulioko katika utaratibu wa ubinafsishaji.

Hii ni mali ya Watanzania wote, inathamani inayokisiwa kuwa ni zaidi ya milioni 500, imeuzwa kwa dola milioni moja wakati mkataba unataja milioni 26; hata *stamp duty* ya Serikali mkataba unatamka kwamba madhumuni ya *stamp duty* tutatoa tu milioni moja, haya siyo mambo ambayo tunaweza kuyapuzia, kwa sababu yanaleta utata wa uwazi katika mkataba huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni huyu mtu ambaye ana asilimia 99; tuliuliza ni sheria gani inaruhusu mtu amiliki asilimia 99.988 halafu hayupo kwenye mkataba na kwenye kampuni ile hajulikani; hivi tukipata utata katika nchi hii tunamuuliza nani? Tumefanya uchunguzi mpaka *British Virgin Island*, ambako anadhaniwa kwamba amesajiliwa huyu mtu hatujampata. Tulimwambia Waziri atupe namba yake ya usajili kule hajatupa, tulimwambia hata kama amesajiliwa *BRELA* atupe hiyo namba hatujaipata; je, kwa kuwa Waziri amesema atafuatilia; yupo tayari sasa kuunda Kamati ya Wizara yake; iufanyie kazi utata wote huu ambao bado upo katika utaratibu mzima; uweze kueleweka kwa Wabunge wote kwa niaba ya Watanzania na labda hata hizi nyaraka ziwekwe kwenye Maktaba ya Bunge; kwa sababu amesema atafuatilia hakuweka *timeframe*, tungependa *timeframe* ili tujue utata huu wote tunaumalizaje?

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilieleza kwa ufasaha kwamba, *SPM* ambayo baadaye imebadilishwa jina baada ya kubinafsisha kuwa *MPM*, ilikuwa kiwanda ambacho kimetangazwa kwa miaka 12 hakikupata mwekezaji na katika miaka hiyo wakati uzalishaji ulisimama.

Serikali ikabidi iwe inagharimia mashine zile zisiharibike kabisa na vile vile zile dawa zisileté athari za mazingira na usalama wa afya za watu. Bado Serikali ile ile ikaona kwamba, inahitaji bidhaa zinazotokana na *SPM* na kwamba inahitaji ajira ambazo kama *SPM* ikiendelea kuzalisha itawanufaisha Watanzania na vile vile teknolojia mpya.

Kwa ajili hiyo, ingeliuza mali za *SPM* kwa dola milioni 26. Yule alikuwa na hiari ya kukongoroa mashine na kila kitu akaondoka nazo au akapeleka mahali anapotaka, lakini tulijadiliana naye kwamba aendelee na uzalishaji kwa ajili ya manufaa niliyoyataja. Kwa hiyo, ikatumika *concept* ya *one dollar* kwamba, iuzwe kwa bei yoyote ili Watanzania wapate huduma hiyo ambayo tuliamini kwamba ni muhimu na bado Serikali inaamini kwamba, huduma ya *SPM* kuwepo pale ni muhimu kwa sababu nilizotaja, ndiyo maana zile dola milioni 25, Serikali ikaona iondokane nayo ili irudi kwenye uzalishaji kusudi *MPM* iendelee kuwepo, ndiyo maana ya *concept* ya *one dollar*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza tukapishana mitazamo, jinsi ya kuelewa suala lenyewe, sasa nimeomba kwamba, kwa pamoja tuendelee kuliangalia hilo; tueleweshane ili mambo yetu yakae kwa maslahi yetu sote. Suala la Wizara yangu kufuatilia, nalichukua hilo halina tatizo kujua zaidi juu ya *SPM* na hii ni kwa madhumuni ya kuiimarisha *SPM*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yule mtu aliyepewa *ninety nine point something shares*, wakati *RAI Group* inanunua *Angel* hazitakuwepo, wamenunua baadaye katika kufufua wamepata mwenzao wa kuweza kufufua naye kiwanda. *Angel* taarifa zake zimepelekwa *BRELA* na amekuwa *allotted* zile *shares*; ni jambo la kawaida kwenye *business*. zile *shares* 100 ambazo ziliwu *RAI Group*, zimekuwa *allotted* kwa *Angel* na hilo linajulikana kwa *BRELA* na bahati nzuri tumehangai ka kueleweshana, tumepiga simu *Registrar of Companies, British Virgin Island* na kuongea na Afisa anayeitwa *Benedin Smith* na kupata taarifa zifuatazo; wakati mimi niliporudi huku, Maafisa wangu walikuwa wanahangaika hiyo yote ni kujali na kutia umuhimu kwenye hoja ambazo mnatuletea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanayo kwenye rekodi zao kampuni inayoitwa *Angel Hurst Industries Limited*, yenyé namba za usajili 395195, taarifa anazotoa ni jina na namba za usajiti tu, ukitaka *anything more* ni lazima ufanye *official search* na kulipa dola 25. Kwa hiyo, tumejitahidi na katika kupata ukweli tutafanya wote, ukweli wa Watanzania wote. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Bado Mheshimiwa Dr. Slaa?

MHE. DR. WILBROD P. SLAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sitasisitiza kwa sababu Waziri anasema kwamba, amepokea hoja ya kuunda Kamati ya Wizara na kwamba atatuletea taarifa, lakini nataka kuweka rekodi sahihi. Waheshimiwa Wabunge, mimi nimefanya *research* mwenye; nataka kusema hivi mkataba hausemi dola moja, ungekuwa mkataba unazungumzia dola moja sina tatizo kwa sababu inapofika shirika ni la kutupa unatoa ile dola moja, Mkataba huu kwa nini uandike dola 26 lakini unasema

unalipa dola milioni moja? Mimi nafikiri tufanye utafiti, *this is the serious Problem* na ni vyema tukafanya utafiti kabla hatujaanza kupiga kelele ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri tulimpa hizi taarifa na tumeongea naye ofisini kwetu, ndiyo maana napiga kelele.

MWENYEKITI: Naomba muwe mnaongea msiwe mnapiga kelele. (*Kicheko*)

MHE. WILBROD P. SLAA: Nashukuru Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini inaudhi unapofanya kazi ya kitaifa watu wengine wanadharau tu. Nakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, *Angel Hurst* pia taarifa si sahihi kwamba, hakuwepo wakati *RAI Group* wanarekodi; tuna rekodi ya *TIC* ambayo inaonyesha hata hizo hela Mheshimiwa Waziri anazozitaja. *Actually*, wanataja zaidi; ni dola milioni 61 wala siyo 46 walizowekeza. Kwa hiyo, walikuwepo toka mwanzo; kuna nini katika maficho haya?

Tunaposema kwamba, tunataka ni kwa sababu tunataka kusiwe na utata ili kesho na keshokutwa mali ya wananchi isiuze kwa bei hiyo. Mali ya kiwanda kile hata ingeuzwa gari moja moja ni zaidi ya milioni 500 dola za kimarekani, hatuwezi kuziua tu kwa dola milioni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anasema kwamba, atafanya kazi, lakini ningeomba *timeframe* ni lini atawasilisha kwenye Bunge lako Tukufu?

MWENYEKITI: Sasa naagiza mimi kwamba, hizo *documents* zote mshirikiane na hao watakaokuwa kwenye Wizara halafu mlete wote taarifa Bungeni; ninyi mpeleke na wao wapeleke halafu mtaleta hapa Bungeni kitu tunachokubaliana. (*Makofî*)

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru na ninakupongeza kwa uamuzi wa muda mfupi uliopita, lakini pia nimekuwa *impressive* sana na majibu ya Waziri, anajitahidi sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliulizia na pia Mheshimiwa Kaboyonga aliulizia suala hili na bahati nzuri mimi na Mheshimiwa Kaboyonga, tumekuwa *very consistent* kwenye suala la *Economic Partnership Agreement*, lakini kwa bahati mbaya Waziri hakuweza kupata muda wa kujibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa napenda kufahamu na nilileta katika mchango wa maandishi kwamba, baada ya kuwa tumeamua kubadili *configuration* yaku-negotiate *Economic Partnership Agreement*, tulihitajika kufanya *impact study* na hasa hasa *revenue impact study*, kuweza kuona makubaliano yetu ndani ya *East African Community* na *European Union* yataatuathiri namna gani katika upande wa *revenue* ili tuweze kuona tutarekebisha vipi sera zetu za mapato ya ndani na kuweza kuziba hilo *gap* au misaada gani ambayo tutaipata kutoka *European Union* ili kuweza kuziba hilo *gap*. Bahati mbaya Waziri hakuweza kujibu. Tungependa kupata maelezo katika eneo hilo la

Economic Partnership Agreement na madhara ya *Joint Trade Negotiation Act*, ambayo ilipitishwa na Bunge la Afrika Mashariki kwamba, nchi zote za Jumuiya ya Afrika Mashariki ziweze kujadili kwa pamoja Mkataba huu lakini vilevile nani ambaye ana-*lead* hiyo *negotiation* kwa upande wa eneo lote hilo na kama vile vile tumeweza kuchukua ushauri wa kuishawishi nchi ya DRC iweze kuingia katika *EAC, EU-EPA* kwa ajili ya sisi kuweza kufaidika kwa sababu wale ni soko letu sisi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ambalo ningependa kufahamu ni kuhusiana na *CES*; ukurasa wa 37 wa Hotuba ya Waziri anaonyesha kwamba, Serikali ipo katika mchakato wa kuunganisha *EPZ* na *CES*. Ninapenda tu niweke hili wazi kwamba, huu ndio ushauri ambao ultolewa na Kambi ya Upinzani toka mwaka 2006. Wakati tunapitisha Sheria ya *Special Economic Zone* mwaka 2006, tulisema kwamba, hakuna sababu ya kuwa na *EPZ* na *SEZ*. Imechukua miaka miwili na Serikali imepata hasara kiuchumi, imekuja kukubaliana na wazo hilo lakini katika Hotuba ya Waziri kuna mchanganyiko; ukiangalia ibara ya 37 ya hotuba na ibara ya 40 ya hotuba ni kama kuna kutofautiana.

Ukiangalia katika ibara ya 40 yale maneno yaliyopo kwenye mabano yanaonyesha kwamba, *EPZ, CES* na *EDZ* zitaendelea kuwepo. Napenda nipate uhakika wa Waziri kwamba, tunachokifanya katika huo mchakato ni *ku-repeal EPZ Act* na *SEZ Act* na kuunda sheria mpya ya *EDZ* na nini itakuwa madhara ya maeneo ambayo tayari yana *EPZ* kwa mfano, Kigoma tuna *Kigoma Special Economic Zone* na toka mwaka jana tumekuwa tukipata fedha kwa ajili hiyo. Mkuu wetu wa Mkoa ndugu Simbakalia, napenda nichukue fursa hii kumpongeza sana, yupo *serious* katika suala hili la *Kigoma Special Economic Zone*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napenda kufahamu ni nini madhara ya kuleta *EDZ* kwa sisi ambao tayari tumeshaanza ku-*develop CEZ* yetu?

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na suala la *EPA*, Mheshimiwa Zitto na Wabunge wengine wanaelewa kwamba, tunaingia *EPA* kwa sababu tulikuwa na *arrangement* nyininge awali ya *Cotonou Agreement* kwamba, kulikuwa na *preferential trade arrangement* baina ya nchi ambazo zilikuwa kwenye mamlaka ya Ukoloni wa Uingereza wakati huo na Uingereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uingereza ilipoingia *EU* ikaingia na hiyo *preferential trade*, sasa *rules* za *WTO* haziruhusu *preference*. Sasa tunataka kuingia kwenye *arrangement* ambayo tuna-*abide by the WTO rules* lakini wakati huo huo tunakuwa na *even plain grant* na kwa hiyo *EPA* ndio namna pekee. *Cotonou Agreement* iliisha mwaka jana, tusinganzisha biashara yetu kati ya nchi zile zilizokuwa zinafanya biashara; *EU* ingekatika kwa sababu tusingekuwa na *arrangement*. Kwa hiyo, tukawa na *interim arrangement* kwa kuanzisha *EPA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana kwamba, tunahitaji kuwa waangalifu na tunahitaji sana kuuelimisha umma na kupata ushauri ili *arrangement* tutakayoingia iwe ni

ile ambayo itanufaisha nchi yetu vizuri, ikiwa ni pamoja na *configuration* ipi ambayo tunaingia nayo, *ESA, SADC* au *ECA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tumechagua Afrika Mashariki kwa sababu tupo kwenye *Custom Union* moja na kwanza ndiyo *natural* na ni hii ya pamoja. Kwa hiy, katika kwenda kwenye kusaini ile *agreement*, kunahitajika umakini mkubwa sana na kuangalia kwamba, nchi zetu zinanufaika. Hapa tulipo tuna bidhaa za asilimia 85 zinaingia kwa sababu tunahitaji bidhaa hizo hapa kwetu kama mashine, trekta na vitu vingine ambavyo ni vya lazima. Kwa hiyo, tunaloongelea ni ile asilimia kidogo iliyobaki, lakini hata hiyo ndogo inabidi tuwe waangalifu sana. Mimi naahidi nitatumia ujuzi wako na wa wengine wote, ili tupate kikubwa zaidi kwa sababu katika majadiliano kila mmoja anataka apate zaidi na tulipofikia hapa tumeona kwamba ni vizuri kuingia tukiwa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *EPZ* na *CEZ* tunachounganisha ni hizi *Authority* ziwe chini ya mamlaka moja; sasa *EPZ* maana yake ni *Export Processing Zones* kwamba, ukiwa pale kwenye *EPZ* inabidi bidhaa unazozizalisha asilimia 80 kama sikosei, kama nikikosea mnisamehe kwa sababu si rahisi kukumbuka mambo yote, lazima upeleke *for export* nje ya nchi hata kama zinatakiwa hapa wewe ni lazima upeleke kwa zile *incentives* ulizopewa. *SEZ* siyo tu kwa ajili ya *export* ni kwa nje na ndani ya nchi. Mimi sidhani kama kutakuwa na athari zozote kwa *EPZ* ambazo zipo, tunaweza tukaziimarisha zaidi kama watu wa Kigoma wanataka zaidi, lakini na *export* nayo inakuwa pale pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaboresha zaidi na katika kufanya hivyo tutaangalia maslahi ya maeneo yale.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu ya Waziri ni mazuri lakini kiasi kikubwa umejibu hoja za Mheshimiwa Kaboyonga alizozitoa asubuhi. Hoja niliyouliza mimi hapa ni kwamba, mmeshafanya *revenue study* mpya baada ya kuwa tumeamua *configuration* mpya na inaonyesha nini hiyo *revenue study* mpya? Ndilo lilikuwa swali langu hilo.

MWENYEKITI: Ulisema mengi mno ndiyo maana ukamchanganya.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea kufanya *Revenue Impact Assessment* za *preliminary zinaonyesha* kwanza hatuna uchaguzi ni lazima tuingie kwenye *arrangement*, sasa *arrangement* gani ambayo inatupa manufaa; tumefanya *assessment* nyingi ikiwepo ya *Revenue Impact Assessment* na tunaendelea mpaka tutakapofika mwisho.

MHE. SIRAJU J. KABOYONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kupata ufanuzi. Namshukuru Mheshimiwa Kabwe, kwa kunitangulia, amenisaidia kwa sababu nafasi tulizonazo ni za hoja moja tu. Hoja moja niliyobakia nayo kwa sasa ni kwamba, pale Tabora tuna Kiwanda cha Nyuzi, eneo ni kubwa linalotosheleza kuwa na *full textile mill* au tunaita *intergrated textile mill*, lakini ni

vigumu sana kumpata mwekezaji atakayeweza kufanya shughuli hiyo katika mazingira ya Tabora.

Katika mchango wangu nilitaka ufanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri; je, Tabora na kwa maana ya kiwanda kile, Serikali ipo tayari ku-*declare* eneo lile kama *SEZ* ili tuweze kuvutia wawekezaji watakaokuja kukipanua kiwanda kile cha kutengeneza toka uzi mpaka nguo ya mwisho kwa mtumiaji wa mwisho? Naomba ufanuzi.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Kaboyonga, kwanza mawazo anayoyatoa yanatusaidia sana kwenda mbele. Kuhusu kiwanda cha kutengeneza nyuzi, tija inakuwa kubwa zaidi kama tuki-*intergrate* mpaka mwisho. Kwa hiyo, nasema kwamb, tutakuja; nitawatuma wataalamu wa *EPZ* au *SEZ* waangalie uwezekano huo na kwa pamoja na Mheshimiwa Mbunge, tutatoa *informed decision*.

MHE. MHONGA S. RUHANYWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu niliishauri Serikali kuona umuhimu wa kuwa na *Intergrated Sector Strategic Master Plan*, kwa sababu kwa mfano Wizara hii inatakiwa iende sambamba na Wizara ya Miundombinu kama wanataka kuanzisha kiwanda mahali, kuwe na uhakika wa soko na kama mali ghafi inayotakiwa pale ni ya kilimo, mali ghafi hiyo izalishwe eneo hilo na kuwepo na uhakika wa maji na mambo mengine ikiwemo umeme, ili kuondoa matatizo ambayo tunaya-*face* sasa hivi. Nilitoa mfano wa Kiwanda cha Chumvi Uvinza ambacho ni kiwanda pekee tulinacho katika Mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, toka mwaka 1999 kimebinafsishwa, watendaji wa pale pamoja na kwamba hawajalipwa, lakini kinatumia magogo badala ya umeme. Ndiyo tatizo ambalo naliona kwa sababu hakuna *Intergrated Sectral Strategic Master Plan*, kwa sababu kiwanda kinaanzishwa sehemu hakuna hakuna umeme na matokeo yake ndiyo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika eneo lile la uvinza magogo yatakwisha, watahamia maeneo mengine ya Mkoa wa Kigoma, kwa hiyo kigoma itakuwa jangwa. Nataka kujua hali hii itakuwa mpaka lini na nini hatima ya wafanyakazi wa kiwanda kile, kwa sababu mpaka sasa hawajalipwa mafao yao na toka mwaka jana niliuliza swali hili katika Wizara ya Kazi? Naomba majibu.

MWENYEKITI: Sasa hapo ni *Intergrated Approach* ama ni suala la Kiwanda cha Uvinza?

MHE. MHONGA S. RUHWANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichosema nimeshauri kwamba, kuna umuhimu wa kuwa na *Intergrated Sector Strategic Master Plan*, kwa maana kwamba, Wizara hii iweze kushirikiana na Wizara nyingine, kwa mfano, kama eneo lina kiwanda, kuhakikisha kwamba kuna barabara na umeme. Tatizo lililopo Uvinza hakuna umeme na mpaka sasa hivi wanatumia magogo na jangwa linaendelea kuongezeka.

MWENYEKITU: Tumekuelewa, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri jibu swali la Uvinza sasa?

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mhonga kwamba, kuna umuhimu wa kuwa na *Intergrated Sectral Master Plan* na ndiyo Serikali inachofanya.

Sasa hivi Serikali imeiweka nchi yetu kwenye *corridors*; kuna *Mtwara Corridor* tunafanya hivyo, tuna *Central Corridor* ambako Uvinza itakuwepo na tuna *Nothern Corridor* ambayo Tanga itakuwa ni bandari na kwa *Central Corridor* kutakuwa na Dar es Salaam, vilevile kutakuwa na bandari kule *Lake Tanganyika*. Madhumuni ya kufanya hivyo ni kuhakikisha kwamba, miundombinu inatapatikana kwenye maeneo yote kusudi kuanzishwa kwa viwanda iwe ni rahisi na ndiyo namna pekee ya kuleta maendeleo.

Sasa kuhusu kuwalipa wafanyakazi, mimi nitaifuatilia pamoja na kwamba ipo kwenye Wizara nyingine; Serikali ni moja na tutasaidiana kuona kwamba nini kinafanyika.

MWENYEKITU: Ahsante, tunaendelea Mheshimiwa Mnyaa. Aaa! Karibu naanza kuwa-*limit*, kwanza Waheshimiwa Wabunge natumia Kifungu cha 104(1) kuongeza dakika 30. Sasa zikibakia hapo tena narudi kwenye kubanana. Mheshimiwa Mhonga ndiyo wa mwisho wa kuongeza.

MHE. MHONGA S. RUHWANYA: Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. Suala la mwisho ambalo nataka kuongeza; nataka kujua tutatumia magogo katika Kiwanda cha Uvinza mpaka lini, yaani nini hatima yake kwa sababu eneo lile linaendelea kuwa jangwa na watahama maeneo mengine vile vile? Kwa hiyo nataka kujua.

MWENYEKITU: Mheshimiwa Waziri au mwingine anayetaka kujibu.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia MCC nafikiri Kigoma itakuwa imebahatika; ni eneo moja ambalo linaweza kupata umeme na kwa hiyo ninaamini na Uvinza vile vile na ndiyo wakati huu ambapo magogo yataacha kutumiwa.

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Nashukuru Mwenyekiti na mimi kwa kunipatia nafasi. Sina haja ya kunyang'anya shilingi katika mshahara wa Waziri. Ningomba ufanunuvi katika eneo la viwanda na nadhani hutaniambia kwamba narukaruka, ni eneo lote la viwanda vidogo na vikubwa. Katika mchango wangu, nilitaka ufanunuvi kuhusu Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala, ambayo ndiyo inatumika inatoa dira na nikasema katika hiyo Ilani, ukurasa wa 101 kifungu cha (d), ilizungumzia kuhusu kuimarisha viwanda Zanzibar, kwa sababu ya matatizo ya ajira na Serikali ya Jamhuri ya Muungano itaisaidia na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hii ni Ilani ya 2005 mpaka 2010.

Muda ndiyo hivyo unayoyoma. Sasa vipi Wizara yako Mheshimiwa Waziri; imeisaidia vipi na imelenga vipi kuhusu viwanda hivyo vya Zanzibar? Halafu nikataka ufanuzi kwa Ilani hiyo hiyo ya 95 mpaka 2005; 2005 mpaka 2010 inazungumzia kuhusu viwanda mama na tukizungumza viwanda mama kuna maana ya Mchuchuma na Liganga, mara nyingi sana. Miradi hii imejulikana au mradi huu miaka mingi sana toka 1896. Hizi *research* au tafiti zimefanywa miaka mingi sana. *NDC* tayari wameshafanya upembusi yakinifu wa kutosha na kujua kuna hiyo *TITAN* gesi kiasi gani, *Iron* kiasi gani na wawekezaji katika hotuba yako ukurasa wa 22, 23, 24 unasema wawekezaji wapo 81 na makampuni kumi, lakini sasa wawekezaji wako miaka saba nyuma wamejipanga. Utafiti gani huu uliobakia wan a wa kutafuta nini; hawa wawekezaji watacaa kwa muda gani na miaka mingi inapita?

Halafu nyingine kiwanda cha mwisho nikasema ...

MWENYEKITI: Aaah!

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Haya ahsante. Hayo hayo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi tunaanza kwenda nje ya muda.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Mnyaa, amenihakikishia kwamba, watoto wangu wataendelea kuishi. (*Kicheko*)

Kuhusu Viwanda vya Zanzibar, hata mimi nakubaliana na Ilani yetu ya Uchaguzi ya CCM kwamba, Zanzibar ni eneo dogo. Kwa hiyo, shughuli nyingine za uchumi pengine hazitakuwa na tija sana kama ilivyo viwanda. Sasa kwa sababu Wizara hii si ya Muungano, nitashirikiana kwa karibu sana na Waziri wa Viwanda wa Zanzibar ili tuone basi nini kimefanyika na nini tuongeze kasi ili Ilani yetu itekelezwe. Ahsante kwa kutukumbusha tutekeleze Ilani. (*Makofi*)

Sasa kuhusu viwanda mama nimesema ni kweli utafiti umefanywa, lakini utafiti uliofanywa hautoshelezi kwa sababu ni wa juu juu sana. Sasa hivi ni viwanda vya msingi sana na maliasili ni kubwa sana na maslahi ya Taifa ni makubwa sana. Tumeangalia ni namna gani ya kuharakisha pengine kwa kuwaruhusu wawekezaji wachoronge nusu ya udongo watupe twende maabara kuupima. Hiyo haichukui muda mrefu, nakuhakikishia kwamba Mradi wa Liganga na Mchuchuma utaanza kutekelezwa. Naomba uwe na imani kama hivyo ulivyoamua kutotaka mshahara wangu.

MHE. HALIMA J. MDEE: Nashukuru Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi.

MWENYEKITI: Sasa naenda kwa *item* moja moja tu, maana yake muda umeisha.

MHE. HALIMA J. MDEE: Nashukuru Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa hii nafasi. Nina hakika umenipa wakati mgumu, lakini inabidi ...

MWENYEKITU: Tumia muda wako vizuri. Endelea tu.

MHE. HALIMA J. MDEE: Katika majibu ambayo Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko amemjibu Mheshimiwa Cheyo, kuhusiana na suala zima la *General Tyre*, ametoa jibu kuhusiana na *guarantee* ya Serikali ...

MWENYEKITU: Kawaida kama suala limeshazungumzwa harudii mwininge suala lile lile. Ndiyo Kanuni hiyo. (*Makofî*)

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, siulizii swali la Mheshimiwa Cheyo, naunga swali lake kujenga hoja ya suala jipya. Kwa hiyo, naomba unisikilize hadi mwisho, kama nikiwa nimeenda kinyume ...

MWENYEKITU: Mbona unatumia muda endelea kusema mimi nikusikilize.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, si ndiyo nimekujibu.

MWENYEKITU: Wewe ukisema nitakukatisha tu. Endelea kusema mimi nitakusikiliza, halafu nikiona haifanani nitakwambia hapana.

MHE. HALIMA J. MDEE: Nashukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti. Niendelee sasa pale ambapo niliishia; Waziri alikuwa anazungumzia *guarantee* ya Serikali ya asilimia 100 na mwenyewe amekiri kwamba, *General Tyre* ipo katika hali ngumu sana. Sasa huu ni ushauri kabla ya swali kwamba ni muhimu kusema kwamba, Serikali ina-*guarantee* asilimia 100, pesa za Serikali nazo ni kodi za wananchi; kwa hiyo *hai-make sense* kusema kwamba *General Tyre* ipo katika hali ngumu, *then tunapeleka pesa uzitupe ziende kupotea*.

Sasa nikija kwenye hoja yangu; mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma na katika taarifa ambayo Kamati sisi tunayo inaonyesha kwamb, Serikali haina mkakati wowote wa kuisaidia *General Tyre*. Mkakati ambao unaonekana ni wa kuweza kuinyanyua au kuikomboa *Kagera Sugar* kutokana na hali iliyoko sasa hivi. Sasa nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri anisaidie, inawezekana ile ripoti kuna mabadiliko ambayo yametokea labda mwaka mmoja uliopita. Aniambie kama kuna mkakati wa kuisaidia *General Tyre* na mkakati huo ni upi?

Swali dogo la pili linahusiana na suala zima la *Tanganyika Packers*.

MWENYEKITU: Hapana, Mheshimiwa Waziri jibu.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ukweli kabisa tupo kwenye majadiliano na Serikali ina nia ya kuifufua *General Tyre. (Makofi)*

MHE. LUCY F. OWENYA: Nashukuru Mheshimiwa Mwenyekiti. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, mimi nina swali dogo tu kwa faida ya Wizara yake. Katika kifungu namba 260700 - *Rent Expenses*, Wizara imeomba milioni 744.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Owenya katika mshahara wa Waziri?

MHE. LUCY F. OWENYA: Ndiyo ipo hapo hapo kwenye mshahara wa Waziri.

MWENYEKITI: *Okay!* Eleza vizuri.

MHE. LUCY F. OWENYA: Sawa! Wizara imeomba milioni 744,900,000 kwa ajili ya *Rent Expenses*; ina maana kwa miaka mitano tangu 2005 mpaka 2010 Wizara itakuwa imelipa bilioni 3,630,000,000 kwa kodi tu; ukizingatia Wizara hii ina matatizo ya fedha kwenye Taasisi zake nyingi za maendeleo, imetoa fedha pungufu ambapo fedha hizi zingeweza kutumika katika kuzisaidia taasisi zile.

Mimi ningependa nipate majibu kutoka Serikali Kuu, maana yake itakuwa namwonea Mheshimiwa Waziri. Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha kwamba, inatenga kiwanja kwa ajili ya Wizara hii kama inavyofanya kwenye Wizara nyingine ili iweze kuwa na Ofisi yake yenye? Naomba maelezo.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, tupo kwenye mchakato wa kutafuta eneo la kuweza kuanza kujenga jengo la Wizara badala ya kuendelea kulipa hii *rent*. (*Makofi*)

MHE. BENITO W. MALANGALILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimpe pole sana Mheshimiwa Waziri kwa namna anavyohangaika na suala la MPM au SPM Mgololo. Mimi ni Mbunge wa eneo hilo, nilimshukuru sana Mungu kiwanda hicho kilipobinafsishwa. (*Makofi*)

Swali langu linahusiana kwamba, wakati mimi nachangia nilizungumzia juu ya mafao ya wafanyakazi wa Kiwanda cha Pareto pale Mafinga. Jambo hili nililizungumzia kwa kirefu sana, nadhani Mheshimiwa Waziri analikumbuka; sijui anatoa majibu gani?

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Malangalila kama atakumbuka, Mheshimiwa Naibu Waziri alilijibu akasema kwamba, tutachacharika na tutashirikiana na Wizara ya Kilimo kuona ni nini wanadai na tufanye nini ili kutekeleza madai yao.

MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile mimi ni mtu wa mazingira na kutokana na uwekezaji unaotaka kuanza Ludewa, hasa kwa kuunganisha Miradi ya Mchuchuma ya Makaa na ile ya Chuma, pamoja na miundombinu. Imeelezwa kwenye hotuba kwamba, wanatafuta wawekezaji wa kuunganisha yote kwa pamoja.

Kwa hiyo, mimi nilitaka ufanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri na nilizungumza kwamba, tunganeza sasa kufanya *strategic environmental assessment* ya huo utaratibu. Hapa ni mahali pazuri sana kufanya *strategic environmental assessment* ili tuju vitu hivi vinaingiliana vipi, athari na faida kwa nchi, kwa wilaya na kwa mkoa zitakuwaje, pamoja na kufanya *land use plan* ili kuwe na utaratibu unaoeleweka wa matumizi ya ardhi wakati tunaanza viwanda hivi kwa sababu italeta watu wengi sana Ludewa kutakuwa ni fujo tupu. Je, Mheshimiwa Waziri anatoa maelezo gani kwenye hili?

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na ushauri wa Mheshimiwa Mbunge; tutafanya hivyo, tutaanza kuangalia *strategic environmental impact assessment* ili tuweze kuibua mambo haya na nini tufanye.

MHE. ANNE K. MALECELÀ: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali dogo sana. Kabla ya hapo, niseme kweli kabisa kwamba, Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, mmejitahidi sana kutujibu maswali yetu vizuri na tumepata nguvu kwenye Wizara hii kubwa. (*Makofî*)

Swali langu ni dogo sana, ambalo ni la kuweka rekodi sawa. Wabunge wengi kuanzia jana mpaka leo wakati tunachangia suala la *SIDO*, tulikuwa tunapigania kwamba *SIDO* ilikuwa imeomba bilioni tano, lakini imepewa bilioni moja. Jambo la kwanza, nimefurahi kwamba Waziri umeonyesha kwamba, *SIDO* ndiyo atakayeokoa Watanzania. Lakini wakati Mheshimiwa Naibu Waziri anachangia, nilimsikiliza vizuri, nikapata picha tofauti na ile ambayo tulikuwa nayo jana kwamba, mpaka tunalala mpaka leo tulikuwa tunajua *SIDO* wameomba bilioni tano wamepewa bilioni moja. Alipojibu Naibu Waziri, nikapata picha tofauti. Bado nikaandika *ki-note* Katibu Mkuu akanijibu hapa hapa ndani, nikapata picha ya kwamba kwa sura hii *SIDO* wamepewa bilioni 8.6.

Kwa hiyo, nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri ili kuweka rekodi sawa kwa Wabunge, pamoja na Wananchi kwa ujumla, *SIDO* wametengewa bilioni 8.6 au ni bilioni moja ambayo tulikuwa tunaifikiria jana?

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, *SIDO* imepewa shilingi bilioni 1.1 OC na *SIDO* imepewa bilioni 7.234 na zingine huko kwa ajili ya maendeleo. Kwa hiyo kwa ujumla *SIDO* imepewa bilioni 8. (*Makofî*)

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nipate ufanunuzi. Ufanunuzi ambao ninauhitaji ni mdogo tu.

Katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri na katika maelezo yake amekiri kuwa, viwanda ni muhimu sana katika Sekta ya Kilimo kuleta maendeleo ya nchi hii.

Katika ukurasa wa 39 amesema kwamba, hivi sasa na siku za usoni, tutaongeza juhudhi katika kuongeza thamani mazao ya kilimo. Ukweli ni kwamba, viwanda ama havijengwi au vinajengwa kwa kasi ndogo sana, kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wengi wameonyesha.

Mimi nilitaka kujua kama Serikali ina mpango unaoonyesha kiwanda gani, kinajengwa wapi na lini ili kukidhi haja ya wananchi na Waheshimiwa Wabunge kuona kwamba, hili jambo linafanyika au halitafanyika na kupunguza masuala mengi ambayo yamekuwa yakiulizwa Bungeni. Ahsante.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: *I am sorry.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Viwanda ni kujenga viwanda na kipaumbele viwanda vitakavyosindika mazao ya kilimo ili kwenda haraka. Viwanda vitakavyojengwa itategemea malighafi iliyopo mahali hapo. Kwa mfano, Singida wamesema wanalima alizeti. Kwa hiyo, tutaelekeza viwanda vidogo vya alizeti kule na kikubwa cha kusafisha mafuta ya alizeti na kwingine na hivyo tutafanya hivyo kutegemea na malighafi iliyopo na hali inavyotegemea. Kwa hiyo, ukija pengine tutatafuta nafasi Mheshimiwa Mbunge tutaongea vizuri, tutaeleweshana vizuri. (*Makofi*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 1002 – <i>Finance and Accounts</i>	Sh. 265,585,100
Kif. 1003 – <i>Policy and Planning</i>	Sh. 1,345,317,800
Kif. 1004 – <i>Information, Educat. Communication Unit</i>	Sh. 156,954,700
Kif. 1005 – <i>Internal Audit Unit</i>	Sh. 135,996,900
Kif. 1006 – <i>Legal Services Unit</i>	Sh. 36,012,100
Kif. 2001 – <i>Industry</i>	Sh. 2,083,006,600
Kif. 2002 – <i>Small and Medium Enterprises Division</i>	...	Sh. 3,139,051,600
Kif. 3001 – <i>International Trade</i>	Sh. 1,522,564,900
Kif. 4002 – <i>Commodity Market Development</i>	Sh. 3,521,227,000

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 44 – Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko

Kif. 1001 – *Administration and General* Sh. 105,000,000

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya*

(Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1003 – *Policy and Planning* Sh.19,838,423,000

MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hiki cha 400949420 - *Tanzania Mini-Tigers Planning 2020* kuna bilioni 12. Mimi nina swali; je, katika hii *plan* ya bilioni hizo kuna utekelezaji wa *commitments* alizozitoa Mheshimiwa Waziri kwa Mheshimiwa Nyawazwa, kuhusu kuimarisha viwanda vya usindikaji samaki (sangara, sato, ngere na furu) katika Wilaya ya Ukerewe ili tuweze kupeleka kwenye *export* kuchangia zaidi katika uchumi wa nchi hii? (*Makofit*)

MWENYEKITI: Anauliza; je, hizi ndiyo hizo? Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASARA NA MASOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hizo lakini tutatafuta kwenye mafungu mengine. (*Makofit*)

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2001 – *Industry* Sh. 75,000,000

MWENYEKITI: Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya ni *Urban Development and Environmental Management*. kifungu chote kinasema hivyo. Ndiyo hicho Mheshimiwa Stella?

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Samahani Mheshimiwa Mwenyekiti, nakingojea 4002.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2002 – *Small and Medium Enterprises Division* .. Sh. 6,569,917,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3001 – *International Trade* Sh. 2,197,779,600

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba ufanuzi kama kifungu hiki kinahusiana na *International Trade Fair*, yaani Saba Saba? Naomba kujua kama kinahusika kwa sababu hii *International Trade Fair* imekuwa ikifanyika Dar es Salaam peke yake; naomba kujua kama Wizara ina mkakati wa kuhakikisha kwamba ile Siku ya Saba Saba pia mikoani kunakuwa na Maonyesho ya Biashara?

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki siyo cha *International Fair* au *fair* ya hapa ndani, lakini tunashiriki kwenye *fair* mbalimbali na kuna maeneo mengine ambayo yatatusaidia katika kwenda kwenye *International Fairs*.

MWENYEKITI: Kwa hiyo, si chenyewe hicho?

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 4002 – *Commodity Market Development* Sh. 2,476,015,000

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. Katika kifungu kidogo cha 4486, naona kuna pesa za *Basket Fund* kwa ajili ya *Agriculture Sector Development Programme*. Nilikuwa naomba kwa kuwa zile shughuli za uyoga kule Ruvuma zinakwama kutokana na mbegu za uyoga na tulikuwa tunaomba msaada wa karibu, hawa akina mama wasikatishwe tama; na kwa kuwa hizi programu zinaendeshwa ndani ya Wizara yake na ndiyo waliofundisha; je, tunaweza tukaponea hapo?

MWENYEKITI: Unaulizwa je, hapo ndiyo penyewe? Siyo kuponea tu hapo ndiyo penyewe? (*Kicheko*)

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo penyewe na shughuli zimepangwa, tutaangalia kama inawezekana kumsaidia Mheshimiwa Stella Manyanya.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

(*Bunge lilirudia*)

T A A R I F A

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kupitisha kifungu kwa kifungu, makadirio ya matumizi ya fedha ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa mwaka wa fedha 2008/2009 na kuyapitisha bila ya mabadiliko yoyote. Hivyo, naomba kutoa hoja ya kwamba, makadirio hayo sasa yakubaliwe na Bunge lako.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa mwaka
2008/2009 yalipitishwa na Bunge)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Wabunge, nafurahi kusema Mheshimiwa, *we are proud of you.* Kwa sababu tunapokaribia *fifty fifty* mambo kama ndiyo haya, hakuna sababu ya watu kutunyima *fifty fifty.* (*Makofi*)

Sisi tuko *very proud* kwa ulivyoweza kujieleza na kuweza kuji-commit; Wabunge wamekuuliza maswali, tumepata imani kubwa sana kwako wewe na Wizara yako yote na watumishi wote wa Wizara hiyo na sisi tunapenda kusikia Wizara zenye nguvu kama hii. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kesho tutaingia Wizara ya Katiba na Sheria nayo ni mjadala wa siku mbili. Kwa hiyo, nategemea Waheshimiwa Wabunge, mtashiriki kama mlivyoshiriki vizuri sana katika hii Wizara na Waziri anayekuja nayo ndiyo *land mark* hii. Kwa hiyo, naomba nimshukuru sana. Nawatakia jioni njema na mapumziko mema mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.57 usiku Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Jumatano,
Tarehe 13 Agosti, 2008 Saa Tatu Asubuhi)*